# KUFUWAWA KWA MIIKO NA KUPOTOKA KWA MAADILI

# UCHUNGUZI KIFANI WA JAMII YA WABUNGU

**JOACHIM ALOYCE NDAMBA KISANJI**

**IMEWASILISHWA IKIWA MAHITAJI PEKEE YA KUTUNUKIWA**

**SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA**

**CHA TANZANIA**

**2013**

## UTHIBITISHI WA MSIMAMIZI

Aliyetia saini hapa chini alithibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa ***"Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili Uchunguzi Kifani wa Jamii ya Wabungu".*** Kwa ajili ya kusahihishwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ili kukamilisha mahitaji ya Shahada ya Uzamili wa Kiswahili (Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Prof. Dkt. Sheikh T.S.Y.M.Sengo

(Msimamizi)

Tarehe

## HAKIMILIKI

Tasnifu hii ni mali ya Mwandishi na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Hivyo haki zote zimehifadhiwa na hakuna ruhusa ya kunakili, kutoa nakala za fotokopi, elektroniki, kurekodi au kwa njia yoyote bila idhini ya maandishi kutoka kwa Mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# TAMKO LA MTAHINIWA

**Mimi, Joachim Aloyce Ndamba Kisanji,** ninatamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii iitwayo “Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili Uchunguzi Kifani wa Jamii ya Wabungu” ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuhudhurishwa popote kwa lengo la kufuzu shahada yoyote.

……………………………………………

Joachim Aloyce Ndamba Kisanji

…………………………………………

Tarehe

## TABARUKU

Kazi hii naiweka wakfu kwa ajili ya Wazazi wangu wapendwa Baba yangu Aloyce Kisanji na mama yangu Isabella Simon Bangu ambao wamepumzika katika usingizi wa amani, mke wangu mpenzi Deodata, watoto wangu wapendwa Daudi, Josephine, Aloyce na Mercylydia ambao wamekuwa chachu na taa yangu katika kuifanya kazi hii.

## SHUKRANI

Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mweza wa yote kwa kunijalia afya njema na nguvu za kuweza kufanya kazi hii. Kipekee nawashukuru marehemu wazazi wangu Aloyce Kisanji na Isabella Bangu kwa kunilea katika maadili mema ya Kibungu halisi na kunifanya niwe jinsi nilivyo leo hii. Ninawaenzi kwa kila fanikio langu kimaisha leo hii.

Pili, shukurani zangu za dhati zimwendee Prof. Dkt. Sheikh T.S.Y.M. Sengo kwa kunizalishia wazo hili ambalo kwalo mimi binafsi lilikuwa linanitatiza kwa sababu nyingi zilizokuwa nje ya uwezo wangu, hasa kwa kuchelewa kupata matokeo yangu ya Shahada ya Kwanza. Penye watu hapaharibiki jambo, pasi yeye sidhani kama ningeweza kuanza chembe ya tasnifu hii.

Tatu, namshukuru mke wangu mpenzi Deodata, ambaye amekuwa akinivumilia wakati wote nilipochelewa kurudi nyumbani na kunitia moyo wa kufanya kazi hii kwa muda mrefu usiku. Siwezi kuwasahau watoto wangu wote wapendwa, Daudi, William, Josephine, Aloyce na Mercylydia. Utulivu wao, sauti zao na uvumilivu wao kwa kunikosa mara nyingi hasa nyakati za jioni vilinitia hamasa katika kukamilisha tasnifu hii.

Kwa fursa hii pia namshukuru mwanafunzi mwenzangu Roda Msemo kwa kunitia moyo na kutumia muda wake kujadiliana nami kuhusu mswada wa tasnifu hii. Kwa dhati ya moyo wangu, sitakuwa na fadhila nisipowataja Dkt. Rose Oluochi wa MS.TCDC-Arusha na Dkt. Deogratias Ngonyani wa Michigan State University - USA kwa kunisaidia katika Mbinu za Utafiti.

Uongozi wa MS TCDC nao unastahili kupokea shukrani zangu azizi kwa kuniweka katika mazingira bora ya kazi ambayo yameniwezesha kukamilisha kazi hii. Kipekee kabisa namshukuru Mkuu wa Chuo ambaye alikuwapo wakati ninaaza kazi hii Ndugu Prudence Kaijage kwa kunitia moyo wa kuthubutu.

Shukrani maridhawa pia zimwendee Mkuu wa Idara Steven Ndosi, Mkuu wangu wa kitengo cha Lugha Yusta Mganga pamoja na wafanyakazi wenzangu wa kitengo kicho, walimu Gaudentia Lwakatare na Frida Teri kwa kunisaidia shughuli zangu wakati nilipokwenda kukusanya data. Dada Yusta, kama kiongozi bila hiyana ametumia muda wake mwingi katika kuhakikisha ninamaliza kazi hii kwa wakati. Rafiki yangu Winston Makere aliyekuwa Mwenyekiti wa chama cha wafanyakazi (RAAWU) tawi la MS-TCDC Arusha, amekuwa nguzo yangu na kengele yangu ya asubuhi kuniamsha kila niliposinzia na kunieleza kuwa inawezekana kusonga mbele.

Pia, ninapenda kumshukuru kwa dhati rafiki yangu mpendwa na mshauri wangu Mwalimu Fidelis K. Kyarwenda - Mkaguzi wa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu Kanda ya Kaskazini Magharibi-Arusha, kwa kutumia muda wake mwingi kupitia na kuisoma kazi yangu kisha akanipa ushauri faafu katika kuikamilisha na kuifanya kazi hii kuwa furufu.

Mwisho kabisa ninapenda kuwashukuru wale wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine katika kukamilisha tasnifu hii. Ni wengi sana na ni vigumu kutaja majina yote, itoshe tu kusema kwamba wote ninawaombea kwa Mungu. Yeye awabariki na kuwajaza pale pote walipotoa kwa ajili ya utafiti huu.

## IKSIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza na kutafuta miiko ya jamii ya Wabungu. Mada ya utafiti ilikuwa ni kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili uchunguzi kifani kwa jamii ya Wabungu. Mtafiti alitumiya njia ya uchunguzi kifani ili kumwezesha kupata data alizozikusudiya. Njia hii ilimwezesha mtafiti kuwasaili watafitiwa wakati huo huo akifanya uchunguzi. Ukweli ni kwamba katika utafiti huu, mtafiti aliongozwa na nadharia za Elimu ina Kwao na Fasihi ina Kwao pamoja na nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake. Kwa hali hiyo utafiti ulikuwa umesanifiwa vizuri na kumwezesha kupata data za awali na za msingi kwa wakati. Jumla ya watafitiwa 23 walisailiwa. Kati ya hawa wanaume walikuwa 15 na wanawake 8 tu. Katika utafiti huu mtafiti aliweza kukusanya miiko takribani 114 kati ya miiko hiyo yote ni miiko 20 tu ndiyo iliyojadiliwa kwa kiwango cha maadili na mingine ilijadiliwa kifalsafa na miiko mingine iliorodheshwa tu. Baada ya uchambuzi wa data zote za maelezo mtafiti alibaini kuwa ni kweli kuwa maadili ya jamii ya Wabungu yamepotoka. Watafitiwa walimweleza mtafiti usasa ni chimbuko kuu la kupotoka kwa maadili. Usasa huo ni pamoja na elimu isiyokuwa na misingi ya maadili mema na ujumi wa jamii inayowazunguka. Aidha taalimu ina kwao na fasihi ina kwao ilishadidia kupotoka kwa maadili katika jamii ya Wabungu. Mwisho mtafiti alitowa mapendekezo kwa Wizara husika kama Elimu na Utamaduni kuliangalia suala hilo kwa mtazamo wa kufuwawa kwa miiko na maadili. Pia tafiti nyingi iwezekanavyo zifanywe ili jamii za Kitanzania ziweze kuuhisha miiko ambayo ni nyanja adhimu katika sanaajadiiya.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHI WA MSIMAMIZI .......... ii**

**HAKIMILIKI .......... iii**

**TAMKO LA MTAHINIWA .......... IV**

**TABARUKU .......... v**

**SHUKRANI .......... vi**

**IKSIRI .......... viii**

**VIAMBATISHI .......... xxi**

**ORODHA YA VIFUPISHO .......... xxii**

**SURA YA KWANZA .......... 1**

**1.0 UTANGULIZI WA JUMLA .......... 1**

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Mada ya Utafiti .......... 2

1.3 Usuli wa Mada .......... 2

1.4 Usuli wa Tatizo .......... 2

1.5 Kauli ya Tatizo .......... 7

1.6 Nia Kuu ya Utafiti .......... 8

1.7 Madhumuni Mahususi ya Utafiti .......... 8

1.8 Maswali ya Utafiti .......... 8

1.9 Umuhimu wa Utafiti Huu .......... 9

1.10 Eneo la Utafiti .......... 10

1.11 Vikwazo vya Utafiti .......... 10

1.11.1 Utatuzi wa Vikwazo .......... 11

1.12 Hitimisho ........................................................................................ 11

**SURA YA PILI ........................................................................................ 13**

**2.0 MIKABALA YA NADHARIA ........................................................ 13**

2.1 Utangulizi ........................................................................................ 13

2.2 Dhanna ya Nadharia ........................................................................ 13

2.2.1 Mawazo ya Jumla Kuhusu Nadharia ............................................ 15

2.2.2 Matatizo ya Nadharia ...................................................................... 17

2.2.3 Hitimisho ........................................................................................ 18

2.3 Nadharia ya Nadharia ........................................................................ 18

2.3.1 Chimbuko la Nadharia ya Nadharia ................................................ 18

2.3.2 Wazo Kuu la Nadharia ya Nadharia ................................................ 19

2.3.3 Umuhimu wa Nadharia ya Nadharia ................................................ 19

2.4 Nadharia ya Taalimu ina Kwao na Fasihi ina Kwao ........................ 20

2.4.1 Chimbuko la Nadharia ya Taalimu ina Kwao na Fasihi ina Kwao ........ 21

2.4.2 Wazo kuu la Nadharia Taalimu ina Kwao na Fasihi ina Kwao ........ 21

2.4.3 Umuhimu wa Nadharia ya Taalimu ina Kwao na Fasihi ina Kwao ........ 23

2.5 Nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake ........................................ 24

2.5.1 Umuhimu wa Nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake ................ 26

2.5.2 Hitimishi ........................................................................................ 29

2.6 Nadharia ya Ndani-Nje ........................................................................ 29

2.6.1 Chimbuko la Nadharia ya Ndani Nje ................................................ 29

2.6.2 Wazo kuu la Nadharia ya Ndani Nje ................................................ 31

2.6.3 Umuhimu wa Nadharia ya Ndani Nje ................................................ 31

2.7 Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika ........................................................ 33

2.7.1 Chimbuko la Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika ............ 33
2.7.2 Wazo Kuu la Uhalisia wa Kiafrika ............ 34
2.8 Nadharia ya Ufeministi ............ 35
2.8.1 Chimbuko la Nadharia ya Ufeministi ............ 35
2.8.2 Mawazo Makuu ya Nadharia ya Feministi ............ 35
2.8.3 Umuhimu wa Nadharia ya Ufeministi ............ 37
2.9 Hitimisho ............ 38
**SURA YA TATU ............ 40**
**3.0 KAZI TANGULIZI ............ 40**
3.1 Utangulizi ............ 40
3.2 Eneo la Utafiti ............ 41
3.2.1 Asili ya Wabungu ............ 41
3.2.2 Shughuli za Kiuchumi ............ 42
3.2.3 Elimu ............ 43
3.3 Maana ya Miiko ............ 43
3.3.1 Kudhalilishwa kwa Utu na Wageni ............ 44
3.4 Mapisi ya Miiko katika Sanaajadiiya ............ 46
3.5 Umuhimu wa Miiko ............ 47
3.5.1 Kuhifadhiwa kwa Sanaajadiiya ............ 48
3.5.2 Kukengeuka kwa Maadili ............ 49
3.5.3 Ulimbe wa Miiko na Mali Asili ............ 50
3.5.4 Miiko na Mgawanyo wa Kazi ............ 52
3.6 Hali ya Miiko katika Jamii ya Wabungu ............ 53
3.6.1 Miiko na Kifo ............ 54

3.6.2 Miiko ya Uzazi na Ndoa ..... 54
3.6.3 Miiko na Adhabu ..... 55
3.6.4 Miiko na Maendeleo Imarishi ..... 56
3.6.5 Pengo la Kuzibwa na Utafiti ..... 57
3.6.6 Hitimisho ..... 58
**SURA YA NNE ..... 59**
4.0 NJIA ZA UTAFITI ..... 59
4.1 Utangulizi ..... 59
4.2 Usanifu wa Utafiti ..... 59
4.3 Umuhimu wa Usanifu wa Utafiti ..... 60
4.4 Njia za Utafiti ..... 60
4.4.1 Njia ya Kielezeo Stahilifu na Kielezeo cha Kiasi ..... 61
4.5 Ukusanyaji wa Data ..... 62
4.5.1 Data za Awali ..... 62
4.5.2 Data za Upili ..... 62
4.6 Uteuzi wa Watafitiwa ..... 64
4.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ..... 65
4.7.1 Njia ya Usaili ..... 65
4.7.2 Mtihani wa Njia ya Usaili ..... 66
4.7.3 Ushuhudiaji ..... 67
4.7.4 Hitimisho ..... 67
**SURA YA TANO ..... 68**
**5.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI ..... 68**
5.1 Utangulizi ..... 68

5.2 Maana ya Miiko ........................................................................................ 70

5.3 Miiko na Ushirikina........................................................................................ 71

5.4 Maana ya Maadili........................................................................................ 74

5.4.1 Wajibu wa Wazazi Katika Kuwafundisha Watoto Wao Miiko .................... 76

5.4.2 Wajibu wa Jamii katika Kufundisha Miiko kwa Watoto .............................. 78

5.4.3 Wajibu wa Viongozi Katika Kuwafundisha Miiko Watoto ........................... 79

5.5 Miiko Yenye Maadili ........................................................................................ 80

5.5.1 Miiko ya Chakula........................................................................................ 80

5.5.2 Miiko Kuhusu Wizi Katika Jamii ya Wabungu ............................................ 83

5.5.3 Miiko ya Kutamka Maneno........................................................................ 84

5.5.4 Miiko na Mazingira........................................................................................ 85

5.5.5 Mwiko wa Kumpita Mtu Mzima na Mzigo Bila Kumpokea ......................... 86

5.5.6 Mrejesho wa Miiko Wanayofundishwa Watoto Salamu............................... 86

5.6 Mtazamo wa Watu Wazima Kuhusu Ulimbe wa Miiko ya Wabungu ........... 88

5.6.1 Miiko na Mavazi ........................................................................................ 90

5.6.2 Miiko Ubunguni Bado Inafundishwa kwa Watoto ....................................... 92

5.6.3 Mgongano wa Elimu ya Miiko ya Wabungu na Muziki wa Kisasa............... 93

5.7 Ulimbe wa Miiko ya Wabungu ........................................................................ 93

5.7.1 Ni Mwiko kwa Wanawake Kuoga Ziwani au Mtoni, Samaki Watakimbia.... 95

5.7.2 Ni Mwiko kwa Mwindaji Akiwa Mawindoni Kuruka Mti au Gogo Lililolala, Akiumwa na Nyoka si Rahisi Kupona ........................................................ 98

5.7.3 Ni Mwiko kwa Mvulana au Msichana Kuoa au Kuolewa na Kilema, Watazaa Mtoto Kilema ........................................................................................ 99

5.8 Viongozi Waonavyo Ulimbe wa Miiko ya Wabungu ................................... 100

5.9 Watoto Waonavyo Ulimbe wa Miiko ya Wabungu ..................................... 101
5.10 Watu Wazima Wanavyoona Matatizo Yanayojitokeza Katika Kuitumia Miiko ya Wabungu..................................................................................... 102
5. 10.1 Dini............................................................................................. 102
5.10.2 Luninga / Televisheni ................................................................... 103
5.10.3 Elimu ............................................................................................ 104
5.10.4 Shughuli za Kiuchumi ................................................................... 105
5.10.5 Ndoa ............................................................................................ 106
5.10.5.1Ni Mwiko Kula Ukiwa Umesimama, Utakuwa Mkimbizi au Utaoa au Kuolewa Mbali ............................................................................ 107
5.10.6 Tabia za Wazazi ............................................................................ 108
5.11 Mtazamo wa Viongozi Kuhusu Matatizo Yanayojitokeza Katika Kuitumia Miiko ya Wabungu...................................................................... 109
5.12 Mtazamo wa Watoto Kuhusu Matatizo Yanayojitokeza Katika Kuitumia Miiko ya Wabungu...................................................................... 110
5.13 Suluhisho la Wabungu kutumia Miiko Mtazamo wa Watu Wazima.......... 110
5.13.1 Utunzaji wa Siri............................................................................. 111
5.13.2 Mimba Kabla Ndoa ....................................................................... 112
5.14 Suluhisho la Wabungu Kutumia Miiko – Mtazamo wa Viongozi ............... 112
5.15 Suluhisho la Wabungu Kutumia Miiko – Mtazamo wa Watoto ................. 112
5.15.1 Maadili Mema – Salamu ................................................................ 113
5.16 Miiko Kuhusu Heshima (Mavazi)........................................................ 121
1.16.1 Ni Mwiko kwa Wanawake Kuvaa Suruali.......................................... 123
5.16.2 Ni Mwiko Kuvaa Nguo za Kubana kwa Wanaume na Wanawake ............ 124

5.16.3 Ni Mwiko kwa Wanawake Kuvaa Nguo Fupi ........................................... 125
5.17 Miiko kwa Viongozi ............................................................................... 126
5.17.1 Ni Mwiko kwa Mwene Kuingia Katika Eneo la Mwene Mwingine Bila Taarifa, Ataleta Balaa Katika Nchi Yake ................................................... 127
5.17.2 Ni Mwiko Kukalia Kiti cha Mwene ........................................................ 128
5.17.3 Ni Mwiko Kukataa Amri Yoyote Kutoka kwa Mwene .............................. 129
5.17.4 Ilikuwa ni Mwiko Kutoa Siri za Baraza au Kikao Chochote cha Usuluhishi au cha Baraza la Wazee .................................................................................. 130
5.17.5 Ni Mwiko kwa Mwene Kwenda Kuoga/ Kuogelea Mtoni au Ziwani ......... 131
5.17.6 Ni Mwiko kwa Mwene Kwenda Kuwinda Wanyama, Kuvua au Kutega Samaki, Wanyama au Samaki Wataadimika Kabisa .................................. 132
5.17.7 Ni Mwiko Kufanya Tambiko kwa Kutumia Wanyama au Mazao Kutoka Nje ya Miliki ya Mwene au Wabungu ............................................................ 132
5.17.8 Ni Mwiko Kutoa Mali au Viti vya Mwene Nje ya Miliki ya Wabungu ...... 133
5.17.9 Mawasiliano Kati ya Mzazi na Mtoto ....................................................... 134
5.17.10 Ni Mwiko kwa Mvulana au Msichana Kutabii Tabia au Maadili Mabaya Kutoka Nje ya Ukoo ...................................................................................... 135
5.17.11 Usipite Katikati ya Watu Wawili au Kundi .............................................. 135
5.17.12 Mwiko Kuiba, Mtu Ataugua Ukoma ....................................................... 136
5.17.13 Ni Mwiko kwa Mvulana Kuwategemea Wazazi, Hawezi Kuoa ................ 137
5.17.14 Wavulana Walio Balekhe ni Mwiko Kulala Katika Nyumba ya Wazazi, Hawataoa ....................................................................................................... 137
5.17.15 Ni Mwiko Kumpa Mimba Msichana Nje ya Ndoa Kama Ikitokea, Mhusika Alilazimishwa Kumwoa Huyo Binti ......................................................... 138

5.17.16 Ni Mwiko kwa Mtoto au Kijana Kuingilia Mazungumzo ya Watu Wazima au Kuzungumza Bila Ruhusa ........ 138
5.17.17 Ni Mwiko kwa Mtoto Kuanza Kunawa na Kula Kabla ya Wakubwa na Pia Hawezi Kuondoka Mahali pa Kulia Chakula Kabla ya Wakubwa ........ 139
5.17.18 Ni mwiko Mtoto Kuanza Kula Mboga Kabla ya Wakubwa ........ 139
5.17.19 Ni Mwiko Kuondoka, Unapompa Mtu Maji ya Kunywa Kabla ya Kumaliza ........ 139
5.17.20 Ni Mwiko kwa Binti au Mvulana Kuoa au Kuolewa na Mtu Kutoka Familia ya Watu Wenye Ukoma, Kifua Kikuu, Surua, Kifafa au Ndui, Atazaa Watoto Wenye Maradhi Hayo ........ 140
5.17.21 Ni Mwiko Kukalia Ungo ........ 140
5.17.22 Ni Mwiko Kujisugulia Mchanga wa Mtoni Unapooga, Unawatabiria Kifo cha Mapema Wazazi Wako ........ 140
5.18 Miiko kuhusu Kuoa / Kuolewa/ Ndoa ........ 141
5.18.1 Ni Mwiko kwa Binti au Mvulana Kuowa au Kuolewa na Mtu wa Jamii Tafauti ........ 141
5.18.2 Ni Mwiko Kuoa au Kuolewa Bila Ridhaa ya Wazazi ........ 142
5.18.3 Ni Mwiko kwa Mtu Kufanya Tendo la Ndoa Nje ya Ndoa Kabla ya Safari, Mtu Atapata Balaa Njiani ........ 142
5.18.4 Ni Mwiko Kuzungumza Masuala ya Ngono na Uzazi Mbele ya Watoto ........ 142
5.18.5 Ni Mwiko Kutoka Nje ya Ndoa, Mke Akiwa Mjamzito, Mimba Itatoka ........ 143
5.18.6 Ni Mwiko kwa Mwanaume Kulala Nje ya Nyumba Kama Mke wake ni Mjamzito, Atashindwa Kujifungua ........ 143
5.19 Miiko Iliyokusanywa na Mtafiti ........ 143

5.20 Miiko Kuhusu Heshima (Vyakula) ............................................................ 144
5.20.1 Mwanamke ni Mwiko Kula Mayai, Atazaa Mtoto Mwenye Kipara ........... 144
5.20.2 Mwanamke ni Mwiko Kula Firigisi, Akila Anaonesha Dharau kwa Mumewe
............................................................................................................ 145
5.20.3 Ni Mwiko Kula Gizani, Utakula na Shetani ............................................... 145
5.20.4 Ni Mwiko kwa Mwanamke Kula Nyama ya Mnyama Mwenye Mimba,
Atapata Shida ya Kujifungua ...................................................................... 146
5.21 Miiko Kuhusu Bahari na Uvuvi .................................................................. 147
5.21.1 Ni Mwiko Kuoshea Vyungu Vyenye Masizi Ziwani, Samaki Watakimbia/
Wataadimika.................................................................................................. 147
5.21.2 Ni Mwiko kwa Wanawake Wakiwa Katika Siku Zao Kwenda Ziwani,
Samaki Watakimbia ...................................................................................... 148
5.21.3 Ni Mwiko Kuingia Kwenye Mtumbwi na Viatu.......................................... 149
5.22 Miiko Kuhusu Kazi (Uvivu na Uwindaji)................................................... 150
5.22.1 Ni Mwiko Kwenda Porini Kuwinda Kama Mwindaji Amegombana na Mtu,
Atapambana na Wanyama Wakali .............................................................. 150
5.22.2 Ni Mwiko kwa Wanawake Kwenda Kuwinda Porini Usiku, Wanyama
Watakimbia ................................................................................................... 151
5.22.3 Ni Mwiko Kwenda Kulala Nje ya Ndoa Kama Mtu Anakwenda Kuwinda,
Wanyama Watakimbia .................................................................................. 151
5.22.4 Ni Mwiko Kucheka au Kupiga Kelele Mawindoni, Utapotea ..................... 152
5.22.5 Ni Mwiko Kuruka Nyama Baada ya Kuua Porini, Walaji Wataharisha...... 152
5.22.6 Ni Mwiko Kukung’uta Mkia wa Mnyama Aliyeuliwa, Walaji Wataharisha
153

5.23 Miiko Kuhusu Kilimo .................... 153
5.23.1 Ni Mwiko Mtu Kula Chakula Shambani Akiwa Amesimama, Mazao Yataliwa na Wanyama .................... 154
5.23.2 Ni Mwiko Kukimbia Ndani ya Shamba, Unaingiza Nguruwe.................... 155
5.23.3 Ni Mwiko Kumpa Mbegu Mtu Mkononi .................... 155
5.23.4 Ni Mwiko Kuingia au Kuchukulia Mbegu za Kupanda Shambani Katika Chungu Chenye Masizi, Mtu Hawezi Kupata Mazao Mengi .................... 156
5.23.5 Ni Mwiko Kuingia na Ndara au Viatu Katika Shamba la Karanga, Hazitakomaa Vizuri .................... 157
5.24 Miiko Kuhusu Wanawake .................... 157
5.24.1 Ni Mwiko kwa Mtoto wa Kike Kukaa Katika Kizingiti cha Mlango, Atachelewa Kuolewa .................... 157
5.24.2 Ni Mwiko kwa Mwanamke Kupika Akiwa Katika Siku Zake .................... 158
5.24.3 Ni Mwiko kwa Mwanamke Kuchuma Mboga za Majani Akiwa Katika Siku Zake, Mboga Zitakauka .................... 159
5.24.4 Ni Mwiko kwa Mwanamke Kumshika Mtoto Mchanga Ambaye si Mtoto Wake Akiwa Katika Siku Zake .................... 159
5.24.5 Ni Mwiko Kupakua Ugali Bila ya Kuuviringa Vizuri, Hasa kwa Wageni, Wakwe na Mume .................... 160
5.24.6 Ilikuwa ni Mwiko kwa Mwanamke Kumpa Mume Chakula Bila Kuonja .. 160
5.24.7 Ni Mwiko kwa Mwanamke Kutoka Nje ya Ndoa Mumewe Anapokwenda Safari ya Kuwinda, Mumewe Atapata Balaa au Hawezi Kuua Nyama .................... 161
5.24.8 Ni Mwiko Kufunga Mlango Mchana Mume Akiwa Amekwenda Kuwinda, Mke Atakuwa Amefunga Pori na Mume Hawezi Kuona Wanyama .................... 161

5.25 Miiko Kuhusu Watoto ..... 162
5.25.1 Ni Mwiko Kumshtua Mtoto, Usiku Ataota Ndoto za Kustuka Usiku ..... 162
5.25.2 Ni Mwiko Kufulia Nguo za Mtoto Mchanga Mtoni ..... 162
5.25.3 Ni Mwiko Kwenda Msalani na Nguo ya Kubebea Mtoto ..... 163
5.26 Miiko Kuhusu Wanaume ..... 164
5.26.1 Ni Mwiko kwa Mwanaume Aliyeoa Kuingia au Kupika Jikoni, Atakuwa Ameolewa na Mwanamke ..... 164
5.26.2 Ni Mwiko kwa Mwanaume Kukalia Kinu Ataota Majipu Makalioni ..... 165
5.26.3 Ni Mwiko kwa Mwanaume Kukalia Kinu Akikijambia, Atakapoowa Kila Mke Atakuwa Anakufa ..... 166
5.26.4 Ni Mwiko Kumpiga Mwanaume kwa Ufagio, Atapooza ..... 166
5.26.5 Ni Mwiko Kukojowa Mtoni au Ndani ya Maji Uume Wako Utavutika ..... 167
5.26.6 Ni Mwiko Kuingia Kaburini na Viatu ..... 167
5.27 Miiko Kuhusu Maradhi ..... 167
5.27.1 Ni Mwiko Kuishi au Kuchangia Vitu na Wagonjwa wa Ukoma, Kifua Kikuu, Surua, Kifafa au Ndui ..... 168
5.28 Miiko Kuhusu Usafiri ..... 168
5.28.1 Ni Mwiko kwa Mwanamke Mjamzito Kutembea Mwendo Mrefu Usiku ..... 168
5.28.2 Ni Mwiko Kutangaza kwa Watu Kuwa Mtu Anasafiri, Atarogwa/ Ataviziwa / Atategwa Njiani ..... 169
5.29 Miiko Inayohusu Usafi (Kazi) ..... 169
5.29.1 Ni Mwiko Kuacha Mwiko uliosongewa Ugaki na Ukoko ..... 169
5.29.2 Ni Mwiko Mtu Kufagia Usiku, Akifagia Anafukuza Wageni Nyumbani ..... 170
5.29.3 Ni Mwiko Mtu Kutupa Takataka Usiku, Anatupa Baraka ..... 170

5.30 Miiko Mingine ........ 170
5.30.1 Ni Mwiko Kujinyonga ........ 171
5.30.2 Ni Mwiko kupakaa Mafuta Kuanzia Miguuni Kwenda Kichwani ........ 171
5.30.3 Ni Mwiko Kushona Nguo Mwilini Ukiwa Umevaa, Unajitabiria Kifo ........ 171
5.30.4 Ni Mwiko Kukoroga Chakula kwa Kisu, Walaji Wataumwa Tumbo la Kukata na Kuharisha Damu ........ 172
5.30.5 Ni Mwiko Kwenda Usiku Kisimani au Mtoni Kuchota Maji ........ 172
5.30.6 Ni Mwiko Kwenda Dukani Kununua Chumvi Usiku ........ 173
5.30.7 Ni Mwiko kuinamisha Kichwa na Kunywa Maji Mtoni, Utapigwa na Mkia wa Mamba ........ 174
5.30.8 Ni Mwiko kuitika Wito Bila Kumwona Mtu Anayeita ........ 174
**SURA YA SITA ........ 176**
**6.0 MUHUTASARI WA MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 176**
6.1 Utangulizi ........ 176
6.2 Muhtasari ........ 177
6.3 Matokeo ya Utafiti ........ 181
6.4 Mapendekezo ........ 187
6.5 Hitimisho ........ 190
**MAREJELEO ........ 192**
**VIAMBATISHI ........ 200**

## VIAMBATISHI

Kiambatishi I: Msamiati........................................................................................ 200

Kiambatishi II: Gharama za Utafiti........................................................................ 202

Kiambatishi III: Ratiba ya Utafiti .......................................................................... 203

Kiambatishi IV: Maswali ya Utafiti........................................................................ 204

Kiambatishi V: Miiko ya Kibungu na Tafsiri ......................................................... 208

Kiambatishi VI: Ramani ya Eneo la Utafiti ............................................................ 218

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| TUKI | - | Tasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| Kk | - | Kabla ya Kristo |
| Nk | - | Na kadhalika |
| NKS | - | Nadharia ya Kelelezo Stahilifu |
| NKK | - | Nadharia ya Kielelezi cha Kiasi |
| KK | - | Kabla ya Kristo |
| MS-TCDC | - | MS- Training Centre for Development Cooparation |
| RAAWU | - | Reseachers, Academician, and Allied Workers Union |
| DS | - | Development Studies |
| Kv | - | Kama vile |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti amezungumzia kwa kina kuhusu chimbuko na tatizo la utafiti huu. Utafiti huu unahusu kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili katika Jamii ya Wabungu. Mtafiti amebainisha usuli wa mada ya utafiti kwa kubainisha umuhimu wa miiko katika jamii.

Suala jingine lililojadiliwa na mtafiti ni kuhusu maadili ya jamii ya Wabungu. Mtafiti ameangalia kwa upeo matatizo yanayosababisha kukengeuka kwa maadili ya wanajamii. Miiko kama kanuni, sheria, amri, taratibu au mwongozo wa namna ya kuishi katika jamii, inapaswa kufuatwa.

Katika utafiti huu mtafiti anakubaliana na nadharia ya nadharia inayosema kuwa mawazo yote yanabadilika kila uchao, na mawazo ya mtu yamejengwa katika uzoefu wa matukio katika maisha, aghalabu mtafiti anaona kuwa miiko ni mhimili wa maadili ya jamii mabadiliko yoyote yanapaswa kuchunguzwa na yanapaswa kuwa mabadiliko chanya (Barry, 2009; Masalu na wenzake 2010; Watts, 2007).

Utafiti huu umefanywa katika vijiji vya Mwambani na Udinde vilivyoko katika mkoa wa Mbeya wilaya ya Chunya. Wilaya hii ipo Kaskazini Magharibi ya mji wa Mbeya, kati ya latitudo nyuzi ya 7 na 9 Kusini mwa Ikweta na kati ya longitude nyuzi ya 32 na 34 Mashariki ya Greenwich (Planning Commission Tanzania, 1997; Rugemalira, 2009). Utafiti unahusu Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili katika jamii ya Wabungu.

## 1.2 Mada ya Utafiti

Kuchunguza Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka Kwa Maadili, Uchunguzi Kifani wa Jamii ya Wabungu.

## 1.3 Usuli wa Mada

Katika sura hii mtafiti ameeleza umuhimu wa miiko katika jamii. Mtafiti ameeleza nafasi ya miiko katika malezi ya jamii ikiwa ni sehemu ya sanaajadiiya. Pia amejadili matatizo ya kufuwawa kwa miiko katika jamii ya Wabungu. Katika utafiti huu mtafiti anabainisha kuwa utandawazi, matumizi ya pataninga, mitandao, picha za senema, muziki wa kizazi kipya ni mifano michache inayotoa ithibati ya kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

Mtafiti anabainisha juhudi za Tanzania katika kulinda maadili ya Watanzania na kutoa mifano juu ya juhudi hizo za Tanzania. Jamii ya Wabungu haiishi katika ombwe, hivyo nayo ipo katika nchi ya Tanzania na kwa hali hiyo inaathirika na matatizo ya kimaadili yanayotokea nchini Tanzania. Maelezo haya yanashadidiwa na usuli wa tatizo la utafiti.

## 1.4 Usuli wa Tatizo

Mwanadamu hujiundia njia za kuelezea namna anavyouelewa ulimwengu aishimo kwa kupitia tanzu mbalimbali za sanaajadiiya k.v. ngano, nyimbo, methali, miiko n.k. Tanzu hizi za kisanaajadiiya zipo katika mzunguko mzima wa maisha ya jamii tangu kuzaliwa, makuzi, kifo na baada ya kifo. Miiko huchukuwa nafasi kubwa katika kuonesha na kurekebisha mienendo ya wanajamii (Masalu na Wenzake, 2010; Palmer, 1996; Vuzo, 1989; Sengo, 1985; Sengo na Kiango, 1972; Watts, 2007; Mulokozi na wenzake 1985; Kipacha, 2009).

Katika miaka ya hivi karibuni, hali hii ya miiko katika Tanzania, imekuwa ni tete sana. Inaonekana kana kwamba Watanzania wengi wa kada mbalimbali wameathirika kimaadili kwa kuacha kuitumia miiko. "*Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo*". Kabla ya kuuelewa wasifu wa mtu, si rahisi kuona na kujua wasifu wa ndani, bali ni rahisi kuona wasifu wa nje kwanza. Tabia ya mtu hujitokeza katika matendo na maneno. Kwa mfano, mavazi ya kubana na kuonesha maungo ya mwili ambayo ni mwiko katika jamii, ni dhahiri kuwa mvaaji ana tabia yenye kuleta mashaka katika jamii ya Wabungu. Kama mtu huyo akiwa katika mavazi haya ya kuonesha gimba na akaonekana katika maeneo ya ulevi au kasino, basi walimwengu watakuwa na hoja mbalimbali kuhusiana na tabia ya mtu huyo bila hata ya kuona vitendo anavyovifanya vya kuvunja miiko. Wahenga walisema, "*kila mchuma janga hula na wa kwao*" (Karama, 1983; Kipacha, 2009).

Karama katika methali hii anawakumbusha Wabungu kuwa, kwa mtu kukengeuka katika maadili anavunja miiko na anakaribisha matatizo kwake mwenyewe. Matatizo hayo aliyojisababishia hayaishii kwake tu, ila matatizo haya yataikumba pia jamii yake kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, mtu akivunja mwiko wa kuiba kitu kwa jirani. Mtu huyu aliyeiba anakuwa ameleta aibu, kwanza kwake binafsi na familiya yake kwa upande mwingine. Licha ya aibu, mtu huyu atahitaji msaada wa ndugu katika kuomba dhamana, kufuatiliya kesi na hata kwenda kutazamwa magereza. Kama mtu huyu aliyeonekana katika kasino au kutembeya nusu utupu ni Mbungu basi aibu itakwenda kwanza kwa familia na pia kwa Wabungu wote.

Binadamu hujifunza tabia na maadili kwa kutumia akili, hasa katika harakati za kutimiza haja zao. Maadili hupatikana katika mafundisho mbalimbali ya jamii na

hasa katika tanzu za fasihi simulizi. Miiko ni moja ya tanzu za kutolea mafunzo hayo ya kurejelea tabia na adabu njema za wanajamii (Haralambos na wenzake, 2004; Mponda, 1962; Sengo na Kiango, 1973).

Wanataalimu wengi ambao wamerejelewa kazi zao na mtafiti, ni mwanataalimu mmoja tu ndiye aliyeandika ingawa hakubainisha kama miiko ni tanzu au kipera cha sanaajadiiya au ya fasihi simulizi. Katika utafiti huu mtafiti anabainisha kuwa, miiko ni utanzu mojawapo wa fasihi simulizi au sanaajadiiya. Utanzu huu una sifa sawa kabisa na methali, nahau, vitendawili na hata misemo. Hiki ni kipera kinachojitegemea. Kwa wapenzi wa kuchora majedwali ya matawi ya kuelezea vipera vya sanaajadiiya, basi sasa waongeze miiko katika majedwali yao.

Wamitila, (2008) anasema kuwa tangu enzi ya akina Plato na Arestotle, limekuwako suala hili la uhusiano uliopo kati ya maadili ya jamii na fasihi. Licha ya watangulizi hao, wanataalimu wengi wa Magharibi, Asia, Mashariki ya mbali na Afrika, nao wamezungumzia uhusiano wa maadili na fasihi. Kinachojadiliwa hapa ni mchango wa fasihi katika kuathiri maadili ya jamii. Suala kuu limekuwa ni kuangalia na kuchunguza mchango wa fasihi katika kuyaendeleza na kuyalinda maadili ya wanajamii wake. Jee, kama upo mchango huo, unajitokeza katika kazi zipi za kifasihi na unaweza kupewa kongole gani katika kuuendeleza? Hapa ndipo mtafiti anapoona kuwa kuna haja kubwa ya kufanya utafiti kuhusu nafasi ya miiko katika kuiadilisha jamii ya Wabungu.

Hakuna maadili katika muktadha fulani hasa katika maisha, matendo au maneno ya mtu (Wamitila, 2008). Kwa mfano, nchini Tanzania, kuna baadhi ya kazi za fasihi

zilizopigwa marufuku kwa matumizi ya darasani kutokana na misingi ya kuwa zimekosa maadili. Mfano ni kitabu cha *Rosa Mistika* kilichoandikwa na *E. Kezilahabi*. Msingi wa kupiga marufuku kitabu hicho ulikuwa ni lugha ya udhalilishaji wa watoto wa kike wa shule kulikofanywa na walimu wao. Lengo la msingi katika kupiga marufuku kazi hiyo lilikuwa ni kulinda maadili ya Watanzania, ingawa baadaye kitabu hicho kiliruhusiwa kuendelea kutumika katika shule za sekondari nchini. Hali kadhalika, Tanzania ilianzisha Bodi ya Filamu ili kudhibiti filamu zinazotoka nje na hata za ndani. Kazi kubwa ya bodi hiyo ni kutoa ithibati kwa filamu ambazo hazikengeushi maadili ya Kitanzania na kuruhusiwa kuoneshwa katika kumbi za senema nchini Tanzania.

Kwa kuwa maadili hujikita katika uhusiano wa mtu na mtu, mtu na jamii yake, au mtu na mazingira yake, na kwa kuwa uhusiano huo humfanya mtu kuishi vema na jamii yake, mtafiti kwa kuzingatia kufuwawa kwa miiko katika jamii ya Wabungu, ameona kuna haja ya kuiangalia miiko na sababu za kufuwawa kwa miiko hiyo katika mazingira ya kupotoka kwa maadili ya jamii ya Wabungu. Maendeleo ya kimaadili ni muhimu zaidi kuliko maendeleo ya kisiasa ambayo kwa karne nyingi yamekuwa yakirandana sana (Jastraw, 2009). Kuwa mwanasiasa mashuhuri na wa kuogopwa kwa uwezo wa kifedha ambazo haifahamiki kazipataje, hakutampa heshima ya utu wake kisawasawa. Watu watajua kuwa yeye ni mwongo na mlaghai tu.

Kufuwawa ni kuachwa, kupuuzwa, kutokuzingatiwa, kutokutumiwa kwa makusudi au kwa kutokujua kwa kitu fulani. Kwa mujibu wa mazungumzo ya mtafiti na Prof. Sengo, neno *kufuwawa* linatokana na msamiati wa watu wa pwani, ambapo chombo

cha baharini huwepo majini kikielea tu bila kufanya kazi yoyote. Hali hiyo ya kufuwawa kwa *miiko* kumeifikisha jamii ya Wabungu katika janga la kupotoka *kimaadili*. Katika utafiti huu, mtafiti amechunguza miiko ya jamii ya Wabungu na athari zake katika kulinda na kukuza maadili miongoni mwa wanajamii (Bathawab na Sengo, 2007).

Wamitila (2008) anatoa mfano muhimu sana katika suala la maadili. Kazi za fasihi zenyewe zinapaswa kuwa na maadili au uadilifu. Miiko ni moja ya kipera cha fasihi ambacho kina uwezo wa kuijenga jamii kimaadili. Miiko ni fimbo ya kumwongoza mwanajamii aliyekengeuka ili ajione dhahiri kuwa ayafanyayo ni makosa. "*Mwacha asili ni mtumwa*" (Karama, 1983). Anayeacha mwenendo mwema, mila zake za asili, utamaduni wake ulioshika mizizi yake ndani ya jamii, na kufuata utamaduni wa wageni ambao hajuwi hata chimbuko lake, mtu huyu ni mtumwa. Mtumwa ndani ya akili yake, hisia zake na hata utu wake. Miiko ya jamii ya Wabungu ndiyo kimbilio la Wabungu wenye utu. Miiko ina ulimbe, falsafa na ujumi wa Mwafrika.

Katika Sera ya Utamaduni Tanzania, imetamkwa wazi kuhusu kutafiti, kuhifadhi, na kufasiri lugha za jamii (Sera ya Utamaduni, 1997:17). Katika kutekeleza sera hii, mwaka 2009, Chuo Kikuu cha Dar es salaam kilitoa Atlasi ya kwanza ya Lugha za Tanzania. Kongole kwa Mradi huu. Katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kuna mradi mwingine mkubwa wa Fasihi za Kinchi. Mtafiti anatoa kongole kwa mshika bendera wake Prof. Dr. Sheikh T.S.Y.M. Sengo, kwa kuhimiza kuwako kwa Fasihi ya Tanzania, Fasihi ya Kenya na hatimaye, Fasihi ya Afrika itakayotokana na jadi asiliya. Wabungu hawana kazi yoyote ya fasihi wala mapisi yaliyoandikwa na

kusambazwa katika mfumo wa vitabu vya fasihi andishi au elektroniki iliyoandikwa na Wabungu au Watanzania tangu tupate uhuru.

Kazi ambazo mtafiti alibahatika kuziona ni zile zilizoandikwa na wageni. Kazi hizo hazijaelezea fasihi au mapisi ya Wabungu kwa kina bali wametaja tu baadhi ya matukio ya kihistoria. Misafara ya biashara na safari ya kaka wa Mwene Wangu III – Zunda alipokwenda kwa Nyungu ya Mawe kupitia Kiwele. Maelezo hayo yamo katika historia ya *Nyungu ya Mawe and 'The Empire of The Ruga Rugas'*, (Shorter 1968). Hii ni moja ya sababu zilizomsukuma mtafiti kuandika kuhusu jamii ya Wabungu.

## 1.5 Kauli ya Tatizo

Tabia ya mtu binafsi inaweza kusababisha madhara, maumivu au kupotea kwa amani katika jamii. Jamii ya Wabungu inakabiliwa na mtihani mkubwa wa kupotoka kwa maadili, hasa maadili ya watoto, vijana na hata ya watu wazima. Miiko inatumika kama sheria, kanuni, haiba, matakwa ya jamii, heshima na adabu. Kila mwiko wa jamii katika Tanzania una maana kubwa ndani ya jamii kimaadili na kifalsafa.

Tanzania kuna pengo kubwa la kazi za miiko, au uhusiano wa miiko na maadili ya jamii katika mtazamo wa kisanaajadiiya. Kulingana na Faharasa ya mwaka 1978 ya utafiti uliyofanywa na Ndaki ya Dar es Salaam, kati ya jamii zaidi ya mia moja na ishirini, ni tafiti mbili tu zilizokwishafanyika, nazo ni za jamii ya Wangulu wa Mororgoro na Waha wa Kibondo Kigoma (Owino, 1978).

Kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili katika jamii ya Wabungu, ndiyo sababu kuu iliyomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu. Mtafiti anaona kuwa jamii ya

Wabungu imekosa kazi au mapisi yaliyofanyiwa utafiti na kuandikwa. Kwa hali hiyo, mtafiti ana wasiwasi kuwa miiko iliyokemea wizi, uvivu, uchoyo, umalaya, heshima kwa wakubwa na wageni imefuwawa. Hivi ni vitu ambavyo mtafiti anaona sasa vinapotea kwa kasi, na wazee waliokuwa wakijua na kuitumia miiko hiyo wakirudi kwa Muumba kila kunapokucha. Mtafiti anaona kuna haja kubwa ya kufanya utafiti wa miiko kuihuisha na kuihifadhi ili iweze kutumika katika jamii ya sasa na ijayo. Tatizo kuu la kufuwawa kwa miiko kunakosababishwa na utandawaza na kuiga usasa. Muziki wa kisasa, matumizi ya runinga ni sehemu ya sababu za kufuwawa kwa miiko katika jamii ya Wabungu.

## 1.6 Nia Kuu ya Utafiti

Kusudi la Utafiti huu ni kujadili matatizo ya kufuwawa kwa miiko kunakosababisha kupotoka kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

## 1.7 Madhumuni Mahususi ya Utafiti

(i) kuchunguza asili, maana na aina ya miiko, uhusiano uliopo kati ya miiko na maadili ya mtu binafsi katika jamii ya Wabungu.

(ii) Kuchunguza kufuwawa kwa miiko katika jamii ya Wabungu.

(iii) Kukusanya, kuchunguza na kujadili mbinu za kuihuisha na kuitumia miiko ili kulinda maadili yalyiomo katika jamii ya Wabungu.

## 1.8 Maswali ya Utafiti

(i) Kuna ulimbe gani katika miiko ya jamii ya Wabungu?

(ii) Mambo gani yanasababisha kufuwawa kwa miiko katika jamii ya Wabungu?

(iii) Mambo gani yafanyike ili Wabungu waweze kuiishi miiko na maadili ya jamii yao?

## 1.9 Umuhimu wa Utafiti Huu

"Sisi wanataalimu kwa wakati wote tunasimama juu ya mabega ya wazazi wetu". Hii ni kauli ambayo mtafiti alipewa na rafiki yake akimrejelea mwanataalimu mmoja wa sayansi aliyeitwa Newton. Kabla, wazazi walikuwa na mfumo thabiti wa maisha. Mfumo huo uliiweka jamii yote pamoja na katika utengamano. Wazazi wa sasa wanasema maadili yameporomoka sana. Kauli hii ina ukweli. Kwa mujibu wa mjomba wa mtafiti, mwenye umri wa zaidi ya miaka sabini na tano, *"watoto wa siku hizi hawana adabu. Hawana miiko"*. Umuhimu wa utafiti huu unajikita katika kuibua miiko kama kipera cha sanaajadiiya na kuanza kufundishwa katika shule na vyuo mbalimbali.

"*Mtoto hujifunza kisogo cha mama yake*". Usemi huu unashadidia kuwa taswira yoyote inayoonekana kwa mtoto juu ya uumbuji wake lazima uanzie kwa mzazi. Mzazi ni kama ubao ulioandikwa mafunzo na maadili kwa mtoto. Mtoto anajifunza na kupokea mafunzo, miiko ma maadili hayo. Utafiti huu utaisaidia jamii ya Wabungu katika kuitumia miiko kati ya watu wazima na kwa watoto wao pia. Hali hii itasaidia kurejesha maadili mema ya jamii ya Wabungu. Kwa sasa kama wazazi wanalalamika juu ya kukengeuka kwa maadili ya watoto wao, basi jambo hili ni lazima litupe walakini juu ya wazazi wanavyowafundisha watoto wao mambo mema. Kwa hali hiyo mtafiti anaona umuhimu wa kutumia miiko katika kuchunguza tatizo la kukengeuka kwa maadili ya watoto na watu wazima katika jamii ya Wabungu.

Kazi mojawapo kubwa ya fasihi ni kuelimisha. Sanaajadiiya inajitokeza kwa fani na maudhui. Umbo la ndani la fani ni mjumuiko wa falsafa, ujumbe, hisi, mawazo au mafunzo. Miiko huwakilisha sheria za kiutamaduni za kijamii ambazo hurekebisha

tabia za binadamu (Kedibone, 2007; Nkwera, 2009). Kwa hali hiyo sanaajadiiya ndiyo mkombozi katika kuifanya jamii kurejelea maadili mema ambayo sasa kila mja anamlaumu mwenzake kuwa amepoteza maadili ya jamii.

Utafiti huu ni chachu ya kuleta mwamko wa watafiti wa sanaajadiiya hasa katika nyanja ya miiko ya jamii mbalimbali. Watafiti wanapaswa kujitoa kwa moyo, kusoma kwa mzamo nyanja hii na kuandika makala zitakazosaidia kuhifadhi hazina hii adhimu, ambayo kwa sasa ipo hatarini kupotea. Kwa kuwa hazina hii ililinda heshima na utu wa Mbungu, basi, hata sasa iweze jamii kutumia hazina hii katika malezi ya watoto na kurekebisha maadili yanayokengeuka kila uchao.

### 1.10 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maskanini katika vijiji vya Mwambani na Udinde. Mtafiti alilenga kupata miiko kutoka kwa watu wa kawaida katika mazingira yao. Aidha kijiji cha Mwambani kipo karibu kadiri ya kilometa tatu kutoka mji mdogo wa Mkwajuni na kijiji cha Udinde kipo kadiri ya kilometa arobaini na tano. Mtafiti alichagua vijiji hivi kwa sababu ya kuchunguza athari za kufuwawa kwa miiko kutokana na shughuli za mijini katika kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

### 1.11 Vikwazo vya Utafiti

Muda ni tatizo ambalo mtafiti alikabiliana nalo. Kwa kuwa mtafiti ni mtumishi katika taasisi binafsi, na alipaswa kufanya kazi za shirika kwa muda wote kama ilivyo katika mkataba wa kazi. Vikwazo vingine vilikuwa pamoja na uhaba wa fedha za kufanyia utafiti huu, watafitiwa kukataa kutoa habari kwa sababu za imani zao na

utandawazi, utandawizi na kukataa kwa sababu ya kutojua taarifa sahihi za kutoa na tatizo la kutokuelewa umuhimu, maana na ulimbe wa miiko kutokana na kuvizwa na utandawazi na maisha ya usasa (Kothari, 1985).

### 1.11.1 Utatuzi wa Vikwazo

Pamoja na matatizo haya, mtafiti aliweza kutatua matatizo makuu katika utafiti huu kwa njia mbalimbali kutegemeana na muda na tatizo husika. Watafitiwa ambao hawakuwa tayari kutoa taarifa muhimu kwa sababu ya imani zao au kuvizwa na utandawazi, walishawishiwa na kupambanuliwa juu ya umuhimu wa utafiti huu, wengi wao walikubali kutoa ushirikiano. Ushirikiano huo, ndio uliomwezesha mtafiti kupata taarifa zilizohitajika katika kukamilisha utafiti huu.

## 1.12 Hitimisho

Utafiti huu wa kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili – katika jamii ya Wabungu, ni utafiti wa sanaajadiiya. Kazi mbalimbali za kisanaajadiiya, zimejikita katika mzunguko mzima wa maisha ya wanadamu, hapa mtafiti aliangalia jamii ya Wabungu. Mtafiti aliangalia na kuchunguza kwa kina shughuli za kila siku za Wabungu, kazi za Wabungu zilizoandikwa kama zipo. Maana ya miiko pia iliangaliwa ili kumfanya mtafiti kuwa na mwega wa kurejelea mada kwa njia iliyo wazi zaidi.

Mapisi ya miiko yanaonesha kuwa miiko ilikuwapo katika jamii nyingi za watu duniani na Afrika tangu utangu. Miiko ilijenga imani, maadili na kuleta heshima na utengamano katika jamii. Miiko pia ipo katika dini. Tatizo linalojitokeza ni kuwa

watu wabaya watajibagua na kuacha kuifuata miiko hii, kwa visingizio kadhaa kama vile, itikadi za kidini na kupendelea usasa unaojikita kwenye lindi la usasa. Wabungu wachache wanapokengeuka kimaadili basi wanasababisha jamii nzima ya Wabungu kuwa katika hatihati ya migongano isiyo na mwisho. Utafiti huu unatarajia kuwa jicho la wanajamii ya Wabungu, wanataalimu na watawala wa ngazi zote kuirejelea na kuitumia miiko katika kumbo zote za maisha.

# SURA YA PILI

## 2.0 MIKABALA YA NADHARIA

### 2.1 Utangulizi

Ili mtafiti aweze kufanikiwa katika kufanya utafiti, ni lazima awe na nadharia za kumwongoza ili aweze kujua anapaswa kufanya nini na mahali gani na kwa kufuata vigezo gani. Kwa hali hiyo, katika sura hii mtafiti ametumia mwega wa nadharia za sanaajaadiya ambazo zimemsaidia kuchambua data alizozipata wakati wa kufanya utafiti huu. Nadharia ya nadharia, nadharia ya "Ndani Nnje", "Fasihi ina Kwao na Taalimu ina Kwao", "Kila Jamii ina Ujumi wake" na dhanna ya nadharia (mikabala) ndizo zilizomsaidia mtafiti kubainisha kwa kinagaubaga nyenzo muhimu katika utafiti wa kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

### 2.2 Dhanna ya Nadharia

Mzee Prof. Dkt. Sheikh Sengo, alimweleza mtafiti kuwa, dhanna au chimbuko la nadharia yoyote ile ni matatizo. Kwanza kunakuwa na tatizo. Tatizo linapowasumbua wanajamii kwa muda, mwanajamii mmoja au jopo la wanajamii wakakaa na kuanza kusugua vichwa kwa kutafuta ufumbuzi wa tatizo hadi wakapata ufumbuzi wake. Njia ya kutatua tatizo hilo inapotumika mara ya kwanza na kuleta mafanikio na mara ya pili, na mara ya tatu, na kuendelea, basi hii huitwa NADHARIA (Sengo, 2012 mazungumzo).

Utatuzi wa tatizo hili hauwezi kuwa ni wa jumla. Utatuzi huu utategemea mazingira halisi na wakati halisi. Mzee Sengo alifafanua kuwa tatizo linalotatulika masika, si sawa na linalotatulika wakati wa kiangazi. Tatizo la jangwani haliwezi kutatulika sawa na lile la misitu ya Kongo (Berry, 2009).

Katika taalimu ya mitishamba, mizizi ya mitishamba ya Ubunguni haiwezi kutibu ugonjwa ule ule Ukwereni. Mizizi ya Ubunguni itatumika kutibu Ubunguni na mizizi ya Ukwereni itatumika kutibu Ukwereni. Ulimbe wa taalimu hii unakwenda ndani zaidi ya miti hiyo. Chumvi chumvi za udongo wa Ubunguni si sawa na zile za Ukwereni. Ukwereni kuna chumvi chumvi zaidi. Je, taalimu hii unahitaji Mzungu kumfundisha Mbungu? Huu ni ukweli.

Dhanna ya nadharia imejadiliwa na kufafanuliwa kijuu juu na wanazuoni wengi. Kati yao ni kama (Kiango na Wenzake 2006; Ogechi na wenzake 2008; Wamitila 2002; Wamitila 2008). Katika ujumla wao wanakubaliana kuwa nadharia ni jumla ya dhanna, nyenzo, kauli, ushauri, mapendekezo, mawazo, maelezo au mwongozo mkuu uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kuelekeza jambo fulani. Wanazuoni wote wanakubaliana kuwa nadharia ni nyenzo katika kumwongoza mtafiti. Mtafiti katika utafiti huu, pamoja na maelezo yake hapo juu amepiga mbizi kilindini, hivyo, katika utafiti wa kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili, mtafiti ametumia nadharia katika kupambanua na kueleza nia kuu ya utafiti ambayo ndiyo tatizo la msingi lililotafitiwa.

Nadharia si imani wala maelezo ya kawaida. Haya ni maelezo kuntu juu ya vipengele muhimu vya sanaajadiiya vinavyopaswa kuzingatiwa na kila mwanasanaajadiiya wakati wa kuhakiki, kuandika, kuzungumza, kusikiliza au kutafiti kazi za sanaajadiiya. Hili ni zao la tafakuri nzito, utafiti, uchunguzi, utazamaji na upembuzi wa kina na wa muda mrefu (Ogechi, 2008) na kwa mujibu wa mtandao wa wikipedia (imepakuliwa 1/2/2011). Nadharia ni mwavuli wa wanataalim katika kukabili kusikiliza, kusoma au kuandika kara mbalimbali za sanaajadiiya kwa kuzingatia njia

mbalimbali muhimu za kifalsafa na jinsi mtafiti au msemaji atakavyotafsiri maana za dhanna mbalimbali.

### 2.2.1 Mawazo ya Jumla Kuhusu Nadharia

Musau (2002) anasisitiza kuwa nadharia huchochea uhakiki wa kitaalimu kwa kuibua maswali ya kisayansi ambayo huimarisha tabia ya udadisi ya kusaka ukweli. Mtafiti anaona na kukubaliana na Musau kuwa, miiko katika sanaajadiiya inahitaji maelezo kuntu ambayo kwayo yatawasaidia Wabungu na wanajamii wengine Watanzania na Afrika kwa ujumla wake kuweza kutalii kwa mzamo athari chanya za kusaka ukweli wa miiko uliomo katika jamii husika. Athari ambazo zitaifanya jamii ya Wabungu kuweza kuulinda utu wao dhidi ya kukengeuka kwa maadili ya watu wazima, vijana na watoto katika malezi na vita dhidi ya uguberi, ufisidi na ufisadi unaoikabili jamii ya Wabungu. Maadili mema ni utu wa mtu.

Kama ilivyo kwa wanasanaajadiiya watangulizi (Nchimbi, 1979; P'Bitek, 1972; Sengo, 2007), pia mtafiti ana wasiwasi kuwa Waafrika wanaiacha miiko yao kwa kutabii utamaduni wa wageni, huu ni ugonjwa mbaya sana. (Nchimbi, 1979) anasema;

> *"Humpumbaza Mwafrika, hata akaacha kutumia akili yake; akaacha kuuthamini utu wake; Uafrika na hata weusi wake; Badala yake, Anajichukia mwenyewe, Utu wake, Uafrika na hata rangi yake"* (Nchimbi, 1979).

Utu wa Mwafrika, utu wa Mbungu unakabiliwa na ugonjwa wa kutabii mila, tamaduni, maadili, ustaarabu, miiko na falsafa za Wazungu na kuukana UTU wa Mbungu.

Kama ada, miiko katika sanaajadiiya inahitaji maelezo kuntu ambayo kwayo yatawasaidia Wabungu na wanajamii wengine Watanzania na Afrika kwa ujumla wake, kuweza kutalii kwa mzamo athari chanya za miiko. Athari chanya ni athari ambazo zitaifanya jamii ya Wabungu na ya Watanzania kwa jumla kuweza kuulinda utu wao dhidi ya kukengeuka kwa maadili ya watu wazima, vijana na watoto katika malezi na vita dhidi ya uguberi, ufisidi na ufisadi unaoikabili jamii ya Wabungu. Maadili mema ni utu wa mtu.

Nchimbi (1979) katika shairi lake anashadidia matatizo ambayo Waafrika wengi wanakabiliana nayo ambayo anayaita ni ugonjwa mbaya sana. Katika beti hizi anasema:

> "Ugonjwa unawanasa Waafrika wengi,
> Ndani na nje ya Afrika;
> Ni ugonjwa uambukizao sana.
> Unamshambulia Mwafrika, alikotoka,
> Makuu aliyofanya,
> Na vikubwa alivyovivumbua!
> Humpumbaza Mwafrika
> Hata akaacha kutumia akili yake;
> Akaacha kuuthamini utu wake;
> Uafrika na hata weusi wake;
> Badala yake,
> Anajichukia mwenyewe,
> Utu wake,
> Uafrika na hata rangi yake".

Mtafiti anashadidia mawazo ambayo (Nchimbi, 1979) anawakumbusha Wabungu wote. “UTU wa Mwafrika”. Mbungu kama Waafrika wengine, ana ugonjwa mbaya sana na huu si mwingine, bali ni ugonjwa wa kutabii mila, tamaduni, maadili, ustaarabu, miiko na falsafa za Wazungu na kuukana UTU wetu kama Waafrika, Watanzania – Wabungu, (P’Bitek, 1972) naye anashadidia maneno haya na anasikitishwa kuona kuwa Waafrika hawapendi Uafrika wao na wanataka kujibadili kuwa kama Wazungu. Wanaukana Uafrika wao na kusahaku kuwa, Kila Jamii ina Ujumi Wake.

### 2.2.2 Matatizo ya Nadharia

Mtafiti anaona kuwa, kuna nadharia nyingi sana ambazo zinafafanua mambo mengi yanayofanana. Kwa mfano nadharia za Marx zinatumika katika kuelezea masuala ya uchumi, utawala, utamaduni n.k. Wingi wa nadharia ni hatari sana hasa kwa watafiti na watumiaji kama wanataalimu wachanga katika nyanja ya utafiti. Hali hii inapigiwa mbizi na (Ogechi, 2008; Musau, 2002; Berry, 2009). Kwa upande mwingine, kuna shida ya kuwa na nadharia kuu chache zinazofafanua vipengele vingi. Hali hii inaleta ugiligili ambao unaweza kumchanganya mtafiti wakati wa uchambuzi wa data.

Nadharia nyingi zina asili ya nchi za kimagharibi. Kwa hali hiyo zinaendana na mazingira, utamaduni, uchumi na hisia za kimagharibi. Kwa hiyo mtafiti anaona bila shaka yoyote, nadharia za aina hii haziwezi kukidhi mahitaji ya kujadili na kufafanua athari za kufuwawa kwa miiko ya jamii ya Wabungu, kauli hii inakubaliana na kauli ya (Musau, 2002; Sengo, 1978; Sengo, 2009) pamoja na mazungumzo ya mtafiti na Mzee, Prof. Dkt Sheikh. Sengo yanayohusu dhana ya nadharia.

### 2.2.3 Hitimisho

Mtafiti anahitimisha kwa kusema kuwa, nadharia zina nafasi muhimu sana katika kubainisha ukweli na utu wa Mbungu. Nadharia zitapembuwa na kupepeta ili kubaki na kilicho bora kwa matumizi ya jamii ya Wabungu. Kutokana na maelezo juu ya dhana ya Nadharia mtafiti amezama na kuangalia kwa undani nadharia zifuatazo;

## 2.3 Nadharia ya Nadharia

Nadharia ya nadharia si nadharia ya mwisho kwa umuhimu katika utafiti huu. Nadharia hii ni kichwa cha nadharia mtafiti anachokitanguliza. Lengo lake ni kueleza kwa mnato ili kushadidia umuhimu wa nadharia. Hakuna mwiko muhimu zaidi ya mwiko mwingine wowote. Kila mwiko una umuhimu wa pekee katika dhima na kazi zake. Kuvunja mwiko ni kukengeuka kimaadili. Kwa hali hiyo nadharia ya nadharia ni mwongozo mkuu. Mwongozo wa mtu au wa watu au jamii, wa pahala fulani - Ubunguni, wakati fulani, kwa sababu fulani (Sengo, 1978; Sengo, 2009).

Uwezo wa akili ya mtu mmoja haiwezi kuushinda Uwezo wa akili za watu wote katika jamii, (Sengo, 1978; Sengo, 2009). Piga ua, maarifa na uhalisiya haulazimishwi. Hata kama ungekuwa na akili za kupindukiya, dhana nyingine, piga ua, hazipo na ni batili tupu. Maneno yenye maelezo mazuri yanapofafanuliwa na hao wenye akili za kupindukiya, kana kwamba upande wa pili wa shilingi hawauoni.

### 2.3.1 Chimbuko la Nadharia ya Nadharia

Hii ni kati ya nadharia kongwe zaidi katika kazi za sanaajadiiya. Plato aliyeishi mwaka 427 – 347 kk, katika kitabu chake cha *The Forms*, kwa kurejelea elimu iliyokuwamo katika Qurani Takatifu, alianza vuguvugu la ujenzi wa Nadharia ya

Nadharia. Katika Afrika mwanzoni mwa miaka ya sitini Kwame Nkuruma aliyezaliwa tarehe 21 Septemba 1909, alishika bendera juu na kuanza kuweka misingi ya Afrika Moja. Kwame Nkuruma ni mwasisi wa nadharia ya nadharia katika miaka ya 1947.

### 2.3.2 Wazo Kuu la Nadharia ya Nadharia

Wazo kuu la nadharia hii ni Umoja wa Afrika. Kwanza alianza na ujenzi wa mshikamano wa Waghana – watoto kwa wazee, vijana kwa akina mama, wakulima kwa wafanyakazi, wafanyabiashara kwa wanataalimu. Aidha nadharia hii inasisitiza Waafrika wote waipende Afrika na Uafrika wao. Huwezi kuipenda Afrika kama hujipendi mwenyewe. Hivyo watu waanze kupenda familia zao, jamii zao, lugha zao, utamaduni wao uliowakuza babu zao, itikadi zao, miiko yao Wilaya zao, mikoa yao, nchi yao na kwa maana hii wanaweza kulipenda bara lao la Afrika na ujumi wao.

### 2.3.3 Umuhimu wa Nadharia ya Nadharia

Manufaa ya nadharia hii ni katika kuleta Umoja wa Waafrika wote. Waafrika waipende na kuleta umoja bila kujali kama ni mtu wa kaskazini au kusini, mashariki au magharibi. Mwisho wa umoja huo kuwa na nchi moja ya Afrika. Hivi karibuni mshika bendera hiyo Rais wa Libya alitutoka bila kujua aliyemkabidhi kijiti cha kuendeleza wazo la Umoja wa Afrika.

Licha ya nadharia hii kushadidiwa na viongozi zaidi na hivyo fukuto lake kubakia kwa viongozi wa nchi tu, jambo la kufurahisha wazo hilo bado linatambaa katika

nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki labda siku moja ndoto ya Nadharia ya Nadharia itakuwa kweli.

Katika utafiti huu, nadharia hii imemsaidiya mtafiti katika kuchunguza uzalendo wa Wabungu katika kuipenda nchi yao – Ubunguni. Licha ya hayo nadharia hii inawaonesha na kuwasisitiza Wabungu wote kuwa na Umoja wa dhati, na kusahau tafauti zao zozote kama zipo. Umoja wa Wabungu wa kada zote watoto hadi wazee na watu wenye kipato cha chini hadi Wabungu wa kipato cha juu. Kuwaweka pamoja Wabungu wote waliosoma Ngumbaru hadi wale walioziona Ndaki za Tanzania na duniani kote.

## 2.4 Nadharia ya Taalimu ina Kwao na Fasihi ina Kwao

Taalimu ni kweli. Kweli ni dhana. Kweli ni sifa. Kweli ni Mwenyezi Mungu. Kweli ya kitaalimu hupatikana kwa utafiti (Sengo, 1978; Sengo, 2009; Wamitila, 2008) wote wanakubaliyana na taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao, na kupingana na (Frye, 1990) kuwa uigizaji wa uasili katika kazi za sanaajadiiya, hauleti ukweli. Mtafiti anakubaliana na Sengo na Wamitila kwa sababu ukweli hupatikana katika jamii husika na si Ughaibuni.

Mwiko wa Wabungu hauwezi kuwekwa rehani na kutumiwa mwiko wa wageni. Huu ni ukweli. Shughuli za kila siku za Wabungu wa Maleza, Mbangala au Udinde, Mbungu hawezi kuzikana na kuona kuwa kazi za kuuza mitumba ya kafa-ulaya ndizo kazi bora zaidi au kupoteza nguvu na muda kwa kushinda akiangalia picha katika mtandao.

Mapisi ya sanaajadiiya yanaonesha kuwa Waafrika wamedharauliwa sana. Dharau hii imesababisha Waafrika kujidharau wenyewe na kuanza kuwaabudu wageni kutoka ughaibuni. Waafrika bila haya wakajiita ni mataifa yasiyoendeleya. Mataifa ya duniya ya tatu. Mtafiti anajihoji je, ni maendeleo gani katika sanaajaadiya yanayosifiwa na wageni na hata Waafrika kujiona bado hawajaendeleya? Sababu kuu ya mawazo haya ni ile ya mapisi ya kukandamizwa, kutozwa kodi ya kichwa na kufanyishwa kazi ya shokoa na manokoa kutwa na kuwekwa utumwani.

#### 2.4.1 Chimbuko la Nadharia ya Taalimu ina Kwao na Fasihi ina Kwao

Mwanataalimu na mwanasanaajadiiya Profesa, Dr. Sheikh Sengo Tigiti Y.M.S, katika miaka ya 1978 alianzisha nadharia hii ya Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao. Mwanasanaajadiiya huyu alianza kuwafundisha wanasanaajadiiya wachanga katika Ndaki ya Zanzibar alikokuwa amealikwa kama mwalimu wa utafiti wa sanaajadiiya. Nadharia nyingi zilizopo hasa za kutoka kwa waanzilishi wa ughaibuni hasa Uzunguni au nadharia za Kimagharibi, zinakasumba za Kizungu. Nadharia hizi zina pengo la mashiko ya kujivuniya Uwafrika wetu, Ubungu wetu. Nadharia ya Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao inaziba pengo la wanasanaajadiiya kuurejelea ujumi wa Mbungu, Mkwere, Mkinga na wengine wote kuwa sanaajadiiya yao ina thamani na mashiko katika jamii yao husika (Sengo, 1978).

#### 2.4.2 Wazo kuu la Nadharia Taalimu ina Kwao na Fasihi ina Kwao

Kwa kutumia mifano maridhawa, mwanafunzi anaweza kukumbuka na kujenga moyo wa kujiamini kuwa afanyacho ni sahihi au anabananga. Katika jamii zote za Kiafrika hasa Uswahilini na Ubunguni, “mama ni nambari wani” kuna sifa nane za

mwanamke katika jamii za Kiafrika. Kwanza kuna mama, pili ni shangazi - dada wa baba, tatu ni mkwe - mke wa mjomba (kwa Kiswahili safi), nne ni mama mkwe - mama wa mke wa mwanaume, tano ni dada, sita ni nyanya (bibi) - mama wa wazazi wa mtu yeyote, saba ni shemeji - mke wa kaka wa mwanamume, na nane ni mke - mwanamke aliyeolewa na mwanaume. Sifa hizi nane za mwanamke huwezi kuzipata Uzunguni, zinapatikana Afrika – Ubunguni na kwamwe huwezi kuzipata *London.* Anayeweza kuibeza nadharia hii ni mwendawazimu na hayawani tu. Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao na kwao ni Ubunguni. Hata ukienda Ukwereni au Uswahilini hali ya heshima ni hiyo hiyo. Huu ni utu si uhayawani.

Kila sanaajadiiya ya jamii inafuata utamaduni wa jamii hiyo. Mbungu anaposema ni mwiko kwa mtu wa kiume au wa kike kuvaa nguo zinazoonesha utupu, au kuonesha maungo ya mwili kama Muumba alivyomleta duniani, ingawa ujauzitoni kiumbe huvikwa nguo tatu, mwiko huu ni wa Wabungu. Wabungu si Wazungu. Wapare wana miiko yao. Kijana wa Kipare hufundishwa asiwe mwongo, asikosane na jirani yake, asiwe mwizi na miiko mingine mingi ambayo ilikuwapo katika jamii hiyo ya Wapare. K.m. Kutoa siri za jamii nje ya jamii au kwa mtu asiyepaswa kujua habari hizo ni mwiko mkubwa katika jamii ya Wapare au jamii ya Wabungu. Mtu aso kwao ataona ni haki yake kupata habari kutoka kwa yeyote. Habari za Wapare ni habari za Wapare, haziwahusu Wabungu (Mlacha na wenzake, 1995; Sengo, 2008; Simeon, 1977; Bathawab na Sengo, 2007).

Ntarangwi, (2004) anashadidia maelezo ya wanataalimu wenzake kuwa, mtunzi au mtoaji wa mwiko ni mwanajamii. Mwanajamii huyu ana nafasi na tabaka katika

jamii husika na kwa hali hiyo hawezi kukwepa wajibu wake katika kulea na kufundisha maadili ya jamii yake. Kwa msingi huo, Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao ina mihimili yake ambayo ni Jamii. fasihi haiishi katika ombwe, hivyo kwao ni ndani ya jamii. Pia katika jamii kuna taalimu maalumu ambayo hubeba ulimbe wa jamii na kazi. Hapa kuna ujuzi mbalimbali wa jamii husika. Mhimili mwingine ni taalimu ya maneno mateule. Maneno yanayobeba ishara za jamii – miiko. Mwiko wa Kibungu si mwiko wa Kizungu, na hata kama utataka kutumia maneno sawa lakini maana ya mwiko huo haitakuwa sawa. Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao inaweza kuelezewa kwa ubunifu, sanaa na usanii, uumbuji na umahiri, uwezo wa kuimudu lugha katika kutoa miiko katika jamii kwa kutumia maneno kisawasawa. Utamu wa matumizi wa maneno au tungo tata katika kusadifu mwiko unaotolewa kwa jamii.

Sasa kuna wakubwa, au nchi kubwa ambazo zinafikiri kwao kupata habari za mataifa mengine ni haki yao. Katika fasihi hakuna Upolisi wa Duniya. Ili kujua fasihi ya jamii, mtatiti anapaswa kuwa sehemu ya watu hao. Hivyo mtafiti huyo napaswa kujifunza ulimbe na mapisi ya jamii na si kupapasa kisha anatamba kuwa na yeye ni mwanajaadiya ya Wabungu kumbe si lolote si chochote.

### 2.4.3 Umuhimu wa Nadharia ya Taalimu ina Kwao na Fasihi ina Kwao

Nadharia hii ni muhimu sana katika kufanya utafiti wa sanaajadiiya ya jamii. Fasihi ya Kibungu kwao ni wilaya ya Chunya, tarafa ya Kwimba vijiji vya Mwambani, Maleza, Mbangala, Udinde n.k. Matatizo yanayojitokeza katika fasihi hiyo yanayotokana na kuingiliwa kwake na wageni kwa muda mrefu kwa kupitia shughuli zao za kiuchumi k.v. uchimbaji wa dhahabu na uvuvi wa samaki katika ziwa Rukwa.

Shughuli hizi za kiuchumi kwa upande mwingine zimekuwa na manufaa kwa wageni na kuwaacha wenyeji wakibaki fakiri.

Katika jamii ya Wabungu, wakati wa ukame au maradhi, wote walimrudiya Muumba wao. Wabungu walipofikwa na kadhia hiyo, walikimbilia mlima Kwimba kwenda kuwaomba Mababu ili wasaidie kuondoa matatizo hayo. Wabungu walipokwenda Kwimba kuomba kuondolewa matatizo yanayowakabili hawakuzungumza kwa kilatini ati kwa sababu wengi wao ni Wakatoliki. Wote waliohusika na utoaji wa sadaka hiyo walizungumza Kibungu. Sadaka iliyotolewa ilikuwa na inapaswa kuwa ni zao la Ubunguni na si zao la Unyamwanga au Ukimbu au Uswahilini imani ya Mbungu ni wazi kuwa ni kichekesho kwa Mzungu, vivyo hivyo imani ya mzungu ni kichekesho kikubwa Ubunguni. Kwa hiyo nadharia hii imemsaidia mtafiti kukurejelea mawazo, hisia, falsafa, uelewa na ukweli kutoka Ubunguni na si ukweli wa kutoka Uzunguni katika kupembua na kubainisha matatizo ya kimaadili yanayowakabili Wabungu.

## 2.5 Nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake

Jamii za Kiafrika na watu wa bara lake lote wamekuwa kama kichwa cha mwendawazimu. Watu kutoka ughaibuni wanakuja katika bara la Afrika na hata katika jamii ya Wabungu na kuwabeza wazawa. Wazawa wamekubaliana na hali hii. Wabungu wamekuwa watu wa kupokea mila na desturi kutoka Uzunguni na kusahau kuwa na wao wana mila, utamaduni, nyimbo, mashairi, tambo mbali mbali na miiko kwa kulinda maadili ya jamii ya Wabungu. Suala la kulinda sanaajadiiya linashadidiwa na wanataalimu wa sanaajadiiya wengi (Dickinson, 1972; Sithole, 2006; Chisenga, 2002).

Wageni walikuja wakawabeza Waafrika na utamaduni wao na wao Waafrika wakakubali na sasa wanajidharau wenyewe. Wabungu walisalimu amri na kuacha hata mlima wenye dhahabu nyingi Ubunguni kuitwa jina la mlima Elizabeti badala ya kuuita mlima Ilonga, Kapala, Zunda, au Sigonda. Utu wa Mwafrika umepotea kabisa, badala ya kukataa utamaduni mpya, Wabungu wamelewa usasa na kuukana utu wao ambao ndio utamaduni wao wa asili. Utamaduni uliowakuza baba na mama zao, babu na bibi zao. Wabungu wamesahau kuwa Mwafrika ndiye chimbuko la ustaarabu na elimu duniani.

**Chimbuko la Kila Jamii ina Ujumi Wake**

Nadharia hii imetokana na mawazo ya John Frederick Dewey (1850 - 1952) mwanafalsafa na mwanasaikolojia Mmarekani. Dewey aliamini kuwa ujumi ni wazo la maadili na tabia ya mwanadamu inayoongozwa na kupenda (Alexander, 1987). Wafuasi wa nadharia hii ni wengi. Katika Afrika nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake iliyoanzishwa na Leopold Sedar Senghor katika miaka ya 1930. Msenegali huyu shujaa wa sanaajadiiya tangu miaka ya sitini na kuzama zaidi mwanzoni mwa miaka ya sabini. Nyota ya mwanasanaajaadiiya huyu ilizimikia mwaka 2001.

Kuzimika kwa nyota hii, ndiko kunakoendeleya kutuunganisha wanasanaajadiiya wote pamoja na mtafiti, kuyabetua mawazo yake na kuyaweka mahali peupe ili uzuri wa miiko, thamani ya miiko, kazi za miiko, ulimbe uliokuwamo ndani ya miiko na maadili yaliyolimo katika jamii ya Wabungu ambayo sasa yamefuwawa kuanza kuenziwa upya. Kwa kutumia nadharia hii, Wabungu wote wanakumbushwa, wanaamshwa kutoka katika lepe la usingizi na kuanza kuuenzi Ubungu, Uafrika na Utanzania wao na tunu zilizomo ndani ya miiko, (Sengo, 2008; Sengo, 1978). Aidha

nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake, inasaidia kuamsha ari ya watafiti wengine wa sanaajadiiya katika nyanja ya miiko, kuondoa fikra, hisia za kimagharibi na kuurejelea utu wa mtu mweusi utu wa Mbungu.

Katika jamii ya Wabungu, mwingiliano wa wageni ambao walileta dini na elimu ya kufisha lugha na fikra za Wabungu, kulisababisha jamii ya Wabungu kuanza kujikana yenyewe. Kuukana utu wao, Kukana ukweli wao (Thiong'o, 2009; Zimunya, 1982; Zirimu, 1971). Wabungu wakajiona wao si kitu mbele ya watu kutoka Uzunguni au ughaibuni. Wabungu wakatawaliwa na wakoloni na kutozwa kodi kwa nguvu. Kodi zikapewa majina kama, koda ya kichwa, kodi ya miguu, kodi ya mali uliyonayo, kodi ya maendeleo na nyingine nyingi. Mwili wako unaulipia kodi, kwa manufaa ya nani? Mbungu akajengewa woga wa kuinua kichwa mbele ya *Masinjala* (makarani wa kukusanya kodi wakati huo) na kukimbia baada ya kushindwa kulipa kodi. Wabungu wakaacha hata kutumia lugha yao. Lugha ni kasiki la kumbukumbu ya kila jambo katika jamii. Kuacha kutumia lugha ni sawa na kupoteza kumbukumbu zote za sanaajadiiya. Sasa Mbungu amebaki kuwa mtumwa wa usasa.

### 2.5.1 Umuhimu wa Nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake

Nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake inalenga kuurejesha Utu wa Mbungu uliopotea kabisa. Kila Jamii ina Ujumi Wake ni nadharia inayomfanya Mbungu kuurejesha utu wake ulioporwa na wageni hawa kutoka Uzunguni. Kila Jamii ina Ujumi Wake inatusisitiza kuurejesha utu wetu. Nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake inatualika Wabungu, Watanzania, Watu wa Afrika ya Mashariki na Waafrika

wote kwa ujumla wake, kuupenda, kuuenzi, kuulinda na kuuendeleza Utu wetu kama Waafrika. Nadharia hii inatutaka kuandika, kusimulia / kulumba, kutunga nyimbo, mashairi, kutega vitendawili, kutumia Methali na Miiko inayolenga kusifu na kutangaza uzuri wa watu weusi. Uzuri wa Wabungu.

Nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake inatoa wito wa maendeleo ya mtu mweusi. Maendeleo imarishi yatatokana na Wabungu kufanya kazi kwa bidii. Kutunza miiko yao ambayo inalinda uoto wa asili. Kutumia miiko amboyo inamkinga Mbungu dhidi ya maradhi na kifo. (Wafula, 2007; Sengo, 2009) wanabainisha matumizi ya sanaajadiiya kulingana na jamii husika ambayo hapa ni jamii ya Wabungu. Uzuri wa miiko katika malezi na maadili ya watoto na watu wazima katika jamii ya Wabungu.

Kila Jamii ina Ujumi Wake ni nadharia inayoshadidia kuwa Wabungu wana miiko. Wabungu wana maadili. Wabungu wanafanya kazi si wavivu na kwamba uvivu ni zao la wageni kufifisha maadili ya Wabungu ili waweze kupenyeza kafaulaya na kuchukua dhahabu kutoka Chunya. Wazungu wameacha alama za kudumu Ubunguni. Mlima wenye dhahabu nyingi Chunya ukapewa jina la mlima Elizabeti. Mwene wa Wabungu akashindwa kustahimili na kusalimu amri mbele ya madhabahu ya wakatoliki na kupewa jina la Simoni, na kuacha majina ya asili ya Wabungu Ilonga, Wangu, Njalaleiko nk. Huu ni mwanzo wa miiko ya Wabungu kupigwa mweleka. Kila Jamii ina Ujumi Wake unatuamsha, tufunguke macho ya ndani ya mtima na kuanza kutumia vilivyo vyetu. Wabungu watumie miiko yao, nyimbo zao na majina yao huu ndio utu wao.

Mawazo ya wanasayansi na falsafa wanasema kuwa, utambuzi wetu ndio unaojenga duniya. Imani yetu ndiyo inayotafsiri na kujenga vitu vinavyoonekana. Hakuna

ukweli unaokuwapo bila akili inayotafsiri ukweli huo, hivyo ukweli huelezewa na akili inayouona ukweli. Kila Jamii ina Ujumi Wake ni zao la Mwafrika Mtanzania, Mbungu anayeuona ukweli huo katika mazingira ya Ubunguni.

Mtafiti anaona kuwa nadharia nyingi alizozisoma katika utafiti huu, zinaonesha namna ya kuchanganua na kupambanua sanaajadiiya kwa mtazamo wa kimapokeo kutoka Uzunguni au Ughaibuni. Thamani ya miiko katika jamii ya Wabungu, inapaswa kumrejesha Mbungu katika kuuona, kuutambua, kuuthamini na kuugeukia Ubungu wake na kuishi kama Mbungu na si Mzungu. Mbungu anapaswa kutambua kuwa utu wake ulioporwa unarejeshwa. Hapa ni Mbungu tu ambaye anaweza kuurejesha utu wa Mbungu. Mbungu asitegemee hata siku moja kwa Mzungu kumsaidia ajitambue, aijue miiko yake, kwani anajua wazi kuwa huo utakuwa mwisho wa ukoloni wake mamboleo.

Kwa hali hiyo mtafiti anaona kuwa nadharia ya Kila Jamii in Ujumi Wake ni nadharia iliyoasisiwa na watu weusi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya sanaajaadiya ya mtu mweusi. Nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake haijaasisiwa Uzunguni. Nadharia hii inaziba pengo la nadharia kutoka Uzunguni ambazo kwa miaka mingi zimekuwa zikitumiwa na waandishi, wasomi, na watafiti wa sanaajaadiya katika mazingira ya Kiafrika na kwa uhalisia hazikuweza kukidhi, kuendana na mahitaji kwa kuzingatia thamani ya ulimbe na mapisi ya Mwafrika.

Aidha nadharia hii ya Kila Jamii ina Ujumi Wake ina nguzo zake nyingi. Katika utafiti huu, matafiti alishughulika na nguzo moja tu ambayo ni miiko inayomfanya Mbungu awe na maadili mema. Maadili yanayoshadidia uzuri wa mila, desturi, kazi,

uongozi, na makuzi ya vijana wa Kibungu wake kwa waume. Ujumi utakaobainisha kukengeuka kwa maadili ya jamii ya Wabungu na kutabii maadili ya Uzunguni (Sengo, 1981; P'Bitek, 1972). Miiko itakayoonesha staha na thamani ya Mbungu mahalia popote atakapokuwepo.

### 2.5.2 Hitimishi

Ili mtafiti aweze kufanikiwa katika kufanya utafiti, ni lazima awe na nadharia ambazo zitakuwa kama kurunzi yake katika kumwongoza ni kipi akifanye wapi na kwa kufuata misingi gani. Kwa hali hiyo mtafiti katika utafiti huu alitumia nadharia mbili kuu katika kazi hii. Nadharia ya kwanza ni ile ya Kila Jamii ina Ujumi Wake na ya pili ni ile ya Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao.

## 2.6 Nadharia ya Ndani-Nje

Nadharia ya Ndani Nje inaonekana kuwa ni moja ya nadharia kongwe za sanaajadiiya. Pamoja na kuwa na mapisi ya muda mrefu, kumekuwa na mfululizo wa mabadiliko ya matumizi ya nadharia hii. Jambo la msingi katika nadharia hii ni kuimanya jamii hisika Ndani Nje, mapisi, ada, kazi, maadili na ulimbe wa kazi katika jamii husika kama mzee Prof. Dkt. Sheikh Sengo alivyoanza kutoa mwelekeo mpya wa nadharia hii tangu katikati ya miaka ya 1970.

### 2.6.1 Chimbuko la Nadharia ya Ndani Nje

Yuri Long, (2010) katika makumbusho ya Taifa ya Marekani anabainisha chimbuko la nadharia ya Ndani Nje kuwa ni katika karne ya 13. Wanataalimu wa sayansi inayohusu mwili wa binadamu wakishirikiana na wanataalimu wa sanaa za maonesho, walitumia taalimu hiyo kutengeneza jukwaa la maonesho. Katika karne

ya 17 Ndaki nyingi Ulaya zilikuwa zimeshaanza ushirikiano wa kimasomo kati ya wanafunzi wa sayansi na wale wa sanaa. Mwaka 1315 huko Bologna nchini Italia, ndiko kulikorekodiwa ukumbi wa kwanza wa aina hii. Mchakato huu unatufikisha katika karne ya 18 ambapo mwanatazaalimu *Sir Charles Bell* alipoandika kitabu kilichoitwa "*Essays on the Anatomy of Expression in Painting*" mwaka 1806. Katika kitabu hiki mwandishi alionesha imani yake kuhusu umuhimu wa sayansi  inayohusu mwili na viungo vyake jinsi vilivyo, vinavyohusiyana na namna mwanadamu anavyoelezeya hisia zake.

Miaka mingi imepita na mawazo mengi yamepita pia. Wanataalimu wengi wametumiya nadharia hii katika mambo mengi kama, sheria, biashara na hata katika kuulinda na kuuelezeya uhayawani wa binadamu walioumbwa na Mwenyezi Mungu wanapojiona wao ni bora na wanajuwa kuliko Muumba wao, wakaona ushoga ndiyo jibu kwa maisha yao.

Katika karne ya 20, mwanasanaajadiiya na mtafiti mkongwe katika fani ya sanaajadiiya Afrika, Mzee Prof  Dkt Sheikh Sengo T.Y S M, akaja na nadharia iliyo bora katika mazingira ya Kiafrika na inayokidhi mahitaji ya jamii za Kiafrika kwa sasa. Nadharia ya Ndani Nje mwanataalimu Mzee, Prof, Dkt Sengo anasema kuwa mwalimu na mhakiki wa fasihi ya jamii fulani ili aweze kuitafiti, kuifundisha au kuihakiki ni shuruti aimanye vizuri. Kuijuwa fasihi ya watu, ni muhimu kwanza kuwajuwa watu wenyewe, utamaduni wao, mila zao, ada na desturi zao, bahari yao ambayo ndiyo chemchemi ya ishara na dhana zao. Mawazo hayo yanaungwa mkono na **(**Bathawab na Sengo, 2007; Sengo, 2009; Sengo, 1978).

### 2.6.2 Wazo kuu la Nadharia ya Ndani Nje

Mtafiti anakubaliana na maneno ya (Sengo, 2009) ambayo yanashadidiwa na wanataalimu wengine kama (Wamitila, 2008; Mtesigwa, 1989; Mulokozi, 1989; Balisidya, 1982). Kila jamii ya watu ni tafauti. Kwa hali hiyo, ili kuihakiki au kuuelewa ukweli uliyomo katika semi za miiko ya jamii ni lazima msemaji na msikilizaji wawe na hisia za aina moja.

Kujua jamii fulani si kutabii vitu wanavyovifanya. Mtu inampasa abadilike kwa kujua kuwa jamii ni ya watu wa namna gani na wana imani ipi kwa Muumba wao. Kuna msemo usemao, *"Ukienda Roma fanya kama Warumi"*, na Wabungu wana msemo unaosema "*Ukifika katika nchi ya watu wenye jicho moja na wewe toboa jicho lako moja*". Misemo yote hii inabainisha kuwa ni muhimu kwa mtu awaye yeyote kuheshimu mila na utamaduni wa wenyeji anapofika katika mazingira yao. Kwani kila jamii ina Ujumi wake.

Katika kila jamii mna miiko ambayo, si kila mja anaweza kutenda atakacho. Kabla ya kuuangalia mwiko huo, inampasa mtafiti kwenda ndani zaidi katika kuijuwa jamii hiyo kama daktari bingwa wa upasuaji aujuwavyo mwili wa binadamu kabla ya kufanya upasuwaji. Na Roma, muungwana hatakubali aige ya Waziri Mkuu fulani aliyewataka Waafrika wajiunge na kuteketezwa kwa Sodoma na Gomora ati, kwa sababu ya misaada. Afrika itowe mali na vyakula, mlaji ageuke aseme yeye anatoa msaada. Huu ni mwiko mkubwa kwa Mwafrika.

### 2.6.3 Umuhimu wa Nadharia ya Ndani Nje

Ngoma ya *Makala* inapopigwa basi kuna jambo. Labda *isiche lyakumbuka*, Kisiki kimeng'oka. Mtu mkubwa anapofariki katika jamii ya Wabungu, basi ngoma hiyo

maalumu hupigwa. Ngoma hii huchezwa na *Ilombwe*. Ilombwe ni watu maalumu waliofundwa na kuwa na sifa maalumu za kuweza kuingia na kuicheza ngoma hiyo. Ni mwiko kwa mtu asiyehusika kuingia ndani na kucheza ngoma hiyo. Ni mwiko kwa Mwafrika mwanaume kuwa msenge (shoga) au basha na mwanamama kusagana na mwingine. Kama kwa kufanya hayo ndizo haki za binadamu, ambazo hata haziwafai mahayawani, sembuse Waafrika, wazazi wa watu wote (Bathawab na Sengo, 2007).

Nadharia ya Ndani Nje inamlazimisha mtafiti na mwanasanaajadiiya, kabla ya kufanya au kutoa hitimisho la aina yoyote linalohusu jamii, jambo la msingi kwake ni kuijua jamii hiyo Ndani Nje. Mtafiti wa aina hii atakuwa na papasi za kupapasa, pua za kunusa ngozi ya kuhisi masikio ya kusikia, macho ya kuona na ubongo wa kuelewa miiko inayotumika katika jamii ya Wabungu na kuihusisha na Wabungu na si kuihusisha na Wazungu. Katika utafiti huu Nadharia ya Ndani Nje ni muhimu sana katika kufikia hitimishi sahihi la tatizo la utafiti linalosema kuhusu matatizo ya kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

Tatizo la nadharia ya ndani nnje ni kwamba, kama mtafiti ni kutoka ughaibuni, ni rahisi kwake kupotosha ukweli wa maana ya miiko ya jamii anayoitafiti. Hii ni kwa sababu mtafiti hatakuwa na hisia za kuoanisha lugha ya picha inayotumika katika jamii, ulimbe na miiko yenyewe. Mtafiti wa ughaibuni hawezi kuona kufuwawa wala kupotoka kwa maadili kwani atakuwa na hisia za kwao ughaibuni na si Ubunguni. Mtu yeyote anayefanya utafiti wa Wabungu anapaswa kujua na kuheshimu mila na utamaduni wa Wabungu. Atakuwa ni mtovu wa nidhamu na mtu asiyefundwa kwao kama atajitia anajua zaidi ya Wabungu kuhusu mila na utamaduni wa wenye nao.

## 2.7 Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika

“Msibani hapaombwi jamvi”. Kwa mgeni wa kutoka ughaibuni, akiomba jamvi, hashangazi. Ni kichekesho kwa nchi kama Tanzania kufikiria kununua mvua kutoka Mashariki ya mbali badala ya kufikiria kupanda miti na kurejesha ukijani kibichi wa asili nchini mwake.

Uhalisia ni hali ya kuangalia ukweli. Ukweli ni kuwapo kwa Mungu. Fisidi au fisadi anapofikiria mradi na kuwashawishi wenzake waukubali, nyuma yake kuna siri. Kama Mtera limejaa tope na mwingine kasema bwawa halijajaa tope, huu ni ukweli wa kifisidi, ni uongo mtupu wa kuihujumu nchi.

### 2.7.1 Chimbuko la Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika

Vuguvugu la nadharia hii lilianza huko Uingereza kati ya miaka ya 1950, ingawa katika miaka ya 1930 huko Ufaransa kulikuwa kumeanza mawazo ya nadharia hii ikielezeya Ujumi katika Ushairi. Mwaka 1960 Pierre Rwstany na Yves Klein walianza kuelezea uhalisia katika mafungu mafungu kama mafungu ya nyanya sokoni (Carrick, 2010). Walielezeya uhalisia wa jikoni, ukalisiya wa ushairi, uhalisia wa sanaa za maonesho, uhalisia wa Kimarekani nk. Uhalisia huu wa Ulaya una misingi yake thabiti Ulaya na haujakidhi Uhalisia wa Jamii za Kiafrika.

Katika miaka ya mwishoni miaka ya 1970, Mzee Prof. Dkt. Sheikh Sengo T.Y.S.M, alikuja na Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika. Nadharia hii ina misingi yake katika jamii za Kiafrika na imejengwa katika mazingira halisi kuna mambo maalumu yanayofanyika. Kwa mfano, katika jamii ya Wakwere kipindi cha mavuno wanajamii

wanatumiya chakula kuonesha ufahari wa kuwa nacho. Mgeni anapofika nyumbani anapikiwa chakula kwa wingi zaidi ya uwezo wa mlaji. Mwanajamii huyo huyo, wakati wa masika chakula kinakwisa hadi kusababisha familiya hiyo kula mlo mmoja tu. Huu ni uhalisia wa Kiafrika Uhalisia wa Kikwere, Uhalisia wa Kibungu. Uhalisia unaolenga hali halisi ya maisha ya jamii maalumu kwa msimu au wakati maalumu. Huu si uhalisia wa Kizungu.

### 2.7.2 Wazo Kuu la Uhalisia wa Kiafrika

Uhalisia ni kweli ambayo ni sawa kabisa na msemo usemao, *"afichaye maradhi, kilio humuumbua"*. Sengo, (2009) anataja uhalisiya wa kiuchumi, uhalisia wa hali, uhalisia wa wingi wa kina mama dhidi ya wingi wa kina baba, uhalisia binafsi wa utu, wa hulka na tabiya, wa kuzaliwa, kutupwa na kuokotwa, wa kuzaliwa na kulelewa hadi kufikiya utu uzima wa kutegemewa ....."

Kwa Mbungu, uhalisia wake ni mwiko. Kutenda kisichompendeza mwenzake. Kuna Wabungu ambao hawakufundika ingawa na wao wanapaswa kuwafunda watoto wao. Watu hao Makanisani hawako, Misikitini hawako, Mizimuni nako hawako. Labda wako vilabuni wakishambulia *visado* vya *kangara* na *dizeli*. Wengi wa hao ndio tuliopewa madaraka ya kuongoza nchini. Mtu wa ibada ya dhati hawezi kuwa fisidi. Wala hatahitaji kukaa viti vya mbele Makanisani au kusimama mistari ya mbele Misikitini. Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika ni muhimu sana katika utafiti huu kwani ni kurunzi la kumulikia mwanajamii mmoja mmoja katika jamii ya Wabungu na kubainisha tabiya na mienendo yao ambayo inapambanuwa kufuwawa au kutofuwawa kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

## 2.8 Nadharia ya Ufeministi

Katika jamii yoyote ya watu waliostaarabika, ni muhimu sana kwao kuwa na utaratibu unaofaa katika kuyashughulikia masuala yote yanayohusiana na jinsia na mgawanyo wa kazi. Jamii ambayo inakiuka kutumia fursa hii ya kufuata jinsia, basi wanajamii watakuwa na matatizo yasiyokwisha. Mgawanyo wa kazi si suala la ninataka au sitaki hili ni suala lenye ulimbe na ni suala la Mwenyezi Mungu. Hivyo hili ni suala la ukweli. Kitu cha msingi katika nadharia hii ya Ufeministi ni kuchunguza ukweli wa kitu kinachodaiwa na wanajamii kuwa hakipatikani kwa kundi moja la watu kisha kuwapatia haki hizo wale wanaozikosa.

### 2.8.1 Chimbuko la Nadharia ya Ufeministi

Feminism ni itikadi ya kuamini kuwepo kwa haki kati ya mwanamume na mwanamke. Aidha Feminist ni muumini wa itikadi ya kuwepo kwa haki sawa kati ya wanaume na wanawake, nadharia hizi zilizuka katika miaka ya 1792 na 1920. Katika machapisho ya *"The Changing Woman", "Aint I a Woman", "Speech after Arrest for Illegal ss Voting* n.k. Makala zote waandishi wanamwangalia mwanamke kama mtu aliyekosa haki na sasa wanataka kumwingiza katika dunia mpya ya haki (Levi_Strauss, 1966; Wikipedia, 2011).

### 2.8.2 Mawazo Makuu ya Nadharia ya Feministi

Katika harakati za wanawake kupigania haki walizoona kuwa wanazikosa walikuja na orodha ndefu ya misimamo au falsafa nyingi zinazohusiana na madhumuni yao. Mkataba wa kwanza wa haki za wanawake ulifanywa huko *Seneca Falls, New York*. Baada ya siku mbili kikundi cha wanawake 68 na wanaume 32 walitia saini azimio lililoelezea manung'uniko yao na kuanzisha harakati za haki za wanawake wakidai

kupewa haki sawa kati ya wanaume na wanawake kisheria na haki sawa za wanawake kupiga kura (www.about.com/od/sociological-theory/a/Feminist).

Katika nadharia hii tunaona kuwa mwanamke ni mtu asiye na haki ya vitu vingi. Hali halisi huu ni mtazamo wa watu tu. Sasa wakati umefika wa wanataalimu kuuangalia tena msimamo wa nadharia hii ya ufeministi. Mtafiti ataangalia fikra hizi kama ni fikra za kawaida kabisa. Fikira ambazo zitauangalia ufeministi kama ni nuru ya maadili na imani muhimu za jadi za Waafrika. Katika historia ya ufeministi tunaona baadhi ya sababu ya nadharia hii ilikuwa ni haki ya kupiga kura miaka ya 1800. Hebu tuangalie miaka hiyo na baadaye hadi miaka ya 1960, kama kura ilikuwa ni tatizo katika jamii ya Wabugu. Masuala ya kura au kula si jadi ya Wabungu. Jadi ya Wabungu ni kuhakikisha mwanamke wa Kibungu anaishi salama. Tatizo jingine kubwa linalojitokeza katika nadharia hii ni kuwa waitifaki wengi ni wanaume. Tunapaswa kujihoji, kulikoni?

Mitizamo mingi ya nadharia hii inaonesha uhusiano kati ya wanaume na wanawake. Hili ni jambo zuri sana, katika kuangalia uhalisia wa mawazo ya jumla ya utamaduni na miiko ya Wabungu ninaona kuwa kunautata mwingi sana katika kuikubali nadharia hii moja kwa moja. Katika kitabu cha Hiba ya Wivu kilichoandikwa na mwanamke, aitwaye Zainab, tunaona kuwa Zainab anaonesha wajibu wa mwanamke katika jamii. Zainab anaonesha wazi mambo muhimu yampasayo mwanamke kuyafanya ukiachilia mbali suala zima la wivu lililojitokeza katika riwaya hii. Ibrahim Hussein katika tamthiliya ya Wakati Ukuta, tunamwona anavyo shadidia suala zima la nidhamu ya mtoto wa kike. Mavazi, kwenda kutembea usiku na

mwamaume ambaye si kaka yake. Huu ni uigaji wa mila za watu bila ya kujua mazingira yao na miiko yao (Hussein, 1967; Mwanga, 1984).

Katika jamii ya Wabungu ufeministi ni sawa na kuwakengeusha Wabungu katika maadili na miiko yao. Kwanza, Wabungu wana miiko mingi, miiko yao inamtazama mwanamke katika hali ya kumlinda au kumkataza kufanya vitu vingi. Wanawake wa Kibungu, kwa mfano, walikatazwa kula mayai, kwenda kuchuma mboga za majani wakati wakiwa katika siku zao. Hizi si shughuli za Wazungu. Hapa ni Wabungu, Waswahili, Wanyamwanga au Waafrika kusini mwa jangwa la Sahara ambao wanaweza kuwa na shughuli kama hizi.

### 2.8.3 Umuhimu wa Nadharia ya Ufeministi

Nadharia hii sasa itasaidia kubadilisha uhusiano uliokuwapo kati ya wanawake na wanaume. Uhusiano huu mpya utaleta mivutano inayotokea sasa na kuzingira miundo ya maisha ya familiya, elimu, kazi na siasa. Tusisahau kuwa utamaduni wote utawekwa rehani. Kuangalia maadili kwa mtazamo wa nadharia hii ya ufeministi. Nadharia ya ufeministi inaangalia fikra za kawaida, fikra huru katika maadili na imani muhimu za jamii husika kwa wakati uliopo (Levi_Strauss, 1966; Barry, 2009).

Nadharia hii inakiuka mifumo ya wanaume ambayo imetumika sana katika fikra za watu wengi katika jamii mbalimbali. Nadharia hii hudhamiria kuonesha jinsia na uhusiano kati ya mwanamke na mwanaume. Nadharia hii huangalia kwa kina uhalifu wa uana uliopo katika jamii. Kwa kutumia mifano maridhawa, mwanafunzi anaweza kukumbuka na kujenga moyo wa kujiamini kuwa afanyacho ni sahihi au anabananga.

Katika jamii zote za Kiafrika hasa Uswahilini na Ubunguni, “mama ni nambari wani”.

Katika jamii za Kiafrika kuna sifa nane za mwanamke. Kwanza kuna mama, pili ni shangazi - dada wa baba, tatu ni mkwe - mke wa mjomba (kwa Kiswahili safi), nne ni mama mkwe - mama wa mke wa mwanaume, tano ni dada, sita ni nyanya (bibi) - mama wa wazazi wa mtu yeyote, saba ni shemeji - mke wa kaka wa mwanamume, na nane ni mke - mwanamke aliyeolewa na mwanaume. Kwa mawazo ya mtu wa kawaida mwanamke ni mtu wa kuheshimiwa. Kati ya wanawake hawa ni mwanaume gani anayemdharau au kumkandamiza? Fasihi ina kwao na kwao ni Ubunguni.

Hata ukienda Ukwereni au Uswahilini hali ya heshima ni hiyo hiyo. Huu ni utu si uhayawani. Mtafiti anaona kuwa nadharia ya Ufeministi kama anavyosema Mzee, Prof. Sengo, T. S. Y. M, ina kwao. Kwa kuwa nadharia hii ya Ufeministi ilifanya kazi huko kwao, basi tuwaachie hao hao. Katika jamii hii iliyofanyiwa utafiti nadharia hii haiwezi kukubalika. Nadharia hii haiwezi kulinda, wala kuhuisha miiko ya jamii ya Wabungu ambayo sasa inaonekana kuwa imefuwawa. Huku Ubunguni nadharia hii haiwafai Wabungu. Hali hii inajitokeza katika miiko ya jamii ya Wabungu na kuthibitisha kuwa taalimu ina kwao na fasihi ina kwao. Ubunguni nadharia hii si kwao kwao ni Uzunguni, basi waachiwe wenye nayo huko huko Uzunguni (Sengo, 2011 mazungumzo).

## 2.9 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti ameeleza kwa kinagaubaga nadharia za sanaajadiiya ambazo ni muhimu katika utafiti huu. Kuna nadharia nyingi sana za sanaajadiiya, lakini

mtafiti katika utafiti huu amechagua nadharia sita na kuzifafanua. Kwanza dhana ya nadharia ilijadiliwa kabla ya nadharia zenyewe. Nadharia hizo ni kama Nadharia ya nadharia, Nadharia ya Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao, nadharia ya kila jamii ina Ujumi wake, nadharia ya Ndani Nje, Nadharia ya Uhalisia wa Kiafrika na Nadharia ya Ufeministi.

Nadharia hizi zina ugiligili mwingi hasa kwa wanataalimu na watafiti wachanga. Hali hii inasababishwa na chimbuko na falsafa ya nadharia nyingi kati ya hizi kutoka Ughaibuni. Nyingi hazina asili Bara la Afrika (Barry, 2009), hivyo zinakosa misingi na mashiko mujarabu kutoka kwa Waafrika wenyewe. Aghalabu sasa kuna wanasanaajadiiya ambao wameanza kujitowa kimasomaso katika kuunda na kufundisha misingi ya nadharia na kuja na nadharia zenye kuzama katika mapisi, ulimbe na falsafa za Kiafrika.

# SURA YA TATU

# 3.0 KAZI TANGULIZI

## 3.1 Utangulizi

Madhumuni ya kazi tangulizi ni kukusanya data za upili. Hapa mtafiti alitalii mabuku mbali mbali na kuzungumza na wanajamii ili kumwezesha kujua ni kwa upana na kina gani eneo hili limeshashughulikiwa. Hapa alipata kujua apige mbizi kwa kiasi gani zaidi. Aidha kazi tangulizi ilimsaidia mtafiti kupata mwega wa kurejelea wakati wa kuchambua data za awali.

Miiko ni utanzu kama tanzu nyingine za fasihi. Kutokana na taarifa za mwanasanaajadiiya (Prof. Sengo T. S. Y. M. 12/01/2012 saa 11 jioni), mwiko ni utanzu moja kwa moja wa sanaajadiiya na kazi tangulizi zake ni wanajamii wenyewe katika maisha na shughuli zao za kila siku. Ikumbukwe kwamba maktaba ya Sanaajadiiya (*folklore*) ni watu/ jamii, katika utafiti huu mtafiti ametafiti kuhusu jamii ya Wabungu.

Faida za data za upili ni urahisi wa upatikanaji wake. Kazi hizi zipo maktabani na katika mtandao na gharama yake ni ndogo. Hapa mtafiti hupanua uelewa wake kijiografia, kwani hutalii makala za ulimwengu mzima akiwa amekaa maktabani.

Matatizo ya kazi tangulizi ni pale ambapo, kazi tangulizi si sahihi, zimepitwa na wakati, au hazipo (Sengo, 1978; Hart, 1998; Kothari, 1985). Tatizo hilo linajitokeza hata katika kazi tangulizi katika jamii ambayo ni maktaba kuu ya sanaajadiiya. Katika jamii unaweza kupata taarifa mbili au zaidi zinazoelezeya jambo moja au mapisi ya kitu kimoja.

Katika sura hii mtafiti amepiga mbizi na kuangalia kazi tangulizi za sanaajadiiya zinazohusiyana na miiko. Ameshughulikia maana, mapisi ya miiko na kukengeuka kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

### 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu wa Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili umefanywa katika mkoa wa Mbeya wilaya ya Chunya. Wilaya hii ipo Kaskazini Magharibi ya mji wa Mbeya, kati ya latitudo nyuzi ya 7 na 9 Kusini mwa Ikweta na kati ya longitude nyuzi ya 32 na 34 Mashariki ya Greenwich (Planning Commission Tanzania, 1997). Wilaya ya Chunya inapakana na mikoa ya Singida na Tabora upande wa Kaskazini mkoa wa Iringa na wilaya ya Mbarali upande wa Mashariki; wilaya za Mbozi na Mbeya upande wa Kusini na Mkoa wa Rukwa katika ziwa Rukwa kwa upande wa Magharibi.

Wabungu wanapatikana upande wa Magharibi ya wilaya ya Chunya katika tarafa ya Kwimba, vijiji vya Mwambani, Maleza, Mbangala, Udinde, Kapalala, na Mkwajuni. Pamoja na jamii ya Wabungu wilaya ya Chunya inakaliwa na jamii za Wakimbu upande wa Kaskazini – Magharibi ya wilaya ya Chunya, Waguruka upande wa Mashariki, Wanyamwanga upande wa Kusini. Wilaya ya Chunya pia inakaliwa na wahamiaji wa jamii nyingine kutoka sehemu mbalimbali nchini Tanzania kama; Wanyakyusa, Wahehe, Wasukuma, Wanyamwezi, Wafipa, Wakinga, Wamasai kwa kuwataja baadhi tu (Rugemarila, 2009).

#### 3.2.1 Asili ya Wabungu

Kwa mujibu wa mzee Aloisi Ndamba, Wabungu chimbuko lao ni kutoka Kusini mwa Afrika. Wabungu zama hizo waliingia nchini Tanzania ya sasa kupitia upande

wa kusini katika mpaka wa Tanzania na Zambia. Walipoingia walielekeya upande wa Mashariki mpaka sehemu za Tukuyu, halafu sehemu za Songea. Safari yao haikuishia hapo, waliendelea kuelekeya upande wa kaskazini hadi Mkoa wa Morogoro ya sasa sehemu za Kilosa. Inasemekana katika sehemu hii walikaa kwa muda mrefu zaidi na kuacha alama za majina kama Ilonga, ambalo ni jina la Mwene wa Wabungu.

Safari haikuishia hapo, walianza safari kuelekeya Magharibi na kuvuka Bonde la Ufa la Mashariki na kuingia Ukimbu, wakielekea upande wa ziwa Rukwa hadi walipofika Mlima Kwimba. Hapa waliwakuta wenyeji wao Wanyamwanga. Kwa kuwa wenyeji hawa hawakuwa na uongozi thabiti waliwafukuza kwa urahisi. Waliingia Bonde la Ufa la Magharibi katika ufukwe wa ziwa Rukwa. Waliposhuka kutoka katika mlima Kwimba walikwenda Kapalala na kushuka ndani ya bonde la ufa katika kijiji cha Udinde.

"*Toudinde*" kwa Kibungu maana yake tuzuwie kijiji hiki sasa kinaita Udinde na "*koupalala*" kwa Kibungu neno hili likiwa na maana ya kunowa. Sehemu ya kunoleya mikuki na silaha zao nyingine za asili, sasa kijiji hiki kinaitwa Kapalala. Baada ya hapo, Wanyamwanga walielekeya Kusini mwa ziwa Rukwa na kuwaachiya Wabungu kusambaa katika vijiji vya Mbangala, Maleza hadi Mwambani vyote vikiwa kando kando ya ziwa Rukwa.

### 3.2.2 Shughuli za Kiuchumi

Kwa asili Wabungu ni wawindaji na wavuvi. Wabungu walifanya shughuli za uwindaji wa wanyama wa mwituni kama viboko, nyati swala, ngiri na paa. Pia

Wabungu walifanya shughuli za uvuvi kwa ajili ya chakula na biashara. Shughuli hizi zilifanywa katika ziwa Rukwa na mito inayomwaga maji katika ziwa Rukwa upande wa Mashariki.

Kilimo cha mazao ya chakula kama ulezi, uwele, mtama, mahindi, karanga na mihogo. Mazao ya biashara kama pamba sasa zao hili limepigwa marufuku kulimwa kwa sababu ya ugonjwa wa pamba na ufuta. Kwa sasa wanajamii hawa wanalima alizeti na zamani walilima nyonyo.

Madini ni shughuli mojawapo ya kiuchumi iliyoanza zamani yapata miaka ya 1930 na makampuni ya Kiingereza hadi sasa inaendelea na shughuli hii inafanywa na Wabungu na Watanzania wengine pamoja na makampuni makubwa ya kigeni.

Uvunaji wa rasilimali za misitu hufanywa zaidi na wageni kama Wakinga kutoka Njombe (Planning Comission Tanzania, 1997).

### 3.2.3 Elimu

Zamani watoto wa kiume wa Kibungu walipewa kipaumbele zaidi katika kupewa elimu kuliko watoto wa kike, ingawa hakukuwa na msisitizo mkubwa wa watoto wa kike kwenda shule. Sasa watoto wote wana haki sawa ya kupata elimu kwa kadiri ya uwezo wa mtoto na mzazi (Planning Comission Tanzania, 1997).

## 3.3 Maana ya Miiko

Katika mtandao wa (www.encyclo.co.uk/define/taboos 2009) mwandishi ameandika maana kumi na tano za miiko. Kwa ujumla wake maana ya miiko iliyochukuliwa

kutoka jamii ya Wapolynesian, inasema kuwa miiko ni mfumo wa makatazo au mtu hapaswi kufanya, kugusa au kusogelewa. Makatazo haya yalitokana na vitu vyenyewe kuwa vitakatifu kwa asili kutokana na utamaduni wa jamii kutokuwa radhi kufanya jambo hilo au kulikataza. Kwa ujumla miiko inamaanisha kuwa ni makatazo ya vitendo, matumizi ya vitu au adhabu inayosababisha maumivu.

Hii ilikuwa inahusishwa na utakatifu au kufanya vitu viwe vitakatifu au kukataza kuwa ni hatari au vichafu. Miiko ilikuwa ni aina ya nguvu kutoka juu nguvu hii iliitwa "mana" na ni watu maalumu tu walioweza kuruhusiwa kusogelea vitu au mahali hapa. Ili kuleta maana katika maisha ya kawaida miiko iliwekwa katika uzazi, vifo, jando na unyago na kuoa au kuolewa. Miiko inajitokeza katika koo na mababu kama walinzi wa familia au koo hizo. Kwa kuvunja miiko hii mvunjaji alikabiliwa na adhabu hata ya kufa kwa sababu ya hofu ya nguvu hizi.

Katika jamii kama za Wapolynesia, Melanesia na Nyuzilandi miiko ilijumuisha sheria kwani makatazo haya yalihusishwa na utakatifu wa uongozi kama Miungu, Uchifu, Ukasisi na kuleta matumizi maalumu hasa makatazo ya wanawake kufanya baadhi ya vitu. Miiko hii ilikuwa ni miiko ya muda au ya kudumu. (Onions, 1960) anasema lengo kuu la miiko lilikuwa ni kuleta umoja na heshima katika jamii ya watu wa kabila au jumuiya moja. Kufuata miiko haikuwa jambo la ninataka au sitaki, hili lilikuwa jambo la lazima na kila mwanajamii aliwajibika.

### 3.3.1 Kudhalilishwa kwa Utu na Wageni

Katika kitabu cha *Makala za Semina ya Kimataifa* (Temu, 1983), utu wa Mtanzania au Mwafrika wakati wa miaka ya 1770 hadi 1831, enzi za George Friedrich Hegal,

Wazungu ambao sasa utamaduni na miiko yao inaabudiwa na watu kama wasokwao alisema, “Mtu mweusi ni picha ya mtu wa asili katika hali yake ya ushenzi na unyama wa pori. Kama tunataka kumwelewa mtu huyu hatuna budi kusahau kabisa fikira na hisia zote za staha na maadili, maana ndani ya “kiumbe” wa aina hii hampatikani jambo lolote lenye kupatana na utu ….” na wengine wakaliita bara la Afrika “Bara la Giza” (Sengo, 1978). Je, hii ni sababu ya kuusujudia utamaduni wa kigeni na kuukana utu wa Mwafrika? Jibu ni laa. Tunapaswa kuuonesha ulimwengu kuwa Mwafrika ana miiko na utamaduni wake ambao una utu na maadili ya kibinadamu.

Miiko ya jamii mbali mbali inatoa fursa ya malezi bora ya wanajamii. Jamii ya Wabungu inatukumbushwa kuwa, maadili ya watu wanaoiacha miiko na kushika mila za wageni ambao hawajui hata asili ya jamii za Kiafrika, ni zahama wanawatafutia Waafrika kwani hawataacha kusambaratika na kupukutika kama majani makavu. Matororo, (2004) katika gazeti la Alasiri namba 6429 la tarehe 3/2/2004, aliandika kuwa Wamasai walikuwa wanaongoza katika kufuata mila na desturi za kabila lao, na hii inaonesha kwa kiasi gani wanafuata miiko ya babu zao.

Mwandishi wa habari hii alikuwa anaelezea jinsi maadili yalivyomomonyoka kwa kuangalia kuwa, zamani watoto walipomwona mzee akipita walimkimbilia na kumpokea mizigo, kitu hiki kwa sasa ni kinyume kabisa, kwani hata kama wataombwa kufanya hivyo watakimbia au kuendelea kucheza bila ya soni. Hali hii ni uthibitisho tosha kuwa maadili ya jamii ya Wabungu sasa yamemomonyoka na sasa kama Wabungu na Watanzania wanapaswa kuchukua hatua za haraka ili kurudisha heshima ya jamii.

### 3.4 Mapisi ya Miiko katika Sanaajadiiya

Kwanza, ingawa wanataalimu wengi wanasema kuwa miiko ilikuwepo katika jamii za Kiafrika tangu utangu hata kabla ya kuingia kwa dini na ukoloni, (Chenya, 1998; Wamitila, 2003) wanathibitisha kuwa, jamii nyingi za Kiafrika katika nchi mbali mbali, kama za Afrika ya Magharibi, Kaskazini mwa Afrika na hata Kusini mwa Afrika, zilikuwa na miiko inayofanana na kuthibitisha kuwa Afrika ni moja. Wanataalimu hawa wanakwenda mbali zaidi na kuangaliya dhima ya fasihi kuwa ilikuwa ni kuonya, kuadibu, kufundisha, kuonesha njia, na pia kutunza hazina ya jamii ili isipotee hazina hii adhimu ambayo ndimo mlimo na mapisi na ulimbe wa jamii.

Pili mtafiti anapiga mbizi katika mchango wa wanataalimu (Sengo na wenzake, 1978; Sengo, 1978) wanavyouangaliya mchango wa wageni katika kukengeusha fasihi na mapisi ya Mwafrika wakimnukuu Gurr na Carder katika kitabu chao cha *Writers of East Africa* kuwa Afrika waliliita kuwa ni "Bara la Giza" ikiwa na maana kuwa hakuna Ustaarabu wala Ilimu yoyote. (Mdee, 1983; Sengo na wenzake, 1973), wanabainisha wazo la wakoloni kuwa Afrika ni nchi ya Utoto na imezongwa na shuka jeusi la usiku.

Finnegan, (1970) naye anasema kuwa kabla ya karne iliyopita hapakuwapo na fasihi kwa mtazamo wa Wazungu wa Ulaya. Mtafiti hakubaliyani na hoja hii. Hoja hii ni hoja ya kukengeusha mitizamo ya sanaajadiiya, asili au chimbuko na utu wa Waafrika kuwa hawakuwapo Afrika hadi Wazungu walipofika. Mtafiti anaona kuwa huu ni udhalilishaji wa sanaajadiiya uliofanywa na wakoloni ili kupoteza umoja wa

Waafrika. Mtafiti anashadidia kuwa Afrika ina mapisi yenye Utu na Maadili kama inavyojitokeza kati ya vipera vya sanaajadiiya tulivyonavyo na miiko ikiwa ni mojawapo (Sengo, 1978; Nkwera, 2009).

Kama inavyoonekana hapo juu, tafiti nyingi zimefanywa kuhusu sanaajadiiya lakini tafiti hizi zimekuwa za jumla mno. Kwa mfano ni ule utafiti wa (Finnegan, 1970) ambao ulitalii takriban bara lote la Afrika na haukuweza kuchambua sanaajadiiya ya Kiafrika katika jamii moja moja kwa undani wake na pia haukuangaliya vikumbo vingi vya sanaajadiiya. Hali hii inajidhihirisha kuwa utafiti ulikuwa ni wa kijuu juu sana. Aidha tafiti hizo hazijabainisha nafasi ya miiko katika kudhibiti maadili. Kwa hali hiyo, kutokana na pengo linalojitokeza, mtafiti anaona umuhimu wa kutafiti kuhusu kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili katika jamii ya Wabungu kwa sababu wanataalimu wamejadili kuwapo kwa miiko lakini hawajajadili kufuwawa kwa miiko katika jamii. Katika utafiti huu matafiti amechunguza jamii moja tu ya Wabungu na ameangaliya kikumbo kimoja tu cha kufuwawa kwa miiko na kukengeuka kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

### 3.5 Umuhimu wa Miiko

Hadi leo nchini Tanzania hakuna machapisho mengi ya sanaajadiiya yanayohusu miiko ya jamii kama ilivyo katika nahau, methali na misemo. Wanataalimu wakongwe walianza kuonesha hima za sanaajadiiya tangu miaka ya 1970. Wanataalimu hawa walibainisha kuwa watafiti wa sanaajadiiya wamepewa msukumo mkubwa wa kufanya utafiti wa sanaajadiiya katika tanzu mbali mbali na utafiti huu unalenga kuwamo katika kundi hilo. Miiko ina pengo kubwa la kazi zilizorekodiwa (Sengo, 1985; Sengo, 1978; Mdee, 1978).

Hata hivyo ingawa juhudi hizi zilianza kuonekana tangu miaka ya 1970, lakini bado mtafiti anachelea kusema kuwa juhudi hizi za utafiti zinakwenda pole pole sana. Kwa mujibu wa (Owino, 1978) katika Farahasa ya Utafiti wa Amali za Fasihi Simulizi, ni tafiti mbili tu za miiko zilizorekodiwa. Licha ya kurekodiwa, nyaraka hizi zimehifadhiwa katika kasiki la lugha na kuhodhiwa kama lulu ambayo kama itaonekana na watu inaweza kuwa hatarini kuporwa. Hii ina maana kuwa hata hicho kidogo ambacho tayari kimeshatafitiwa bado hakijatolewa kwa matumizi ya wazi ya kiakademia. Mwaka huo huo (Sengo, 1978) aliingia darasani huko Zanzibar kuongoza mafunzo juu ya *"Utafiti katika Fasihi Simulizi"*. Bado mazao ya juhudi hizi hayajaungwa mkono vya kutosha na wanataalimu wenza. Hali hii inaonesha kuwa bado hatujaipa miiko umuhimu unaostahili katika malezi na kuimarisha maadili ya Watanzania ambapo utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo lililopo na kuongeza idadi ya kazi za miiko zilizoaondikwa na kutumika kwa jamii na wanataalimu.

### 3.5.1 Kuhifadhiwa kwa Sanaajadiiya

Mawazo ya (Sithole, 2006) ni muhimu sana katika kusukuma mbele utafiti huu. Umuhimu wake unakuja pale ambapo anagusiya suala la kuhifadhi mambo ya miiko na maadili ya jamii ambapo utafiti huu umelenga kufanya hivyo kwa kutafiti miiko ya Wabungu na kuiweka katika maandishi kwa ajili ya marejeleo kwa watafiti na jamii kwa ujumla. Kinyume na hali halisi ya sasa kuwa ni kiasi kidogo sana cha elimu ya asili ambacho kimehifadhiwa kwa kurekodiwa kwa ajili ya kumbukumbu. Mawazo hayo yanaungwa mkono na (Chisenga, 2002) kwani tasnifu hii si tu itawekwa katika maandishi bali pia itawekwa katika mfumo wa elektroniki kwani

hali halisi ni kuwa elimu ya wenyeji wa Afrika haijawekwa katika mpangilio mzuri na kisha kuchapwa na kuwekwa katika mfumo wa elektroniki kwa sauti au video ili iweze kupatikana katika mifumo mbalimbali ya mawasiliano duniani. Hivyo basi utafiti huu wa miiko kutoka katika jamii ya Wabungu, unaanza kuziba pengo kubwa lililopo la tafiti za sanaajadiiya utanzu wa miiko hasa jamii za Tanzania.

### 3.5.2 Kukengeuka kwa Maadili

Katika jamii ya Wabungu, kuna viashiria vya kukengeuka kwa maadili. Hali hii inajitokeza kwa watu wazima kuwatupia lawama watoto na vijana kuwa hawana adabu au watoto wa siku hizi hawana miiko. Juhudi hizi zinashadidia kuwako na miiko inayoachwa na watu wasiokuwa na mizizi yao wenyewe (Sengo, 1985). Utafiti huu unakwenda hatua moja mbele zaidi na kuchukuwa hatua za kupunguza kama si kumaliza kabisa tabiya inayosababisha kufuwawa kwa miiko katika jamii ya Wabungu. Mwiko ni kama lulu katika malezi ya jamii, ndani ya miiko ndimo mlimo utu. Pamoja na wanasanaajadiiya kubainisha kuwa utu ni maadili ya jamii na miiko hii hujikita katika kuhakikisha kuwa sheria zinafuatwa (Sengo, 2008; Sengo na wenzake, 1978). Katika utafiti huu mtafiti aliona kuwa utafiti alioufanya una nafasi kubwa ya kuondoa ugiligili unaojitokeza katika tafsiri na utendaji wa falsafa, mapisi na ulimbe wa miiko katika jamii ya Wabungu.

Sheria haziwezi kufuatwa bila kuwa na miongozo na kipimo cha kutazamia viashiria vya maadili kuwa yanafuatwa au la. Aidha utafiti huu unaonesha kuwa miiko ni kipimo cha maadili ambayo ni utu wa mtu. Utu wa mtu ni kitu cha kwanza na ubinadamu ni kitu cha pili. Ubinadamu unaweza kuathiriwa na mazingira ya mahali

mtu azaliwapo au akuliapo. Lakini utu wa mtu hubaki pale pale (Sengo, 1981; Berry, 2009). Katika utafiti huu mtafiti amebainisha ni mavazi gani mtu au mtoto anapaswa kuyavaa na athari za mavazi yaliyokinyume na miiko ya Wabungu. Utafiti unabainisha mifano kama, mtoto anapoambiwa kuvaa nguo ya kubana mwilini mwiko, basi, ieleweke kuwa jamii hii ina maadili tafauti na jamii nyingine ambazo labda kwao wanaweza kuvaa hata *kishida* au *bikini* kwa kisingizio cha kuwa ni vazi maalumu (p'Bitek, 1972; Njogu, 1999) na kitabu cha Utamaduni na Mila Zetu. Mtafiti anatarajia kuwa utafiti huu utaziba pengo la kimaadili linalijitokeza katika kazi za sanaajadiiya zinazobainisha wazi kuwa ni vazi lipi ni mwiko kuvaliwa hadharani au katika kadamnasi.

Wabungu kama zilivyo jamii nyingi Afrika zina miiko. Miiko hii ina umuhimu mkubwa sana katika makuzi na malezi ya jamii nzima. Kila mara kwa kutumia miiko, mwanajamii wa Kibungu anaoneshwa njia na wajihi wa Mbungu.

### 3.5.3 Ulimbe wa Miiko na Mali Asili

Mtafiti anatowa kongole kwa Ndaki, wanataalimu na watafiti wa sayansi ambao kwa dhati wanaona kuwa miiko inapaswa kuchukua mkondo mpya. Kama wanasayansi na wanataalimu hawa walivyoona umuhimu wa jamii kuanza kutumia miiko katika kufanya utafiti na kutafuta mbinu jadiiya katika kutafuta kinga ya afya ya watu, kutafuta tiba ya maradhi mbali mbali na kulinda na kuhifadhi mazingira. Aidha kama ilivyoonekana katika miiko kulinda matumbawe ya bahari ambayo hutumiwa kama mazaliya ya samaki Zanzibar, kulikofanywa na watafiti wa Chuo kikuu cha Dar es Salaam. Mtafiti anaona kuwa kwa kiasi hicho hicho ni muhimu katika kuhifadhi

elimu ya fasihi simulizi hasa *utanzu wa Miiko* katika kutafuta ulinzi wa maadili ya jamii ya Wabungu.

Kufuwawa kwa miiko kumesababisha hali ya kuporomoka kwa maadili katika jamii hii ya Wabungu (Masalu, 2010; Sithole, 2006; Chisenga, 2002; Dale, 1896). Kwa mfano, katika utangulizi wake Mkurugenzi wa Kitengo cha Mali asili ya Bahari Zanzibar, ndugu Kyewalyanga alisisitiza kuwa, katika miaka ya hivi karibuni jamii imeanza kutumia miiko kama sehemu ya elimu jaadiiya katika kuhifadhi mali asili na mfumo wa ikolojia umepewa umuhimu wa hali ya juu licha ya maendeleo na utandawazi.

Sanjari na utafiti huo murua, mtafiti anaona kuwa, tafiti na wanataalimu hao hawajashughulikia suala la maadili katika jamii walizoziandikia kazi zao. Kwa hali hiyo, katika utafiti huu mtafiti ameshughulikia utanzu huu wa miiko kwa kupiga mbizi katika jamii moja tu ya Wabungu. Hapa mtafiti anabetua suala la kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili ambalo bado halijafanyiwa utafiti. Hivyo utafiti huu unasaidia kuziba pengo la kupotoka kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

Tangu utangu miiko imekuwa na umuhimu mkubwa kwani imekuwa ni ghala ya asili zetu, bohari ya Uafrika wetu, utu wetu na ubinadamu wetu. Miiko katika fasihi simulizi ina ulimbe. Kufuwawa kwa miiko ni sawa na kufuwawa kwa ulimbe. Ulimbe huo ndio sasa wanasayansi wanautumia kwa kuthibitisha kuwa tangu utangu babu zetu waliijua sayansi na ndiyo maana waliishi kwa miaka mingi wakilindwa na miiko (Masalu, 2010). Sasa miiko hiyo wanaibatiza majina ya kufuata miiko ni

kubaki nyuma kimaendeleo. Mtafiti ametumia upungufu uliopo kubainisha ulimbe wa miiko.

### 3.5.4 Miiko na Mgawanyo wa Kazi

Kama mwanasanaajadiiya anavyoona kuwa, kuna umuhimu mkubwa kwa jamii kuwa na mgawanyo wa kazi. Kazi ni muhimu kugawanywa kwa kufuata umri na jinsia. Hivi ndiyo ilivyokuwa tangu utangu wa fasihi ya mwanadamu. Mgawanyo huu ulilenga kuulinda utu wa mwanamke. Wanawake walikuwa na kazi zao maalumu. Wanawake wa Kibungu walipaswa kufanya kazi za nyumbani na si kazi za kwenda kuwinda na kuvua samaki. Kazi kwa Mbungu ndiyo kielezeo cha kuonesha kuwa utu wa mtu una staha (Sengo, 1981; Mwanga, 1984). Mtafiti katika utafiti huu anachukuwa nafasi hiyo hiyo kubainisha umuhimu wa miiko katika kuonesha kazi na wajibu wa jamii katika kafanya kazi kwa kufuwata jinsi na kuleta heshima na kuthamini staha ya mtu.

Miiko ni muhimu sana katika kulinda na kulea jamii ya watu waliowaadilifu na wanaojua maana ya utu wa mtu na maadili mema. Umuhimu mkubwa wa miiko ni kuwa ni kwa kiasi gani Wabungu wanaienzi na kuitumia kwa mtazamo chanya. *Mchelea mwana kulia hulia yeye*. Kabla ya Taifa kulia basi, kwa kazi hii mtafiti amesaidia kutoa majibu ya baadhi ya matatizo ambayo hayajapata majibu.

Methali ya *mchelea mwana kuliya hulia yeye*, ina maana kuwa mtoto anapaswa kuadhibiwa anapokosa au kukengeuka. Mtafiti anaona kuwa miiko inaweza kutumika kumchelea mwana badala ya bakora ambazo si adhabu asiliya katika jamii

ya Wabungu katika malezi bora ya watoto. Hivyo jamii ya Wabungu inaweza kulinda heshima na maadili yake kwa kufuatiliya shughuli sahihi za wanajamii.

### 3.6 Hali ya Miiko katika Jamii ya Wabungu

Wanazuoni wakongwe wa Tanzania kutoka katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzia miaka ya 1970, walianza kuchimbua fasihi Tanzania. Kitu cha kushangaza hadi leo ni majina hayo hayo ambayo yanajitokeza katika uga huu wa fasihi. (Senkoro, 1982) anasema hivi katika utangulizi wake, dhana ya fasihi ilianza kushika mizizi miongoni mwa walimu, wanafunzi na wanazuoni mbalimbali wa somo la fasihi ya Kiswahili, kuwataja baadhi ni T.Y.S. Sengo, S.D. Kiango, Pennina Muhando, Ndyanao Balisidya na F. Nkwera.

Kwa kuwa hadi sasa bado machapisho ya wakongwe wa taalimu hii ya fasihi ndio wanaojitokeza na kuwa mhimili wa sanaajadiiya ya Mtanzania. Mtafiti anaona kuwa pamoja na ujuzi wao adhimu na wa kutukuka katika taalimu hii ya sanaajadiiya katika Tanzania, bado taalimu hii inahitajika kuibua wanataalimu wa ngazi mbali mbali, wachanga kwa wakongwe ili wanataalimu hawa wakongwe waweze kuwaleya na kufikiya nadharia ya Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao. Kwa hali hii mtafiti anadiriki kusema kuwa nyanja hii imesahaulika sana na wanataalimu wengi wa zamani na wapya na kuifanya kama ni nyanja ndogo na isiyo na umuhimu wowote kwa jamii.

Kwa utafiti huu mtafiti anaona kuwa inawapasa kuitaamali kwani hapa ndipo penye malezi na maadili na utu wa Mbungu na utafiti huu unapenyeza mkono ili

kuwaamsha wale wote waliolala ili waamke na kupiga mbizi katika taalimu hii adhimu ya miiko na maadili ya jamii.

### 3.6.1 Miiko na Kifo

Kama ilivyo ni muhimu kwa fasihi kuonesha wazi na kukemea tabia mbaya za wanajamii, ili kuiweka jamii pamoja kwa misingi ya kimaadili. Inaonekana kuwa katika jamii ya Wasukuma ilifanya hivyo na kuwa mwiko unaosema kuwa *ni mwiko kuua*. Pia *ni mwiko kula nyama ya mtu*. Je, kama jamii hiyo, watu wangekuwa na uhuru wa kuua au ruhusa ya kuifanya nyama ya binadamu kitoweo, maadili ya kuyalinda maisha ya wanyonge yangekuwaje?

Kwa mujibu wa wana taalimu wengi mtafiti anaona kuwa kuua ilikuwa mwiko. (Mirambo, 1999; Allan na Burridge, 2006; Achebe, 1958) pia katika jamii ya Waibo mtu aliyejiua alikuwa ni najisi katika jamii na kwa hali hiyo ilikuwa ni mwiko kwa mtu wa kabila hilo la Waibo kugusa mwili wake na kazi ya kumzika ilifanywa na wageni hivyo alizikwa kama mbwa. Katika utafiti huu mtafiti anabainisha ni kwa namna gani jamii ya Wabungu ilithamini na kuulinda uhai wa Mbungu na mgeni katika jamii ya Wabungu kwa kuwa na mwiko unaokataza kuua au kujinyonga.

### 3.6.2 Miiko ya Uzazi na Ndoa

Miiko ya Wabungu ilitumika kama ishara ya kinga ya maradhi kama ilivyokuwa katika miiko ya watu wa Benin. “Kwa kukiuka baadhi ya miiko au kuzikasirisha nguvu zisizoonekana kama, miungu au uungu, unaoweza kuharibu amani ya akili na mwili” (Idehen na Oshodin, 2007). Miiko hasa ni makatazo au misemo yenye maana ya kuwakataza watu wa jamii hiyo kufanya jambo au kitu fulani. Kwa kuwa katika

jamii nyingi za Watanzania miiko hii iliwahusu zaidi wanawake kuliko wanaume. Kwa mfano, katika kabila la Wajita kutoka mkoa wa Mara Musoma vijijini, Mashariki ya ziwa Victoria, kuna mwiko unaosema; *ni mwiko kwa mwanamke kusimama katikati ya mlango, siku ya kujifungua mtoto atakuwa anachungulia na kurudi tumboni* au *usile chakula ukiwa umesimama utaoa au kuolewa mbali*. Pia (Farsi, 1965; Sengo, 2008), wanasema Zanzibar kuna mwiko unaosema ni mwiko kwa mwanamke mjamzito kula ndizi yenye mapacha kwani atazaa watoto mapacha, wanataalimu hawa katika kazi zao hawajaonesha na kubainisha miiko katika kumbo mbali mbali.

Sengo, (2008) amezungumzia miiko katika mazingira mbali mbali ya maisha hasa kuzaliwa na malezi ya watoto ambao ndio kizazi kijacho cha Watanzania. Sengo anasema "Ikishafahamika kwa dhati kuwa yaliyosikiwa ni ya kweli, kwa jamii zilizostaarabika, mama huyu mwenye uja uzito huwa ni mtu mwenye miiko maalumu ya kuifuata". Miiko hii ilikuwa na maana kubwa katika makuzi ya mtoto tumboni, na pia makuzi ya kiroho na nidhamu katika jamii. Katika kazi hii mtafiti amebainisha miiko mbali mbali katika kumbo tafauti tafauti.

### 3.6.3 Miiko na Adhabu

Katika mtandao wa *The African Tribes and Cultures*, miiko, makosa na adhabu katika jamii ya Wakikuyu wa nchini Kenya, ilikuwa ni mwiko kukataa chakula ulichopewa kwani ilikuwa ni kuzuia baraka zisiingie katika nyumba hiyo uliyopewa chakula. Pia katika jamii hii ya Wakikuyu ilikuwa ni mwiko kuua mtu, na aliyepatikana na kosa la kuua alifungwa kwenye majani makavu ya mgomba na

kuchomwa moto hadi kufa, na baada ya kufa alitupwa msituni ili aliwe na wanyama wa porini.

Ni shida kubwa kwa mtu wa sasa kuona umuhimu wa kuwa na miiko hii. Mwiko uliweka nidhamu ya watu na upendo wa kibinadamu. Sheria ni sehemu moja tu ya mambo ya kufuatwa katika jamii, lakini miiko ilimfanya mtu kila wakati kujirudi hata alipopandwa na hasira. Waswahili husema, hasira hasara. Mwiko ulikuwa ukumbusho wa watu wanaojisahau na kurudisha utu tena hivyo kujizuia kutenda uhalifu.

Mwanasanaajadiiya (Sengo, 1992) amezungumziya kwa kina mapisi ya itikadi za Waislamu wa mwambao wa Kenya ni pamoja na imani ya kuwepo pepo – majini na mashetani. Nguvu na uwezo wa pepo hao katika kulinda mashamba, mali, miji, kusaidia kutibu maradhi, na mashetani kuroga na itikadi hizi zina nafasi katika upwa wote wa Waswahili. Pamoja nazo, Waswahili wana mila kama vile miiko mbalimbali. Mifano: kula gizani ni kula na shetani. Kunywa maji msalani mtu huwa mwongo. Bundi akilia juu ya nyumba anatangaza kifo. Licha ya hayo, (David na Liz, 2009; Sengo, 1992) wote kwa pamoja wanakubaliyana kuwepo kwa miiko lakini hakuna aliyeongelea kuhusu kufuwawa kwa miiko na namna ya kudhibiti maadili ya jamii.

### 3.6.4 Miiko na Maendeleo Imarishi

Mwanataalimu (Osei, 2002) anaeleza kwa kina kabisa juu ya uhusiano wa miiko na maendeleo imarishi katika jamii za Waafrika. Maelezo haya ni muhimu sana katika kusukuma mbele utafiti huu. Miiko ina umuhimu mkubwa sana katika kuzifanya

jamii zetu za Kiafrika kudumisha maendeleo imarishi. Masuala makubwa yanayoongelewa yamegawanywa katika makundi mawili ya miiko ambayo ni miiko ya imani na ulimbe wa miiko hiyo.

Hii ni sababu inayomfanya mtafiti kujizatiti katika kufanya jitihada za kuziba mwanya unaojitokeza katika maeneo ambayo wanataalimu wengine wameshayafanyia utafiti na kwa hali hiyo kuijenga jamii ya Wabungu iliyo na maadili mema na maendeleo imarishi kwa kuibua sayansi yetu iliyoporwa na wageni na kujimilikisha hazina hiyo yenye asili ya Afrika (Omari, 1981).

### 3.6.5 Pengo la Kuzibwa na Utafiti

Tafiti na makala mbalimbali ambazo mtafiti amezitalii hazija onesha matatizo yoyote ya kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili. (Sengo, 1985; Sithole, 2006; Chisenga, 2002, Allan, & Burridge, 2006 na Owino, 1978) wote wanazungumza kuhusu miiko kuwapo lakini ni kiasi kidogo sana cha miiko kimetafitiwa. Hili ni pengo mojawapo ambalo utafiti huu unajaribu kuliziba.

Pia pengo lingine linalotarajiwa kuzibwa na utafiti huu ni lile la kukengeuka kwa maadili ya Wabungu. (Sengo, 1981; Sengo, 2008; p'Bitek, 1972; Mirambo, 1999; Achebe, 1958; Idehen na Oshodin, 2007; David na Liz, 2009) wote wamezungumza kuhusu miiko na maadili au utu. Utafiti huu unaziba pengo la tafiti za sanaajadiiya pamoja na utanzu wa miiko zilizokwishafanywa. Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili katika jamii ya Wabungu kwa upande mwingine ni kipengele ambacho hakikushughulikiwa katika kazi za wanataalimu hawa.

Kama ilivyo kwa jamii mbalimbali duniani, miiko hubeba ulimbe fulani katika jamii husika, hivi ndivyo ilivyo pia katika miiko ya Wabungu nayo ina ulimbe wake. Ingawa Watafiti na waandishi wengi wameandika kuhusu miiko hawakugusia suala la kufuwawa kwa miiko katika jamii, hivyo basi katika utafiti huu, mtafiti amejishugulisha sana na pengo kubwa linalojitokeza la kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili ya jamii ya Wabungu. Kwa kuwa miiko ipo na haijasahaulika, mtafiti amekusanya miiko na kuiambatanisha kwa manufaa ya jamii ya Wabungu, wanazuoni, Watanzania wote, wanajamii wa Bara la Afrika na kwingineko. Maadili mema yanaweza kuleta amani, utengamano na maendeleo katika jamii, hivyo miiko hiyo itakuwa hazina ya jamii.

### 3.6.6 Hitimisho

Katika utafiti huu mtafiti amepitia mabuku kutoka katika maktaba na mtandao. Pia mtafiti amefanya mazungumzo na wanajamii wazee wachache maskanini mwao. Ikumbukwe kuwa maktaba ya sanaajadiiya ni wanajamii wenyewe, basi ili kukamilisha kazi hii ya sanaajadiiya ilimpasa mtafiti kutumia maktaba jamii, Watu maskanini. Taarifa zilizopatikana zimesaidia kbainisha pengo lililopo katika jamii na kwa hali hiyo zimetumika katika kujenga mwega wa kazi hii ya utafiti na zilimsaidia mtafiti katika kufikia Hitimisho imara la utafiti huu.

# SURA YA NNE

# 4.0 NJIA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Kabla ya kuanza kazi ya utafiti kwanza kabisa kazi kubwa ni kupangilia kuhusu namna utafiti utakavyofanyika. Mpangilio huu ndio unaoitwa Usanifu wa Utafiti. Hapa mtafiti anapaswa kupanga kuhusu nini, wapi, lini kwa kiasi gani na kwa namna gani utafiti huu utafanyika na kufuata mkondo sahihi. Kwa maneno mengine, usanifu wa utafiti ni mpangilio wa utaratibu wa kukusanya na kuchambua data katika mpangilio maalumu bila kupoteza nia kuu na madhumuni ya utafiti (Hart, 1998; Kothari, 1985; Sengo, 1978; Dekeba, 2012). Katika utafiti huu mtafiti ametumia maneno mbinu na njia kuwa yana maana sawasawa.

## 4.2 Usanifu wa Utafiti

Mwanadamu anapofikiria kufanya kazi yoyote kama kulima au kujenga nyumba, haanzi kujenga au kulima kwa sababu ana pesa na eneo la kujenga au kulima tu. Kwanza mtu huyu anapaswa kujiuliza maswali muhimu, je anahitaji kujenga nyumba au la. Kama anahitaji lazima ajue ukubwa wa nyumba na mahitaji ya nyumba yenyewe. Hili si pambo hata kama ni pambo lazima ujue utaliweka wapi ili nyumba yako ipendeze. Hivyo unahitaji kumwona mwanataalimu na kupanga hatua kwa hatua mahitaji yako hadi nyumba itakapokamilika.

Hivi ndivyo ilivyo katika utafiti. Mtafiti anahitaji kuwa na mpango kabla ya kwenda kukusanya data. Huu si mpango kazi tu, bali ni mpango kamili unaobainisha mtiririko wote wa utafiti tangu mwanzo wa utafiti hadi mwisho. Ikumbukwe kuwa

usanifu wa utafiti si njia za utafiti, na usanifu wa utafiti hutumia njia mbali mbali za kukusanyia data. Hii ina maana kwamba kabla ya kuanza kuandaa njia za utafiti ni muhimu kuwa na umbo la utafiti wenyewe unaohitaji kuufanya. Usanifu ndio utakaopima ubora wa utafiti, kwani usanifu hutathmini ubora na udhaifu wa njia za utafiti. Usanifu wa utafiti unaweza kuwa ni wa uchunguzi, Utafiti Kifani, na njia za kukusanya data ni maswali ya usaili, maswali ya hojaji, , kusaili, kuchunguza na kuchambua data (Kothari, 1985).

## 4.3 Umuhimu wa Usanifu wa Utafiti

Umuhimu wa usanifu wa utafiti unakuja pale ambapo, usanifu wa utafiti ni kama uchoraji wa ramani ya nyumba kabla ya kuanza kazi ya ujenzi. Usanifu wa utafiti hurahisisha kazi ya utafiti kwani huonesha kila ngazi ya utafiti na vitu vinavyopaswa kufanywa kwa kinagaubaga. Katika usanifu wa utafiti mtafiti anabainisha njia za ukusanyaji wa data na mbinu za uchambuzi wa data zilizokusanywa. Mtafiti anapaswa kuanza kuandika usanifu kabla ya kuanza kazi ya utafiti.

Usanifu uliobora ni ule unaolenga kutatua au kubainisha tatizo la utafiti au nia ya utafiti, kwa kuangaliya namna ya kupata taarifa, kubainisha ujuzi wa mtafiti katika kukusanya na kuchambua data, madhumuni ya nia kuu ya utafiti kuwekwa wazi na kwa mantiki sahihi na mipango sahihi ya upatikanaji wa muda na fedha za kufanyia utafiti.

## 4.4 Njia za Utafiti

Utafiti huu umejikita katika njia ya Uchunguzi Kifani. Njia hii ni mwavuli wa njia zote za utafiti zinazolenga kutoa maamuzi sahihi wakati wa kuchanganuwa data na

kufanya Hitimisho la utafiti. Inatoa utaratibu maalumu wa ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na utoaji wa taarifa ya utafiti husika (Bell, 1999). Njia hii imetumika ili kumpa mtafiti data za msingi kwa kina na kwa muda mfupi.

### 4.4.1 Njia ya Kielezeo Stahilifu na Kielezeo cha Kiasi

Katika kufanya utafiti wa kazi hii mtafiti ametumia njia ya kielezeo stahilifu na njia ya kielezeo cha kiasi. Njia ya kielezeo stahilifu ni njia ya kukusanya data kwa kutumia maelezo. Na njia ya kielezeo cha kiasi ni njia ya kukusanyia data za idadi, hata hivyo mtafiti hakuzama sana katika kuitumia njia hii. Njia hizi husaidia sana katika kutafiti hali halisi ya maisha ya watu kwani uhusiano wa watu ndio uliosababisha njia hizi kuibuka. Njia ya kielezeostahilifu huwafanya mtafiti na watafitiwa kuwa karibu sana hivyo kumsaidia mtafiti kupata data za awali, halisi na sahihi.

Kwa kuzingatia kuwa kutumia kielezeo stahilifu mtafiti hufanya shughuli zake kama sehemu ya watafitiwa au jamii. Mtafiti huchunguza mienendo, mawazo na tabia za wanajamii. Data zinazokusanywa kwa njia hii huwa ni data zilizo katika hali ya maelezo kuntu. Kwa upande mwingine njia ya kielezeo cha kiasi husaidia kukusanya data za idadi ambazo ni mhimili wa kufikia kura ya wengi wape. Hapa uwingi wa watafitiwa katika kutoa maelezo ya aina moja kuwa wengi ni uthibitisho wa kuwa jambo linalotafitiwa lina mashiko ya kukubalika au kukataliwa na jamii husika (Borg na Gale, 1989; Coolica, 1994; Kothari, 1986).

Njia ya kielezeo stahilifu kwa hali hiyo hufanya kazi vizuri zaidi katika mazingira halisi. Kwa mfano, somo linalotafitiwa, “Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa

Maadili katika jamii ya Wabungu”. Njia hii  imekuwa ni njia sahihi ya kupata data stahilifu za msingi kwa kushiriki na kuzungumza na Wabungu katika mazingira yao maskanini.

### 4.5 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ni hatuwa mojawapo muhimu sana katika utafiti. Kabla ya kuanza kukusanya data mtafiti anapaswa kujua ni aina gani ya data anazohitaji kuzikusanya, na ni kiasi gani cha upeo utakaomwezesha kuamini kuwa data anazozikusanya zinatosha kukidhi hitaji la utafiti wake. Sehemu hii mtafiti anabainisha aina za data alizozikusanya kwa ajili ya utafiti huu.

#### 4.5.1 Data za Awali

Hizi ni data ambazo mtafiti alizipata masikanini. Hizi ni data ambazo bado hazijakusanywa na mtu yeyote kabla. Mtafiti aliweza kukusanya data hizi kwa kushuhudia, kusaili na kuzungumza na Wabungu katika masikani yao. Mambo haya yalimsaidia kuthibitisha matini aliyoyasoma katika mabuku yanayohusiyana na utafiti wake (Hart, 1998; Kothari, 1985; Sengo, 1978; Dekeba, 2012).

Katika njia ya ushuhudiaji mtafiti hutumiya muda mwingi kushuhudia vitendo halisi na mienendo ya wanajamii. Hapa mtafiti alishuhudiya mavazi, miondoko – namna wanajamii wanavyosalimiana na shughuli za kila siku za Wabungu ambazo ni pamoja na chakula na heshima wakati na mara baada ya chakula.

#### 4.5.2 Data za Upili

Hizi ni data ambazo ni za kazi tangulizi na ambazo mtafiti alizipata kutoka katika maktaba na mazungumzo na Wabungu. Data hizi ni zile ambazo watafiti wengine

wameshatafiti au kuandika kuhusu mada inayotafitiwa. Mtafiti aliweza kusoma kwa mzamo kabla na wakati wa kufanya utafiti. Makala haya yanatoka katika mabuku, matini, wavupepe na nyaraka mbali mbali kutoka katika maktaba.

Data za upili si data zilizo chapwa tu, bali pia ni kumbukumbu ambazo hazijachapwa kama senema na video. Kwa kifupi data za upili ni data ambazo zipo tayari bila ya kujali zilikusanywa lini na wapi. Kwa hiyo data za upili zimetumika kama marejeleo ya utafiti. Kwa hali hiyo data hizo zimekuwa ni zana ya kujaribia ugunduzi wa mtafiti. Pia data za upili zilitumiwa na mtafiti kama chanzo cha taarifa (Kothari, 1985; Sarantakos, 1993).

Faida za data za upili ni kuwa, ni za uhakika na ni rahisi kuzipata. Data hizi zilipatikana karibu na mtafiti bila ya kujali jiografia ya mahali alipo na kumwokolea muda. Kwa kutumia data za upili mtafiti alipanua wigo wa hazina ya maarifa ambamo mtafiti aliweza kupata mawazo ya ujumla yenye ulimbe uliofanyiwa utafiti. Licha ya hayo data za upili zilimsaidia mtafiti kutibitisha matokeo ya data za msingi.

Matatizo ya data za upili ni kuwa data zilizopo zinaweza kushindwa kukidhi mahitaji maalumu ya utafiti. Wakati mwingine data zilizopo zinaweza zisiwe sahihi kama zinavyotarajiwa na kupotosha utafiti. Mara nyingine data za upili zinakuwa zimepitwa na wakati au kutokuwepo kabisa kwa watafiti wote, kwa hali hiyo kusababisha mwigiliano wa uhalisiya wa taarifa. Mtafiti alishindwa kupata tafiti za miiko zilizofanywa na Ndaki ya Dar es Salaam miaka ya sabini. Kwa hali hiyo mtafiti anakubaliyana na mawazo ya wanataalimu wa utafiti (Kothari, 1985;

Sarantakos, 1993; Hart, 1998; Sengo, 1978; Dekeba, 2012) kuhusu matatizo haya. Mtafiti alitumiya data za upili kutoka kwa waandishi mbali mbali wa zamani, zaidi ya miaka ishirini na waandishi wapya miaka ishirini iliyopita hadi sasa ili kudadavua usahihi wa kumbo zilizotafitiwa.

## 4.6 Uteuzi wa Watafitiwa

Utafiti huu unawahusu Wabungu na ndio waliohusishwa toka mwanzo hadi mwisho wa utafiti. Kwa kuwa Wabungu ni wengi, basi, mtafiti aliteua watafitiwa ishirini na tatu. Idadi hii ilimsaidia mtafiti kufanya mahojiana ya kina na wasailiwa. Mtafiti alitumia uteuzi lengwa na uteuzi tajwa kwa sababu alihitaji kupata data maalumu ambazo alijua kuwa watafitiwa lengwa wanazo na baada ya hapo watafitiwa lengwa walimwelekeza mtafiti kwenda kwa watafitiwa tajwa.

Mtafiti aliteua watafitiwa kwa kuzingatia kuwa watafitiwa ni watu kutoka katika jamii ya Wabungu, watu hawa ni wale waliojua Kibungu vizuri, watoto vijana na wazee wa jinsia zote. Watafitiwa walikuwa wameishi ndani ya eneo la vijiji vya jamii ya Wabungu, kama; Mwambani, Maleza, Mbangala, Udinde, Kapalala, au Mkwajuni kabla ya kuanza kuishi nje. Sifa hizi zilimwezesha mtafiti kupata miiko yenyewe, jinsi ilivyotolewa hapo zamani na sasa vijana wanavyoiona na kuitumiya (Mdee, 1978; Kothari, 1985).

Watafitiwa walisailiwa kwa kuzingatia makundi yao, wazee wanaume na wazee wanawake, vijana wa kiume na wa kike walisailiwa peke yao kwa kila jinsi. Makundi yote yalitoa uhalisiya wa miiko, ulimbe na matumizi kwa jinsi

wanavyoiona miiko hiyo na kuizingatia. Kila kundi lilikuwa na nafasi ya kuibua miiko inayowahusu, faida na matatizo yanayokabili miiko ya jinsi yao. Viongozi nao kwa upande wao walieleza hali halisi ya matatizo yanayotokea kama yana uhusiano wowote na kufuwawa kwa miiko katika jamii ya Wabungu.

**Jedwali 1.1: Linaonesha Idadi ya Watafitiwa kwa Idadi na Jinsi**

| Na. | Watafitiwa | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Watu wazima | 07 | 05 | 12 |
| 2. | Vijana | 06 | 03 | 09 |
| 3. | Viongozi | 02 | 00 | 02 |
| | **Jumla** | **15** | **08** | **23** |

## 4.7 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Katika ukusanyaji wa data mtafiti alitumia zana zifuatazo; usaili na ushuhudiaji. Njia hizi zilikuwa muhimu sana katika kumsaidiya mtafiti kukusanya data ambazo alizitumiya katika uchambuzi na Hitimisho la utafiti.

### 4.7.1 Njia ya Usaili

Enon, (1998), anaeleza kuwa usaili ni mbinu ya kukusanya taarifa au data kwa kunena au kwa sauti au mazungumzo kutoka kwa wasailiwa. Mbinu hii huwakutanisha msaili na msailiwa ana kwa ana na hivyo kumfanya mtu kutoa maelezo yake mwenyewe. Maelezo kutoka kwa wasailiwa hurekodiwa na kufanyiwa uchanganuzi. Kwa kutumia njia hii mtafiti alikusanya data za ana kwa ana ambapo wasailiwa waliulizwa maswali na kuombwa kutoa majibu yao moja kwa moja kwa mtafiti. (Kothari, 1986; Robson, 1993).

Katika usaili, mtafiti huanzisha mazungumzo kwa lengo maalumu ili kupata data za awali alizozihitaji na zilizolenga maudhui na madhumuni ya utafiti wake. Njia hii ni shirikishi na kwa kuwa mtafiti alihitaji kupata maelezo kuntu na ya kina, hivyo basi watafitiwa walihitaji kujua miiko ina maana gani na si ilimradi wamesema au kutaja idadi kubwa ya miiko. Maelezo ya msingi yaliyohitajika yalikuwa ni yale yanayoshabihiana na miiko. Kwa hali hiyo, mtafiti aliwasaili watu wa jamii ya Wabungu kwa kutumia maswali ya usaili yaliyoandaliwa (angalia kiambatishi *ii*).

### 4.7.2 Mtihani wa Njia ya Usaili

Njia ya Usaili ni njia iliyotumia muda mrefu zaidi katika kukusanya data za awali na ni ya gharama kubwa kwa kuwa mtafiti alihitaji kusafiri ili kukutana na wasailiwa maskanini mwao. Pia njia hii ilihitaji vifaa vingi ambavyo ni ghali, kama kilimbo, pataninga au simu zenye uwezo mzuri wa kurekodi, ngamizi kwa ajili ya kuchapia pamoja na CD au kinyonyeo cha kuhifadhia au kuhamishia kumbukumbu zilikuwa ni muhimu sana wakati wa utafiti.

Vifaa hivi vilisaidia kubeba data za mazungumzo halisi ambayo ni muhimu wakati wa kuchambua data. Njia hii ni bora zaidi kuliko kuandika mazungumzo ambapo mambo mengine yanaweza kusahaulika au kuachwa kwa kufikiria si muhimu kwa sababu ya uchovu wa kuandika. Katika utafiti wa sanaajadiiya, hii ni njia bora zaidi licha ya kuwa ni ghali na ilitumia muda mrefu. Katika utafiti huu mtafiti alisafiri toka Arusha hadi wilayani Chunya, katika vijiji vya Udinde na Mwambani kukusanya data. Vile, vile alitumia vifaa vyote alivyovitaja awali katika kuwasiliana na kuzungumza na baadhi ya watafitiwa.

### 4.7.3 Ushuhudiaji

Huu ni mchakato wa mtu mmoja au zaidi kuangalia kwa makini kinachoendelea katika maisha halisi ya jamii na kukiweka katika makundi ili kurekodi mambo mazuri hima zinazotokea katika jamii kulingana na mipango maalumu. (Koul, 1984). Mtafiti alichagua mbinu hii ili kuondoa mtazamo binafsi. Hivyo, data zilizokusanywa ni halisi na sahihi kwa kuwa mtafiti hakutegemea kupata taarifa kutoka kwa mtu mwingine tu bali yeye mwenyewe pia alikuwa na nafasi ya kuona matukio katika jamii iliyomzunguka wakati wa kukusanya data za utafiti huu wa kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili uchunguzi kifani wa jamii ya Wabungu.

### 4.7.4 Hitimisho

Katika huu utafiti mtafiti amefanya kazi nzuri na kupata data alizozitarajia ambazo zimemwezesha kuthibitisha kuwa kuna uhusiano kati ya kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili ya jamii ya Wabungu. Hivyo katika kazi hii mtafiti ametoa mapendekezo ya namna ya kurejelea mila na miiko ya jamii ya Wabungu.

# SURA YA TANO

# 5.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti amewasilisha na kufanyia uchambuzi data za awali na taarifa alizozikusanya kutoka kwenye eneo la utafiti. Data alizoziwasilisha hapa ni zile tu alizoziona kuwa ni muhimu katika utafiti huu. Eneo hili ni vijiji vya Mwambani na Udinde wilayani Chunya mkoa wa Mbeya. Kwanza mtafiti amewasilisha data za mazungumzo na Wabungu ambao aliweza kuzungumza nao. Mtafiti ameyagawanya mazungumzo haya kwa kufuata mtiririko wa maswali ya utafiti. Katika sehemu ya pili mtafiti amejadili miiko aliyoikusanya kutoka kwa watafitiwa katika eneo la utafiti pamoja na maelezo ya mtafiti akirejelea sura ya pili na sura ya tatu ya utafiti huu. Pia mtafiti amejadili miiko ambayo watafitiwa wanaiona kuwa imefuwawa au sasa haifuatwi au imeachwa na sababu za hali hiyo.

Licha ya mtiririko huo, mtafiti alianza kwa kuwahoji watafitiwa kuhusu maana ya maneno ya msingi katika utafiti. Maneno haya hayajaulizwa katika maswali ya usaili wa utafiti huu. Maneno hayo ni maana ya Miiko na maana ya Maadili. Lengo la maswali haya ni kumsaidia mtafiti na watafitiwa katika kuchanganua maswali ya usaili na kujiridhisha katika usaili kama kinachosailiwa na majibu ya maswali ya usaili yalimpa mtafiti ufafanuzi uliotarajiwa kubainisha, Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili katika Jamii ya Wabungu.

Katika uwasilishaji na uchambuzi wa data hizi, maswali muhimu ya kujiuliza na kuyazingatiya ni; Je, katika sanaajadiiya ya Mbungu kuna kitu gani cha asili ya

Wabungu cha kuringia au kujivuniya? Je, kuna uwezekano wowote wa kuenzi utamaduni wao, mapisi yao, lugha yao, miiko yao dhidi ya kukengeuka kwa maadili ya Wabungu? Je, ni lazima kutabii kila kitu bila kujali uzuri wa maadili ya Kiafrika kama mavazi, miondoko, lugha, mitindo ya kujiremba hata kujikandika madini ya mekyuli ili kukoboa rangi ya ngozi kwa sababu ya ati urembo? (P'Bitek, 1972; Sengo, 2008 na Mulokozi, 2002) wanashadidia hali hii.

Kitu cha msingi tunachotakiwa kukifanya ni kuirejelea Miiko. Miiko ina Kwao, Elimu ina kwao na kila jamii ina ujumi wake. Dhana hizi zote zinasisitiza kuhusu kuurudia utu wa Mwafrika, kuuthamini, kuuheshimu na kuupenda Utu wa Mbungu na vikumbo vyake vyote vya sanaajadiiya. Kuirejelea miiko iliyopotea, au kufuwawa na kusababisha kukengeuka kwa maadili ya Wabungu.

Vijiji vya Mwambani na Udinde vimo ukingoni, ndani ya bonde la ufa Mashariki ya Ziwa Rukwa. Kijiji cha Mwambani sasa kina umeme, na wanakijiji wachache wameshaingiza umeme nyumbani mwao. Wanakijiji wachache sana wana runinga, ingawa kuna mabanda ya kuoneshea picha za runinga ambamo mnauza pombe na soda kwa watu wanaokwenda kuangalia picha. Watu wengi wanatumia redio kupata habari. Katika kijiji cha Udinde hakuna umeme wa umma lakini kuna watu wachache wana mashine ndogo za kufuwa umeme unaowawezesha kutumia runinga kuangalia video.

Hapa mtafiti anawasilisha data zote kwa maswali ya usaili. Maswali ya usaili ya watu wazima, maswali ya usaili ya viongozi na maswali ya usaili ya watoto. Maswali yote ya usaili yalitumiwa na mtafiti kuwahoji watafitiwa.

### 5.2 Maana ya Miiko

Awali ya yote mtafiti alijadili na watafitiwa kuhusu maana ya miiko katika jamii ya Wabungu. Wote walionesha uelewa mkubwa juu ya miiko kuwa ni makatazo ya kufanya, kusema, kuangalia, au kula kitu kilichokatazwa. Mtafiti alihoji kama kuna uhusiano wowote kati ya miiko na ushirikina. Majibu yalikuwa mwiko hauna uhusiano wowote na ushirikina au uchawi.

Bibi mmoja alisita kidogo na kueleza kuwa, kama mtu anafuata miiko ya zamani basi anaoneka kama ni mchawi. Wazo hili halikukubaliwa na watafitiwa wengine kwani walieleza kuwa tabia ya watu sasa ni kutaka mambo ya kisasa na kutaka kuulinda usasa huo kwa kutoa sababu wanazofikiri kuwa ni sahihi. Mkataa asili ni mtumwa na Kila Jamii ina Ujumi Wake.

Mzee mmoja alisema kuwa hali hii inasababishwa na dini. Katika mafundisho ya dini, watu wanakatazwa kufuata mila za wenyeji Wabungu kwa madai kuwa huo ni upagani. Mjadala huu ulikuwa na haja ya kuleta sababu za kufuwawa kwa matumizi ya miiko katika jamii ya Wabungu.

Kitu cha mwiko ni katazo ambalo mtu akifanya atapata madhara yeye aliyefanya au jamii yote bila ya mchawi kuweka nguvu zake. Wachawi wapo lakini hawana sehemu katika miiko ya maadili ya jamii ya Wabungu. Hata wachawi wanaogopa kuvunja miiko hii. Miiko haijawekwa na wachawi. Mzee huyu alisisitiza kuwa, miiko waliikuta, japokuwa alikiri kuwa, siku hizi watu wengi hawaifuati. Wanaivunja kila uchao na ndiyo maana kuna matatizo mengi. Kwa mfano, zamani

mtu akiwa porini, ilikuwa ni mwiko kukanyaga maua ya mmea unaoitwa kafauongo (eindouwalouwa). Endapo mtu anakanyaga maua haya porini basi akili ya mtu aliyekanyaga mmea huo itafungwa na atapotea njia hawezi kurudi nyumbani. Je kuna uhusiano wowote kati ya mchawi na kafauongo? Mtafitiwa alihoji.

Dhana hii iliwafundisha Wabungu kutotembea peke yao porini. Kama mtu atakanyaga mmea huu, mwenzake ataweza kumsaidia, kumwongoza na mwishowe kurudi nyumbani salama. Pia ilikuwa ni njia ya kuwaonya watu waendao msituni kwa kutafuta kuni au mahitaji mengine kuwa waangalifu.

Licha ya hayo, umoja wa wanajamii ni muhimu sana katika maisha ya kila siku ya Wabungu. Mwiko huu ulimfanya mtu kila wakati kufikiria kuhusu umoja na si ubinafsi. Msituni kuna hatari nyingi. Pia mwiko huu unasisitiza uangalifu wakati mtu au watu wanapokuwa msituni. Kutembea bila kuangalia chini unaweza kukanyaga nyoka ambao wengi ni hatari sana kwani wana sumu kali ya kufisha kwa haraka. Hadi sasa mwanamke haendi peke yake mwituni kusenya kuni, lazima aandamane na wenzake wengi.

## 5.3 Miiko na Ushirikina

Mtafiti alitaka kujua kama watafitiwa walikuwa na maoni yoyote kati ya uhusiano wa Miiko na Ushirikina. Watafitiwa wengi walikuwa na maoni tafauti tafauti. Ingawa wengi walikana kuwepo uhusiano kati ya ushirikina na miiko, lakini wengine walisema kuwa ushirikina ni Uchawi. Bibi Kotilda dhamira yake ilichanganyika na woga wa kizazi kipya kinachosema mtu anayefuata miiko ni mchawi. Kwa dhati ya

moyo wake anaamini kuwa miiko si uchawi wala ushirikina. Walisema ushirikina ni imani ya kuamini mambo ya zamani.

Mtafitiwa mwingine alisema kuwa Wabungu wana imani ya ishara mbali mbali kama:

- Bundi akilia karibu na nyumba yako anaashiria msiba.
- Kuku mweupe akikurukia begani au kichwani anaashiria bahati au kupanda cheo
- Kiganja cha mkono wa kushoto kikikuwasha katikati utapata pesa au kitu kizuri
- Kiganja cha mkono wa kulia kikikuwasha katikati utatoa pesa au kupoteza kitu kizuri.

Mawazo haya yalishadidiwa na watafitiwa wengine na kumfanya mtafiti kuongeza baadhi ya imani hizi ambazo hazikuwa lengwa katika utafiti huu wa kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

Maelezo haya yanaonesha kwamba, watafitiwa wengi wana uelewa mzuri kuhusu uhusiano au tafauti ya miiko na ushirikina. Watafitiwa wengine walionesha hali ya kuchanganya miiko na ushirikina. Hali hii inajitokeza pia katika kitabu cha Swahili Sayings – 2 (Farsi, 1965).

Mtafiti anaona kuwa kuna haja kubwa ya dhana hizi mbili kubainishwa kwa kinagaubaga ili jamii yote ielewe tafauti za msingi kati ya miiko na ushirikina. Aidha mtafiti anaona kuwa, ushirikina ni imani wakati miiko ni makatazo mbali mbali

kutoka katika jamii. Mtafiti anaona kuwa miiko na ushirikina ni vitu viwili tafauti. Nadharia ya Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao, pia inatuongoza katika kuifikia Nadharia ya kila Jamii ina Ujumi Wake. Mtafiti anaona kuwa wakati umefika wa wanataalimu kuielezea jamii dhana za kupenda bara lao, nchi yao, maskani yao bila kuusahau utu wao – utamaduni uliowaleya wao na babu wa babu zao (Sengo, 2009).

Kwa mujibu wa (Farsi, 1965), yeye alichanganya miiko na ushirikina. Hivi vyote ni vitu muhimu sana katika utamaduni wa Wabungu. Mtafiti anaona ni vizuri vikumbo vyote vya sanaajadiiya vikabaguliwa kufuatana na umuhimu na kazi zake katika sanaajadiiya. Kwa maana hii, ni vizuri miiko ijadiliwe tafauti na ushirikina. Kwa sababu miiko ni makatazo yenye ulimbe katika jamii na ushirikina ni imani ya kuona, kusikia au misisimko ya mwili kutoa ishara ya neema, baa au kutokea kwa kitu kizuri au kibaya katika jamii au kwa mtu binafsi (Vuzo na Amina, 1989).

Kwa mujibu wa ndugu Omari Mohamed na Prof. Sengo (Mzungumzo 11/09/2012), Ushirikina ni neno lenye asili ya Kiarabu *Shirik* likimaanisha kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Wakitowa mifano kutoka katika vitabu vitakatifu vya Wakristo na Waislamu wanasema, Mungu alimpa Musa amri ya kupiga maji kwa fimbo na maji yakaacha njia wana wa Israeli wakapita ndani ya bahari kavu hapa kuna ushirikiano kati ya Mungu na mwanadamu.

Wanasema kuwa, wanataalimu na waandishi wa makamusi wamewakengeusha watumiaji wa Kiswahili kwa kuwapa neno lisilo na mashiko sahihi katika jamii.

Mwanafasihi (Farsi, 1965), naye amekengeuka na kuongeza utata katika matumizi ya neno ushirikina anapoziweka baadhi ya semi za Kiswahili katika kundi la ushirikina. Mtafiti anaona kuwa kubagua vikumbo hivi kutasaidia kuondoa mkanganyiko wa kimsamiati kwani hadi sasa tafsiri katika Kamusi zetu za Kiswahili bado hazitoi mifano maridhawa ya kubainisha tafauti za vitomeo hivi. Utafiti huu uwe chimbuko la tafiti nyingine za kubainisha tafauti baina ya miiko na ushirikina.

## 5.4 Maana ya Maadili

Suala la maadili limeelezwa katika sura ya tatu. Mtafiti ameeleza kuhusu kukengeuka kwa maadili na kwa hali hiyo mtafiti alihitaji kuwahoji watafitiwa kama wanajua lolote kuhusu maadili. Suala la maadili halikuwa na majibu marefu isipokuwa mtafiti aliulizwa, "je, wewe mtafiti huoni kuwa watoto wa siku hizi hawana adabu?" Watoto na hata watu wazima siku hizi hawana heshima kabisa. Mtoto anamwona mzee anakuja au amebeba mzigo, hawezi hata kumpisha njia licha ya kumsaidia mzigo hata kama anamfahamu au anaelekea njia moja na mzee huyo. Hali hii inasikitisha sana. Mzee mwingine akitoa mfano alisema, "ni mwiko kwa mtu kupita katikati ya watu wanaoongea". Siku hizi hili si jambo la ajabu. Mtoto au mtu mzima na akili zake anaweza kuwapita watu wazima katikati hata bila ya kuwaomba radhi. Licha ya hayo watoto wanaonekana kuchukia hata kukaa vijijini wanataka kwenda Mkwajuni au Mbeya. Hawapendi kwao. Mkataa kwao ni mtumwa. Mzee huyu aliongeza aliongeza.

Mtafiti alielezwa kuwa, heshima huonekana kwa urahisi kutoka kwa watoto kwenda kwa wakubwa. Mtoto anapomsalimu mtu mzima, anapaswa kusimama na

kubadilishana salamu. Mtoto kumsalimia mtu mzima akiwa anaendelea kutembea ni kukosa adabu. Kwa upande mwingine hali hii huonesha uhalisiya wa tabia ya wazazi au watu wazima katika jamii. Mzazi ni mlezi wa kwanza wa mtoto anayeweka misingi ya utu bora wa mtoto. Jamii huuleya huo utu bora wa mtoto huyo. Mtoto akifanya kosa mahali popote, basi mtu mzima aliyemwona akifanya kosa hilo atachukuwa hatua ya kumkanya papo hapo bila kumsubiri mzazi wake. Mzazi ataambiwa tu kosa la mtoto na adhabu au onyo alilopewa mtoto huyo. Hali hii ililinda maadili ya jamii ya Wabungu, sasa kila mtu ni msomi, anajua kuleya watoto wake na hali kama hiyo.

Maadili ni kufuata masharti, amri au makatazo kutoka kwa wakubwa katika jamii ya Wabungu. Mwiko ni amri, sheria na utaratibu wa maisha. Madhara ya kuvunja mwiko hayaji siku moja, kwa kuvunja mwiko. Mathalani, mwiko unaomkataza mwanamke kuoga ziwani au mtoni madhara yake yataonekaka baada ya muda mrefu na si madhara ya papo kwa papo. Madhara ya miiko yanaweza kuwa ni kwa jamii nzima na si kwa mtu mmoja aliyevunja mwiko, bwana Joseph alisisitiza. Ukweli wa mawazo haya unapatikana katika nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi Wake, mapisi na ulimbe wa jamii ya Wabungu upo Ubunguni. Jambo la kukumbuka ni kuwa Elimu ina kwao na kwao ni Ubunguni.

Watangulizi wanataalimu akina Plato na mwanafunzi wake Aristotle, waliyaona na kuyajadili haya maadili kwa kina. Katika zama hizo na hata leo bado jamii ya Wabungu inakabiliana na matatizo katika jamii. Katika Kila Jamii ina Ujumi Wake, Waafrika, Wajaluo, Wanyakyusa, Wamatengo na hata Waswahili wa Uswahilini, wanapaswa kuurejelea utu wao. Mapisi yao, fahari yao kuwa wao ni waafrika na

wana Fasihi yao, Ilimu yao na makuzi yao yenye mizizi katika Afrika yao. Mwiko wa malezi bora ya Mgiriki yanaweza kuwa tafauti na mfumo wa malezi bora ya Kibungu, Kinyakyusa, au Kikwere. Hii ni kwa sababu ulimbe, mazingira, itikadi na ada ni tafauti. Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao na kwao ni Ubunguni.

### 5.4.1 Wajibu wa Wazazi Katika Kuwafundisha Watoto Wao Miiko

Mzazi wa Kiafrika ana wajibu mkubwa sana katika kumfunza mtoto au watoto wake maadili mema. Hata hivyo, malezi ya familia kwa sasa yamekuwa hayana mwelekeo wa Kibungu kwa sababu wazazi hawawafundishi watoto wao miiko. Zao la hali hii ni kukengeuka kwa maadili. Wajibu wa kwanza wa elimu ya miiko ni kutoka kwa wazazi. Wazazi wanapowafundisha watoto wao miiko, wanawajengea misingi bora ya kuielewa miiko ya Wabungu, miiko ya familiya na miiko mingine watakayoisikia au kuambiwa kutoka kwa watu wengine katika jamii ya Wabungu. (Sengo, 2008; Lindgren, na Byrn, 1974; P'Bitek, 1972; Nchimbi, 1979).

Katika hatua za makuzi ya mtoto awaye yeyote jamii inayomzunguka huchukuwa nafasi kubwa. Wazazi wakiwa ni wanajamii wa kwanza katika kumwongoza mtoto asikengeuke. Sanaajadiiya ina kwao na kwao kunapatikana katika jamii. Mtoto hupata ujumi ndani ya jamii yake (Sengo, 2009).

Ikumbukwe kuwa ukweli ni kama mwitu usio na njia. Mtu awaye yeyote hawezi kutoka humo bila ya yeye mwenyewe kuamua. Kila wakati mtu hutumia misingi ya kutoka ndani yake anamoamini katika kujenga mwega wa maamuzi yake. Mawazo hujengwa na uzoefu. Kama mtu hana mwega wa uzoefu wa aina yoyote, hawezi

kujenga hoja ya kukubali au kukataa kuwa kitu hiki ni kizuri au ni kibaya. Mzazi ni msingi wa mawe wa fikra, imani, maono na baadaye tabia na maadili mema ya mtoto. Kwa Mbungu mtu asiye na mwiko ni sawa na mtu asiye na maadili wala malezi kutoka katika jamii yake. Mbungu asiye na mwiko ni sawa na kusema kuwa, Mbungu asiye na adabu. Kukataa jambo moja ni kukubali jambo la kinyume chake. Kama ni mwiko kuvaa nguo fupi, ina maana ni vizuri kuvaa nguo ndefu.

Wazazi wa leo wamesahau wajibu wao kama wazazi. Wazazi wanafikiri kuwa kuwakanya watoto wao kwa kutumia miiko ya Kibungu kutawafanya kuonekana kuwa wamepitwa na wakati. Katika ngazi ya familiya mtoto hakufundishwa kwa viboko. Mtoto wa Kibungu alifundishwa maadili kwa kuona matendo ya watu wazima na maneno ya kuwaambia watoto wao. Maneno hayo ni pamoja na miiko. Sasa wazazi wanavaa nguo fupi au za kubana kana kwamba vitambaa vimekwisha madukani. Watafitiwa walitoa mawazo yao kuhusu mavazi na kubainisha kuwa siku hizi wazazi hasa wanawake, mavazi yao hayaleti picha nzuri au mfano mzuri kwa watoto. Kwa hiyo, hakuna uwezekano wa mtoto kumsikiliza mzazi juu ya uvaaji wake usiofaa kwa kuwa tayari mzazi huyo hatoi picha njema kwa mwanawe. Maelezo haya yanashadidiwa na methali za Kiswahili zinazosema, saamaki mkunje angali mbichi na mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Huu ni wajibu wa wazazi kuhakikisha kuwa wanawakuza watoto wao kwa kufuata misingi bora ya maadili na miiko ya Kibungu.

### 5.4.2 Wajibu wa Jamii katika Kufundisha Miiko kwa Watoto

Kwa kuwa wanajamii ya Kiafrika wana wajibu mkubwa wa kufundisha maadili katika jamii nzima, mtafiti wa kazi hii alitarajia kuwaona wengi wakiwa mstari wa mbele katika kuhimiza na kuhamasisha tabia njema kwa vijana wao wa kike kwa wa kiume. Lakini hali ya mambo si hivyo ilivyo, kwani wazazi wengi wamekuwa mfano mbaya wa malezi ya watoto wao, hasa katika suala la mavazi na kujiheshimu. Tangu zama za utangu, jamii ya Wabungu haikuishi katika ombwe kwa hali hiyo, mtoto hakuishi au hakulelewa na wazazi wake peke yao. Mtoto akizaliwa wazazi wake wakuu ni jamii inayomzunguka.

Jamii ya Wabungu ina mhimili mkubwa sana katika malezi ya watoto kwa ujumla. Mtu mzima awaye yeyote ni mwalimu kwa wote walio wadogo. Ilikuwa ni aibu kwa mtu mzima kuambiwa amekosa na mtoto mdogo. Hali hii ina maana kuwa katika jamii ya Wabungu, kila wakati mtu mzima alitarajiwa kuwa ni nuru ya wadogo, kurunzi ya maadili mema katika jamii. Watu wazima walipaswa kuwaelekeza, kuwaongoza, kuwafundisha na kuwakemea watoto wadogo wanapokosa. Ni wajibu huu wa jamii ya Wabungu, ndio uliomfanya mtu mzima kuonekana hawajibiki katika malezi ya jamii. Kama mtu mzima atafanya kosa ambalo lilipaswa kurekebishwa na mtu mzima (P'Bitek, 1972; Achebe, 1958; Sengo, 2008).

Hali ya sasa ni tata. Watoto wamekuwa wakijilea na kujiongoza katika mazingira yote. Watoto katika vijiji vya Mwambani na Udinde hawafundishwi kwa kutumia miiko. Kwa mujibu wa mtafitiwa mzee Paza, yeye alisema kuwa wazazi siku hizi, kwa sababu ya uvivu wao hawajishughulishi na malezi ya watoto. Watoto wanaweza

kuleta kitu cha gharama nyumbani na mzazi haulizi kuwa mtoto amekipata wapi kitu hicho. Kama ni msichana labda ameleta kitu basi mzazi anakaa kimiya hadi mtoto anapata mimba ndipo anapojifanya kushtuka. Mimba ni nafuu, lakini akiletea UKIMWI nyumbani basi mzazi atauguza mpaka afe. Tatizo hili si la mtoto bali ni la mzazi. Mtafiti anakubaliana na maelezo ya mtafitiwa na anaona kwamba ipo haja ya kuchukua hatua za makusudi kudhibiti hali hii.

### 5.4.3 Wajibu wa Viongozi Katika Kuwafundisha Miiko Watoto

Sasa viongozi wamejikita katika kutoa adhabu kwa makosa yanayotendeka kijijini. Miiko inayotolewa na viongozi ni vitisho vya mahabusu ambazo hata asili yake hawaijui. Viongozi wamekuwa ni wasomi zaidi kwa kurejelea miongozo ya Kipolisi na kujifanya Miungu watu. Hii ni hali halisi katika kijiji cha Udinde anabainisha mtafitiwa katika maelezo yake. Fundisho linalopatikana katika mfumo huu ni kukengeuka kwa maadili kunakosababishwa na viongozi kufuwawisha miiko. Miiko inayoangaliwa ni ile miiko ya viongozi ya mwaka 1971. Ni mwiko kwa kiongozi kula rusha na sasa wamegeuza rushwa kuwa chakula kwa sababu hawajuwi asili ya miiko hiyo na athari zake katika kuujenga utu wa Wabungu. Katika kazi tangulizi pia mtafitiwa mmoja alikumbuka miiko ya viongozi kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa TANU wa mwaka 1971. Mwongozo huu unasema kuwa RUSHWA na adui wa haki, sasa imekuwa ni kinyume, rushwa ndiyo imekuwa nguzo ya haki batili inayodhulumu na kuficha ukweli ambao ndiyo haki (Chenya, 1998; Msokile, 1990) wanashadidia suala hili.

Tangu utangu, kuwa kiongozi, kulikuwa na maana ya kuwa mtu mwenye Adabu, Maadili, Mtunza siri, Mpatanishi na si mchonganishi, si mwongo na si mtu wa sifa za ndumila kuwili. Kiongozi ni mchapakazi. Kiongozi hana muda wa kupumzika ufukweni au mtu wa njoo kesho. Kiongozi ni mja wa watu. Wakati wote huwafikiria watu wake na si kufikiria kujilimbikizia vijisenti ughaibuni. Kiongozi hakupimwa kwa alicho nacho. Kiongozi alipimwa kwa utu wake. Kiongozi ni mtu wa watu. Kila wakati alifikiria watu wake kwanza. Huyu ndiye kiongozi wa Wabungu.

## 5.5 Miiko Yenye Maadili

Katika sehemu hii mtafiti amebagua na kuchambua miiko kwa kutumia maelezo kuntu ya maadili. Watafitiwa walibainisha maana na mitazamo yao kuhusu maadili, hali kadhalika mtafiti alitowa mawazo yake kuhusu maadili ya Wabungu.

### 5.5.1 Miiko ya Chakula

Kwa mujibu wa mtafitiwa bwana Liberatus, kuvunja mwiko wowote ni kukosa adabu. Alimweleza mtafiti kuwa, hakuna mwiko wa maadili mema na miiko mingine isiyo ya maadili. Akitoa mfano wa mwiko wa wanawake wajawazito kukatazwa kula baadhi ya vyakula kama mayai, Liberatus alieleza kwamba kunasababisha matatizo kwa jamii - dalili ya mvua ni mawingu. Kama mwanamke atavunja mwiko huu kwa makusudi, basi madhara hayatakuwa kwa mvunjaji wa mwiko tu bali msukosuko utakuwa kwa kila mwanajamii. Madhara ya kula mayai si mtoto kuzaliwa na upara tu. Hapa tatizo laweza kuwa kubwa na kusababisha hata kifo kwa mama, mtoto au wote wawili mama na mtoto.

Wanataalimu (Sengo, 2008 na P'Bitek, 1972), wanafafanua kwa kina maelezo haya. Wanasema, heshima na adabu haviombwi. Mambo haya hayapatikani Uzunguni, kwa nini kuwarejelea watu waso na mizizi katika jamii ya Wabungu ambayo kwayo watu hawa wana Ujumi Wao ambao ni tafauti ili kuwapatia Wabungu ufumbuzi wa matatizo yao? Afrika ni chimbuko la elimu ya sasa. Hakuna mazungumzo yaliyo katika ombwe. Lisemwalo lipo, kama halipo basi lingoje laja. Sasa wanataalimu wanahitaji kulipeleka yai katika maabara ili kuthibitisha ukweli wa kuwa mwanamke mja mzito kula mayai ni mwiko. Ulimbe katika jamii za Kiafrika umejengwa katika imani ya Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao. Kitu cha msingi ni kuamini ukweli. Ukweli wa kujiamini kuwa taalimu ni kweli. Sayansi ina mipaka lakini imani ya asili haina mipaka anashadidia maneno haya (Mbiti, 1969).

Tabia nzuri inatokana na matendo ya mwanajamii. Mtu au mtoto mwenye tabia nzuri ni yule anayesikiliza miiko au miongozo na anawasaidia wenzake hasa wakubwa. Watafitiwa walimpa mfano mtafiti Kuwa, Wabungu wana mwiko unaosema kuwa, mtoto aliyebalehe au miaka karibu ya balehe ni mwiko kulala nyumba moja na wazazi wake. Kwa kuangalia kijuu juu unaweza usipate maana ya mwiko. Miiko ina kwao na kwao ni Ubunguni. Miiko ya Mmwera kwao ni Umwerani.

Hapa jamii ya Wabungu haihitaji wanataalimu ili kuchukuwa sampuli za aina yoyote na kuzipeleka Dar es Salaam kwa mkemia mkuu ili kuthibitisha kuwa ni mwiko kwa mtoto aliyebalehe kulala nyumba moja na wazazi wake. Maadili ya watoto hayapimwi kwa mizani ya kunyumbuka wala mizani ya mawe. Huu ni Ukweli, Kila Jamii ina Ujumi Wake. Mbungu katika mazingira yake na anavyomleya mwanawe ili

asijejuwa na kuanza kutaka kufanya mazoezi ya vitu ambavyo bado hajafikiya muda wake, basi mtoto alitengwa kutoka katika zizi kuu ili kuacha maisha ya wazazi yaendelee kama zamani bila kuathiri Mwenendo wa watoto wao.

Kila Jamii ina Ujumi Wake unapingana na maisha ya wazazi kulala nyumba moja na watoto wao. Kulala katika chumba kilichotenganishwa kwa pazia au karatasi zito na kusababisha watoto kusikiliza umbeya wa usiku. Katika mzingira haya ya chumba kimoja huwezi kumlaumu mtoto kusema matusi ambayo hapa tunasema ni mwiko. Swali la kujiuliza ni kuwa je, ni nani aliyeuvunja mwiko, ni mtoto au wazazi? Hapa mtoto anasingiziwa kuwa hana maadili kwa sababu tu hana mahali pa kusemea. Mtoto mchanga wa Mbungu hulala na mama yake kifuani wakati mtoto wa mzungu hulazwa mbali na wazazi ndani ya kikapu.

Kwa Mbungu, mkwe kulala nyumba moja na mkamwana wake ni mwiko mkubwa. Hii si heshima, haya si maadili ya Kibungu. Msingi wa mwiko kama huu hauhitaji mwanafalsafa wa Kigiriki au Kiyunani kumrejelea ili kuthibitisha kama ni kweli au laa. Kwa nini Wabungu wasimrejelee mzee Sengo, mzee Sigonda, Mzee Bangu au bibi Zazi Mwalego Sigonda. Je, ni kwa sababu wao ni Watanzania au kwa kuwa wengi wao hawana Shahada ya Uzamivu hivyo hawajuwi hata yanayoihusu jamii yao?

Ukweli wa miiko hii yote utapatikana katika falsafa za Ubunguni, Tanzania, Uswahilini, Uluguluni au Afrika tu. Huko ndiko kwao, wao ndio wanaoujua Ujumi wao. Elimu ina kwao, huko ndiko utakakopata sababu, ulimbe na msingi wa maadili yanayojengwa na mwiko huu. Ukienda Roma wewe ni mgeni usilete ujuvi, kwa nini Mzungu akija Ubunguni awe mwalimu wa Utu, Utamaduni, Mila na ada za

Wabungu? Maadili ya Mbungu yatabaki kuwa ni tunu na Ujumi wa Mtu Mweusi, (Sengo, 1985 , Kisanji, 2010).

### 5.5.2 Miiko Kuhusu Wizi Katika Jamii ya Wabungu

Katika mazungumzo kuhusu wizi katika jamii mtafitiwa, Mzee Thomas alieleza kwa masikitiko makubwa kuhusu tabia ya wizi. Alimwambia mtafiti kuwa Wizi ulikuwa ni mwiko mkubwa kwa Mbungu. Kuiba lilikuwa jambo baya sana. Siku hizi hata mtoto mdogo anaanza kujifunza wizi kwa sababu ya fedha na elimu. Hizi ni dhana mbili changamano. Elimu ni muhimu na fedha ni muhimu na kila moja ina nafasi yake katika jamii. Kwa Mbungu wizi ni tabia mbaya, ni kuvunja mwiko. Madhara ya wizi yanaweza kuwa halali katika jamii nyingine, lakini ni haramu kwa Mbungu kwani mwizi hana nafasi katika jamii ya Wabungu. Wizi Ubunguni si kwao.

Watafitiwa walitoa mfano wa wizi kwenye Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Pamba Wilaya ya Chunya, wenyeji waliita ”ushirika”. Kwa kauli yao watafitiwa wote walisema kuwa makarani wote wa Ushirika walikuwa wezi. Hata vijana waliozaliwa hapo kijijini ambao wazazi wao walijulikana na hali yao ya maisha ilijulikana, ghafla baada ya kupata kazi ya kununua pamba kutoka kwa wakulima, maisha yao yaligeuka na kuwa watu wenye pesa kuliko hata madaktari au walimu ambao walifanya kazi katika sehemu mbali mbali hapo wilayani hadi wakastaafu wakiwa masikini Pio, Yozofina, Zazi, Mahella na wengine wengi walishadidia jambo hili.

Kutokana na maelezo ya watafitiwa mtafiti anaona kuwa hali ya sasa ya kukithiri kwa wizi wa mali ya umma hata ya mtu mmoja mmoja ni matokeo ya kufuwawa

kwa miiko katika jamii. Jamii haijali tena wala kujishughulisha na miiko mbalimbali ambayo ililinda utu wa jamii nzima. Matokeo ya utafiti huu yanaamsha ari ya kutaka kuihuisha miiko ya jamii mbali mbaili ili kuiepusha na zahama inayoinyemeleya. Mtafiti katika suala la elimu anaona kuwa elimu inapaswa kuwa taa, kioo, mfano kwa jamii. Watu waliosoma wanapojiingiza katika ufisadi, wizi na uporaji wa haki za watu ndio wanaosababisha elimu kuonekana kama chimbuko la uhalifu na uchafu. Mtafiti hawezi kuwazuwia watu kusema wanavyoiona elimu, bali wasomi wanapaswa kuionesha jamii waishimo, wafanyiamo kazi na dunia kwa ujumla kuwa wao ni waadilifu na hawajakengeuka kimaadili bali wanaijua miiko na kuienzi. Elimu ni ufunguo wa maisha.

### 5.5.3 Miiko ya Kutamka Maneno

Katika mazungumzo baina ya mtafiti na mtafitiwa, mtafitiwa alisisitiza kuwa maadili yanajikita katika shughuli zote za kijamii. Kama mtoto anakatazwa kufanya jambo na akalifanya huko ni kukosa maadili. Zamani Mbungu alikatazwa kutukana, kufanya hivyo ilikuwa ni kumkosea adabu Mbungu mwenzake na mtu mwingine aliyesikia tusi hilo. Sasa kuna watu wanatoa matusi hadi yale ya nguoni hadharani bila ya shaka yoyote. Huku ni kukosa maadili mema. Kila katazo lilikuwa na maana katika jamii ya Wabungu. (Allan na wenzake, 2006). Mtafiti anakubaliana na madai ya mtafitiwa kwa kuwa hali hii kwa sasa inasikitisha. Wazee kwa vijana siku hizi hawaoni haya kutamka mbele ya wenzao matusi ya nguoni. Wabungu wameacha kutumia tafsida kabisa katika mazungumzo yao, labda ni kwa sababu ya utandawizi wa ukweli na uwazi. Imekuwa ni jambo la kawaida kusikia matusi yakitumiwa kama wasifu. Katika jamii ya Wabungu mtu aliyekuwa na tabia ya kutukana alikuwa

hawezi kuoa au kuolewa na Mbungu mwenzake kwa sababu alichukuwaliwa kuwa ni mtovu wa nidhamu.

### 5.5.4 Miiko na Mazingira

Watafitiwa walimweleza mtafiti kuwa vifo vya watoto vinasababishwa na wazazi kuvunja miiko. Waliongeza kuwa watoto wanakufa, maji yanakauka mitoni na katika chemchemi na hata mvua inaacha kunyesha hii yote ni kwa sababu ya watu kukosa maadili ya kuwasikiliza wakubwa. Hii ina maana kuwa kuna miiko imevunjwa na Wabungu wanahitajiwa kumrudia Muumba wao na kumwomba radhi kwa makosa waliyoyafanya.

Watafitiwa walisema kuwa, zamani wazee walikwenda kufanya tambiko la kuomba radhi katika eneo maalumu la mlima unaojulikana kwa jina la “Kwimba”. Ibada maalumu ilifanywa na watu waliotumwa na Mwene kufanya tambiko hilo. Mara baada ya ibada hiyo, msamaha ulitolewa na watu walipata mvua hata kabla ya wajumbe waliotumwa mlimani kurejea nyumbani. Aidha kama ni samaki, basi samaki walianza kupatikana kwa wingi.

Siku hizi mambo si hivyo, ukiwaambia wanawake ni mwiko kwenda kuoga ziwani au mtoni au kwenda na chombo chenye masizi wanamwona mzungumzaji kuwa yeye ni mshamba na amepitwa na wakati. Mtu akiambiwa ni mwiko kukata miti katika eneo fulani, watu wanaingia na kukata mti hiyo kana kwamba wanaikomoa jadi na kusahau kuwa wanajikomoa wenyewe. Watafitiwa waliweka bayana maelezo haya kwa mtafiti. Hata hivyo mtafiti anaona kuwa dhima iliyojikita katika mwiko

huu ililenga kulinda na kutunza mazingira na mali asili iliyomo. Na kwamba iwapo hali hiyo ingedhibitiwa huenda jamii ya Wabungu na Watanzania kwa ujumla wasingeshuhudia uharibifu mkubwa wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu (Masalu, 2010; Chisenga, 2002).

### 5.5.5 Mwiko wa Kumpita Mtu Mzima na Mzigo Bila Kumpokea

Kutokana na maelezo ya watafitiwa mtafiti anaona kuwa mwiko huu ulibeba falsafa njema sana. Ulikusudiwa kuwafundisha vijana adabu njema na kuwa watu wenye msaada kwa jamii yao. Heshima iliendana na rika na umri, kila wakati wadogo walipaswa kuwaheshimu watu wazima. Kuwasaidia wazee zamani lilikuwa ni jambo la wajibu.

Watafitiwa walisema kuwa zamani ilikuwa ni mwiko kwa mtoto kumpita mzee mwenye mizigo bila kumpokea. Mdogo yeyote alipaswa kubeba mzigo wa mzee hadi mahali anapoishia na kumwacha mzee aendelee na mzigo wake. Mtafiti akizungumza na bibi Paskalia, mwenye umri wa miaka sitini na tano, alimweleza mtafiti kuwa, hali hii siku hizi haipo kabisa. Vijana hawawasaidii wazee hata kama wanawafahamu wazee hawa na wanaongozana nao njia moja.

### 5.5.6 Mrejesho wa Miiko Wanayofundishwa Watoto Salamu

Mtafiti alimhoji mtafitiwa mmoja kama anawafundisha watoto wake miiko hii. Mtafitiwa alijibu kuwa anawafundisha watoto wake, lakini kwa kuwa watoto wengi wamekengeuka, basi mazingira yanawafanya watoto kutokufuata maelekezo ya

wazazi. Lakini kama kuna mtoto anayesikiliza maelekezo na kufuata basi lazima mzazi atapata habari kutoka kwa watu wengine kuwa, mtoto ana tabia nzuri. Hawezi kumpita mtu bila kumsalimu au kumsaidia mzigo. Bibi alisisitiza kuwa siku hizi dunia imegeuka na watoto hawawasaidii wala kuwasikiliza wazee. Katika mazungumzo hayo mtafiti aligundua kuwa, hakuna mrejesho wa moja kwa moja kwa tabia nzuri au mbaya ya mtoto. Katika mazungumzo baina ya watu wazima ndipo ukweli wa maadili ya wanajamii huwekwa wazi. Hii ni kama kumshukuru mzazi husika kwa malezi bora ya mwanawe. Hakuna siri katika kuzielewa tabia za wanajamii (Sengo, 2008).

Mtafiti akiwa katikati ya mazungumzo, kijana mmoja alipita na kusalimia akiwa anaendelea kutembea. Bibi alitumia nafasi hii kuonesha mfano halisi wa tabia mbaya. Alisema;

> *"Kijana huyu kwa umri wake (kama miaka ishirini hivi) alipaswa kusimama na kusalimia kwa heshima kwa kupiga magoti na si kubonyea tu au kama anataka kukusitua na kuendelea na safari"*.

Mtafiti aligundua kuwa kijana huyo aliposalimia Mzee Thomas na bibi Paskalia hawakuitika salamu hiyo. Mtafiti alikuwa wa kwanza kuitika na vijana wengine waliokuwapo mahali hapo. Miiko ina kwao.

Mtafitiwa alimweleza mtafiti kuwa, zamani wao walifundishwa na wazazi wao kuhusu tabia njema. Kwa mfano kama kijana anafuatana na mtu mzima na kijana anamwacha mtu mzima akiwa amebeba mizigo basi atafokewa na mzazi au mtu mzima mwingine yeyote kuwa kwa nini anafuatana na mtu mzima bila ya kumpokea mzigo, hiyo ni tabia mbaya na ni kukosa maadili. Mtoto alipaswa kusikiliza na

kuomba radhi kwa kosa hilo. Umbali wa kusaidia ulikuwa si hoja, suala lilikuwa ni kutoa msaada kwa wazee wanapokuwa na kazi. Haya yalikuwa ni mafundisho kwa wote. Kila mzazi aliwajibika katika kutoa malezi bora kwa wanawe na watoto wote Ubunguni.

Kabla ya kumaliza mazungumzo na mtafitiwa huyu, kijana mwingine (alikuwa na umri kama miaka ishirini pia) alipita na kusalimia kwa kituo. Alisimama, akashuka katika baiskeli, akapiga magoti na kusalimia. Mtafiti akiangalia muda salamu ilichukua kadiri ya dakika tatu. Na baada ya kuondoka mtafitiwa alimweleza mtafiti kuwa;

> *"Sasa umeona mfano wa tabia njema. Mtoto anasalimia na unapata nafasi ya kujua habari za nyumbani. Watoto wengine wanasalimia kana kwamba mmelala nyumba moja. Hata kama mmelala nyumba moja mnapaswa kusalimiana kwa kituo, Usiku ni Mwaka" alimalizia.*

Ulimbe unaojitokeza katika salaamu unahusiana na uhai. Kwa mfano, Waafrika ni watu wanaoheshimu sana masuala ya uhai na hivyo kusalimiana ni jambo la msingi sana, tafauti na wazungu. Salamu ziliwafanya wanajamii kupata habari kamili za afya na misiba kwa urahisi tafauti na ilivyo sasa ambapo watu wengi hawasalimiani kwa kituo.

### 5.6 Mtazamo wa Watu Wazima Kuhusu Ulimbe wa Miiko ya Wabungu

Mtafiti aliwahoji watafitiwa kuhusu ulimbe wa miiko. Watafitiwa hawakuwa na majibu ya moja kwa moja kuhusu ulimbe wa miiko. Kwanza watafitiwa wote walieleza athari za kuvunja miiko. Maelezo ya Thomas na Joseph yalishadidiwa na bibi mmoja kuwa zamani kwa wanawake ilikuwa ni mwiko kabisa kwenda kuoga au

kufanya shughuli zozote ziwani. Bibi huyu aliongeza kuwa zamani ilikuwa ni mwiko kwa mwanamke kwenda kusafisha chombo chenye masizi kama chungu au sufuria linalotumika kupikia ziwani. Aidha watafitiwa walimweleza mtafiti kuwa watu wanapovunja miiko inayohusiana na kwenda kuoga ziwani basi samaki waliadimika kabisa.

Watafitiwa walitoa mfano:

Hivi karibuni katika mwambao wa ziwa Rukwa upande wa Mashariki, kulikuwa na uhaba mkubwa wa samaki na kila mara wavuvi walipokwenda ziwani kuvua usiku kucha walirudi bila hata na samaki wa mboga za kutosha familiya. Taratibu za kimila zilipofanyika zilizoambatana na ibada maalumu ya kimila, na kutengeneza dawa maalumu (Ipande) ambayo watu wote kijijini walipaswa kuilamba. Mara baada ya zoezi hilo kukamilika, ufukwe wote ambao wavuvi walikuwa hawapati samaki, walianza kupata samaki.

Watafitiwa walitoa mfano wa mwiko mmoja kuwa:

> *”Ni mwiko kwa mwindaji anapokuwa porini kuruka gogo la mti lililolala, kama mwindaji ataumwa na nyoka hawezi kupona kwa urahisi / atakufa. Mwindaji anapokuwa porini anapaswa kuzunguka mti wowote uliolala na si kuuparamia au kuuruka. Mwiko huu ulithibitishwa kwa matukio ya wawindaji ambao walikufa baada ya kuumwa na nyoka na baada ya kufuatilia wawindaji wenzao walisema marehemu waliruka mti uliolala na alikuwa ameonywa na wenzake kabla ya tukio la kuruka gogo”.*

Miiko ina kwao, mwiko huu kwao ni Ubunguni. Ulimbe wa mwiko huu ni ujuzi na utambuzi wa tabia za nyoka, hasa nyoka ambao wana sumu ambao tabia zao zinafanana mara nyingi nyoka hawa hujinyoosha na kulala sambamba na miti au magogo yaliyolala. Kumruka nyoka ni hatari kuliko kumpita mbele au nyuma yake.

Taalimu hii inapatikana Ubunguni. Mababu wa Wabungu walifanya utafiti na kuja na majawabu yenye kutoa mafunzo kwa karne zote zijazo. Mwanataalimu kutoka Uzunguni hawezi kuja kuwafunza Wabungu kuhusu mwiko huu.

Aidha mwiko mwingine uliotolewa mfano ni, "Mwiko kupiga mluzi usiku unaita nyoka". Wabungu wa asili, mababu zetu waliimanya sayansi. Si ulimbe wa kileo wa kutabii kutoka Uzunguni na kujimilikisha hata amali za jamii kuwa ni mali ya mtu binafsi. Waafrika wangalifanya hivyo labda hadi leo ulimbe ulioporwa na kwenda ughaibuni taalimu hii ingalikuwa na wachache tu. Nyoka anapenda muziki. Kwa kupiga mluzi usiku ukizingatia uhafifu wa mwanga, ni rahisi kuingia katika matatizo ya kuumwa na nyoka kwa kosa la kumwita nyoka wewe mwenyewe.

Mbungu mwanamke hakuruhusiwa kupiga mluzi, akiwa shambani, msituni akisenya kuni, au usiku. Kama huu ni urongo basi nenda Ubunguni na vunja mwiko ndipo utakapojua kuwa Miiko ina kwao na kwao ni Ubunguni. Suala zima si kupiga mluzi tu, bali pia ni utayari wa mwanamke kupambana na nyoka kama atajitokeza. Kwa kawaida mwanamume kila wakati alitembea na fimbo. Mwanaume aliyetembea bila fimbo alifananishwa na mwanamke aliyehitaji kulindwa na mwanaume. Silaha si lazima iwe bunduki. Mwanamume alipaswa wakati wowote aendapo safari au anapotembea nje au shambani awe na silaha mkononi, mundu (esengo) au bakora (enduwa).

### 5.6.1 Miiko na Mavazi

Mtafiti alielezwa kuhusu mwiko wa mwanamke kuvaa nguo fupi, nguo za kubana au nguo zinazoonesha gimba maungo ya ndani "*koulangezya outoupou*" kuonesha utupu. Pia mzee Thomas alibainisha kuwa mvulana au mwanamume kuvaa nguo

zinazobana na kuonesha gimba lake kuwa ni mwiko na ni matusi makubwa kwa Mbungu. Mtafiti alitaka kujua sababu za mwiko huu. Watafitiwa walikuwa na majibu mengi na hisia kali kuhusu mavazi.

Kwanza wote walieleza kuwa ni uhuni ni tabia za watu wa mijini. Bibi mmoja alitoa mfano wa mwanamke mtu mzima kuvaa suruali, afadhali iwe pana lakini suruali hiyo inabana na kumwonesha maungo yake kama alivyozaliwa. Picha hii si nzuri kwa watoto wetu na sasa wameleta tabia hiyo hata katika vijiji vya Mwambani na Mkwajuni.

Mtafitiwa mmoja alirejelea operesheni nguo fupi na za kubana mwanzoni mwa miaka ya sabini. Katika opareshni mavazi lilitolewa tamko kutoka kwa waziri mkuu wa wakati huo marehemu Mzee Rashid M. Kawawa, Mola amweke pema Peponi. Tamko hilo lilibainisha kuwa vazi lolote, gauni / kanzu, sketi kwa wanawake na wanaume kaptula au bukta ni lazima iwe na urefu wa kufunika magoti. Kama juu umevaa shati, gwanda au blauzi basi ni lazima iwe na urefu wa kufunika kiwiliwili bila ya kuonesha mgongo wala kitovu. Tamko hili liliihusu jamii yote ya Tanzania, kuanzia watoto wa shule za msingi, sekondari, vyuo pamoja na ndaki hadi wafanyakazi wa Ikulu wake kwa waume. Madhumuni ya tamko hili yalikuwa kuilazimisha jamii iliyokengeuka kimaadili hasa katika mavazi ili kuurudia utu wa Mtanzania. Wazee wa Kibungu waliufurahia sana uamuzi huu, kwani uliurudisha utu wa Mbungu.

Utu wa Mbungu unaonekana kwa namna anavyovaa gauni la marinda. Gauni linalofunika magoti. Mbungu havai taiti. Mbungu anavaa rinda la solo. Kunapokuwa

na msiba Mbungu bado utamwona katika mavazi yanayomsitiri maungo yake. Mama wa umri aliye na familia, basi huyu atakuwa na makenzi (kitenge). Mama wa Kibungu popote alipo nyumbani au kanisani. Msikitini au maskanini bado atakuwa nadhifu (P'Bitek, 1972; Sengo, 2008).

Ounsomeko (suruali) au kaptula pamoja na gwanda (shati) ni vazi la wanaume na vijana. Ounsomeko hauvaliwi na wanawake. Ounsomeko hauvaliwi nusu makalio na vijana. Ounsomeko hauvaliwi ukiwa umeng'ang'ania mwilini mpaka sehemu nyeti kukosa hewa kwa kubanwa na nguo. Vazi halikuvaliwa kwa makusudi ya kuonesha gimba la mtu. Huko si kusitiri mwili huko ni kuudhalilisha mwili. Mwili unahitaji hewa ya kadiri ili uweze kusitawi na kuepuka magonjwa kama ya kuvu.
Mbungu hakuzaliwa kutabii kila aonacho au akipendacho binafsi. Mbungu ana staha, (Janetius, 2009). Suala hili linashadidiwa katika sura ya tatu ya utafiti huu na (P'Bitek, 1972; Sengo, 2008). Taalimu ni kweli, ukweli wa Mbungu utaupata Ubunguni. Mzamivu wa elimu ya sanaajadiiya ya Wabungu ataipata Ubunguni na si Uzunguni.

### 5.6.2 Miiko Ubunguni Bado Inafundishwa kwa Watoto

Watafitiwa waliozungumza na mtafiti katika kijiji cha Udinde na kijiji cha Mwambani, wote walisema kuwa wanaitumia miiko. Walisisitiza kuwa katika mazungumzo na watoto au watoto wanapoagizwa kitu ziwani au shambani ni lazima kuwakumbusha miiko. "mnapokwenda huko angalieni msifanye hivi au vile, ni mwiko".

Katika kijiji cha Mwambani ni watafitiwa wawili  tu kati ya watafitiwa saba waliosema kuwa wanatumia miiko na wanawafundisha watoto wao miiko ya Wabungu. Watafitiwa wengine waliobaki walisema hawatumii miiko kuwafundisha watoto wao. Ingawa wote wanaona kuwa maadili ya jamii ya Wabungu yamekengeuka. Watoto hawana adabu na heshima. Mtafitiwa mmoja alisema kuwa sasa vijana wa kike kwa wa kiume wanabaka. Hili ni tishio kubwa kwa jamii na maisha ya wanyonge na usalama wa wanajamii kwa ujumla. Miiko ilikuwa ni mlinzi kwa wanajamii kwa wakati wote.

### 5.6.3 Mgongano wa Elimu ya Miiko ya Wabungu na Muziki wa Kisasa

Mzee Paza na wenzake walitoa mfano halisi wa vitu vinavyokengeusha maadili. Siku hiyo ilikuwa Jumapili ya tarehe 22 mwezi wa Nne mwaka 2012, karibu wanakijiji wote wake kwa waume pamoja na watoto wao walikuwa kilabuni wakiangalia wanenguaji wa muziki wakitangaza bidhaa ya Dawa ya Kusafishia Maji. Watafitiwa ambao walikuwapo mahali hapo, kauli yao kwa kifupi ilikuwa, “sasa wanawafundisha nini watoto wetu?”  Hapa mtafiti anaona kwamba swali kama hili linafanana na hoja ya msingi ya utafiti huu, “Kufuwawa kwa miiko katika jamii ya Wabungu, watoto wanakosa nini kimaadili?” hili ni tatizo katika jamii ya Wabungu.

## 5.7 Ulimbe wa Miiko ya Wabungu

Mtafiti akishirikiana na watafitiwa waliweza kujadili miiko mingi ili kubainisha mifano ya ulimbe wa miiko ya jamii ya Wabungu. Ifuatayo ni baadhi ya miiko ya mfano iliyojadiliwa:

- Ni mwiko kwa wanawake kwenda kuoga mtoni au ziwani, samaki wataadimika wakati wa kuvua.
- Ni mwiko kwa mwindaji akiwa mawindoni kuruka mti au gogo lililolala, akiumwa na nyoka si rahisi kupona.
- Ni mwiko kwa mvulana au msichana kuoa au kuolewa na kilema, watazaa mtoto kilema.

Mtafiti hapa anarejelea sura ya pili, nadharia ya Miiko ina kwao. Mwiko hutolewa na mwanajamii husika. Ulimbe wa kila mwiko kabla ya kutolewa mababu walichunguza matatizo yaliyotokana na jambo hilo kabla ya kuja na suluhisho la kudumu ambalo ni Mwiko. Kwa kuwa mwiko haupo katika ombwe, basi ni muhimu kwa mtu kuuheshimu na kuufuata. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yasiwafanye Wabungu kuuzika utu wao katika kaburi la sahau, eti kwa sababu ya binadamu kutengeneza gari au kurusha ndege na kusahau kuwa Mbungu alianza kufua mikuki hata kabla wa wageni kuja Ubunguni.

Miiko kamwe haipitwi na wakati ila watu ndio wanaokengeuka kupindukia. Kinachotakiwa kuchunguzwa na kutolewa maelezo kuntu ni ulimbe wa miiko na umbo la mwiko ni msaada wa kufikia ulimbe huo. Kwa mfano, wa mwiko wa mwanamke kuoga mtoni au ziwani, kama utahusisha na kichocho ugonjwa unaoweza kuua baada tu ua kuoga maji machafu. Athari za kichocho kwa mwanaume na mwanamke ni tafauti. Mwanaume atajitambua haraka kuwa ni mgonjwa kuliko mwanamke na kupata tiba haraka zaidi. Aidha mfumo dume wa kuwaacha wanawake kufanya kazi bila ya kupumzika. Mwanamke katika siku zake anapaswa

kupumzika ili kujisitiri na hali yake. Haya ni maumbile kutoka kwa mwenyezi Mungu.

Kama maendeleo yameshafunika shughuli za wanajamii basi ieleweke kuwa maendeleo ya kisasa ni sehemu ya sababu ya kufuwawa kwa miiko ya jamii ya Wabungu (Berry 2009; Masalu 2010). Mtafiti anaona kuwa bado kuna hima kubwa ya watafiti kufanya tafiti za kina za kifalsafa, kisanaajadiiya na kisayansi katika kubainisha ukwali huu.

### 5.7.1 Ni Mwiko kwa Wanawake Kuoga Ziwani au Mtoni, Samaki Watakimbia

*(i) Madhara ya kuvunja miiko ni kwa jamii nzima*

Uzito wa mwiko upo katika wanajamii ambao kwa kuvunja kwake kunaweza kusababisha matatizo katika jamii ya Wabungu, kama mtafiti alivyomnukuu bwana Joseph akimrejelea mtuhumiwa ambaye aliadhibiwa kwa kuwatukana waliomwonya kuhusu mke wake kuoga ziwani. Wakati wa adhabu ya viboko alisema ”mnaniumiza” jibu lilikuwa je, wewe unaona ni bora kuwaumiza wabungu wote? Mtuhumiwa hakuwa Mbungu lakini alikuwa ni mvuvi wa muda mrefu pale kijijini, hivyo alijuwa miiko ya uvuvi na bahari (ziwa Rukwa kama wenyeji wanavyoliita). Hivyo basi ulimbe uliomo katika mwiko huu, ni huu;

*(ii) Ulinzi na usalama wa wanawake*

Wanawake ni watu muhimu sana katika jamii zote. Kwa hali hiyo jamii ya Wabungu iliona umuhimu wa kuwalinda na hivyo kuwawekea miiko ambayo ingewalinda. Mito inayoingia ziwa Rukwa pamoja na ziwa Rukwa lenyewe, lina mamba wengi na

viboko ambao walikuwa na hadi sasa ni hatari sana kwa maisha ya wakaazi wote, hasa kwa watoto na wanawake. Kutokana na hayo, hii jamii ilihofia maisha ya wanawake kwani walikuwa hawawezi kujilinda. Ikumbukwe kuwa kila mara wanaume hutembea na silaha kama bakora, kisu, panga, au mkuki.

Unyago wa mtoto wa kike wa Kibungu unalenga malezi bora ya watoto na utunzaji wa nyumba. Ni kichekesho kwa kigoli kumfunda kungwi. Mtoto alifundishwa kila liwalo jema na wazazi na watu wazima. Shoka na panga kwa mwanamke wa Kibungu ni kwa ajili ya kusenya kuni au kupasua kuni. Mwanamke wa Kibungu hakufundishwa kutoa damu ya mnyama hata kuku. Kwa hali hiyo kila aendako mwanamke alipaswa kuchukua tahadhari kubwa ya usalama wake. Mwanamke wa Kibungu hatembei peke yake kama tembo mzee aliyekataliwa kundini. Kikongwe hadi kigoli, wote walipaswa kutembea katika vikundi (Sengo, 2009).

*(iii) Utunzaji wa ikolojia ya ziwa na mito*

Uvuvi ulikuwa ni shughuli kuu ya Wabungu. Kwa kutumia sababu ya kuadimika kwa samaki ilikuwa na uwezekano mkubwa wa kujenga hofu kwa Wabungu na kufanya watu wote kuhakikisha mwiko huu unafuatwa ili wasije wakakosa samaki. Mazalia ya samaki yanapatikana kando kando ya ziwa. Kwa mtazamo wa kisayansi, tunaweza kusema kuwa watu wa wakati huo wa zamani, walijua kuwa kama mazaliya ya samaki yataharibiwa basi moja kwa moja samaki watapotea au wataadimika kwani watakuwa wameharibu mazalia ya samaki.

Tukiangalia zama hizo, jamii ya Wabungu haikuwa na maji ya bomba. Mito na maziwa vilikuwa ni vyanzo vya maji katika uasili wake. Maradhi ya mlipuko kwa

wakati huo yalikuwa ni ndoto, kwa sababu ya miiko iliyolinda au kutunza sehemu ambazo zingesababisha maambukizi ya magonjwa. Elimu ya wazee wetu ilikuwa kubwa na yenye manufaa ya moja kwa moja kwa maisha ya jamii kuliko kisomo cha kisasa kingi kilichojaa uharibifu wa mazingira, hali na ukengeufu wa maadili.

*(iv) Utupu wa mtu mzima ni mwiko kuuonesha*

Kwa kuzingatia maumbile ya wanawake, si vizuri kukaa utupu mahali ambapo kila mpita njia atamwona. Sehemu za kuchotea maji yamkini ndizo ambazo wanawake wanaweza kuoga, na kwa mazingira yaliyoelezwa hapo juu kuhusu hatari ya mamba, basi ni dhahiri kuwa mwanamke atakuwa anaoga mahali ambapo watu wengine wote wake kwa waume wataweza kumwona kwa urahisi. Wabungu hawana jadi ya kuoga baharini pamoja na familia zao. Huku ni kukosa radhi (Allan na Burridge, 2006).

Kitendo cha mwanamke kuinama akionesha utupu, ilikuwa ni ishara ya kulaani. Katika mazungumzo ya mtafiti na mzee Thomas, mzee huyu alisisitiza kuwa hii ni laana. Hata kama mwanamke atainama na kuelekeza utupu wake baharini, basi hiyo ni laana kubwa. Jambo hili kwa Wabungu si kitu kizuri, kwani wanalinasibisha na hali ya kukengeuka kwa maadili kama mwanamke anakwenda kuoga baharini. Mtafiti anaona kuwa ulimbe uliokitwa ndani ya mwiko huu, ulikusudiya kulinda faragha ya utu wa mtu hasa mtu mwanamke. Kwa Mbungu si jambo la fahari kwa mwanamke mtu mzima kuonesha gimba sembuse kukaa na kuonesha utupu.

### 5.7.2 Ni Mwiko kwa Mwindaji Akiwa Mawindoni Kuruka Mti au Gogo Lililolala, Akiumwa na Nyoka si Rahisi Kupona

Katika mazungumzo baina ya Thomas na mtafiti, mengi yalijibainisha kuhusu ulimbe uliomo katika mwiko huu; Wabungu wanapokabiliwa na matatizo wanajua chanzo ni nini. Kwa mtafiti kukaa kijijini kwa mwezi au mwaka mmoja na akajifanya anajua kuliko Wabungu ni kichekesho. Mbungu anaposema ni mwiko kuruka gogo ukiwa mawindoni, ukiumwa na nyoka huwezi kupona kwa urahisi, ujue kuwa Mbungu anajua ulimbe na alishafanya utafiti. Utafiti wake aliuandika katika vichwa vya Wabungu. Utafiti huu ni mali ya Wabungu wote hivyo hawajajimilikisha kama utafiti wa Wazungu na kujiwekea hati miliki. Pia mazungumzo yalibainisha zaidi kuwa Wabungu wanajuwa kuhusu sifa kama ukali, upole au ni nyoka yupi ana sumu na yupi hana. Mtafiti alielezwa mambo mengi kama;

*(iv) Tabia za nyoka*

Katika misitu ya Ubunguni kuna aina moja ya nyoka mwembamba mrefu (kwa Kibungu anaitwa Kangaloukwi). Nyoka huyu ana sumu na tabia kama koboko. Mara nyingi hupenda kulala kando ya miti au magogo lililolala. Nyoka huyu ni hatari, kama mtu ataruka gogo ni rahisi kumkanyaga au kumstua na mvunja mwiko kuambulia kugongwa au kuumwa. Kama atapita mbali na nyoka huyu kwa kawaida hana madhara kwa mpita njia ili mradi asimstue.

Mwiko kama huu huwezi kuupata Uzunguni kwani wao hawana kadhia kama hii. Tabia za nyoka huyu zilijulikana na babu zetu tangu utangu. Leo mtu wa kuja anataka kuwafundisha Wabungu kuhusu ubora au ubaya wa miiko yao. Tabia njema ni kusikiliza miiko na kuifuata. Mbungu ambaye anavunja mwiko wowote hana

heshima na adabu kwani madhara ya kuvunja mwiko ni kwa jamii nzima na si madhara ya mvunjaji wa mwiko pekee.

### 5.7.3 Ni Mwiko kwa Mvulana au Msichana Kuoa au Kuolewa na Kilema, Watazaa Mtoto Kilema

*(i) Idhini ya kuowa au kuolewa*

Katika jamii ya Wabungu ilikuwa ni mwiko kwa kijana kujiamulia kuhusu kuchagua mchumba wa kuoa au kuolewa naye. Wazazi ndio waliokuwa na sauti ya mwisho juu ya uamuzi wa ndoa za watoto wao. Wabungu waliamini kuwa vilema vyote vinarithiwa na hii ni hali ya kiukoo. Kama kulikuwa na mtu mwenye kilema au ugonjwa wa kifafa, ukoma, ndui au zeluzele (albino), kuolewa au kuoa kutoka familia hiyo ilikuwa ni mwiko.

Paskalia na Federiko walieleza kwa mifano na kwa majina (hayakuandikwa popote katika utafiti huu) mzee mmoja aliona mwanamke Zeluzelu (Albino) hadi sasa watoto na wajukuu katika familia hiyo wanazaa watoto zeluzelu au wenye kuonesha dalili za kizelezelu. Sasa hii ni kama hadithi kwani mzee huyo aliambiwa naye alikataa akatengwa na familiya akahamia kijiji kingine pamoja na laana yake. Sasa wenyeji Wabungu wanasema ukoo wa Zeluzelu. Mkaidi hafaidi hadi siku ya Idi. Swali la kujihoji ni, Je, ni mtaalamu gani wa JINI na “Mutation” aliyekwenda Ubunguni zama hizo kuwafundisha Wabungu kuhusu; kama mtu ataoa zeluzelu basi atazaa watoto zeluzelu?

*(ii) Kurithiwa kwa maradhi kwa vizalia*

Kisayansi kulikuwa na ukweli mkubwa juu ya mawazo haya ingawa si maradhi yote yaliyodhaniwa kuambukiza yalikuwa yakiambukiza kwa kurithi kama ndui na kifua kikuu. Babu hawa hawakujua Kiingereza na ujuzi wa kufafanua jini za urithi kutoka kwa baba na mama mwenye matatizo kwenda kwa mtoto. Lakini waliweza kueleza kwa kutumia miiko. Miiko ina kwao na kwao ni Ubunguni na si Uzunguni. Ukitaka kuijua itakupasa uijuwe jamii ua uwajue Wabungu Ndani Nnje.

Wazee hawa, waliendelea kutoa mifano ya watu waliokufa kwa sababu ya kukengeuka kwa maadili ya kuikana miiko. Maradhi yaliyoelezwa ni kama Ugonjwa wa kuanguka (kifafa), Ukoma kwa Kibungu "iwala". Mtafiti alitaka kujua kama uganjwa wa UKIMWI nao umo katika kundi la magonjwa haya. Watafitiwa wote walikataa na kusema huo ni ugonjwa wa kisasa. Zamani hawakuwa na ugonjwa kama huo. UKIMWI ni ugonjwa ulioletwa kutoka mijini.

## 5.8 Viongozi Waonavyo Ulimbe wa Miiko ya Wabungu

Mtafiti alifanikiwa kuzungumza na viongozi wa kijiji cha Mwambani. Viongozi wote wanaijua miiko vizuri. Ulimbe uliyomo ndani ya miiko na matumizi yake katika kulinda maadili ya Wabungu kama ulivyofafanuliwa hapo juu na watu wazima. Jambo la kusikitisha ni kuwa hakuna kiongozi anayetumia miiko katika kazi yake ya kuwaongoza Wabungu. Hapa mfumo wa kufutilia mbali uongozi wa kijadi umeleta zahama ya wazi katika malezi ya wanajamii – Wabungu.

## 5.9 Watoto Waonavyo Ulimbe wa Miiko ya Wabungu

Mtafiti aliwasaili watoto katika vikundi. Kati ya watoto sita waliosailiwa kutoka katika kijiji cha Mwambani, walisema wanaisikia miiko kutoka kwa watu hasa wazee lakini hawajui maana yake. Aidha walisema miiko mingine ni vitisho tu wazee hawataki vijana waende kukaa mbali na wao. Pia wengine walishadidia kuwa wazazi wao wanataka watu wa kuwatuma kila wakati.

Mwiko ambao wote wanaujua ni kuwa, ni mwiko kwa watoto kuingia na kucheza ngoma ya makala. Mwiko kwa wanawake kwenda kuoga mtoni. Pamoja na mtafiti kujaribu kuwakumbusha baadhi ya miiko, lakini katika uhalisiya, wote walisema siku hizi miiko hiyo inavunjwa na haifuatwi kabisa. Labda zamani.

Watoto wote walikubaliana kuhusu mwiko wa kumpita mtu mzima bila ya kumsalimu kuwa ni kosa, huku ni kukosa adabu kwa mtu mzima.

Aidha ni mwiko kupita katikati ya watu wanaoongea utapigwa na jinamizi. Kwa Mbungu, mtu mwenye adabu hawezi kupita katikati ya watu wawili au kikundi cha watu wanaoongea, hata kama wamefunga njia. Jambo hili Ubunguni lina taratibu zake. Ughaibuni watu hutembea wakiwa wamefunga macho. Mbungu anapotembea anakuwa macho na anaona kila kilicho mbele yake. Kupita katikati ya watu wanaozungumza kuna maana kuwa wanachozungumza hakina maana. Hivyo mpitaji alionesha kuwakata kauli. Masuala ya kijamii yalizungumzwa mahali popote katika jamii ya Wabungu. Hapakuwa na baraza rasmi la kuzungumzia mambo hayo. Pia hakukuwa na haja ya miadi ili kuzungumza jambo lolote (Nchimbi, 1979; Sengo, 2009).

## 5.10 Watu Wazima Wanavyoona Matatizo Yanayojitokeza Katika Kuitumia Miiko ya Wabungu

Mtafiti anaeleza kwa kina namna Wabungu watu wazima wanavyoiona miiko katika jamii yao. Kuna masuala yanayowakabili katika kuitumiya na kuifundisha miiko hiyo kwa watoto wao katika jamii husika. Vyanzo vya mawazo ya wazee hawa vimebainishwa kuwa ni pamoja na Dini, maendeleo ya miji na Elimu ya Kimagharibi kusababisha sintofahamu hii ya kufuwawa kwa miiko.

### 5. 10.1 Dini

Kwa mujibu wa Thomas, yeye alisema kuwa dini ni imani. Dini ni uhusiano wa mtu au jamii ya watu (Wabungu) na Muumba wao. Wabungu walikuwa na imani hii na wataendelea kuwa nayo milele. Dini za Kikristo; Ukatoliki na baadaye Moravian ziliingia katika nchi ya Wabungu na hazikuwa na hadi sasa hazina shida yoyote na imani ya Wabungu ingawa zililazimisha matumizi ya majina ya watu wabatizwe kwa majina kutoka magharibi. Mwanataalimu Mbiti, anasema kuwa katika jamii mbalimbali za Kiafrika watu walikuwa na imani na waliamini uwepo wa Muumba. Imani hii ilijenga maadili maalumu ya kuheshimiana (Mbiti, 1975). Sasa kuna dini mpya hasa dini ya kilokole ndiyo inayosababisha dharau na kuwakataza watu kuacha kutumia miiko na kusababisha kufuwawa kwa miiko. Ingawa hakuna Wabungu wengi waliojiunga na dini hiyo, lakini wageni ambao wengi wao wameingia Ubunguni kwa sababu ya shughuli za uvuvi. Watu hawa ndio ambao ni tatizo kubwa katika kuhifadhi na kutumia miiko hapa kijijini.

Hapa mtafitiwa alitowa mfano hai. Wakati wa mazungumzo alimweleza mtafiti kuwa wiki mbili zilizopita, kijana mmoja alimwona mwanamke mmoja akioga baharini (ziwa Rukwa). Aliweza kumfahamu mwanamke huyo. Wakati huo huo, mume wa mwanamke huyo alikuja, kijana huyu alimweleza na kumtafadhalisha amwambie mke wake aliyekuwa akioga kuwa alikuwa anavunja mwiko. Hali hii ilizuwa majibizano na matusi kuwa Wabungu wanafuata mila na tamaduni zilizopitwa na wakati pamoja na matusi ambayo mtafitiwa hakuweza kuelezwa. Suala hili lilipelekwa mbele ya viongozi wa kimila hapo kijijini na hatua za kinidhamu zilichukuliwa mara moja.

### 5.10.2 Luninga / Televisheni

Jambo lingine alisema kuwa ni televisheni. Katika televisheni watoto wanaangalia picha mbaya hadi usiku wa manane. Mara tu baada ya chakula cha jioni watoto wanatoroka kwenda kuangalia senema. Watafitiwa walisema kuwa siku hizi watoto hawasimuliwi hadithi. Kwa hali hiyo watoto hawajui hata kutega vitendawili na badala yake ”wanaangalia hata vitu ambavyo sisi wakubwa hatuwezi kuviangalia” alisisitiza. Kulikuwa na miiko ambayo ilizuwia kusikia au kuangalia vitu ambavyo vingesababisha maadili yao kama Wabungu kukengeuka. Haya ni pamoja na mambo ambayo yangesababisha kijana kufanya tendo la ndoa kabla ya kuoa. Watafitiwa walitoa mifano ya miiko hiyo kuwa pamoja na:

- Wavulana waliobalekhe ni mwiko kulala nyumba ya wazazi, hawataoa.
- Ni mwiko kwa mvulana kuwategemea wazazi, hawezi kuoa.

### 5.10.3 Elimu

Watafitiwa hawakusita kutoa malalamiko yao kuhusu elimu kuwa pia imesababisha kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili. Wasomi wameleta dharau ya mila kuwa zimepitwa na wakati na wizi hata vijijini. Watafitiwa walitoa mfano wa wizi katika vyama vya ushirika. Makarani walikuwa wanaiba hadi vyama vya ushirika vikafa. Hapo zamani hawakuwa na shida ya mtu kuchukuwa kitu cha mtu mwingine. Sasa hata watoto wadogo wanajua pesa. Sasa wasomi wanawalea watoto wao kisomi kwa kuwafundisha matumizi ya fedha.

Mtafiti anaona kuwa madhumuni ya elimu kwa mujibu wa Sera ya Elimu Tanzania 1991, yanakengeuka au hayawafikii walengwa. Wasomi hawatimizi wajibu wao kama wasomi. Wabungu wanaona kuwa elimu inayotolewa haiwafanyi wanaoipata elimu hiyo kuimarisha mila, desturi na kuilinda miiko na maadili ya jamii. Wabungu wenye kupata elimu wanaitumia kwa kujinufaisha, kuwaibia Wabungu na kuwatukana Wabungu kuwa hawajuwi kitu chochote kinachoendelea huku Duniani.

Malezi bora ya mtoto si kumpa kila kitu akitakacho. Mzazi anapaswa kuangalia uzuri, umuhimu, athari na matumizi ya kitu ambacho mtoto anataka. Mtoto akitaka peremende unaweza kumpa peremende, wakati ukifikiria athari za peremende kwa mtoto. Aidha, kumpa mtoto pesa kwenda dukani kununua hizo peremende, ni vizuri mzazi kufikiri.

Akitowa mfano mtafitiwa alieleza;

> *"Huyu mjukuu (mtoto mvulana wa kadiri ya miaka mitatu), siku moja tulikuwa tumekaa hapa. Bibi yake aliletewa pesa na jirani, akaziweka hapo alipokuwa amekaa chini kwenye mkeka. Baada ya muda alikwenda jikoni na*

> *aliporudi alikumbuka pesa na kuanza kuzitafuta. Mjukuu alikuwa hajaondoka na alipomwuliza mumewe kama amemwona mtu aliyechukuwa, mjukuu aliyekuwapo hapo anacheza aliondoka na kuhamia alipokuwa amekaa mtafitiwa. Hakusema kuwa alikuwa amechukua alionekana kuwa na wasiwasi na alipomwangalia vizuri mkononi alifumbata kitu alipomfungua mkono alikuwa ameshika pesa!"*

Madhumuni ya elimu katika jamii ni kuleta uwadilifu. Elimu inapotumiwa vibaya katika jamii, basi wote wenye elimu huingizwa katika kundi la waovu wa Elimu. Wasomi wengi sasa wanawapeleka Wabungu mahali ambapo hapakukusudiwa na elimu. Mzee Thomas yupo sahihi katika mazingira yake kutoa suluhisho kama hilo la kuwa wasomi ni wezi. Kwa hali hiyo misingi ya miiko katika jamii ya Wabungu ilikataza wizi. Hapa kukengeuka kwa maadili, na kufuwawa kwa miiko kunatolewa jawabu na mzee Thomas, (Wizara ya Elimu Zanzibar, Aprili 1991)

Kufuwawa kwa miiko katika jamii ya Wabungu, kunasababisha kukengeuka kwa maadili ya Wabungu. Mawazo hasi kuhusu Elimu yanabainisha ni kwa namna gani jamii ya Wabungu inakengeuka kimaadili.

Katika utafiti huu, mtafiti anabainisha kuwa lengo la elimu ni kumkomboa binadamu, Mbungu katika maisha yake. Imebainika wasomi wenye maadili ni walimu na waganga tu. Wasomi wengine wanavunja miiko ya wao kuwa watu. Miiko ya utu, kusema ukweli. Hasira za watafitiwa zinabainisha kuwa wasomi hawatumii elimu waliyoipata ipasavyo.

### 5.10.4 Shughuli za Kiuchumi

Mtafitiwa mmoja alibainisha kwamba, suala la wageni wanaokuja kwa sababu ya uchimbaji wa madini limekuwa ni tatizo kubwa kwa maadili ya jamii ya Wabungu.

Sasa Mkwajuni kuna wageni wengi sana kutoka nchi mbali mbali na karibu mikoa yote ya Tanzania. Tabia za watu ni mseto. Shughuli za biashara walizokuwa wanazisikia mijini sasa zipo katika kijiji cha Mkwajuni sasa wanapaita mjini. Baa za pombe, nyumba za kulala wageni na vyumba vya kuoneshea video usiku. Nyumba hizi za video hazina leseni kwa hali hiyo hakuna udhibiti wa vitu vinavyooneshwa. Hili ni tatizo kubwa aliongeza.

Shughuli hizi zinasababisha vijana, wake kwa waume kwenda Mkwajuni kutafuta kazi. Mkwajuni hakuna hata kiwanda kimoja, kazi watapata wapi? Wasichana wanajikuta wakifanya biashara ya ngono na wafanyakazi wageni katika machimbo ya madini na wenyeji na sasa kuna ongezeko kubwa la vifo mtafitiwa anafikiri ni ugonjwa wa VVU/UKIMWI. Msokile, (1990) anatueleza athari za fedha na kazi hasa kazi katika machimbo ya madini. Sehemu za machimbo ya madini kuna matatizo makubwa ya kukengeuka kwa maadili ya wenyeji – Wabungu.

### 5.10.5 Ndoa

Wabungu wanapooa nje ya eneo la Wabungu au watu wenye utamaduni unaofanana na Wabungu kama wanyamwezi, wafipa na makabila yanayozunguka ziwa Rukwa, au nyanda za juu kusini, wengi wao wanakuwa wamepotea. Hii ni kwa sababu wanakuwa na miiko tafauti. Akishadidia maelezo haya Erick na Peti walitoa mfano kuwa, utamaduni wa Wachagga na Wapare ni tafauti kabisa na utamaduni wa Wabungu katika uhusiano wa mtu na mkwewe. Mkamwana kula chakula na baba mkwe wake ni mwiko mkubwa kwa Wabungu. Pia alisema “wenzao hawapigi magoti wanaposalimu au kupokea kitu. Hii ni tafauti ya utamaduni tu” lakini kila

kitu kina kwao. Hili ni tatizo kubwa katika maadili ya watoto watakaozaliwa na kulelewa na familia kama hii, hasa kama watakuwa wanakaa mijini. Hawawezi kufundishwa kitu ambacho hata baba au mama hakijuwi wala kukiamini.

Bibi mwingine alitoa mfano wa kiburi cha vijana katika ndoa kuwa mara nyingi ni majuto. Wanaume wawili aliowatolea mfano ndoa zao zilikuwa na matatizo na majuto na wanaume hao walisema aghalabu wangewasikiliza wazazi yasingewapata hayo yaliyowapata. Majuto ni mjukuu. Watafitiwa walitoa mifano ya miiko kama;

- Ni mwiko kula umesimama utakuwa mkimbizi au utaoa au kuolewa mbali
- Ni mwiko kuoa bila ya ridhaa ya wazazi, ndoa itakuwa na matatizo
- Ni mwiko kwa mwanamke ambaye mumewe amekwenda mawindoni kufunga mlango mchana, atakuwa amefunga pori na mumewe hawezi kuona au kuua mnyama.

Mtafiti na watafitiwa walijadili mifano ya miiko hii na kubainisha mambo yafuatayo katika miiko ya Wabungu;

#### 5.10.5.1Ni Mwiko Kula Ukiwa Umesimama, Utakuwa Mkimbizi au Utaoa au Kuolewa Mbali

Mtu kula akiwa wima kunaonesha hali ya kuwa na haraka. Aidha chakula ni kitu cha heshima sana katika jamii ya Wabungu, hivyo kilipaswa kupewa heshima ya hali ya juu. Katika jamii ya Wabungu heshima ilioneshwa kwa kukaa chini mtu anapowasiliana au anapopewa kitu chochote. Kwa hali hiyo, wakati wa kula chakula

chochote, mlaji alipaswa kuketi na kula. Suala la kula chakula halikuwa na haraka. Milo yote ililiwa na watu wote nje, chini ya mti wenye kivuli na walaji wote walikaa. Wakati huo huo watoto walifundishwa kukaa vizuri wakati wa kula, Paza alisisitiza.

Wazee walimweleza mtafiti kuwa, hali ya ukimbizi au kuoa au kuolewa mbali, wakati huo ilikuwa na maana ya sasa. Ukimbizi uliozungumziwa ni hali ya kutangatanga katika vijiji mbalimbali bila ya kuwa na makao maalumu. Pia wakimbizi walikuwa hawaoi, kwani kila wakati hawakuwa na miji maalumu ya kuishi. Mwiko huu ulitaka Wabungu watulie na kuwa na familia. Hali hii ni kwa wake kwa waume. Watu wa kuzurulazurula walidharaulika sana na kuchuliwa kama ni watu wavivu. Katika jamii ya Wabungu watu wa aina hii walionekana kuwa hawana maadili na ni watu ambao hawawezi kutunza familia zao.

Mzee mmoja aliongeza kuwa mtu asiyeoa au kuolewa au mkimbizi anafananishwa na mhuni. Mtu wa aina hii ni mvivu, hafanyikazi kwa sababu na anaishia kudowea chakula na malazi kwa watu kwa sababu hana mtu wa kumwajibisha katika malezi (Msokile 1990).

### 5.10.6 Tabia za Wazazi

Jambo lingine lililozungumzwa lilikuwa kuhusu wazazi kuwa chimbuko la maadili mabaya. Kwa mujibu wa Paza, yeye aliwashutumu wazazi wanaoshindwa kuilinda na kuitumia miiko kwa kuacha kuwaonya watoto wao wanapovunja miiko. Yeye alisisitiza kuwa malezi huanzia nyumbani. Akichukulia mfano wa mavazi, mtoto anatoka nyumbani na nguo fupi au nguo ya kuonesha maungo au ya kubana kupindukia na mzazi hasemi chochote. Mzazi mwingine anavaa nguo zinazoacha

maungo yake ya mwili wazi isivyofaa, huku ni kuvunja mwiko. Baada ya muda hii inakuwa ni tabia ya mtoto, halafu lawama zinakwenda kwa jamii badala ya mzazi wa mtoto kulaumiwa kwa kushindwa kusimamia malezi yanayofaa kwa mtoto wake. Aidha alitoa mfano wa matusi, alisema matusi yanaanzia nyumbani. Watoto wanajifunza matusi kutoka kwa watu wa karibu hasa wazazi au kundi la rafiki na mzazi kushindwa kuwaonya.

Paza akitoa mfano wa watoto wa mzee mmoja pale kijijini. Alisema watoto wamerithi matusi ya baba yao kana kwamba ni mali. Mtafitiwa alisisitiza. Mtafitiwa alitowa mifano ya miiko inayoshadidia tabia hii katika jamii ya Wabungu kuwa;

- Ni mwiko kwa mke kwenda nje ya ndoa mumewe akiwa safari, mume atapata balaa au hawezi kufanikiwa.
- Ni mwiko kuzungumza masuala ya ngono na uzazi mbele ya watoto.

## 5.11 Mtazamo wa Viongozi Kuhusu Matatizo Yanayojitokeza Katika Kuitumia Miiko ya Wabungu

Tatizo kubwa lililojitokeza katika matumizi ya miiko katika kazi za uongozi kijijini ni kuwa, hawatumii miiko kabisa. Sababu kubwa ni kuwa wanafuata sheria za uongozi zilizoainishwa na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania peke yake mzee Kiongozi alifafanua.

Viongozi walikiri miiko ingewasaidia katika kutoa maonyo kwa wakosaji. Wao hawana uwezo – kwa maneno ya kiongozi mmoja. Pia aliongeza kusema utawala wa

kimila Tanzania ulifutwa na Mwalimu Nyerere Tanzania mara baada ya Uhuru. Mtafiti anaona kuwa viongozi walikuwa na majibu rahisi kwa maswali magumu.

## 5.12 Mtazamo wa Watoto Kuhusu Matatizo Yanayojitokeza Katika Kuitumia Miiko ya Wabungu

Vijana walisema kuwa hawaijui miiko hivyo hawaoni umuhimu wake. Kijana mmoja alisema hata methali wanazojifunza shuleni hazitumiki katika kuleta mabadiliko ya tabia. Akitoa mfano wa methali ya “asiyesikia la mkuu, huvunjika guu”. Kijana huyo alisema kuwa vijana wengi wanaona kuwa haya ni maneno yenye kuleta ladha ya mazungumzo na si kitu cha kuzingatia.

Vijana walionesha mifano ya watu kijijini ambao sasa maisha yao ni mabaya kiuchumi na kitabia kuwa hii ni kutokana na uvivu na sasa ni wezi. Kama wangeijua miiko na kuifuata hawangekuwa katika hali hiyo. Siku hizi watoto wanakwenda Mkwajuni (kijiji jirani/ mji mdogo Wilaya ya Chunya) kuangalia video mpaka usiku. Aidha kuna michezo ya muziki wa matangazo ya biashara ambayo wanenguaji wake wanawake wanavaa nusu uchi na wanaonesha kilabuni, wazee na watoto wote wanaangalia. Hali hii inawafanya vijana waone hayo ndiyo mavazi ya kisasa na kuanza kutabii kushona au kununua katika mitumba mavazi ya aina hiyo.

## 5.13 Suluhisho la Wabungu kutumia Miiko Mtazamo wa Watu Wazima

Elimu kwa Wabungu juu ya kuthamini utamaduni na mila zao ni jambo ambalo halipaswi kupuuzwa hata kidogo. Kwa mujibu wa akinamama, walisisitiza kuwa ni muhimu kuthamini utamaduni wa jamii ya Wabungu. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao mila na utamaduni wa jamii. Wakati wa mazungumzo na mtafiti, mtafitiwa alitowa mfano wa mjukuu wake aliyerudi nyumbani na kusalimu

na kuendelea kwenda chumbani kwake. Mtafitiwa alisema muda alioutumia kwa salamu hautoshi. Alipaswa kutulia kupiga magoti na kusubiri kubadilishana salamu. Mtafitiwa pia alizungumziya juu ya masuala ya utunzaji siri na mimba kabla ya ndoa kama ilivyobainishwa hapa chini.

### 5.13.1 Utunzaji wa Siri

Zamani kulikuwa na usiri mkubwa katika utoaji wa taarifa mbali mbali. Ilikuwa ni mwiko kutoa siri za mazungumzo ya baraza la usuluhishi. Erik akiunga mkono hoja hii alisema kuwa utaratibu huu ulikuwa ni mzuri sana na jamii ya Wabungu inahitaji kurejelea miiko na kufuata misingi ya miiko na maadili ya jamii ya Wabungu. Ni sawa kabisa tunahitaji kujiuliza upya ni wapi pulipokosea. Hii ilikuwa ni kauli ya pamoja ya watafitiwa, katika kushadidia maelezo haya ya Erick. Mzee mwingine alitoa mfano halisi na kusema kuwa; “angalia siku hizi habari zina sikika hata kabla ya kutangazwa na Ikulu. Rais anapotangaza jambo linakuwa kama marudio masikioni mwa wananchi”.

Thomas alisema kuwa ni muhimu kwa wanajamii kurejelea tambiko na miiko ya Wabungu. Hii ni muhimu kwa sababu hali hii inaleta mshikamano katika jamii ya Wabungu. Zamani Wabungu watoto hawakuwa na ruhusa ya kujifanyia jambo bila ya kuwashirikisha wazazi. Ni muhimu watoto sasa kuwasikiliza wazazi. Aidha Thomasi alisema maadili yanapaswa kufundishwa na wazazi na si dini. Dini zina nafasi yake lakini miiko ya jamii ni muhimu zaidi katika kuweka msingi wa malezi na tabia njema. Hapo hata dini zitapata urahisi wa kuwaadilisha watu wenye mila na miiko kuliko kuwawekea misingi ambayo inasababisha hata kutokuwa na misimamo

ya dini na wanabaki wanahama dini moja baada ya nyingine, asubuhi yupo dini hii na mchana dini ile. Maelezo haya yaliungwa mkono na watafitiwa wengine.

#### 5.13.2 Mimba Kabla Ndoa

Zamani ilikuwa ni mwiko kwa msichana kubeba Mimba au mvulana kumpa mimba msichana. Bibi mmoja, alisema kuwa zamani vijana walikwenda kuzungumza na wazee ili kupata elimu ya jadi, utamaduni na malezi ya jamii ya Wabungu. Huko walijifunza miiko, sheria na taratibu za jamii ya Wabungu. Siku hizi kufanya hivyo kunahesabiwa kama kwenda kutafuta uchawi. Ndiyo maana watoto wa siku hizi hawana adabu na heshima kwa wakubwa hata wazazi wao waliowazaa.

### 5.14 Suluhisho la Wabungu Kutumia Miiko – Mtazamo wa Viongozi

Viongozi wote waliozungumza na mtafiti wanakiri kuwa miiko ingewarahisishia kazi, hasa malezi na kuleta uwadilifu katika kijiji. Viongozi hawa walimweleza mtafiti kuwa kinachohitajika ni serikali kuwapa ruhusa ya kutumia miiko kwani wanaijua miiko hiyo. Mtafitiwa mmoja alimweleza mtafiti kuwa Serikali haina Kabila wala Dini. Kwa hali hiyo watu wote wanapaswa kuhudumiwa bila kuweka misingi ya Kabila au Dini. Ingawa watafitiwa wanaona kuwa maadili yanakengeuka, wao wanawachukulia hatua za kisheriya ambazo ni kuwapeleka Mahakamani au Polisi.

### 5.15 Suluhisho la Wabungu Kutumia Miiko – Mtazamo wa Watoto

Vijana wengi waliozungumza na mtafiti walisema miiko ifundishwe shuleni, Makanisani na Misikitini. Pia wazazi wawafundishe watoto wao kama wanavyowafundisha kusalimia na kazi mbali mbali za kila siku. Kama unajuwa fika

kuwa njia unayopita ina umande, na unafuatana na mtoto wako ambaye unajuwa lazima utambeba atakaposhindwa kutembeya, basi ni vizuri kumbeba mapema kabla hajalowa kwa umande kwani utakapombeba baada ya kulowa na umande atakuchafua. Huu ni msemo wa Kiganda ambao rafiki wa mtafiti bwana Moses Isoba alipenda sana kuutumiya ili kuwatahadharisha watu wazima katika kutatuwa matatizo wanayoyajuwa kuwa yatatokeya kama watu wazima. Hapa wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao miiko ili kulinda maadili ya jamii ya Wabungu.

### 5.15.1 Maadili Mema – Salamu

Kati ya wasailiwa kumi na watano waliosailiwa na mtafiti kuhusu adabu au tabia njema kwa mtoto wa Kibungu walisema wasifu wa kwanza ni salamu. Ni mwiko mkubwa sana kwa mtoto au mtu mzima kumpita mtu au watu bila ya kuwasalimu. Kitendo cha mtoto kuwapita watu bila ya kuwasalimu kinahesabiwa kuwa ni kupotoka kwa maadili. Ni wajibu wa mtoto hata kama ana haraka kusimama na kusalimia. Salamu si kitu cha haraka labda kama mmeshaonana na mtu huyo kwa siku ile.

Kwa mujibu wa mtafitiwa, mtoto yeyote, anapaswa kusimama kama anatembea, kuvua kofia kama amevaa kabla ya kutoa salamu. Mtoa salamu husubiri jibu la salamu hiyo. Mzee mwingine akishadidia hoja hii alisema kwamba, mzee ni mzee tu. Uzee una mambo mengi hasa maradhi. Kuna wazee ambao hawaoni vizuri na wengine hawasikii vizuri. Wote hawa wanahitaji salamu na kutoa baraka kwa watoto. Mtoto anapopita akitembea na kutoa salamu bila ya kusimama na kuonesha ishara za kusalimia basi wazee wengine watamwona na kusema mtoto wa mzee

fulani amempita hata bila ya kumsalimia. Mzee huyu alisisitiza kuwa miondoko na ishara ni muhimu sana katika harakati zote za watu kusalimiana.

Wakati mazungumzo yakiendelea kijana mmoja alipita na ulikuwa ni mfano halisi, kijana huyu alipita na baiskeli akiwa anaendesha na alisalimia bila kusimama na Thomas alisema hii ni hali halisi ya watoto wasio na adabu na heshima. Mtoto aliyelelewa vema lazima atashuka na kusalimia.

Mtafiti alichogundua ni kuwa mzee huyu hakujibu ile salamu. Salamu iliandamana na utambulisho wa mtoto huyo au kujuliwa hali ya watu wengine nyumbani. Kama kuna mgonjwa basi huu ndio uliokuwa muda wa kupeana habari za wagonjwa kutoka pande zote ama kutoka kwa msalimiaji au msalimiwa. Hapa watafitiwa walizungumza na mtafiti kuhusu baadhi ya miiko inayohusiana na salamu kama ifuatayo;

**(i) Ni Mwiko kwa Kijana Kusalimia Wakubwa Akiwa Anaendelea Kutembea, ni Kukosa Adabu**

Salamu ni sehemu ya utambulisho binafsi. Salamu haiishii na maneno ya kusalimia tu bali ni pamoja na staha, adabu, miondoko, utulivu, upendo na kujua hali ya watu wengine katika familiya waliopo nyumbani. Wakati wa kusalimia ndipo hasa mtu asiyemjuwa vizuri mwenziwe, ataweza kumwuliza, yeye ni mtoto wa nani? Kama atasalimia na kuendelea bila kutoa nafasi hiyo ya kupeana maelezo, basi mtu huyo anaonekana ana majuvuno, mbinafsi na mwenye dharau kwa wenzake au wakubwa.

Kwa mujibu wa mzee mmoja, yeye alisema kuwa, watoto wa siku hizi hawana heshima, kinachosababisha hali hii ni kuwa watoto wa siku hizi hawana salamu /

hawasalimii (awana awalelo watakola eindamu). Watoto kwa kujua au makusudi, wanaweza kumpita mtu mzima bila hata ya salamu bila soni. Aidha mtoto anaweza kusalimu akiwa anaendelea na safari zake. Zamani ilikuwa ni wajibu wa msalimiaji *kutungama* au kupiga magoti kidogo kabla ya salamu na kusubiri kidogo kabla ya kuendelea na safari yake.

**(ii) Kijana Anapaswa Kupisha Njia Wakubwa**

Katika jamii ya Wabungu ilikuwa ni mwiko kwa mtoto kupishana na mtu mzima katika njia ndogo kwa umbali ambao watagusana au kupigana vibega. Sikio halikui mbele ya kichwa, mtoto alipaswa kupisha njia. Kabla ya kupisha njia kitu cha kwanza ilikuwa ni salamu, badala ya kumpiga mtu kikumbo. Watafitiwa wanaamini kuwa mtu mmoja hawezi kumpisha mtu mwingine bila kumsalimu kana kwamba hajamwona. Njia za wakati huo zilikuwa ni nyembamba hakukuwa na barabara kama sasa. Wazee ni watu dhaifu kimwili na hata uwezo wao wa kuona unaweza kuwa umeshapungua, na kwa hali hiyo wanahitaji msaada wa vijana.

Mwiko huu ulisaidia kutoa uamuzi wa nani apewe nafasi kwanza kati ya mzee na kijana. Pembeni ya njia kunaweza kuwa na shimo au majani yanayotambaa ambayo yanaweza kumtatiza mzee na kumwangusha kwa urahisi zaidi kuliko kijana. Licha ya hali hiyo kijana kama ataumia bado ni rahisi kupona kuliko mzee. Hivyo mwiko huu ulimpa nafasi mzee kupata msaada wa kijamii kwanza na ulinzi wa afya yake awapo njiani.

**(iii) Ni Mwiko Kumpa Mkubwa Maji au Kitu Bila Kupiga Goti, ni Kumkosea Adabu**

Mara baada ya kuitwa na kupewa kazi ya kuleta maji ya kunywa yumkini mtoto aliitwa na kufika hapo alipo mhitaji wa maji, basi ilikuwa ni wajibu wa mtoto mara baada ya kufika alipaswa kwanza kusalimia. Pia wakati huu mgeni alipata nafasi ya kumjuwa mtoto au mtoto kumjuwa huyu mtu mzima.

Heshima au adabu hainunuliwi, bibi Helena alimwambia mtafiti. Heshima kwa wakubwa ilioneshwa kwa kupiga goti wakati wa kupokea au kutoa kitu kwa wakubwa. Hii ilikuwa na maana kuwa mtu anayetoa huduma kwa mtu mwingine alipaswa kutulia na siyo kuondoka haraka. Kama mtu ana haraka basi aombe radhi na ijulikane kuwa ana shughuli nyingine muhimu na atapewa ruhusa hiyo. Kinyume cha hapo, ilichukuliwa kuwa ni utovu wa nidhamu. Siku hizi mtoto akifika anakupa au anakuwekea hapo anaondoka hata kama unahitaji zaidi inakubidi uvumiliye mpaka unakokwenda.

**(iv) Ni Mwiko kwa Mtoto Kumtanguliza Mtu Mzima**

Elimu ya asili katika jamii nyingi za Kiafrika ilitolewa kwa vitendo. Hapa mtu anayefundishwa hasa mtoto, aliambiwa kwa maneno na kuoneshwa vitu mbalimbali. Wakati huu hakukuwa na madarasa ya kufundishia kama ilivyo sasa. Sehemu iliyorithiwa katika mfumo huu katika elimu ya sasa ni ile sehemu ya elimu ya mazoezi kwa vitendo. Katika matembezi ya kawaida wakati huo, pamoja na kuzingatia mazingira ya uwepo wa misitu na nyika, wakati wa safari hizi ilikuwa ni muhimu kwa mtu mzima kuwatanguliza watoto. Hapa tusifananishe na safari ya bata na wanawe.

Wabungu waliamini kuwa ni hatari kwa mtu mzima kutangulia mbele wakati wa safari. Hii ni kutokana na misitu na wanyama wakali. Kama mtoto atakuwa nyuma basi alikuwa katika hatari ya kushambuliwa na wanyama na kushindwa kujitetea. Pia watoto waliendelea kufundishwa mambo mbalimbali, kama namna ya kutembea vizuri, jambo la kuzingatiya ni kuoneshwa vitu kama mimea na matumizi yake. Kwa mujibu wa bibi Mwalyego Sigonda, alisema mtoto akimtanguliza mtu mzima ni sawa na kuwa mtoto anajua kuliko mtu mzima, hivyo angemwoneshaje vitu?

Maana ya kiongozi wa safari ni kuonesha njia. Wakati wa safari ya bata na wanawe, hakuna mazungumzo. Watoto walipata elimu ya vitendo wakati wa safari za namna hii. Hadithi, miiko, misemo, utabiri, na vingine vingi. (Thiong'o, 1965) katika "The River Between", anaelezea juu ya jinsi elimu ya jadi au asili ilivyo rithishwa kwa mtoto wake Waiyaki akiwa safarini.

**(v) Ni Mwiko kwa Mtoto Akiwa Ugenini Kukaa Bila Kusaidia Kazi**

Jamii ya Wabungu iliamini kuwa kazi ni kipimo cha utu. Kuku mgeni hakosi kamba mguuni, alisema mzee mmoja. Wabungu waliamini kuwa mgeni ni mtu anapofika nyumbani kabla ya salamu. Baada ya salamu hasa msichana au mvulana na watoto ni wenyeji na wanapaswa kufanya kazi zote za nyumbani zinazowahusu. Wanapaswa kuingia jikoni kusafisha vyombo, au kushiriki katika kazi zote zinazoendelea kwa wakati huo.

Wasailiwa wote walisisitiza kuwa ni aibu kwa mtoto au kijana hasa wa kike kuhudumiwa bila ya yeye kujishughulisha ni kitendo cha uvivu au kukosa adabu na makuzi mabaya. Mtoto mgeni aliyesamehewa katika hali hii ni yule tu ambaye amefika hapo akiwa ni mgonjwa.

### (vi) Ni Mwiko Kukataa Kutumwa na Wakubwa, ni Kukosa Adabu

Katika jamii ya Wabungu mara baada ya kumwita mtoto, mtoto huyu alipaswa kuitika wito kwa sauti ya kusikika kwa mtu anayemwita au aliye karibu yake. Mara baada ya kuitika wito, mtoto alikwenda na kusalimu. Salamu kilikuwa ni kitu cha kwanza mahali popote. Mtoto baada ya kuitika wito huo, kwa kawaida aliulizwa kama alikuwa na shughuli aliyokuwa akiifanya.

Jamii yote ilijuwa wazi kuwa mtoto alikuwa ni mali ya jamii na si mali ya baba na mama. Mtu yeyote mzima alikuwa na haki ya kumtuma mtoto wa jirani kumsaidia kazi au kumletea kitu. Mtoto alipotumwa na mkubwa alikwenda bila kuhoji, labda kama ametumwa kitu kingine au mahali pengine. Hii ilisaidia jamii kujua tabia za watoto wote na kupanga kazi za kijamii kwa urahisi.

Mtoto mwenye kiburi hakufaa kupewa wajibati za kuongoza wenzake. Kwa mfano, mtoto anapoitwa na kuendelea na kazi zake, hii ilionesha utovu wa maadili. Wito wa mtu mzima ilikuwa ni amri, baada ya kuitika wito mtoto alikuwa na nafasi ya kueleza jambo lake. Je, kama anaitiwa kutoa msaada wa kuitiwa mganga halafu akapuuza si mtu atakufa! Watoto ni tegemeo la kila mtu mzima kijijini. Ni wepesi wanaweza kukimbia haraka na kutoa taarifa kama kuna shida. Pia wana nguvu za kutenda kazi kuliko wazee. Haya ndiyo yaliyokuwa maelezo ya wazee, Lugwila na Mahella kwa mtafiti kuhusu mwiko huu wa mtoto kukataa kutumwa na wakubwa.

Mponda, (1962) katika Adabu Njema, mwandishi anashadidia kuhusu wepesi huu katika mada yake ya bidii. Yeye anasema kuwa mtu hawezi kufanikiwa jambo lolote hapa ulimwenguni bila kuwa na bidii. Wayao wana methali isemayo kuwa aliyeita

ndiye aliyeona. Wewe uliyeitwa hujui wala hujaona sababu ya wito huo. Kwa hali hiyo wewe uliyeitwa unapaswa kukimbia au kuitika wito kwa haraka sana. Hali hii pia inampasa aliyetumwa kwenda mbio anapotumwa na au kufanya kazi hiyo kwa uangalifu mkubwa pasi visingizio vya aina yoyote.

**(vii) Ni Mwiko Kumwita Mtu Mzima kwa Yowe**

Katika jamii ya Wabungu ilikuwa ni mwiko mkubwa kwa mtoto au hata mtu mzima kumwita mtu mzima kwa kupiga yowe. Kama mtu yupo mbali basi mtoto alitumwa kumkimbilia ili ampashe habari za wito huo. Mtu aliyetumwa kitu cha kwanza ilikuwa ni salamu. Hakuna haraka ya kutoa taarifa bila ya kuanza na salamu. Mawasiliano yoyote yale mahali popote pale yalianza na salamu.

Mtoto au mtu yeyote aliyefunzwa na kuwa na tabia njema au maadili mema alionekana kwa adabu ya salamu. Kumwita mtu kwa kupiga yowe ni kuonesha dharau kwa mtu anayeitwa. Mzee mmoja alimwuliza mtafiti kama anaweza kumwita baba yake kwa kupayuka kana kwamba anawita mtoto mdogo? Ndiyo maana watoto walikuwapo nyumbani wakati wote. Nyumba isiyo na mtoto ilikuwa ni nyumba ya mtu mchoyo. Hata kama mtu hana uzazi lakini ndugu zake walikuwa na watoto ambao anaweza kukaa nao na akaitwa mama au baba wa mtoto huyo akamletea maji ya kunywa au akamtuma anapokuwa mgonjwa.

Mtoto anapotumwa kumwita mtu, mara alipofika alisalimia. Kama walikuwapo watu wengi basi aliomba radhi na kusema, “samahani, ninamwomba mzee ...”, na atamwambia kuwa anaitwa nyumbani au mtu fulani anamwita. Mchakato huu ulikuwa ni wa kawaida kwa watoto wote wanaotumwa. Mtoto asiyefunzwa basi

jambo linapotokea wazee humweleza utaratibu pasi kuhofia mzazi wake kama yupo. “Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo”, mzee mmoja alimalizia. Kwa hali hiyo mtoto alilelewa na jamii nzima, hii ni pamoja na ndugu wa familia pamoja na jirani, wapitanjia, viongozi mbalimbali na wageni waliofika ubunguni.

**(viii) Ni Mwiko Kukataa Wito, Kataa Neno**

Kwa mujibu wa mzee Mahella, kuna baadhi ya watu hawapendi kusalimia, hivyo wanapoitwa tu, hufikiria kuhusu kero la kusalimia. Si kila anayeita basi ana shida ya kutatuliwa. Mara nyingine wazee hupenda kuwaona watoto au wajukuu wao, hivyo huwaita. Katika jamii ya Wabungu mzee yeyote yule ana haki ya kumwita mtoto yeyote na kumtuma bila ya ridhaa ya wazazi. Mtoto mwenyewe anaweza kusema kama ana kazi au laa.

Kuitika wito kwanza kuliendana na salamu. Kama mtoto hatasalimia basi hii ni ishara kuwa hajapendezwa na wito huo, au hataki kusikia chochote kutoka kwa mtu aliyemwita. Kukataa si lazima atamke kwa maneno bali hata vitendo vyake vinaweza kuashiria kukataa wito na hapa kutokusalimu kunaonesha hali hiyo, kwani “mwanzo wa ngoma ni lele” alimaliza mzee Mahella.

Mtafiti akiwa anaendelea kuzungumza na bibi mmoja, mjukuu wake aliingia ndani. Bibi alimwita lakini mjukuu hakuja. Bibi alisema haya ndiyo yanayozungumzwa, hawa ndio watoto wa mjini. Hawana adabu hata kidogo, hajui hata anachoitiwa lakini anakataa. Hawataki hata kuwafahamu watu. Atawajuwaje watu bila kutambulishwa! Bibi alijiuliza.

Mzee mwingine akitowa mfano kama huo alisema, mtoto mwenye adabu na aliyefunzwa na wazazi wake vema, aliwasikiliza wakubwa. Yeye alitowa mfano kuwa, kama anamwomba mtoto kwenda kuloweka minyaa, basi ndani ya minyaa aliweka zawadi ya kitu chochote na kumwambia akifika mtoni au ziwani kabla ya kuloweka afunguwe kwanza kisha afunge minyaa hiyo vizuri ndipo ailoweke. Baada ya kufungua alikuta kitu au zawadi ambayo aliwekewa mtoto mwema na mwenye adabu. Wema ulituzwa. Licha ya hali hii ya kuitwa na kutumwa salamu kilikuwa ni kitu cha kwanza kabla ya kupeana wajibu wa aina yoyote.

## 5.16 Miiko Kuhusu Heshima (Mavazi)

Kuvaa nguo ni lazima kwa watu wote. Hata zamani za kale watu walivaa magome ili kusetiri maungo yao. Ubora wa nguo unaweza kutafautiana lakini suala la mavazi ya kusetiri maungo si jambo la mjadala ni jambo la lazima. Watafitiwa wote waliosailiwa walibainisha jambo hili.

Watafitiwa wote walikereheshwa na mtindo wa sasa wa uvaaji, hasa mavazi ya wanawake. Uvaaji wa suruali kwa wanawake watafitiwa waliona kama ni kumwingilia Mungu shughuli za uumbaji. Kwa dhamiri kuu waliona kuwa mavazi ya kubana na kuonesha maumbile ya mtu au kuvaa suruali na kuacha makalio nusu nje au sehemu za mapaja ama matiti yao yakiwa wazi. Hii si tabia njema. Siku hizi tunashuhudiya wanaume watu wazima wanaweka rangi nywele zao kuficha mvi. Ili wasionekane kuwa wamepitwa na wakati. Pia wanaume wanatoga na kuvaa vipuri puani na masikioni, huku suruali zao zikiwacha makalio wazi au wakionesha nguo zao za ndani. Huu ni usasa, huu ni , haya si malezi ya Kila Jamii ina Ujumi Wake.

Hii si elimu iliyo na kwao Ubunguni. Uvaaji huu hauna mapisi yake Ubunguni, Ubunguni taalimu hii si kwao.

Hali hii ilionekana kuwa haikubaliki hata kidini. Wakristo, Waislamu, na madhehebu mengine mengi. Walitoa mfano wa wachungaji kuweka sheria za mavazi kanisani kuwa huku kote ni kukataa aina hiyo ya mavazi. Swali lililoulizwa ni kuwa wanamvalia nani mavazi haya? Haya ni mavazi ya mjini ambako watu hawapo na wazazi au ndugu zao bibi Wakunyala alisisitiza.

Mtafitiwa mmoja alisema yeye anaona aibu anapomwona mwanamke amevaa suruali. Anajisikia kama yeye yupo uchi. Alimkumbusha mtafiti kuhusu habari ya oparesheni mavazi nchini Tanzania miaka ya mwanzoni mwa sabini. Watu wote wake kwa waume walipaswa kushona na kuvaa nguo zenye urefu wa kufunika magoti. Pia hata kaptula za shule ilipasa ziwe na urefu wa kufunika magoti. Hii ilikuwa sera bora ya mavazi haijulikani baada ya hapo ilikwenda wapi?

Shida ni kuwa maamuzi mengine mazuri yanayotolewa na Serikala yanatolewa na kushika kasi kama moto wa mabua ya mahindi kisha unazimika mara moja hakuna hata mtu mmoja anayekumbuka kama kuna jambo lilitokea hapa duniani. Mavazi yanayositiri maungo ndiyo utu wa mtu. Wanyama wanatembea uchi kwa sababu hawana akili, wao ni hayawani. Je, watu hawa nao hawana akili? Je, wamerukwa na akili? Wamekuwa hayawani! Haya basi kama umependa kuivaa hiyo suruali basi shona yenye ukubwa wa kutosha na si kama uliyomnyang’anya mdogo wako au umeazima baada ya kuunguliwa na nyumba. Katika hali ya dharula mtu huyu atapewa kitenge au kanga ili ajisitiri na hiyo iwe kama nguo ya ndani.

Mzee Federiko alikumbuka visa vya mjini kuwa kuna wanawake siku moja walifuatwa na kundi la wauzaji wa sokoni wakizomewa na kupigiwa miluzi na mwishowe walichaniwa "vimini" walivyovaa ati kwa sababu walikuwa sawa na uchi wa mnyama  hivyo hawakustahili kuvaa nguo. Hali hii watu wa mijini wanaileta huku Ubunguni, wanapokuja kutoka mjini. Hali hii ni hatari sana kwa watoto wetu kwani wanawaiga watu hawa bila kujua wanajikuta wametumbukia katika kilindi ambacho wanapata shida kutoka, au kuwatoa hao waliotumbukia.

Hali ya Mkwajuni na Mwambani ni mbaya zaidi kuliko Udinde na Maleza. Watu wa Mkwajuni wanawaharibia watoto wao wanapokuja huku na wao wanabadilika na kuanza kutabii kuvaa nguo za ajabu ajabu.  Aidha wakati wa kujadili suala hili, liliambatana na miiko ya mavazi ya jamii ya Wabungu ambayo ilikuwa kama ifuatavyo;

### 1.16.1 Ni Mwiko kwa Wanawake Kuvaa Suruali

Mzee mmoja alieleza kuwa hapo zamani wanawake walivaa nguo nyingi za kuwasitiri mitetemo ya maungo yao. Nguo hizi zilikuwa madhubuti kwa upepo na mvua. Yumkini hata kama mwanamke huyu atapata dharura yoyote ya kimaumbile, basi alikuwa salama mbele za watu wote.

Tabia ya mtu ilipimwa kwa Mwenendo wake pamoja na mavazi yake. Kwa mwanamke kuvaa suruali kulifananishwa na kutabii tabia ya watu wa mjini, wahuni

au kutabii vitu visivyomhusu. Kama ilivyo aibu kwa mwanaume kuvaa gauni, ilikuwa ni aibu kubwa kwa mwanamke kuvaa suruali.

Jamii ilimwona mwanamke kama huyu kuwa, anataka mashindano ya kutafuta usawa ambao hauna msingi katika maumbile na kuleta matamanio kwa waume wakiwemo baba zake, wajomba, kina kaka, kwa kuonesha maungo yake ya mwili wazi wazi. Kuvaa suruali kulifananishwa na umalaya. Waliovaa suruali wengi wao walijisasa ndimi zao na kupata athari ya uhabithi, kupewa talaka katika ndoa kwa kukosa hisia za mambo. Kwa Mungu hawana nafasi nyingine ila motoni.

Watafitiwa walikiri kuzidiwa na ongezeko la wanawake wanaovaa suruali za kubana nchini hasa mijini. Katika jamii ya Wabungu katika kijiji cha Mkwajuni waliona kuwa ndilo chimbuko na mahali pa majaribio ya mavazi ya mjini.

### 5.16.2 Ni Mwiko Kuvaa Nguo za Kubana kwa Wanaume na Wanawake

Mavazi yalikuwa ni kielelezo kikubwa cha tabia ya mtu katika jamii ya Wabungu. Watafitiwa walisema kuwa watu wanavaa nguo kama wazungu, kama wapo katika nchi ya wazungu. Mzee Thomas Bangu alitoa mawazo yaliyolingana na (P’Bitek, 1972). Kwa kuangalia mavazi tu tunaweza kueleza tabia ya mtu kama ni mbaya au nzuri. Nguo za kubana zilihusishwa na uhuni au umalaya na mambo ya kutabii makundi mabaya ya mijini, wageni washenzi, wasokwao.

Katika jamii ya Wabungu hakuna nguo au mavazi ya kuogelea au mavazi maalumu ya kuchezea muziki wa kisasa. Kwa hali hiyo vazi ni vazi ambalo linaweza kuvaliwa mahali popote mbele ya watu. Nguo maalumu ni ile ya kuvaa wakati wa kwenda

Kanisani au Msikitini. Hii ni lazima iwe imefuliwa na kupigwa pasi vizuri. Hata wakati wa kucheza ngoma, wachezaji walivaa nguo zilizo sitiri maungo na wanawake walivaa demu ili kuacha mabega wazi wakati wa kucheza *makala* au *simba kaleinde.*

### 5.16.3 Ni Mwiko kwa Wanawake Kuvaa Nguo Fupi

Mavazi yanatafautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Hilo halitoshi, na kila jamii ilikuwa na aina yake ya uvaaji kutegemeana na shughuli za jamii hiyo. Aidha, tafauti ya mavazi tu si hoja bali uvaaji pia ulitafautiana sana. Wabungu si kama Wamasai. Jamii hizi mbili zinatafautiana kwa shughuli na mila ingawa sisi sote ni Waafrika.

Katika jamii ya Wabungu, mavazi ni kielezeo cha tabia njema ya utu uliokamilika kwa mwanaume au mwanamke. *Vazi* ni nguo yoyote inayovaliwa *kusitiri* mwili. Kusitiri ni kitendo cha kuficha jambo la aibu ili lisijulikane au kitendo anachofanya mtu kumkinga na fedheha. Nguo za kubana au fupi zilikuwa zinaashiria usasa na maisha ya mjini ya uhuni. Wabungu walikuwa na desturi ya kuvaa nguo zilizofunika mwili hadi chini ya magoti. Kwa mujibu wa bibi Ilonga na mzee Fredrick Bangu, (P’Bitek, 1972) wao walisema nguo fupi na za kubana ni matokeo ya kutabii mavazi ya wageni wa mijini.

Msichana aliyeonekana kukengeuka kimavazi, alikuwa hafai kuolewa kwani ni muhuni. Mifano hai ilitolewa kwa kuwataja watu majina ambao waume wao walipokuwa katika hatua ya uchumba waliwaonya kuwa msichana huyo au yule ni mhuni na kuhoji kama mtafiti alikuwa haoni hali hiyo. Mtu hawezi kuishi naye wataachana lakini kwa kuwa waume na wao walikuwa wamekaa mijini walikataa na

kung'ang'ania ndoa. Ama kweli "ndoa ndoana" kwa msemo wa kisasa, ya wahenga yalitimiya. "Asiyesikia la mkuu ama kweli huvunjika guu". Ndoa zote hizo zilivunjika. Majuto yakawa mjukuu.

Hali hii inatuonesha kuwa dalili za mvua ni mawingu. Miiko ipo ili kutuongoza na kutukumbusha sehemu ambazo tunakengeuka au kuwaeleza wenzetu athari ya jambo kabla halijatokea ingawa mara nyingine wahenga walisema; "sikio la kufa halisikii dawa".

### 5.17 Miiko kwa Viongozi

Wabungu kama jamii nyingine hapa duniani na Tanzania kwa ujumla walikuwa na viongozi. Kwa mtu kuwa kiongozi alipaswa kuiishi miiko ya viongozi. Mzee mmoja alisema kuwa ingawa "Umwene" ulifutwa kiserikali, lakini bado kama Wabungu wanapaswa kuwaheshimu viongozi wao. "Mwene" bado yupo na wanamheshimu na kumpa stahili zake kama "Mwene". "Mwene" alikuwa na wajibu maalumu kwa jamii ya Wabungu. Hata sasa wanatarajia mtu anayechaguliwa kuwa kiongozi, anapaswa kuwa na maadili na kutimiza wajibu wake. Mtu huyu anapaswa kujiheshimu na kuwaheshimu watu anaowatawala au kuwaongoza.

Mzee mtafitiwa, alisema kuwa hata siku moja Mwene hakutarajiwa kuwa mwizi. Kutoa kisingizio cha kutokutimiza wajibu, kushindwa kutoa uamuzi kwa wakati. Kama kesi au shauri lilikuwa na utata au refu, basi giza ndiyo iliyofanya kuahirishwa kwa suala hilo mpaka kesho yake. Kama mvua imechelewa kunyesha, basi Mwene aliamuru tambiko kufanyika kwa kufuata utaratibu wa mila na desturi za Wabungu.

Tambiko lolote lilikuwa na mahitaji maalumu. Mara nyingi wanyama walitumika katika kutambika. Wanyama kama kuku, kondoo, mbuzi au ng'ombe.

Mnyama wa tambiko alipaswa kuwa zao la ndani ya jamii ya Wabungu. Mnyama wa kununua, kutoka nje ya jamii ya Wabungu au kutoka kwa mkazi ambaye si Mbungu hakuwa halali ya tambiko lolote. Hili lilikuwa ni fundisho kwa wanajamii kuwa na wajibu wa kumiliki mali ya halali wakati wote katika jamii. Mzee huyu alitoa mifano ya hali ya sasa kuwa hali ya uwajibikaji si nzuri. Viongozi na jamii kwa ujumla hawajui wajibu wao. Ukame hata zamani ulikuwapo, lakini sasa umezidi. Hii ni kwa sababu ya kuvunja miiko. Wizi sasa ni balaa zaidi. Kiongozi anadiriki kuiba mpaka chama cha ushirika kinafilisika kabisa. Kiongozi katika kesi anapokea rushwa na kuvuruga kesi kabisa na kutoa ushahidi wa uongo (Msokile, 1990).

Watafitiwa wote walisikitishwa sana na hali ya maadili ya viongozi. Walisema ndiyo maana hadi sasa sehemu hii ni maskini. Uongozi wa sasa waliufananisha na uongozi wa bata ambaye anatanguliza watoto mbele na yeye anabaki nyuma na kama kuna hatari ya shimo au maji, basi mama anakapofika watoto wote wameshaangamia kwa kutumbukia shimoni au majini.

### 5.17.1 Ni Mwiko kwa Mwene Kuingia Katika Eneo la Mwene Mwingine Bila Taarifa, Ataleta Balaa Katika Nchi Yake

Wabungu waliheshimu utawala wao na utawala wa machifu wengine wa jirani. Kuingilia eneo la Chifu mwingine ilisababisha kutoelewana, kutoaminiana, kutoajibika na hata vita. Hivyo Mwene aliwajibika kwa vifo vya watu wake. Hapa

mzee Thomas alifafanua kwamba, ilimpasa Mwene yeyote kutoa taarifa kwa mtawala mwingine iwapo alipaswa kusafiri na kupita ama kuvuka katika eneo ambalo halikuwa chini ya utawala wake. Hii ilisaidia kuepusha zahama zilizoelezwa hapo awali. Pia mawasiliano haya yalileta heshima, uelewano na kujenga moyo wa kuaminiana na umoja kati ya watawala jirani.

### 5.17.2 Ni Mwiko Kukalia Kiti cha Mwene

Kwa jamii ya Wabungu kiti cha Mwene kilikuwa ni mamlaka kamili na alama maalumu ya utawala. Kiti hiki kilitakiwa kuwepo mahali pake wakati wote na kilipaswa kukaliwa na Mwene tu, tena wakati wote. Hakukuwa na ruhusa kwa mtu mwingine yeyote kukalia kiti cha Mwene. Huu ulikuwa ni mwiko. Kiti hiki kilikuwa ni kiti cha kutolea maamuzi na hukumu au usuluhishi. Kukikalia lilikuwa ni jambo baya sana. Kwa mujibu wa watafitiwa kwa mtafiti mwiko huu uliweza kufunza adabu na staha kwa jamii kuwa si vema mtu mgeni kukaa kitini bila ya kupewa ruhusa au kukaribishwa kiti na mwenyeji wake anapokuwa ugenini. Ikumbukwe kuwa kila nyumba ina ada na utaratibu wake wa maisha.

Hata hivyo mtafitiwa Ndevu za Shaba alisisitiza katika mazungumzo na mtafiti kuwa, hatari ya kutokaliwa kiti hicho na Mwene ingeweza kusababisha kiti hicho kukaliwa na mtu asiyestahili kwa makusudi, kwa kutokujua, au kwa kukaribishwa na mtu mwingine asiyejua utaratibu na mamlaka juu ya kiti hicho. Shughuli za Mwene ni takatifu hivyo mahali pasafi na patakatifu hapatakiwi kutiwa najisi. Na hilo kama lingetokea basi, ingemaanisha kuwa huo ndiyo mwisho wa utawala wa Mwene aliye

madarakani na kuwa mwanzo wa utawala wa Mwene mpya, au kiongozi halali wa eneo hilo kwa wakati huo.

Mfumo huu wa maisha kwa viongozi wa Wabungu ulimlazimisha kiongozi kuwa katika eneo lake la utawala wakati wote ili kuwahudumia watu wake. Mara baada ya kutawazwa kiongozi aliheshimu taratibu na alibaki (*koundanda/ ikulu*) nyumbani wakati wote tayari kutatua matatizo ya wananchi wake.

Watafitiwa pia walimweleza mtafiti kuwa katika jamii ya Wabungu ukarimu ulikuwa ni sehemu ya jadi. Mgeni yeyote alikaribishwa na kupewa au kuoneshwa mahali pa kukaa. Hivi ndivyo hata mtoto wa Kibungu alivyofundwa. “Mwanangu unapofika ugenini umekaribishwa subiri uoneshwe mahali pa kukaa au kulala”. Si jambo la kheri wala adabu kujiamulia kukaa tu, mgeni atajuaje kama wana mazungumzo yasiyomhusu! Mgeni hanyimwi maji, lakini mgeni huyo hajichukulii maji mtungini. Kwa heshima mgeni alikaribishwa na kuoneshwa mahali pa kukaa. Huko ndiko kumkaribisha mgeni, kinyume na hivyo mgeni atakuwa bado hajakaribishwa.

### 5.17.3 Ni Mwiko Kukataa Amri Yoyote Kutoka kwa Mwene

Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Hivi ndivyo watafitiwa walivyoanza maelezo yao kuhusu mwiko huu. Walifafanuwa kuwa, Mtoto asiye na utii ni chukizo kwa wazazi wake. Hii ni kama laana, popote aendapo kufanya kazi atakuta watu wakubwa. Kwa kuwa mtoto huyu amezowea ukaidi na kiburi, basi ni dhahiri kuwa hawezi kuyashika yote yale ambayo ataelekezwa na wakubwa wake.

Katika jamii ya Wabungu utii kwa wakubwa hakikuwa kitu cha kujihoji kama anaweza, anataka, anafikiri au kujishauri. Mkubwa yeyote anapomtuma au kumwita mtu ilikuwa ni amri kumsikiliza kwanza kabla ya kutoa uamuzi. Hali hii haikuishia kwa watoto tu bali hata kwa watu wazima. Kila mtu ana mkubwa wake. Juu ya yote kila mtu mwenyeji au mgeni wote walipaswa kumtii kiongozi wa eneo husika. Kwa kuwa wakati huo watu walikuwa ni wachache, basi hata Mwene aliweza kuwajua watu wengi anaowaongoza na labda hata tabia zao.

Mwene kama kiongozi alikuwa na mamlaka. Kwa hali hiyo sauti ya Mwene ni mamlaka na ilikuwa ni amri kwa Wabungu. Ilikuwa haipingwi wala kusailiwa isipokuwa ni kutekeleza tu amri itolewayo na Mwene. Kutii mamlaka ilikuwa ni tabia njema katika jamii ya Wabungu. Hii ilikuwa ni kwa wakubwa na wadogo.

#### 5.17.4 Ilikuwa ni Mwiko Kutoa Siri za Baraza au Kikao Chochote cha Usuluhishi au cha Baraza la Wazee

Watafitiwa walisisitiza kuwa, habari ni muhimu sana katika jamii au utawala wowote ule. Habari zinapaswa kutolewa kwa utaratibu maalumu na msemaji mmoja ili kuondoa utata au kuepusha upotoshaji katika kufikisha ujumbe unaokusudiwa kwa walengwa. Kwa kuzingatia hoja hii, Wabungu walijua shida hii na hivyo walikuwa na mwiko ili kudhibiti na kuondoa hali ya kutokuelewana katika jamii kwa sababu ya kupotoshwa kwa ujumbe uliokusudiwa.

Katika jamii ya Wabungu ilikuwa ni mwiko kutoa au kuzungumza habari za vikao vya Baraza la usuluhishi wa aina yoyote au Baraza la Mwene kama wewe si msemaji wa Baraza hilo. Hata kama ni Baraza la usuluhishi, wahusika hawakuruhusiwa kutoa

habari hizi isipokuwa kwa idhini ya mamlaka husika. Mtu aliyetoa habari za Baraza bila ruhusa alihesabiwa kuwa ni msaliti wa jamii. Pia ilikuwa ni mwiko kuzungumza kuhusu tambiko kwa mtu asiyehusika.

Katika jamii ya Wabungu, watu waliuliza maswali mawili kila walipopata taarifa mpya. Kwanza, nani amekuambia? Na swali la pili lilikuwa, je, Mwene ana habari? Hii ilimaanisha kuwa habari zinaweza kuwa na madhara kwa jamii au kwa mtu binafsi. Ili kuondokana na matatizo yasiyo na msingi ni vizuri kuwa na mfumo imara wa kupashana habari. Habari yoyote ambayo haijapitia au kutoka kwa Mwene ilihesabiwa kuwa ni taarifa ya urongo, uchochezi, uchonganishi au taarifa ya udaku.

### 5.17.5 Ni Mwiko kwa Mwene Kwenda Kuoga/ Kuogelea Mtoni au Ziwani

Mwene alihitaji ulinzi wa hali ya juu. Zamani hatukuwa na mazingira kama haya ya sasa. Mito inayoingia ziwa Rukwa pamoja na ziwa Rukwa lenyewe tangu zamani hadi sasa ziwa lina mamba wengi. Hali hiyo wakati huo haikuwa na hadi sasa si salama sana kwa watu, watoto kwa akina mama, sembuse kiongozi mkubwa kama huyo kwenda kuoga au kuogelea ziwani, ingekuwa tukio la aibu sana kwa jamii yote kama Mwene angalikufa kwa kukamatwa na mamba. Mwiko huu ulizingatia ulinzi na usalama wa kiongozi wa ngazi ya juu wa jamii ya Wabungu.S

Watafitiwa waliendelea kumweleza mtafiti kuwa, kazi kubwa ya Mwene wakati wote wa uongozi wake, ni kutoa miongozo, amri na ni kiongozi mkuu wa kutoa amri ya tambiko la aina yoyote. Yeye ndiye anayewaombea watu wanapokwenda ziwani au wanaopata shida yoyote. Mwene anapaswa kuhudumiwa nyumbani na si kwenda sehemu za hatari akiwa anajua kuwa kuna hatari ambayo ingetokea wakati wowote.

### 5.17.6 Ni Mwiko kwa Mwene Kwenda Kuwinda Wanyama, Kuvua au Kutega Samaki, Wanyama au Samaki Wataadimika Kabisa

Watafitiwa walieleza kuwa mwiko huu ulifahamika sana na kwamba hakua Mbungu ambaye hakujua kuwa, Mwene kwenda porini kuwinda au ziwani kuvua samaki kungalileta madhara makubwa.

Mtafiti na watafitiwa wanaona kuwa mwiko huu ulikuwa muhimu kwa kuwa, ziwani kulikuwa na hatari ya mamba. Porini kulikuwa na hatari kubwa ya wanyama wakali kama chui na nyati, bila kusahau nyoka. Kwa hali hiyo kazi kubwa ya Mwene, ilikuwa ni kutambika na kufanya ibada kama matatizo yoyote yangetokea. Mara nyingine wawindaji waliingia kwenye miliki za machifu wengine ulikuwa ni wajibu wa mwene kuomba suluhu au msamaha, Mwene, kazi yake ilikuwa ni kusuluhisha matatizo.

Kwa upande mwingine kama Mwene angedhurika huko mawindoni, basi Wabungu wangebaki kama yatima kwa kukosa kiongozi kwa kuwa kazi kubwa ya Mwene ilikuwa ni kutawala. Kutawala ni pamoja na kuwa kiongozi mkuu wa ibada zote za Wabungu, kwa hali hiyo alihitaji kuwa salama wakati wote kwa ajili ya maisha na ustawi wa Wabungu.

### 5.17.7 Ni Mwiko Kufanya Tambiko kwa Kutumia Wanyama au Mazao Kutoka Nje ya Miliki ya Mwene au Wabungu

watafitiwa wote walieleza kuwa, Wabungu wanaamini kuwa sadaka au tambiko lolote, ni sala ambayo sadaka yake inapaswa kuwa jasho au kazi halali ya mikono ya mtoa sadaka. Kwa hali hiyo sadaka zote zilitolewa kwa kutumia mazao ya shamba au

wanyama wa wenyeji wa jamii ya Wabungu. Sadaka haikuwa kichaka cha kufichia au kusafishia fedha haramu au wanyama walioibiwa kutoka kwa jamii nyingine.

Mwiko huu unatufundisha kujitegemea. Utu wa mtu ni hali ya mtu kuwa na kauli au sauti juu ya masuala yanayomhusu. Hali ya mtu kuwa na utashi. Utu wa mtu hupimwa kwa kazi. Kazi halali inayomwingizia kipato. Umaskini haukukubalika tangu utangu. Hata mizimu haikubali umaskini, ndiyo maana hata sadaka ya kutoka ugenini haikukubalika ili kuepuka kuleta machukizo kwa kutolea sadaka zisizo safi. Usafi wa sadaka umejadiliwa pia katika vitabu vya dini. Mfano wa sadaka ya Abeli na Kaini. Sadaka ya Abeli ilikuwa sadaka safi na ilipokelewa na Mwenyezi Mungu.

### 5.17.8 Ni Mwiko Kutoa Mali au Viti vya Mwene Nje ya Miliki ya Wabungu

Kutoa vitu vya mtu ndani ya nyumba bila ridhaa yake kuna maana ya kumfukuza. Akufukuzaye hakuambii ondoka. Kumfukuza mtu si lazima kumtimua kwa upanga au marungu. Kumfukuza mtu si kulazima kufunga mlango wake kwa minyororo au makufuli ya aina ya VIRO au SOLEX. Kitendo cha kutoa begi au sanduku la mgeni nje inamaanisha kuwa mtoaji anamfukuza mtu huyo. Mtu mwenye akili timamu hawezi kuhoji kitu kinachoendeleya. Pasi shaka atajuwa kuwa siku zake za kuishi katika nyumba hiyo zimetimia na anapaswa kuondoka mara moja.

Hali kadhalika katika jamii ya Wabungu, tangu utangu mali ya Mwene ilikuwa ni ishara ya mamlaka. Kutoa mali au vitu vya Mwene nje ya himaya yake ilikuwa sawa na kumnyan’ganya au kumpindua Mwene katika mamlaka yake. Heshima kwa viongozi wa Wabungu ilikuwa ni jambo la muhimu na mamlaka ilikuwa ni pamoja

na mali ya Mwene, alimaliza bibi Kotilda. Mwiko huu uliwahimiza Wabungu kuwaheshimu viongozi wao. Kumheshimu kiongozi ni pamoja na kumlinda yeye kiongozi pamoja na mali zake.

### 5.17.9 Mawasiliano Kati ya Mzazi na Mtoto

Watafitiwa walimweleza mtafiti kuwa zamani katika jamii ya Wabungu uhusiano kati ya watoto na wazazi au watoto na watu wazima ulikuwa ni wa hali ya juu sana. Watoto walipaswa kuwaheshimu na kuwasikiliza wazazi na watu wazima kwa jambo lolote. Aidha wazazi na watu wazima waliwajibika ipasavyo kwa watoto katika jamii nzima. Mtu mzima alikuwa na ruhusa ya kumtuma mtoto yeyote. Pia mtu mzima alikuwa na mamlaka ya kumwonya mtoto yeyote anapokosa.

Paza alisisitiza kuwa mtoto asiye na adabu hakuweza hata kutumwa na wala kupewa kitu chochote kama zawadi. Wazee walitumia nafasi ya kuwatuma watoto kuwapa zawadi inapobidi. Akitowa mfano alisema, mzee aliweza kufunga nyama kavu au matunda katika mzigo wa minyaa na kumwomba mtoto kwenda kuloweka. Alipompa mzigo huu alimpa maelekezo ya kuufungua na kuufunga vizuri kabla ya kuloweka.

Zoezi hili lilipofanyika mtoto au kijana mwadilifu alifanya kama alivyoelekezwa. Humo aliona kile kilichofungwa ndani na kukitumia. Hali hii haikuishia kula tu bali mtoto huyu alirudi na kutoa shukurani kwa mzee huyu. Kazi yoyote ambayo mtoto alipewa ilifanywa kwa uaminifu na makini kabisa.

Bibi mmoja akishadidia hoja hii, alimweleza mtafiti kuwa, zamani walikuwa na uhuru wa kumtuma mtoto yeyote bila wasiwasi. Siku hizi kama mzee atamtuma mtoto wa mtu bila ridhaa ya mzazi, basi tarajia matusi au lawama. Malezi yamebaki kwa wazazi wa mtoto, televisheni na kompyuta tu. Watoto wanaona kuwa ni wazazi wao tu ndio wenye mamlaka ya kuwatuma. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, kiburi cha watoto kinakomaa na hata wazazi wenyewe hawazezi kumudu kiburi cha watoto wao.

#### 5.17.10 Ni Mwiko kwa Mvulana au Msichana Kutabii Tabia au Maadili Mabaya Kutoka Nje ya Ukoo

Mtafiti alimwelezwa kuwa, Mtoto alipaswa kufuata maadili mema kutoka kwa wazazi wake. Tabia ya kijana ilifananishwa na tabia ya wazazi wake kila wakati. Kwa hali hiyo ukoo mzuri ulijulikana katika jamii wakati wote na kila mwanajamii. Kama kijana ataiga tabia yoyote mbaya kutoka nje ya ukoo, ilionekana ni mwanzo wa kuharibika kwa ukoo huo na kwa watoto watakaozaliwa baadaye. Ndiyo maana (Sengo, 2009) anasisitiza kuwa ya mwanakupona, waachiwe wenyewe na wale waliozalikana kwa misingi ya baba na mama warithishiwe yao, mtoto hujifunza kisogo cha mamaye.

#### 5.17.11 Usipite Katikati ya Watu Wawili au Kundi

Watafitiwa wengi walimweleza mtafiti kuwa, kupita katikati ya watu wakubwa au wadogo, ilikuwa ni kuwakosea adabu watu uliowapita. Kwa watoto ilikuwa ni kukosa heshima na sitara. Akutukanaye, hakuchagulii tusi. Kupita katikati ya watu wakubwa ilikuwa ni kuwatusi na kuwafanya wao ni kama hayawani. Kwa upande wa pili, mtu aliogopa kurogwa au kuvamiwa na watu wabaya.

### 5.17.12 Mwiko Kuiba, Mtu Ataugua Ukoma

Mtu mwenye ugonjwa wa ukoma, alihusishwa na mtu aliyevunja mwiko. Wizi ulikuwa ni moja ya matatizo yaliyosababisha mtu kupata ugonjwa wa ukoma au ndui. Ukoo au familia ya wezi ilitengwa na mtu hakuruhusiwa kuowa au kuolewa. Ilikuwa ni laana kuowa kwenye familia hiyo. Bibi Sigonda alimalizia kubainisha maneno yake. Wizi ni katazo lililobainishwa katika vitabu vitakatifu, hivyo ni tatizo la tangu utangu. Musa alipewa amri kumi za Mungu kutoka juu Mbinguni. Amri mojawapo inasema usiibe.

Ulimbe wa mwiko huu ni wa kifalsafa zaidi. Katika ushirikiano wa wanajamii, kuna mali za watu wote na mali za mtu binafsi. Jamii inalinda mali za jamii kama ziwa mito uoto wa asili na vivuko. Vitu hivi vilitumika kwa manufaa ya wanajamii wote. Kulikuwa na miiko ya kulinda mali hizi. Licha ya mali hizi za jamii, kulikuwa na mali za familiya. Mali hizi zilimilikiwa na familia na mtu nje ya familiya husika alipaswa kuomba na si kujichukulia mali hizi. Kuchukuwa mali ya familia nyingine bila idhini kuliitwa wizi.

Mtu aliyefanya kitendo cha kuchukuwa mali au kitu cha familiya nyingine bila idhini, adhabu ilikuwa ni halali yake. Katika mali ya familiya, kulikuwa na mali ya mtu binafsi, kutegemea na umri wa mtoto wa familia. Watoto waliweza kumiliki hata shamba dogo ambalo kuvuna kitu kulihitaji mmiliki wa shamba hilo kuarifiwa. Kwa hali hiyo mfumo mzima wa maisha ulibainisha utaratibu wa kuomba au kutoa taarifa kwa mwenye mali kuwa mali yake imetumiwa au kuchukuliwa na mtu mwingine kwa matumizi.

Mtu mwenye njaa kuingia shambani na kuchimba viazi au mihogo ili kuganga njaa anapokuwa safarini haikuhesabiwa kuwa ni wizi, isipokuwa mgangaji wa njaa atakapoamua kuvuna na kubeba katika furushi kwa dhamira ya kupeleka nyumbani kwake au kwenda kufanya biashara. Kama mtu ana njaa, lilikuwa jambo la kheri kuiganga njaa yake pale pale shambani na si kubeba chakula hicho, bibi Sigonda alisisitiza.

#### 5.17.13 Ni Mwiko kwa Mvulana Kuwategemea Wazazi, Hawezi Kuoa

Wabungu waliamini kuwa mwanaume rijali ni lazima aowe. Sababu zozote ambazo zilitoa tishio la kutokuoa, zilikuwa ni aibu kubwa, hasa kwa mwanaume kushindwa kujijengea kibanda na kuendelea kuishi katika nyumba ya wazazi wake. Mwanaume alipaswa kufanya kazi kwa bidii ili kuonesha kuwa anaweza kuihudumia familia yake mara tu wakati utakapofika. Mtafitiwa Ndevu za Shaba alisema kuwa mwiko huu uliwafunza vijana wa Kibungu kujitegemea tafauti na sasa ambapo vijana wengi wamekengeuka kwa kukosa malezi ya msingi yanayowafanya kuzingatiya kufanya kazi. Sasa vijana wanataka kila kitu kukifanya kwa njia ya mkato. Matokeo ya tabia hizi ni wizi na ulevi.

#### 5.17.14 Wavulana Walio Balekhe ni Mwiko Kulala Katika Nyumba ya Wazazi, Hawataoa

Mvulana baada ya kubalehe au kabla, alipaswa kuwa na uwezo wa kujijengea kibanda chake cha kulala nje ya nyumba ya wazazi. Kazi ya ujenzi wa nyumba ilifanywa na wanaume. Wanawake au wasichana walijengewa nyumba ya kulala na wazazi au kaka zao kwa kushirikiana na wazazi wao. Mtoto wa kiume alitegemewa

kuoa. Mtu akiowa, ni lazima awe na uwezo wa kutengeneza mahali pa kuishi yeye mwenyewe. Huu ni mwiko unaohusu Mwenendo na wajibu wa kijinsia katika jamii.

### 5.17.15 Ni Mwiko Kumpa Mimba Msichana Nje ya Ndoa Kama Ikitokea, Mhusika Alilazimishwa Kumwoa Huyo Binti

Mtafiti alielezwa kuwa, tendo la ndoa lilikuwa ni haki ya wanawake au wanaume wenye ndoa tu. Ilikuwa ni mwiko kupata mimba au kuzaa nje ya ndoa. Mwiko huu ulikuwa na umuhimu mkubwa sana kwa watu wote katika jamii. Mtoto wa kiume au wa kike kabla ya kuowa au kuolewa alipaswa kuangalia ukoo anaotaka kuowa au kuolewa nao. Kitendo cha kupata mimba kabla ya ndoa, kilikuwa ni kuvunja taratibu za ukoo na kwa hali hiyo watoto waliopeana mimba walipaswa kuowana. Katika jamii ya Wabungu, hakukuwa na watoto waliolelewa na mzazi mmoja isipokuwa kama mzazi mmoja alifariki dunia.

### 5.17.16 Ni Mwiko kwa Mtoto au Kijana Kuingilia Mazungumzo ya Watu Wazima au Kuzungumza Bila Ruhusa

Mtoto mwenye heshima na adabu ni yule msikivu na mwenye subira. Mtoto hakuruhusiwa kuingilia mazungumzo ya watu wazima na kuanza kudakia maneno bila ya idhini au kupewa nafasi na watu wazima wanaozungumza. Mara nyingi lugha ya wazee ilikuwa ni ya mafumbo na nahau nyingi. Kama mtoto ataingilia mazungumzo bila ya ruhusa, mara nyingine alionekana kuwa ni mharibifu. Mwiko huu ulijikita katika kuwafunza watoto kuwa na staha, usikivu na utunzaji wa siri. Maneno anayoyasikika kama hayamhusu, basi hakupaswa kuyasema au kuyapeleka mahali popote. Sikio halizidi kichwa.

### 5.17.17 Ni Mwiko kwa Mtoto Kuanza Kunawa na Kula Kabla ya Wakubwa na Pia Hawezi Kuondoka Mahali pa Kulia Chakula Kabla ya Wakubwa

Mtoto mwenye heshima na adabu ni yule mvumilivu na mwenye subira. Heshima ilianzia kwa wakubwa. Watoto walipaswa kuwaheshimu wakubwa bila kuhoji. Kama chakula kilikuwa tayari, basi mtu mkubwa kuliko wote, ndiye aliyepewa heshima ya kuanza kunawa maji na kuwakaribisha wengine chakula. Chakula kilianza kuliwa mara wote wanapokuwa wameshanawa. Mkubwa hakuruhusiwa kuanza kula mara anapomaliza kunawa. Umoja, ulezi na ushirikiano katika familia ulishadidiwa na mwiko huu.

### 5.17.18 Ni mwiko Mtoto Kuanza Kula Mboga Kabla ya Wakubwa

Mtoto mwenye heshima na adabu ni yule mvumilivu, msikivu na mwenye subira. Chakula kikuu cha Wabungu ni ugali kwa samaki au nyama ya porini. Samaki au nyama haikupatikana kwa wingi wakati wote wa mwaka. Mtoto alipewa kitoweo chake. Alitakiwa ale ugali ashibe, ndipo mwishoni ale nyama au samaki wake.

### 5.17.19 Ni Mwiko Kuondoka, Unapompa Mtu Maji ya Kunywa Kabla ya Kumaliza

Zamani ilikuwa ni mwiko kumnyima maji mtu aliyeomba maji ya kunywa. ‘Maji hayanyimwi’ ni msemo unaoendana na mwiko huu. Lakini mtu aliyempa mgeni huyo maji, alipaswa kumsubiri mpaka kiu yake iishe. Wakati huo, mara nyingi wageni au wazee walikaa nje, chini ya mti, wakipumzika na walikuwa mbali na mtungi wa maji. Ili kukidhi mahitaji ya maji, mpeleka maji hayo, alipaswa asubiri. Kulikuwa na uhalisia wa kusubiri kwani mgeni hangejua mahali pa kuweka kata ya

maji baada ya kunywa. Kata ya maji ya kunywa ilikuwa haiwekwi chini. Aliyejua mahali pa kuiweka ni mwenyeji, mtu aliyemkirimia maji mgeni.

### 5.17.20 Ni Mwiko kwa Binti au Mvulana Kuoa au Kuolewa na Mtu Kutoka Familia ya Watu Wenye Ukoma, Kifua Kikuu, Surua, Kifafa au Ndui, Atazaa Watoto Wenye Maradhi Hayo

Wabungu waliamini kuwa kuna baadhi ya magonjwa ni ya kurithi na hayaponi. Kutokana na imani hii, waliwatenga wagonjwa wa maradhi haya. Kutengwa huko hakukuishia katika ushirikiano na makazi tu, bali hata katika uhusiano wa ndoa. Hakukuwa na ruhusa ya kuoa au kuolewa na familia ya watu wenye maradhi kama, ukoma, kifua kikuu, sulua, kifafa au ndui.

### 5.17.21 Ni Mwiko Kukalia Ungo

Suala la afya na maradhi lilijulikana tangu utangu. Kwa hali hiyo wazee wazamani kwa kulijua hilo waliweka zuio la kuchezea, kuchafua, au kuharibu vyombo vinavyotumiwa katika mandalizi ya chakula. Ungo ni chombo muhimu sana katika maandalizi ya chakula. Wakati wote ungo ulipaswa kuwa msafi na tayari kwa matumizi. Kukalia ungo kulionekana sawa na kusotea kinyesi kwenye ungo ambao baada ya muda mfupi ungetumika kuandalia chakula. Hali hiyo ilihatarisha afya ya watumiaji wa chakula hicho. Si adabu, si uungwana.

### 5.17.22 Ni Mwiko Kujisugulia Mchanga wa Mtoni Unapooga, Unawatabiria Kifo cha Mapema Wazazi Wako

Kujisugulia mchanga mwilini kulifananishwa na kuwaombea kifo wazazi. Ulimbe wa mwiko huu ni kuwa, katika mchanga wa mtoni au ziwani kulikuwa na minyoo na

konokono walioeneza magonjwa. Watu waliojisugulia mchanga, walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kupata ugonjwa wa kichocho au minyoo. Akiugua ndui alikuwa na vipele vingi vidogo dogo ambavyo si rahisi kuvitoa kwa mchanga bila ya kujidhuru na kudhuru watumiaji wengine wa maji.

### 5.18 Miiko kuhusu Kuoa / Kuolewa/ Ndoa

Suala la ndoa ni suala muhimu sana katika jamii yoyote ya watu waliostaarabika. Kuoa au kuolewa si kuwa na uwezo wa kupata watoto, bali ni ile nia ya dhati ya maisha na kujitoa kwa mwenzi uliyemchagua kwa maisha na si kujaribu maisha. Kujenga familiya ni pamoja na kuwa na uhusiano wa karibu na ndugu, na wanajamii wanaokuzunguka. Jamii ilipaswa kuhakikisha kuwa mwoaji au mwolewaji ndoa yao inadumu.

#### 5.18.1 Ni Mwiko kwa Binti au Mvulana Kuowa au Kuolewa na Mtu wa Jamii Tafauti

Katika jamii ya Wabungu, ilikuwa ni mwiko kuolewa mbali au na mtu wa jamii nyingine isiyojulikana. Wakati huo tiba nyingi zilifuata tambiko. Kama mtu ataoa au kuolewa na mtu wa jamii nyingine yakitokea matatizo, ilikuwa ni vigumu kupata tiba suluhishi kwani Mizimu haingeruhusu mtu wa jamii tafauti kufika mahali pa tambiko kwani angeleta balaa katika jamii nzima. Ikumbukwe kuwa shughuli zote za tambiko zilikuwa ni siri ya watu wa jamii husika. Hao ndio walioruhusiwa tu na haikuwa wazi kwa kila mtu. Wabungu hawakuruhusu kuoa mtu nje ya jamii. Bado wazee wanafikiri ni bora kuoa nyumbani.

### 5.18.2 Ni Mwiko Kuoa au Kuolewa Bila Ridhaa ya Wazazi

Ilikuwa ni mwiko kuowa au kuolewa bila ruhusa kutoka kwa wazazi wa pande zote mbili, kwani, kama mtu ataolewa na familia ya wavivu, atapata shida. Uchaguzi wa mke au mume haukufuata uzuri wa sura. Kitu cha msingi kilichoangaliwa ilikuwa ni tabia ya mtu. Wazee walipokuwa wanamjadili mchumba, waliangalia tabia ya familia anayotoka, maradhi ya kurithi au kuambukiza yaliyomo katika ukoo huo na pia Mwenendo binafsi wa kijana anayeoa au kuolewa. 'Asiyesikia la mkuu huvunjika guu'.

### 5.18.3 Ni Mwiko kwa Mtu Kufanya Tendo la Ndoa Nje ya Ndoa Kabla ya Safari, Mtu Atapata Balaa Njiani

Mke ni baraka ndani ya nyumba. Mtu aliyekuwa safarini na akapata matatizo yoyote ilifikiriwa kuwa balaa hiyo imeletwa na mwanaume au mke wake kwenda nje ya ndoa. Wabungu wanaamini kuwa baadhi ya watu wana mikosi au nuhusi. Kama mtu atashirikiana nao kwa namna yoyote ile atarajiye kupata balaa mbele yake. Mwiko huu ulizifanya familia kuwa pamoja na kupunguza magonjwa ya zinaa kwa wanandoa. Ubishi ndiyo uliyoleta laana na balaa la UKIMWI.

### 5.18.4 Ni Mwiko Kuzungumza Masuala ya Ngono na Uzazi Mbele ya Watoto

Masuala ya uzazi yalikuwa na muda maalumu wa kuyafundisha kwa watoto. Mazungumzo ya ngono au mapenzi yalifanywa kati ya watu wenye rika moja. Ilikuwa si adabu kwa mtu mzima kuzungumza kuhusu ngono mbele ya watoto. Hii ilionesha kuwa mtu mzima hajiheshimu na hana ababu. Kwa upande mwingine ilionesha kuwa watu hawa ni wahuni na wasio na maadili katika jamii ya Wabungu.

### 5.18.5 Ni Mwiko Kutoka Nje ya Ndoa, Mke Akiwa Mjamzito, Mimba Itatoka

Ilikuwa ni kosa kubwa sana kwa mwanaume kutoka nje ya ndoa wakati mke wake ni mja mzito. Tangu zamani kulikuwa na maradhi ya kuambukiza kama kaswende au kisonono. Sayansi ya mwiko huu ni kuwa, kama angepata ugonjwa wa kuambukizwa basi, wa kwanza kuambukizwa ni mke ambaye kwa wakati huu naye atamwambukiza kiumbe aliye tumboni. Hali hii ingeweza kusababisha ugonjwa au kifo kwa mama na kiumbe mtarajiwa.

### 5.18.6 Ni Mwiko kwa Mwanaume Kulala Nje ya Nyumba Kama Mke wake ni Mjamzito, Atashindwa Kujifungua

Katika jamii ya Wabungu ilikuwa ni mwiko kwa mwanaume kwenda nje ya ndoa yake wakati mke wake ni mja mzito. Ulimbe wa mwiko huu ni kuzuiya maradhi ya kuambukiza kwa mama na mtoto. Pili msongo wa mawazo wa kumfikiria mumewe kungeweza kuleta shinikizo la damu au kifafa cha mimba na kusababisha mama kujifungua kwa shida. Mwanamke mjamzito alihitaji huruma na mapenzi makubwa ya mume wakati huo na kuepusha mambo ambayo yangeleta shida ya aina yoyote.

## 5.19 Miiko Iliyokusanywa na Mtafiti

Mtafiti ameigawanya miiko aliyoikusanya katika sehemu kuu kumi na tano. Mgawanyo huu umefanywa ili kurahisisha kubainisha kazi za jamii ya Wabungu na kukengeuka kwa maadili ya Wabungu, ukizingatia kufuwawa kwa miiko hiyo. Aidha mgawanyo huu utrahisisha kazi na kuthibitisha ni kwa miiko gani na kwa kiasi gani miiko hiyo imefuwawa. Miiko yote ina umuhimu sawa katika jamii yoyote. Kwa hali

hiyo mgawanyo uliofanywa haukutumia kigezo chochote cha kufuata umuhimu au uzito wa mwiko au kundi la miiko husika.

### 5.20 Miiko Kuhusu Heshima (Vyakula)

Katika jamii ya Wabungu kuna aina nyingi ya vyakula. Chakula cha Mbungu si sawa na chakula cha Wajapani au Wamakonde au Wakongo. Kwa ujumla chochote kiliwacho na mnyama au binadamu huitwa chakula, ingawa kuna baadhi ya jamii watasema hicho si chakula. Mhaya, Mchagga au Mnyakyusa anaposema ndizi ni chakula kwa asili Mbungu ndizi ni matunda. Chakula hakiliwi na mja yeyote na kwa wakati wowote kwa maadili ya Kibungu. Chakula cha mtoto si sawa na chakula cha mwindaji mvuvi au mkulima mtu mzima. Mtu alipaswa kula chakula ambacho kingeweza kulinda afya ya mja. Pia chakula hakiliwi chumbani huo ni uchoyo.

#### 5.20.1 Mwanamke ni Mwiko Kula Mayai, Atazaa Mtoto Mwenye Kipara

Mtafitiwa mmoja alisisitiza kuwa ni mwiko kabisa kwa mwanamke hasa mjamzito kula mayai na ndiyo maana siku hizi wanawake wengi wanakufa kwa matatizo ya uzazi kwa sababu ya kukiuka miiko. Uchunguzi wa kisayansi unaonesha kuwa kula mayai hakuwafanyi wanawake kuzaa mtoto mwenye kipara. Upara ni kasoro ya kimaumbile ambapo mtoto huzaliwa bila nywele. Mwiko huu umewekwa kwa vile hakuna mzazi anayependa mtoto wake azaliwe na kasoro ya aina yoyote.

Wanataalimu wanaeleza kuwa kula mayai mengi kunasababisha kuongezeka kwa protini katika mwili wa mtu. Protini nyingi mwilini husababisha kunenepa kwa mwili wa mama na mwili wa kiumbe tumboni. Kwa hali hiyo, mja mzito anapokula mayai anajiweka katika hali ya hatari hasa wakati wa kujifungua. Jambo hilo

linahatarisha mtoto kukosa njia pale mama anapotaka kujifungua. Ili kumnusuru mama na mtoto wake hulazimika apasuliwe. Ingawaje uchunguzi wa ndani wa mwiko huu juu ya mjamzito kukatazwa kula mayai mengi mantiki yake inakubalika kuwa na matatizo katika kujifungua, lakini hakuna ithibati ya kuzaa mtoto mwenye kipara.

### 5.20.2 Mwanamke ni Mwiko Kula Firigisi, Akila Anaonesha Dharau kwa Mumewe

Kwa mwanamke wa Kibungu, ilikuwa ni mwiko kula firigisi ya kuku au ya bata. Sehemu hii ilipaswa kuliwa na mume au mwanaume tu. Wanawake ambao mtafiti aliwahoji wote walisema si adabu kwa mume kama mke atakula firigisi, na mwiko huu bado wanaufuata hadi sasa. Firigisi huliwa na wanawake watu wazima kama baba hayupo. Wanasayansi wasema kuwa firigisi ina protini nyingi, na kwa hali hiyo kama wanawake watakula firigisi sana watapata matatizo ya uzazi kama ilivyo katika mayai na kusababisha wanawake wajawazito kunenepa mno wao wenyewe na viumbe waliotumboni. Wakati huo hatukuwa na huduma za upasuaji na kwa hiyo mama na mtoto wangekufa kwa kukosa huduma ya upasuaji. Upasuzi si njia bora ya uzazi hata hivyo.

### 5.20.3 Ni Mwiko Kula Gizani, Utakula na Shetani

Shetani ni kiumbe anayetisha kutokana na vitimbwi avifanyavyo kusababisha matatizo kwa binadamu. Hakuna anayekubali kushirikiana na mashetani licha ya kula na viumbe hao. Imeelezwa kuwa watu wanahadharishwa kula gizani kutokana na kuwa chakula kinaweza kuingia mdudu, miiba au mifupa. Vitu hivi vinaweza

kusababisha madhara kooni na kuleta maafa makubwa kwa afya ya mlaji hata kifo. Miiko ni amri za kijamii, zilizosaidia kuhifadhi maadili ya jamii.

Wakati huu watu wanaweza kuona kuwa mwiko kama huu hauna maana yoyote, lakini ni kweli kabisa kuwa hadi sasa mwiko huu una maana kubwa kwa sababu kama mtu atakula gizani, samaki mwenye miiba, madhara kwa mlaji ni kukwamwa kwa miiba hiyo ya samaki. Ni muhimu kuepuka tabia ya kula gizani ili kupata usalama wa chakula kinacholiwa wakati wote.

Aidha kula gizani ni sawa na mtu kula akiwa amejificha. Hii ni tabiya ya uchoyo ambao hata siku moja haukukubalika na jamii ya Wabungu. Ikumbukwe kuwa wakati wa kula lilikuwa ni darasa kwa watoto na vijana na wanajamii wote kwa ujumla. Kwa hali hiyo maana ya mafunzo yalitolewa ili kuwaadilisha watoto wakati wa kula yasingalikuwapo, jamii ingalishindwa kudhibiti ukaaji na ulaji mwema wa chakula kwa watoto.

#### 5.20.4 Ni Mwiko kwa Mwanamke Kula Nyama ya Mnyama Mwenye Mimba, Atapata Shida ya Kujifungua

Ulinzi wa afya ya mama na mtoto ulikuwa ni wa hali ya juu katika jamii ya Wabungu. Mnyama aliyekufa akiwa na mimba, alionekana kama ni mnyama ambaye angalikuwa na matatizo ya aina fulani. Aidha Wabungu walijuwa kuwa magonjwa ya wanyama yanaweza kuwadhuru au kuwaambukiza binadamu pia. Tukizingatia kuwa mtoto mchanga hana kinga ya kutosha mwilini, kwa hivyo angeweza kuambukizwa kwa urahisi zaidi na kuleta matatizo makubwa kwa mama, mtoto mwenyewe na familia.

Katika jamii ya Wabungu wanawake wote wenye uwezo wa kuzaa walipaswa kuufuata mwiko huu wa kutokula nyama ya mnyama yeyote aliyekufa au kuchinjwa na kuonekana kuwa ana mimba. Sababu ya kujifungua ilikuwa ni muhimu sana kwani matarajio ya jamii kwa kila mwanamke ilikuwa ni kuzaa watoto, na pia ilikuwa ni faraja kubwa sana kwa mwanamke kujifungua bila shida yoyote. Kama mwanamke alivunja mwiko hali hiyo ilileta wasiwasi kwa mwanamke huyo na hata kwa uzao wa mwanamke aliyevunja mwiko.

### 5.21 Miiko Kuhusu Bahari na Uvuvi

Bahari au ziwa Rukwa na mito yake, ni muhimu sana kwa shughuli za maisha ya Wabungu. Kila jamii ina mapisi yaliyosababisha jambo fulani kufanyika au kuwepo katika jamii. Ili kutunza mazingira ya ziwa na mito jamii ya Wabungu ilihakikisha kuwa mazingira kando ya mto na ziwa hayaharibiwi wala kuchafuliwa. Pia usalama wa watumiaji ulikuwa ni muhimu kwa sababu ya mamba na nyoka. Wanyama hawa wengi wao makazi na mazalia yao yalikuwa kando kando ya mto au bahari.

#### 5.21.1 Ni Mwiko Kuoshea Vyungu Vyenye Masizi Ziwani, Samaki Watakimbia/ Wataadimika

Usafi wa mwili na mazingira ni mambo muhimu sana katika jamii ya Wabungu. Kwanza kazi za usafi wa ndani pamoja na vyombo zilifanywa na wanawake, kitendo cha kubeba chungu cha kupikia na kukipeleka mtoni au ziwani kwa ajili ya kukisafisha ilikuwa ni alama ya uvivu na tabia ya uchafu.

Aidha, vyombo hivi wakati mwingine vilikuwa na miiba ya samaki au mifupa ya nyama ambayo ingewaumiza watumiaji wa sehemu hiyo ya kusafishia vyombo. Hali

si hiyo tu, pia kwa maelezo ya Bwana Erick Mahella na bi Kotilda Chambo, wanasema kuwa masizi ni uchafu ambao ulisadikiwa kuwa na balaa au giza na kuwafanya samaki kukimbia sehemu hiyo. Kwa sasa hali hii ni sawa na uchafuzi wa mazingira. Kwa wakati huo huo, wanawake walikuwa na miiko ya kufika ziwani na kufanya shughuli za majini. Kazi za majini zilifanywa na wanaume tu.

Mwiko huu wa kuoshea vyungu ziwani, sehemu ya pili ya madhara au matokeo kuwa samaki wataadimika hauna uzito sana kwa watu ambao si wakaazi wa ziwani, lakini kwa jamii ya wavuvi wa ziwani ilikuwa ni muhimu sana. Mtoto anapokuwa na miiko hii, hujikuta ni mtunzaji mzuri wa mazingira na msikivu.

### 5.21.2 Ni Mwiko kwa Wanawake Wakiwa Katika Siku Zao Kwenda Ziwani, Samaki Watakimbia

Katika mwiko huu tunaweza kusema kuwa, mwanamke wa Kibungu, wakati akiwa katika siku zake alikuwa haruhusiwi kufanya kazi nyingi. Alipaswa kupumzika kwani alihesabiwa kuwa ni mgonjwa. Hivyo, kuzuiwa kufika ziwani au mtoni, ni kumpunguzia safari na shughuli ambazo angezifanya na mahali pake kubaki nyumbani na kujifanyia vitu vidogo vidogo ambavyo haviwezi kumchosha. Amri hii ilimzuwia mwanamke kwa kufika sehemu za mazaliya ya samaki na kulinda afya.

Wanawake ni watu muhimu sana katika jamii zote. Kwa hali hiyo jamii ya Wabungu iliona umuhimu wa kuwalinda na hivyo kuwawekea miiko ambayo ingewalinda. Mito inayoingia ziwa Rukwa pamoja na ziwa Rukwa lenyewe, kuna mamba wengi na viboko ambao walikuwa na hadi sasa ni hatari sana kwa maisha ya wakazi wote, hasa kwa watoto na wanawake. Kutokana na hayo, hii jamii ilihofia maisha ya

wanawake kwani walikuwa hawawezi kujilinda. Uvuvi ulikuwa ni shughuli kuu ya Wabungu. Kwa kutumia sababu ya kuadimika kwa samaki ilikuwa na uwezekano mkubwa wa kujenga hofu kwa Wabungu na kufanya watu wote kuhakikisha mwiko huu unafuatwa ili wasije wakakosa samaki.

Mazalia ya samaki yanapatikana kando kando ya ziwa. Kwa mtazamo wa kisayansi, tunaweza kusema kuwa watu wa wakati huo wa zamani, walijua kuwa kama mazalia ya samaki yataharibiwa basi moja kwa moja samaki watapotea au wataadimika kwani watakuwa wameharibu mazalia ya samaki. Zama hizo, hakukuwa na maji ya bomba. Mito na maziwa vilikuwa ni vyanzo vya maji katika uasili wake. Maradhi ya mlipuko kwa wakati huo yalikuwa ni ndoto, kwa sababu ya miiko iliyolinda au kutunza sehemu ambazo zingesababisha maambukizi ya magonjwa. Elimu ya wazee wetu ilikuwa kubwa na yenye manufaa ya moja kwa moja na maisha ya waja wake kuliko kisomo cha kisasa kingi kilichojaa uharibifu wa hali na mambo yaliyokengeuka adabu.

### 5.21.3 Ni Mwiko Kuingia Kwenye Mtumbwi na Viatu

Mtumbwi ni chombo kinachotumika kwa kuvulia au kwa kusafiria kutoka sehemu moja hadi nyingine. Mwiko huu umewekwa kwa matumizi ya mitumbwi ya uvuvi na kusafiria. Mbali na maelezo yaliyotolewa na mtafitiwa Bwana Erick Mahella, mtafitiwa huyo alisema kuwa, watu wanahadharishwa kutokuvaa viatu wanapokuwa katika mitumbwi ili kujihadhari na ajali kwani ajali inapotokea mtu aliyevaa viatu hata kama anajua kuogelea vizuri , atachoka upesi, kinga ni bora kuliko tiba.

Zamani Wabungu hawakujua kuwa kuna viatu maalumu vya kuogelea na katika mazingira hayo ilikuwa ni rahisi kuogelea bila viatu. Kwa upande wa pili matumizi

ya viatu ni pamoja na kujikinga na maradhi, hivyo, viatu hukanyaga sehemu mbalimbali chafu na safi na hivyo si vizuri kwa mtu kukanyaga samaki ambao sasa ni kitoweo kilichovuliwa kuingia uchafu wa viatu. Ni wazi kuwa kitoweo kama kitaingia uchafu kitaleta madhara kwa mlaji. Ulimbe huu kwa Wabungu ni wa tangu utangu. Ajabu leo, watu wanarimbuka na sayansi na teknilojia, kana kwamba ni jambo geni na jipya katika jamii.

## 5.22 Miiko Kuhusu Kazi (Uvivu na Uwindaji)

Kila kazi katika jamii ina miiko yake. Jamii ya Wabungu kama jamii nyingine duniani walikuwa na utaratibu na miiko ya kazi. Kwenda kuwinda au kuvua samaki kulikuwa na utaratibu maalumu. Miiko hii iliwafanya wanajamii wote kuwa na adabu na utaratibu muhimu wa kufanya kazi. Wakati wowote Wabungu walizingatia mugawanyo wa kazi ambazo zilikua ndio ngome na mhimili wa maisha ya wanajamii wote.

### 5.22.1 Ni Mwiko Kwenda Porini Kuwinda Kama Mwindaji Amegombana na Mtu, Atapambana na Wanyama Wakali

Jamii ya Wabungu ilijishughulisha na uwindaji. Safari ya porini kwa madhumuni ya kuwinda ilikuwa na hatari zake. Hatari mojawapo ni wanyama wakali na hasa nyoka. Wabungu waliamini kuwa uhusiano mwema nyumbani ilikuwa ni baraka na mafanikio kwa msafara wote wa watu waliokwenda kuwinda pamoja. Kama mtu angeondoka nyumbani bila amani basi, safari ingekuwa mbaya. Uhusiano mwema katika jamii uliwapa faraja na nafasi ya kutatua shida bila kinyongo. Hii ilikuwa ni kuwadhibiti wale ambao hupenda kuanzisha ugomvi na kwenda safari wakiwa wamewaacha wenzi wao wakiwa katika majonzi.

#### 5.22.2 Ni Mwiko kwa Wanawake Kwenda Kuwinda Porini Usiku, Wanyama Watakimbia

Wabungu waliamini kuwa mwanamke ni kiumbe dhaifu na hawezi kupambana na matatizo yanayohitaji nguvu nyingi katika kuyatatua, kama kukimbia, kupanda juu ya miti au kupigana na wanyama wakali ili kujihami. Kwa kuzingatia hali hiyo, mwanamke alikatazwa kabisa kwenda au kufuatana na wanaume katika shughuli za kuwinda. Pia jamii iligawa kazi kwa kufuata jinsia, kazi za wanawake zilikuwa hasa zile kazi za nyumbani na kulea watoto. Watoto nyumbani wanahitaji ulinzi hasa wanapoumwa na ni mama ambaye huwajibika katika hali hii. Waigaji wana yao lakini mama wa Kiafrika asiye na dosari yoyote, aliukubali umama wake wa kulea jamii kuu.

Mtafiti alitalii wavupepe, mabuku na makala nyingi zilizohusiyana na shughuli za kuua au kuchinja wanyama na hata vita, lakini mtafiti hakuweza kupata orodha ya wanawake waliohusishwa na shughuli za uuaji, kuchinja au kunyonga. Kutoa maisha ya viumbe aghalabu inaoneka kuwa ni kazi ya wanaume. Hali hii inabainisha kuwa wanawake wote katika jamii ya Wabungu kushiriki katika shughuli za uwindaji kama kazi za kawaida ya wanajamii wanawake.

#### 5.22.3 Ni Mwiko Kwenda Kulala Nje ya Ndoa Kama Mtu Anakwenda Kuwinda, Wanyama Watakimbia

Katika jamii ya Wabungu, mke au mume kwenda nje ya ndoa yake wakati mwenzi wake amekwenda mawindoni iliashiria hatari kwa mwenzi wake. Shughuli za uwindaji zilichukua muda mrefu hadi kufikia mwezi mmoja. Wanandoa walifundishwa uvumilivu na tabia njema katika jamii. Wawindaji walihitajika kuwa

imara wakati wote. Watu wanapokuwa mawindoni walitarajiwa kuwa pamoja wakati wote ili kijilinda, kuhofia kuuana kwa watu kujificha kichakani. Kwa hiyo mwiko huu ulikuwa kiungo kikubwa kati ya wawindaji kwani muda wote walikuwa pamoja.

### 5.22.4 Ni Mwiko Kucheka au Kupiga Kelele Mawindoni, Utapotea

Mtu anapokuwa mawindoni au porini, ni sehemu ya hatari sana kwa wanyama wakali na hata kwa shughuli yenyewe ya kuwinda iliyohitaji utulivu ili kutoafukuza wanyama wanaowindwa. Kupiga kelele kungesababisha wanyama wakimbie na kufanya kazi ya kuwinda porini kuwa ya muda mrefu kwa kushindwa kuua wanyama wanaotafutwa. Aidha kucheka mawindoni kulihusishwa na wanyama au vitu vya kuchekesha. Wabungu waliamini kuwa mizimu ya mababu ipo katika maumbo tafauti na mara nyingine ni ya kuchekesha, lakini kama mtu ataona alipaswa kuwa na huruma na kuomba huruma ya Mungu kwa viumbe hao. Hivyo ilimpasa mtu anayewinda anyamaze kimya na kumwomba Mungu huruma kwa viumbe wake.

### 5.22.5 Ni Mwiko Kuruka Nyama Baada ya Kuua Porini, Walaji Wataharisha

Ilikuwa ni mwiko sana kuruka nyama ya mnyama ambaye ameuawa kabla, wakati wa na baada ya kumtayarisha kwa kumchuna tayari kwa kupikwa au kukaushwa. Miguu wakati wote inaaminika kuwa ni michafu kwa sababu inakanyaga vitu mbalimbali. Wakati wowote miguu huwa imekanyaga vitu ambavyo vimenata unyayoni na vinaanguka wakati mtu anatembea. Huu ni uchafu. Tukizingatia kazi ya kuwinda na kuchuna, watu hawa wanakuwa bado hawajaoga kwa muda na hivyo miili yao ni michafu. Kuruka nyama, kuna uwezekano mkubwa wa kudondoshea uchafu, mchanga na vijidudu kwenye nyama safi na kuifanya iwe chafu kwa

matumizi ya binadamu. Ili kuujuwa ulimbe wa jamii ya Wabungu, itampasa mtafiti kupiga mbizi ndani ya jamii ya Wabungu na kuimanya jamii hiyo ndani nje. Hii ni kwa sababu taalimu ina kwao na fasihi ina kwao, na kwa maana hiyo ulimbe wa mwiko huu unapatikana Ubunguni na si Uzunguni.

#### 5.22.6 Ni Mwiko Kukung'uta Mkia wa Mnyama Aliyeuliwa, Walaji Wataharisha

Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao. Taalimu hii inapatikana Ubunguni, ili kuijuwa inampasa mwanataalimu huyo kuijuwa jamii ya Wabungu ndani nje. Licha ya hayo huu ni msingi wa taalimu zote za afya duniani. Hapa ni wanataalimu wa sayansi waliobobea walipokuja Afrika na kujichukulia taalimu ya Sanaajadiiya na kuipeleka ughaibuni, wakajimilikisha na sasa wanarudi kuwafundisha Wabungu masuala ya afya na usafi na kuwatukana kuwa ni wachafu na sasa wanakabiliwa na ugonjwa wa kipindupindu. Haya ni maradhi yaliyoletwa na wageni miaka ya sabini mwishoni hii si jadi ya Wabungu.

Manyoya ya mkia wa mnyama yeyote ni laini na yana uwezo mkubwa wa kunasa uchafu. Wakati wa kuandaa nyama kwa kuchuna na kutoa matumbo, kunaweza kuchanganyika na uchafu huo kwa urahisi. Pia baadhi ya nyongo za wanyama zinaweza kuwa hatari kwa maisha ya binadamu. Taalimu ya mwiko huu inamfunda mwindaji na mchunaji kuwa mwangalifu ili kuepusha madhara kwa walaji wa nyama hiyo.

### 5.23 Miiko Kuhusu Kilimo

Kilimo ni shughuli mojawapo muhimu katika jamii ya Wabungu. Tangu zamani Wabungu walilima mazao kama uwele, ulezi, karanga, njugu mawe na mahindi.

Katika mchakato wa kilimo tangu kuandaa mbegu, kuandaa shamba, kulima na harakati za kulinda mazao yasishambuliwe na wanyama waharibifu kama nguruwe, nyani na tembo, Wabungu walitumia miiko kuhakikisha kipindi chote cha kilimo hadi wakati wa mavuno kuna miiko inayolinda mazao mashambani.

#### 5.23.1 Ni Mwiko Mtu Kula Chakula Shambani Akiwa Amesimama, Mazao Yataliwa na Wanyama

Wabungu pamoja na shughuli za uwindaji na uvuvi, pia hujishughulisha na kilimo. Katika kilimo, Wabungu walikabiliwa na tatizo la wanyama waharibifu kama nyani na nguruwe. Kwa kuwa wanyama hawa wanapoingia shambani wanakata mazao na kuyala wakiwa wima, basi ilionekana kuwa watu wasile kama wanyama hawa. Mwiko huu unajikita zaidi katika malezi ya watoto na maadili mema wakati wa kula. Wakati wa chakula ulikuwa ni wakati muhimu sana kwa kila mwanajamii. Hivyo wakati wa kula, iliwapasa kuwa na adabu na kula wakiwa wametulia.

Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao, mtu anayetumiya ubongo wake hata kama ni mtoto mchanga anaweza kuelezea ukweli na uhalisiya wa kila kinachotokeya mtu anapokula hasa akiwa anatembeya. Ukweli wwa kudondosha chakula haupingiki. Chakula kilichodondoka ovyo kitasababisha ndege kukifuatilia na kukila. Hapa tusisahau wanyama kama panya, ndezi (eisezi) bila kuwasahau kima tumbili na nguruwe. Wote hawa bila shaka watavutiwa na harufu mwanana ya chakula hicho. Harakati hizo za wanyama hawa kufuatiliya na kula kilichodondoka kutasababisha wanyama hawa na wao kutembeya ndani ya shamba na kuanza kutafuta hata kilichofichwa udongoni. Hawa si hayawani pia wana akili za kutafuta chakula.

Mtafiti anapata kigugumizi cha kutamka kuwa taalimu hii inapatikana Uingereza au Urusi. Taalimu hii inapatikana Unyamwanga, Unyiha, Ukimbu na kwao kabisa Ubunguni.

### 5.23.2 Ni Mwiko Kukimbia Ndani ya Shamba, Unaingiza Nguruwe

Shambani ni sehemu muhimu sana. Kilimo cha Wabungu kilikuwa ni cha matuta. Anapolima matuta anafukia majani na kama watoto watakimbia kimbia shambani, watavuruga matuta na au kutawanya mbegu nje ya matuta. Kwa upande mwingine hali hiyo ilisababisha nyasi kuota mapema zaidi kabla hata ya mbegu kuota. Vile vile, Wabungu waliamini kuwa wanyama waharibifu kama nyani na nguruwe wanapoingia shambani wanaingia kwa haraka sana wakiwa wanakimbia.

Jambo la msingi kwa mwiko huu ni kwa aina ya kilimo cha matuta. Kilimo hiki kiliweza kuathiriwa na wanyama wa porini kama kima na nguruwe na ndege kama kwale. Ni vizuri kuhakikisha mazao yamefukiwa vizuri. Kama watu watakimbia kimbia au kucheza shambani, ni wazi kuwa baadhi ya mbegu zitabaki nje na kuliwa na ndege au kima kabla ya kuota. Mwiko huu ulirahisisha kwa mwenye shamba asubuhi kufuatilia mizunguko ya wanyama hawa kwa kuangalia nyayo zao kutoka shambani hadi msituni na kuwadhibiti kwa kuweka mitego. Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao, na kwao ni Ubunguni. Wabungu wanawakaribisha wanataalimu kwenda kujifunza taalimu hii Ubunguni.

### 5.23.3 Ni Mwiko Kumpa Mbegu Mtu Mkononi

Wabungu waliamini kuwa mbegu ni lazima zitafutwe porini au ziandaliwe na mkulima mwenyewe. Kitendo cha kula mbegu kilikuwa ni dalili ya ukata  na uvivu

wa mtu. Kama mtu atapewa mbegu mkononi, ni sawa na mtu kupanda mwenyewe. Kila mtu ana bahati ya kustawisha mazao shambani. Mtu mwenye bahati ya kuotesha maboga akipewa mbegu mkononi, zile mbegu zitakuwa sawa na kwamba mpaji au mtoaji wa mbegu ndiye aliyepanda. Watu waliweka mbegu chini ili anayepanda awe kama ni yeye aliyezizalisha mbegu hizo. Katika mwiko huu kuna maadili ya kuwafanya watu kuandaa na kutunza mbegu na si kungojea kupewa. Hii ilikuwa ni ishara ya uvivu ambao ulikuwa hautakiwi kabisa katika jamii.

#### 5.23.4 Ni Mwiko Kuingia au Kuchukulia Mbegu za Kupanda Shambani Katika Chungu Chenye Masizi, Mtu Hawezi Kupata Mazao Mengi

Wabungu waliamini kuwa uchafu ni tabia, mtu mchafu alikuwa ni hatari kwa familia na jamii kwa ujumla. Vyombo vya kupikia vilikuwa na nafasi kubwa katika kuonesha ni kwa kiasi gani mtu mwanamke ni msafi. Hii ni kwa kumwona mwanamke akitembea na vyungu au sufuria za kupikia kwenda nazo shambani. Usafi ni pamoja na mpangilio mwema wa matumizi ya vitu mbali mbali. Maleba ya ngonani hayavaliwi Kanisani au Msikitini. Nguo za kanisani hazivaliwi shambani. Huu ni utaratibu wa tangu utangu.

Mwiko huu unaonekana kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na usafi. Pia, zamani baada ya Watanzania kuanza kutumia dawa ya DDT kuulia wadudu shambani, mwiko huu uliwakinga Wabungu na athari za sumu hii. Kwa hali hii, ilikuwa ni sababu ya kuweka katazo hili ili kuepukana na watu kupata madhara ya kula sumu na kufa au kupata madhara ya magonjwa ya mlipuko taalimu ina kwao na taalimu hii kwao ni Ubunguni.

#### 5.23.5 Ni Mwiko Kuingia na Ndara au Viatu Katika Shamba la Karanga, Hazitakomaa Vizuri

Wabungu waliamini kuwa kama ataingia shambani na ndara, basi, hata kama karanga zitasitawi majani, lakini chini, karanga hazitazaa. Ndara au kandambili zilikuwa na nafasi kubwa ya kuharibu mimea ya karanga ikiwa shambani. Karanga zinazotambaa, kama mtu ataingia na ndara, anapotembea, ni rahisi kuziburura na kuziacha nje ya udongo na kushindwa kupata maji na virutubishi kwa urahisi.

### 5.24 Miiko Kuhusu Wanawake

Kila jamii ina Ujumi Wake, na taalimu ina kwao na fasihi ina kwao. Nadharia hizi mbili kwa pamoja zinamwonesha mja wa Ubunguni thamani na ulimbe uliomo ndani ya jamii. Inampasa mgeni aimanye jamii ya Wabungu Ndani Nje ili aweze kubainisha sababu zinazosababisha Wabungu katika mazingira yao wawe na miiko ambayo haipo Uzunguni au Upareni. Wabungu tangu utangu walitafiti na kuandika katika bongo za Wabungu na kuendelea kuwarithisha vizalia hadi vizalia vya Wabungu wajibu wa kumheshimu na kumlinda mwanamke wa Kibungu.

#### 5.24.1 Ni Mwiko kwa Mtoto wa Kike Kukaa Katika Kizingiti cha Mlango, Atachelewa Kuolewa

Mlango ni sehemu ya nyumba ambayo watu wema na wabaya hutumia kwa kupita na mara nyingine watu huweka dawa za kujilinda. Ukubwa wa milango ya wakati huo ulikuwa ni midogo sana. Wanawake wajawazito wangeweza kupata matatizo ya kijiumiza. Afya ya msichana ni jambo mojawapo linalochunguzwa na wanaume wengi wanaotafuta wachumba.

Kwa hivyo, msichana kuwa mgonjwa hasa yanayohusiyana na afya yake ya uzazi, inaweza kuwa sababu ya kukosa au kuchelewa kuolewa. Kwa hali hiyo, mwiko huu unatoa vitisho kwa wanawake juu ya kuchelewa kuolewa, jambo ambalo wasichana wengi hawako tayari. Kiuhalisia, watafitiwa wameeleza kuwa msichana anaweza kuhatarisha afya yake ya uzazi kutokana na kizingiti kilivyo. Watu wengi wanaopenda kukaa kizingitini, hujisikiya maumivu wanapoinuka. Kortilda, alimweleza mtafiti kuwa mwiko huu ni muhimu sana kwa wasichana kwani mlangoni kunawekwa vitu vingi ambavyo vinaweza kumdhuru.

### 5.24.2 Ni Mwiko kwa Mwanamke Kupika Akiwa Katika Siku Zake

Mwanamke katika jamii ya Wabungu ni mtu ambaye alipewa uzito wa hali ya juu sana. Ili kulinda afya yake, ilikuwa muhimu kwa jamii kuweka miiko ambayo ingewafanya wanaume kuwasaidia kazi wakati mwanamke akiwa katika siku zake. Aidha lilikuwa ni suala la kiafya. Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao na ili kuimanya miiko ya jamii ya Wabungu na ulimbe wake inampasa mtafiti kuijuwa jamii hii ndani nje. Humu ndimo ulimo Ujumi wa jamii ya Wabungu.

Wabungu walithamin nakuona umuhimu juu ya suala hili. Katika tafakari ya kina mtafiti alikumbushwa kuhusu maisha ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) katika kambi ya Bulombora mkoani Kigoma na ED - ya matroni. Pamoja na shughuli nzito za jeshi na maafande kutopokea visingizio vya aina yoyote, lakini ED ya Matroni iliheshimiwa kama lulu bila kuhoji. Daktari wa kikosi hakuwa na usemi wala swali juu ya ED ya Matroni. Huu ni ukweli, hii ni heshima ya mwanamke, hii ni haki ya mwanamke.

#### 5.24.3 Ni Mwiko kwa Mwanamke Kuchuma Mboga za Majani Akiwa Katika Siku Zake, Mboga Zitakauka

Mwiko huu licha ya kuzungumzia suala la kuchuma mboga, jambo la musingi linalojitokeza ni kazi na afya ya mwanamke. Wanawake kwa maumbile yao wakati wa siku zao wanapaswa kupumzika ili kuurejeshea mwili uzima wake. Eneo la Wabungu kijiografia halina mvua nyingi sana. Kilimo cha mazao ya chakula ni nguzo ya maisha ya watu wa kawaida. Mazao kama maboga yalitumika kwa mboga hasa kiangazi. Watu walipaswa kulinda mimea hii ili isikauke. Kama ingekauka ingekuwa shida kubwa. Kwa kuwa na amri hii, kulitoa nafasi ya kuwalinda wanawake na kuwaonea huruma kwenda shambani kutafuta mboga badala ya kupumzika na kulinda afya zao.

#### 5.24.4 Ni Mwiko kwa Mwanamke Kumshika Mtoto Mchanga Ambaye si Mtoto Wake Akiwa Katika Siku Zake

Siku hizi zina siri nyingi mno. Ni kwa usalama wa mtoto na hasa akiwa si mtoto wa mama mwenye shida hizo. Siri hizi hubaki kuwa ni mizungu ya kirombo kuwaficha wasungo. Si yote ya kuwekwa wazi. Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao. Ulimbe wa mwiko huu hauhitaji mtafiti kuchukuwa sampuli zozote na kuzipeleka kwa mkemia mkuu wa serikali au TBS ili kuthibitisha ukweli.

Wajibu wa mama hauwekwi rehani kwa mama mwingine mama mzazi angali hai. Hiki ni kichekesho cha maendeleo kwa kumwachiya yaya mtoto kutwa nzima. Wazungu wenyewe waliotuleteya mizungu hii wanaweza kuchukuwa likizo hadi mtoto akatembeya akiwa analipwa rupia. Matokeo ya zahama hii ni matatizo lukuki ya afya za watoto zinazojitokeza.

### 5.24.5 Ni Mwiko Kupakua Ugali Bila ya Kuuviringa Vizuri, Hasa kwa Wageni, Wakwe na Mume

Uhodari na usafi wa mwanamke ulikuwa ni pamoja na maandalizi mazuri ya chakula. Chakula kilipoandaliwa wakati huo, ugali lazima uviringwe vizuri. Ugali ulikuwa haupelekwi sebuleni ukiwa ovyo ovyo ni lazima uwe laini na wenye umbo la kupendeza. Kitendo cha kupeleka ugali bila ya kuuviringa kilikuwa ni sawa na kumdharau mlaji na kwa upande wa pili kuonesha kuwa mpishi hakufundika vizuri unyagoni. Akutukanaye hakuchagulii tusi. Mapambo ya chakula ni ya tangu utangu katika jamii ya Wabungu. Mambo yote haya yalifundishwa nyumbani na unyagoni. Sasa taalimu hii inapatikana katika shule za Upishi bila kuwataja waanzilishi wa taalimu hii kuwa ni Wabungu au Wangoni au Wayao au Wakwere. Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao, na kwao ni Afrika baba wa taalimu ulimwenguni.

### 5.24.6 Ilikuwa ni Mwiko kwa Mwanamke Kumpa Mume Chakula Bila Kuonja

Zamani wanawake na wanaume hata mume na mke walikuwa hawali pamoja. Kwa kawaida chakula kilipikwa na kupelekwa barazani ambako watu wote wa kiume walikula pamoja. Kama mume hayupo au anahitaji kitu chochote cha kula basi ilikuwa ni wajibu wa mke, anapokileta akionje kwanza. Hii ilikuwa ni ishara ya mapenzi kwa upande mmoja na kwa upande wa pili kumhakikishia mume kuwa kitu hiki ni salama kabisa, hakina sumu au dawa ya aina yoyote aliyoiweka au ya kufisha.

Katika jamii ya Wabungu ilikuwa ni tabia ya uchoyo kwa mwanaume kutaka kula peke yake na wote wenye tabia kama hiyo, walikuwa na hofu ya kuwekewa dawa. Mwiko huu ulihusu chakula chochote kwa mgeni, ulikuwa ni wajibu wa mwenyeji kuhakikisha mgeni hali chakula peke yake. Mtu hali chakula peke yake, hii ni tabia

ya uchoyo. Wakati wote katika jamii ya Wabungu chakula kililiwa barazani. Hii ni taalimu ya Wabungu.

### 5.24.7 Ni Mwiko kwa Mwanamke Kutoka Nje ya Ndoa Mumewe Anapokwenda Safari ya Kuwinda, Mumewe Atapata Balaa au Hawezi Kuua Nyama

Ndoa katika jamii ya Wabungu ilikuwa ni kitu cha heshima kubwa sana. Kwa hali yoyote ile, mume akiwa hai mke alikuwa haruhusiwi kwenda nje ya ndoa yake. Wabungu waliamini kuwa kutoka nje ya ndoa ni kuleta balaa na mikosi kwa mume hasa anapokuwa amesafiri au amekwenda kuwinda au kuvua samaki.

Kwa hali hiyo mwiko ukawekwa kuwa, kama mwanamke atakwenda nje ya ndoa basi mumewe atapata balaa kitu ambacho hakuna mtu ambaye alikuwa tayari kuwa chanzo cha kifo cha mume. Kisayansi tunaona kuwa tendo hili lingeweza kuleta matatizo ya magonjwa ya kuambukiza kama kifua kikuu au magonjwa ya ngono kwa wakati huo. Paza alimweleza mtafiti kuwa wakati huo, karibu kijiji chote kilikaliwa na watu karibu wa ukoo mmoja na kwa kwenda nje ya ndoa kulikuwa na uwezekano mkubwa wa kwenda nje ya ndoa na kuleta maradhi ya kuambukiza kwa mwenzi wake ambaye yupo safarini.

### 5.24.8 Ni Mwiko Kufunga Mlango Mchana Mume Akiwa Amekwenda Kuwinda, Mke Atakuwa Amefunga Pori na Mume Hawezi Kuona Wanyama

Kufunga mlango kulikuwa na maana kuwa nyumbani hakukuwa na mtu. Kama mume amesafiri, basi mama alikuwa anabaki kama mkuu wa boma. Kiimani, Wabungu wanaamini kuwa mchana ni salama na kama mtu anafunga mlango basi

anaondoka nyumbani au anafanya kitu cha siri ambacho si ruhusa kwa mila za Wabungu. Kwa wakati huu, mwiko huu unaweza kusaidia kuzuia hatari ya kuacha mlango wazi. Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao, mwiko huu kwao ni Ubunguni.

## 5.25 Miiko Kuhusu Watoto

Katika jamii ya Wabungu utunzaji wa watoto wachanga ulipewa kipaumbele. Mtoto alilindwa kwa mahala alipokuwapo pamoja na mavazi yake. Malezi bora na uwajibikaji wa mzazi hasa mama katika kuhakikisha mtoto hapati maradhi ulizingatiwa kinyume cha hali hiyo basi mwanamke aliwekwa katika kundi la watu wasiowajibika na wenye tabia mbaya katika jamii.

### 5.25.1 Ni Mwiko Kumshtua Mtoto, Usiku Ataota Ndoto za Kustuka Usiku

Helena alimweleza mtafiti na kusisitiza kuwa ni mwiko kabisa kumshtua mtoto. Mwiko huu una msingi wake katika saikolojia na sayansi ya makuzi ya watoto. Aidha mwiko huu unawanusuru watoto na vitisho au kushtuliwa pasi na sababu. Vitisho huwafanya watoto kuwa waoga na kushindwa kujiamini na hata kuchangamka. Kwa vile akili zao hazijakomaa vya kutosha kuhimili mishtuko. Watoto huongeza hofu na kuogopa mambo mbalimbali wanayoyaona. Hofu na woga unaweza kusababisha maradhi. Kwa mfano, mtoto kuingiwa na homa hasa degedege.

### 5.25.2 Ni Mwiko Kufulia Nguo za Mtoto Mchanga Mtoni

Kinyesi ni najisi. Nguo zenye kinyesi zinapofuliwa mtoni huyaharibu maji ambayo watu huyatumia kwa kufanyia shughuli mbalimbali. Maji yenye kinyesi yanaweza kusababisha maradhi ya kuambukiza kama vile kuharisha. Watafitiwa waliongeza kuwa, ingawaje mwiko huu umezitaja nguo za mtoto tu zenye kinyesi kuwa

zisifuliwe mtoni, ni muhimu pia kuacha kufua nguo mtoni bila kujali kama zina kinyesi au la ili kuepusha maji yasichafuke. Mtafiti aliona kuwa mwiko huu umetaja kinyesi kama ndicho kitu pekee kinachochafuwa maji, lakini viko vitu vyingine ambavyo pia vinaweza kuchafuwa maji. Kwa mfano, mkojo na matapishi, Mwiko huu ni muhimu kutekelezwa katika jamii ili kulinda ikolojia ya viumbe hai na ustawi wa jamii ya Wabungu kwa ujumla.

Mtafiti alipiga mbizi zaidi kilindini na kuangaliya mzunguka mzima wa utaratibu na mahali pa kufulia, maji yenyewe na mahali pa kuanika. Nguo za mtoto kufuliwa katika sehemu hizo zinaweza kubeba mchanga au konokoko wa maradhi na kumdhuru mtoto atakapovalishwa nguo hiyo. Licha ya hayo nguo iliyoanikwa kwenye majani inaweza kubeba majani yanayowasha na kumwathiri mtoto atakapovalishwa. Lisemwalo lipo kama halipo basi lisubiri laja. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao, taalimu hii inapatikana Ubunguni. Suala la kupiga pasi nguo halikuwapo wakati huo, hivyo kila kitu kilifanywa kwa tahadhari kubwa ya kumwepusha mtoto na maradhi ambayo yangeweza kuepukika.

### 5.25.3 Ni Mwiko Kwenda Msalani na Nguo ya Kubebea Mtoto

Wabungu wanaamini kuwa msalani ni mahali pachafu. Kuingia na nguo ya kubebea mtoto msalani, kulikuwa na uwezekano mkubwa kwa nguo hiyo kuingiwa na vijidudu au vimelea vya magonjwa na kuleta madhara kwa mtoto. Usafi wa vitu vya kutumiwa na mtoto ni kinga bora ya maradhi. Mtafitiwa mmoja alimweleza mtafiti kuwa kwa kuingia na nguo ya kubebea mtoto chooni, nguo hiyo inaweza kuingiwa

na shetani. Kwa maelezo hayo shetani ni vijidudu vya maradhi. Huu ni ukweli wa taalimu ya Wabungu inayohusiyana na Elimu ya Afya ya Mama na Mtoto.

### 5.26 Miiko Kuhusu Wanaume

Katika kila jamii kuna mgawanyo wa kazi na wajibu wa kila mtu kufuata jinsi. Ujumi wa jamii nyingi sasa unawekwa rehani kwa visingizio vya usasa, uvivu na kutokuwajibika kwa wanajamii. Sheria za jamii zilizotawala mienendo na maadili zilikuwa na nguvu kabla ya kuyeyushwa na maingilio ya wageni na sasa Wabungu wanaona kuwa hali ya kujisasa ndiyo hali yao ya asili. Ulinzi na usalama ilikuwa ni kazi mojawapo ya wanaume. Sasa ni kinyume vitu vyote vilivyowaunganisha Wabungu vimeondoka.

#### 5.26.1 Ni Mwiko kwa Mwanaume Aliyeoa Kuingia au Kupika Jikoni, Atakuwa Ameolewa na Mwanamke

Katika jamii ya Wabungu, kazi ziligawanywa kwa kufuata jinsia. Ilikuwa ni kitendo cha aibu kwa mwanaume kufanya kazi za wanawake au kukaa mahali ambapo wanawake wanafanyia kazi. Basi jikoni ni sehemu muhimu sana kwa kazi za mwanamke. Kwa mwanaume kwenda kukaa au kupika jikoni wakati ameowa, kulionesha ni kwa kiasi gani mwanaume unatawaliwa na mkewe. Mwanaume yeyote hangependa huambiwa kuwa anatawaliwa mke wake, hali kadhalika mwanamke hangependa na ingakuwa jambo la aibu kuambiwa kuwa anamtawala au amemkalia mume wake. Suala zima ni la kuaminiana katika maisha na kupeana nafasi ya kuonesha umahiri katika kutimiza wajibu kama mke.

Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao, Ulimbe wa taalimu unapatikana katika jamii husika, hii ni jamii ya Wabungu. Licha ya mgawanyo wa kazi za nyumbani, na

wajibu wa kila mwanandoa kutimiza wajibu wake, mwanamke anahitaji faragha. Faragha ya mavazi hadi ya maongezi. Wanawake walipaswa kukaa peke yao na kutumia nafasi hiya kuwafundisha wasichana wao mambo yanayowahusu kama wanawake. Hali kadhalika wavulana walikaa na wanaume wakifundishwa kazi za kiume katika jamii. Tabiya mwanamume kukaa jikoni kungemnyima mkewe uhuru wake wa kuchanganyika na wanawake wenzake. Thomas, alimweleza mtafiti kuwa kama mwanamke yupo katika siku zake basi mume alipika na chakula kiliandaliwa bila kujua kama ni mume aliyepika chakula hicho. Mwiko huu ulimlazimisha mume kumpa nafasi mke kushirikiana na wanawake wenzake na si kujifungia ndani na mumewe wakati wote.

### 5.26.2 Ni Mwiko kwa Mwanaume Kukalia Kinu Ataota Majipu Makalioni

Kinu ni chombo muhimu ambacho kinahitajika kuwa kisafi wakati wote. Kinu kilitumika kuandalia chakula. Ni muhimu kuheshimu mahali pa kuandalia chakula kwa ajili ya kuepuka maradhi. Kwa kawaida kinu kiliwekwa jikoni au uwani. Wanaume mahali pao pa kuzungumzia palikuwa Barazani mbele ya nyumba chini ya mti. Kwa hali hii hapakuwa na sababu ya mwanamume kwenda kuchukua kinu na kukitumiya kama kiti.

Pia kwa heshima chakula kiliandaliwa kila mgeni anapofika. Kwa mila na ada za Wabungu, ilikuwa si heshima kwa mwanamke kumtoa mwanamume mahali alipokalia. Hili lingalikuwa tatizo kubwa. Kila kitu kilikuwa kwa ajili ya matumizi maalumu, hivyo wanaume walipaswa kujiandalia mahali pao pa kuongelea na kujitosheleza kwa vifaa vya kukalia.

#### 5.26.3 Ni Mwiko kwa Mwanaume Kukalia Kinu Akikijambia, Atakapoowa Kila Mke Atakuwa Anakufa

Kinu ni chombo muhimu ambacho kinahitajika kuwa kisafi wakati wote. Ni muhimu kuheshimu mahali pa kuandalia chakula kwa ajili ya kuepusha maradhi. Hofu ya kujambia ndani ya kinu ina maana ya ndani zaidi, kama kusotea, huenda mtu alikwenda haja na hajafanya usafi vizuri. Hili lilikuwa na tatizo la kiafya na kimgawanyo wa kazi. Kama mwanaume atakuwa amekalia kinu inaweza kuwa ni vigumu kwa mwanamke kumwomba kuondoka na kukaa mahali pengine. Aidha maelezo ya mwiko wa "*ni mwiko kwa mwanaume kukalia kinu ataota majipu makalioni*" yanahusika.

#### 5.26.4 Ni Mwiko Kumpiga Mwanaume kwa Ufagio, Atapooza

Wabungu wanaamini kuwa ufagio ni mchafu. Kwa mfano, ufagio husafishia maeneo mbalimbali kama vile chooni. Hivyo huchukuwa uchafu mtafiti alielezwa.
Bado maelezo ya kitaalimu zaidi yanahitajika kufafanua athari iliyopo iwapo mwanaume atapigwa na ufagio. Ni wazi kuwa, athari inayohofiwa ni kutokana na kuwa ufagio una ncha ambazo zinaweza kumchoma mtu kama atapigiwa. Vile vile, kwa vile ufagio husafishiwa maeneo machafu kwa hiyo unaweza kuchukuwa vijidudu vya maradhi na kumwingiya mtu mwilini.

Mwiko huu una mantiki ndani yake lakini tunaweza kujiuliza kuwa kwa vipi unasababisha madhara ya kupooza. Vile vile kutokana na ufafanuzi uliotolewa kabla ni wazi kuwa madhara yanaweza kumpata hata mwanamke. Ukweli ni kwamba hakuna mwanamke, mama yeyote ambaye angependa mtoto wake wa kiume apoteze uwezo wa uume wake.

#### 5.26.5 Ni Mwiko Kukojowa Mtoni au Ndani ya Maji Uume Wako Utavutika

Tendo la kukojoa mtoni ni jambo ovu kwani husababisha maji kuchafuka. Mwiko huu unahimiza kutunza vianzio vya maji ili kujikinga na maradhi, kama kichocho ambacho huenezwa kwa kuoga maji yenye vijidudu vya kichocho. Kama mtu mwenye ugonjwa atakojoa majini basi anaweza kueneza vijidudu. Vile vile katika miiko iliyotangulia ilielezewa kuwa nguo za mtoto zenye kinyesi zisifuliwe mtoni. Lengo la mwiko huu ni moja la kutoyaharibu maji ambayo yanatumika kwa shughuli mbalimbali sanjali na kulinda afya na maisha ya Wabungu. Erick na Paza walieleza.

#### 5.26.6 Ni Mwiko Kuingia Kaburini na Viatu

Kaburi ni mahali pa kuheshimiwa kama mahali patakatifu pa kutolea sadaka. Viatu ni vitu vinavyokanyaga uchafu wa aina mbalimbali. Ingawa maiti hulazwa udongoni, lakini mahali hapa panapaswa kuwa safi na kutokutiwa najisi. Kukanyaga kaburini na viatu ni sawa na kupanda kitandani na viatu. Kiimani hapa ni mahali pa tambiko na kutolea sadaka, panapaswa kuhesimiwa. Mzee Mahella na Federiko walimweleza mtafiti. Utakatifu wa mahala na namna ya kupaingia unashadidiwa na vitabu vyote vitakatifu Biblia na Quruan Takatifu.

### 5.27 Miiko Kuhusu Maradhi

Suala la karantini ya maradhi halijaanza leo Ubunguni. Mtafiti anamrejelea mtafiti wa sanaajadiiya Mzee Prof. Dkt. Sheikh Sengo kuwa Afrika ni baba na Mzazi wa taalimu zote. Tangu zama za kuumbwa kwa ulimwengu huu, Wabungu walipoanza kuishi hapa duniani, walijuwa maradhi ya kuambukiza na yale ya kurithi. Kwa sababu hiyo Wabungu wakaweka miiko lukuki kuhusu kuwalinda wanajamii dhidi ya maradhi.

#### 5.27.1 Ni Mwiko Kuishi au Kuchangia Vitu na Wagonjwa wa Ukoma, Kifua Kikuu, Surua, Kifafa au Ndui

Magonjwa ya kuambukiza yalijulikana tangu zamani katika jamii ya Wabungu na kusababisha kuweka miiko ya kuwatenga wagonjwa wa maradhi ya kuambukiza. Wakati huo tiba ya magonjwa hayo, ilikuwa haba na nadra. Ili kudhibiti usambaaji wa maradhi hayo wagonjwa walitengwa na vitu walivyovitumia, havikutumiwa na watu wengine. Mwiko huu unafanana na mwiko wa kuoa au kuolewa na mtu mwenye kilema au maradhi ya kuambukiza.

### 5.28 Miiko Kuhusu Usafiri

Zamani hizo Wabungu walitumiya njia mbili kuu za usafiri. Njia ya maji, mitumbwi na njia ya nchu kavu usafiri wa miguu. Kufuatana na mazingira ya hatari za njiani, msafiri alipaswa kuondoka nyumbani au ugenini salama bila lawama au shari ya aina yoyote. Uchafu wa aina yoyote haukuruhusiwa wakati wa safari au kabla ya safari. Tahadhari zote za afya zilichukuliwa. Misimu ilizingatiwa na msafiri alipaswa kuwa amerudi kabla ya msimu wa kilimo kuanza ili kuepuka njaa.

#### 5.28.1 Ni Mwiko kwa Mwanamke Mjamzito Kutembea Mwendo Mrefu Usiku

Wanawake wajawazito waliruhusiwa kufanya kazi zote nyumbani na jirani na nyumbani. Ilikuwa ni mwiko kabisa kwa mwanamke mjamzito kusafiri muda mrefu na hasa usiku. Ulimbe wa mwiko huu ni wazi, usiku kuna hatari nyingi. Usiku kuna nyoka watambaao ambao wanaweza kuwa hatari sana kwa mama mjamzito, kwani kama ataumwa au kushtuliwa hali hii inaweza kuleta kifafa cha mimba.

Mwanamke alipaswa kulindwa kwa hali yote ili asipate madhara bila ya sababu ya msingi. Huu ni ukweli usiopingika kuwa kama mwanamke muda wa kujifungua

unalifika usiku wakiwa safarini porini, hii inalikuwa ni shida kubwa. Hawangalikuwa na mkunga wa kumsaidiya huyu mama wala huduma ya maji au vifaa muhimu. Hali hii ingesababisha hata kumpoteza mtoto, mama au wote wawili. Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao.

#### 5.28.2 Ni Mwiko Kutangaza kwa Watu Kuwa Mtu Anasafiri, Atarogwa/ Ataviziwa / Atategwa Njiani

Jamii ya Wabungu iliamini kuwa uchawi upo. Wachawi wapo na wanafanya kazi yao. Kwa hali hiyo ilikuwa ni mwiko kusema siku ya kuanza safari kwani wachawi wangeweza kumtegea mtu uchawi njiani na kusababisha ajali au matatizo.

### 5.29 Miiko Inayohusu Usafi (Kazi)

Usafi katika jamii ya Wabungu lilikuwa ni jambo la lazima. Usafi wa ndani ya nyumba na nje ya nyumba. Ingawa zilikuwa ni nyumba za udongo lakini zilikuwa safi sana. Kitendo chochote cha uchafu kilisababisha mtu mchafu kutungiwa nyimbo za kumsuta kwa uchafu wake.

#### 5.29.1 Ni Mwiko Kuacha Mwiko uliosongewa Ugaki na Ukoko

Mwiko ni kifaa cha kupikia. Mtu anapomaliza kupika pasi na kuosha mwiko na vyombo vingine huchukuliwa kama ni mchafu na mwenye kukosa mafunzo muhimu ya maisha. Haya ni hususan kwa kina mama kwani katika jamii ya Wabungu ndio wanaohusishwa na shughuli zote za mapishi na usafi. Imeelezwa kuwa wanajamii wamewekewa mwiko huu ili kutanabahishwa juu ya madhara ya tabia hiyo ya usafi.

Ni wazi kuwa mwiko mchafu hudandamwa na wadudu kama vile inzi, na mende. Hali hiyo inaweza kusababisha maradhi ya kuambukiza kama kipindupindu. Watafitiwa wanakubaliana kuwa mwiko huu ni muhimu sana kutekelezwa na wanajamii wote.

### 5.29.2 Ni Mwiko Mtu Kufagia Usiku, Akifagia Anafukuza Wageni Nyumbani

Usiku ni kipindi cha giza. Watafitiwa walieleza kuwa usiku kuna uwezekano mkubwa wa kufagia vitu vidogo vidogo vya thamani. Kwa mfano pini, wembe au sindano. Hali hiyo imenasibishwa na ufukara kwa vile kila kitendo hicho kitakapofanyika kitasababisha upoteaji wa vitu vya thamani. Kwa upande mwingine nyumba zilikuwa na sakafu ya udongo na ufagiaji wa usiku ulikuwa ni kutimua vumbi ambalo lingeleta mafua na kukohoa usiku. Wakati huo, nyumba zilikuwa na madirisha madogo ambayo hayakuweza kupitisha mwanga na hewa ya kutosha. Kwa hali hiyo, maelezo hayo yanaingia akilini.

### 5.29.3 Ni Mwiko Mtu Kutupa Takataka Usiku, Anatupa Baraka

Mwiko huu unamkinga mtu asiende jalalani nyakati za usiku kwani mtu anaweza kupatwa na madhara kama, kuchomwa miiba na misumari au kuumwa na nyoka. Pia kutupa takataka usiku mtu anaweza kutupa vitu vidogo vidogo ambavyo hawezi kuviona usiku kwa sababu ya mwanga hafifu.

## 5.30 Miiko Mingine

Miiko ni kama sheria, kwa hali hiyo sheria ni nyingi kulingana na shughuli za wanajamii. Katika jamii ya Wabungu, licha ya makundi mengi ya miiko yaliyobainishwa na mtafiti, hapa mtafiti anajumuisha miiko mingine mchanganyiko ambayo aliikusanya na kuijadili kidogo.

### 5.30.1 Ni Mwiko Kujinyonga

Wabungu wanaamini kuwa kujinyonga kunarithiwa. Mtu akijinyonga, hali hii itaendelea kuwapata hata watoto, wajukuu na vitukuu. Ili kuleta hali bora ya maisha ya watu. Kijiuwa kwa kutumia njia yoyote ile kama kunywa sumu kujitundika kwa kamba au kujihatarishia maisha ili mtu afe ilihesabiwa kuwa ni mwiko mkubwa katika jamii. Kila mtu ana haki ya kuishi. (Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977). Watafitiwa walieleza kuwa mwiko huu ulikusudia kujenga maadili yanayothamini utu na uhai wa mtu mmoja mmoja au jamii nzima ya Wabungu.

### 5.30.2 Ni Mwiko kupakaa Mafuta Kuanzia Miguuni Kwenda Kichwani

Jamii ya Wabungu iliamini kuwa miguu ingawa ni sehemu ya mwili, ni michafu hata kama umeoga. Wakati huo watu hawakuwa wakitumia viatu kama sasa na kwa hali hiyo mara baada ya kuoga bado waliendelea kukanyaga chini. Kwa hali hiyo, kama mtu alianza kupakaa mafuta kuanzia miguuni, basi uchafu kutoka miguuni ulipandishwa hadi usoni ambako ilikuwa ni rahisi kwa mtu huyu kusogeza taka hadi kuingia kinywani bila kujua na kusababisha maradhi ya kuharisha. Kwa hali hiyo watu walipaswa kujipakaa mafuta kuanzia kichwani hadi miguuni.

### 5.30.3 Ni Mwiko Kushona Nguo Mwilini Ukiwa Umevaa, Unajitabiria Kifo

Wabungu waliamini kuwa maiti hushonewa sanda na kufunika mwili wote.. Kushona nguo mwilini ni sawa na mtu kujifananisha na maiti, wakati anaposhonewa sanda kwa mazishi. Kwa hivyo, ingawa kifo ni amri ya Mungu, lakini si vyema kwa aliye hai kujifananisha na maiti. Pia ni wazi kuwa nguo inayoshonwa mwilini haiwezi ikashoneka vizuri. Kushona nguo mwilini kunaweza kusababisha kujishona au

kujichoma na sindani na kuleta madhara makubwa mwilini. Mwiko huu una umuhimu kutekelezwa ili kuepuka madhara kwa mshonaji na nguo inayoshonwa.

### 5.30.4 Ni Mwiko Kukoroga Chakula kwa Kisu, Walaji Wataumwa Tumbo la Kukata na Kuharisha Damu

Watafitiwa walieleza kuwa ni mwiko kukoroga chakula kinachopikwa kwa kisu au kitu chenye ncha kali. Wabungu walitumia vyungu kupika chakula. Kwa maana hii kukorogea kisu ilikuwa ni sawa na kunoa kisu kwa kutumia udongo wa chungu. Unaponoa kisu vipande vidogo vya madini yaliyotumika kutengenezea kisu, huchanganyika na chakula na hivyo kuleta madhara kwa mlaji wa chakula hicho. Pia ilikuwa ni hadhari kwa uharibifu wa vyombo vya kupikia kama sufuria na vyungu. Wakati wa kukoroga chakula kilichomo katika sufuria au chungu kikiwa cha moto ni rahisi kutoboa. Mwiko huu unaweza kukubalika kwa vile kisu sio kifaa halisi cha kukorogea chakula.

Mtafitiwa Zazi alifafanua kwa kutoa mfano wa upembuaji wa mchele. Mtu anapopembua mchele mawe yote huzama na kutuama chini ya sufuria. Kama mtu atatumiya kisu au kitu chenye ncha kali kukoroga, mawe na mchanga hauwezi kupata msukosuko wa kutosha kuzamisha. Hali hii inaweza kusababisha chakula kuliwa kikiwa na mawe na kusababisha matatizo ya kidole tumbo kujaa mawe au mchanga.

### 5.30.5 Ni Mwiko Kwenda Usiku Kisimani au Mtoni Kuchota Maji

Mwiko huu umechukulia maeneo ya kisimani kuwa mara nyingi huwepo mabondeni, mbali na makazi ya watu. Watafitiwa walieleza kuwa kwa vile wakati wa usiku huwa

hakuna nuru si rahisi mtu kuweza kuona kijacho na kirudicho. Kwa mfano, mtu anaweza kukanyaga nyoka na wadudu wengine ambao ni hatari na wanaweza wakaleta madhara kwa afya ya mtu. Pia kama mtu ataangukia majini usiku ingekuwa ni vigumu kupata msaada kwani watu wengi hawapiti au kwenda kisimani. Wabungu waliamini kuwa chemchem zinatoa maji mengi usiku kwa hiyo kama mtu atakwenda kisimani atafanya maji yasitoke ya kutosha.

Kwenda kisimani usiku pia kulikuwa na mchango mkubwa juu ya usafi wa maji kisimani. Kama mtu atakwenda kisimani usiku angeweza kuyachafua maji kwa urahisi kwa sababu ya uhafifu wa mwanga. Pia inawezekana watu waovu wakamvamia mtu na kumhujumu pasi na kupata msaada kwa vile eneo la kisima limejitenga na nyumba. Inawezekana pia mtu akaingia shimoni au kukanyaga miiba . Aidha imeelezwa kuwa upo uhusiano kati ya eneo la vianzio vya maji na mashetani wanapenda kukaa maeneo hayo hasa nyakati za usiku. Maelezo hayo kwa kiasi yanakubalika ingawaje sio mara zote kuwa mtu akaenda kisimani atakutana na shetani, bali kuna madhara mengine kama yalivyoelezwa na watafitiwa kuwa yanaweza kumpata mtu. Mwiko huu unachangia harakati za utunzaji wa ikolojia ya vyanzo vya maji, chemchem, visima au mito.

### 5.30.6 Ni Mwiko Kwenda Dukani Kununua Chumvi Usiku

Kwa asili shughuli za Wabungu ni kilimo, uvuvi na uwindaji. Kutokana na shughuli hizi, Wabungu walikula mara baada ya kurudi nyumbani. Chakula kililiwa jioni kabla ya giza. Kwa hali hiyo maandalizi ya kupika chakula yalifanywa mapema zaidi. Maandalizi ya mapema ya chakula yaliendana na kuwepo kwa viungo kama chumvi. Ilikuwa ni tabia mbaya kwa mtu kwenda kwa jirani kuomba chumvi au

kwenda dukani kununua chumvi usiku. Watafitiwa walieleza kuwa mwiko huu ulilenga kuifanya jamii hasa ya Wabungu wanawake ambao ndio walioandaa chakula, wafanye maandalizi ya upishi mapema.

### 5.30.7 Ni Mwiko kuinamisha Kichwa na Kunywa Maji Mtoni, Utapigwa na Mkia wa Mamba

Mwiko huu ni onyo kwa Wabungu kuwa wasinywe maji mtoni au ziwani kwa kuinamisha kichwa. Hii ni kwa sababu ziwa Rukwa pamoja na mito yote inayoingia ziwani, ina mamba wengi ambao ni hatari kwa maisha ya wanadamu. Pia maji yana mchanganyiko wa mambo mengi ambayo yanaweza kuleta madhara kwa binadamu. Kama ilivyoelezwa kabla kuwa watu hufuwa nguo zenye kinyesi au wengine kwenda haja ndogo mtoni. Mtu kuinamisha kichwa na kunywa maji anaweza kuidhuru afya yake kwani hatajuwa ni kitu gani atakachokinywa. Vile vile msukumo wa maji unaweza kuongezeka na maji yakampalia mnywaji. Wabungu wanaamini kuwa kama mtu ana ugonjwa wa kifafa akianguka ndani ya maji, basi, maisha yake yanaweza kuishia hapo.

### 5.30.8 Ni Mwiko kuitika Wito Bila Kumwona Mtu Anayeita

Wabungu waliamini kuwa kama mtu ataitika wito bila kumwona mtu ambaye anamwita, basi sauti yake itachukuliwa. Mtu huyu atakuwa zuzu. Wabungu waliamini kuwa kuna uchawi, na kwa uchawi watu waliweza kurogwa kwa njia ya kuchukuliwa sauti zao. Aidha mwituni ni sehemu ambayo kuna usalama mdogo kwa vile si mara nyingi kuweko  na watu isipokuwa kwa wale wanaofanya shughuli maalum kama vile kulima na kukata kuni.

Eneo hilo pia liliaminika kukaliwa na viumbe wengine kama mashetani na majini. Aidha ni eneo la maficho ya watu waovu kama majambazi na waasi wengine. Maelezo ya wasailiwa juu ya kuwekwa mwiko huu yameeleza kuwa inawezekana watu waovu waliojificha mwituni wakamwita mtu kwa mwito mmoja ili wathibitishe kama huyo wanayemwita ndiye. Ili waweze kutekeleza uovu wao pale watakapobaini kuwa wanayemtaka ndiye aliyeitika.

# SURA YA SITA

## 6.0 MUHUTASARI WA MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 6.1 Utangulizi

Lengo kuu la utafiti huu ni kutafiti juu ya Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili Uchunguzi kifani wa Jamii ya Wabungu. Data zilikusanywa kutoka katika vijiji vya Udinde na Mwambani katika wilaya ya Chunya. Mtafiti alitafuta miiko na maelezo ya miiko hiyo kutoka kwa Watafitiwa wengi ambao walionekana kuijuwa vema miiko ya Wabungu.

Baada ya kazi ya kukusanya data, mtafiti alichambua data alizozipata kwa kutumia nadharia. Licha ya uchambuzi wa data, mtafiti alipata miiko ambayo ameiorodhesha katika utafiti huu wa Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili Katika Jamii ya Wabungu

Ili kuimanya Miiko ya Ubunguni na kuielezeya kwa kina inakupasa kuwa sehemu ya jamii ya Wabungu. Kwenda Ubunguni kwa wiki tatu na kuzungumza na wazee Wabungu si kuimanya Miiko ya Wabungu. Mtu anaweza kuwa mwanataalimu mzuri aliyebobea, lakini inampasa aijue jamii ya Wabungu ndani nje kwa kuwa Miiko ina kwao. Watafitiwa walitoa mifano kuwa, wanataalimu wengi walishafika hapo kijijini ili kuwauliza Wabungu habari zao na kuandika lakini hadi leo hawajaona kitu chochote, kitabu au hata kurudi kusema walifanyia nini taarifa walizozichukuwa.

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa watafiti wengi wanakusanya data kutoka kwa wanajamii kwa ajili ya utafiti lakini wanajamii wenyewe pamoja na Wabungu hawapewi mrejesho wa habari wanazozitoa hata kuzisikia redioni au magazetini.

Nakala moja ya utafiti huu itawekwa katika maktaba ya Wilaya ya Chunya iliyoko Mkwajuni kwa ajili ya matumizi ya Wabungu na wanazuoni kwa ujumla.

## 6.2 Muhtasari

Katika sura ya kwanza mtafiti aliweza kubainisha vitu muhimu vya utafiti. Kwanza mtafiti alianza kuelezea Usuli wa Mada ambapo mtafiti ameelezeya umuhimu wa miiko katika makuzi ya kimaadili ya wanajamii ikiwa ni utanzu katika sanaajadiiya. Hali kadhalika mtafiti aliweka wazi Usuli wa Tatizo ambapo alielezeya kuhusu hali ya kukengeuka kwa maadili katika jamii ya Wabungu kunakosababishwa na kufuwawa kwa miiko.

Pia mtafiti hakusahau kuweka wazi kauli ya tatizo. Kwa nafasi hii mtafiti alibainisha madhara ya tabia ya mtu pekee inavyoweza kuleta madhara kwa jamii nzima. Chimbuko la matatizo hayo limesababishwa na kufuwawa kwa miiko katika jamii nyingi za Afrika. Nia kuu ya utafiti ni kusaka na kuthibitisha ukweli kuhusu kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili. Nia kuu ya Utafiti huu iliambatana na madhumuni ya utafiti, Umuhimu wa utafiti, maswali ya utafiti, vikwazo na utatuzi wa vikwazo vya utafiti. Katika sura hii mtafiti aliweza pia kubainisha kuwa utafiti huu ulifanyika wilaya ya Chunya katika vijiji vya Mwambani na Udinde. Mwanajiografia hawezi kupoteya kufika katika eneo hili. Mwanataalimu huyu atakwenda kulitafuta eneo hili kati ya latitudo nyuzi ya 7 na 9 Kusini mwa Ikweta na kati ya longitude nyuzi ya 32 na 34 Mashariki ya Greenwich

Katika sura ya pili, mtafiti alipiga mbizi katika kusaka na kufafanuwa mwega wa utafiti. Mtafiti alichagua nadharia tano kati ya nadharia nyingi zilizopo katika fasihi

na sanaajadiiya. Hapa, ni nadharia tatu alizozitumiya kwa kina katika kuwasilisha na kuchambua data. Nadharia zilizoteuliwa na mtafiti ni ile ya Taalimu ina Kwao na Fasihi ina kwao na nadharia ya Kila Jamii ina Ujumi wake na Nadharia ya ndani nje. Nadharia hizi zinamrejesha mwanadamu kujipenda mwenyewe, kuipenda asili na vitu vinavyomzunguka na kuzingatia kuwa kuna vitu vingi duniani lakini kila kitu kina asili yake. Ikumbukwe kuwa Mzungu si Mbungu au Mchina. Kila mmoja wa watu hawa ni tafauti hivyo yampasa mtafiti kuijuwa jamii anayoitafiti ndani nje.

Katika sura ya tatu mtafiti alitalii mabuku na maktaba asiliya za sanaajadiiya ambazo ni wanajamii wenyewe. Mtafiti aligunduwa kuwa kuna watafiti ambao wameandika kuhusu miiko, ingawa mada inayojadiliwa ya kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili ya jamii, bado haijashughulikiwa. Hata hivyo marejeleo yote yaliyopitiwa yalimsaidiya mtafiti katika kubainisha pengo na kumsaidiya kusukuma mbele utafiti kwa kuiweka wazi miiko hiyo.

Katika maktaba mtafiti aligunduwa kuwa miiko inatumika katika nyanja za sayansi ya Kuhifadhi matumbawe na mazaliya ya samaki – Zanzibar na pia inatumika katika kutafuta dawa za kutibu maradhi ya wanadamu na masuala ya lishe inavyoathiriwa na miiko katika baadhi ya jamii. Matatizo yanayokabiliyana na utanzu wa miiko ni katika uhifadhi. Miiko kwa ujumla haijashughulikiwa sana katika sanaajadiiya na hivyo wanajamii, wanazuoni wanapaswa kujitowa katika kuitafiti na kuitunza katika njia mbali mbali ikiwemo kuihifadhi katika mtandao.

Sura ya nne mtafiti alibainisha mbinu na njia za utafiti alizozitumiya katika kukamilisha utafiti huu wa Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili

Uchunguzi Kifani wa Jamii ya Wabungu. Kama alivyo mtu anayetaka kujenga, kwanza ni lazima ayajuwe mahitaji halisi ya nyumba anayotaka kuijenga. Kama ni nyumba ya kuishi au ghala, baada ya kuliona hitaji lake. Hivi ndivyo ilivyo katika utafiti. Kitu cha kwanza ni kuwa na hitaji, ambalo katika utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza kufuwawa kwa miiko na kupotoka wa maadili katika jamii ya Wabungu.

Baada ya kuwa na tatizo mtafiti anapaswa kuandaa usanifu wa utafiti. Hapa mtafiti anaandaa utaratibu mzima wa kufanya utafiti kuanziya mwanzo hadi mwisho. Uteuzi wa njia bora ni muhimu. Katika utafiti huu mtafiti alitumiya njia ya Uchunguzi Kifani. Mtafiti aliamua kutumia njia hii kwani ni bora zaidi katika utafiti wa maisha ya wanajamii. Hapa mtafiti anaweza kuona na kufuatilia mambo anayoyatafiti kwa kuishi ndani ya wanajamii wenyewe. Njia hii inampa nafasi mtafiti kuchunguza na kuibuka na majawabu au maswali kwa wanajamii ambayo yatamfikisha katika Hitimisho bora na lenye mashiko kisayansi.

Kazi yote ya utafiti hujengwa katika msingi wa usanifu wa utafiti. Mtafiti alionesha aina za data zilizohitajika, njia za kukusanyia data na namna alivyokusanya data za utafiti huu. Hapa alibainisha data za awali au data za msingi, na data za upili ambazo alizipata maktabani na kwa wanajamii wenyewe (Maktaba kuu ya sanaajadiiya ni wanajamii wenyewe kwa mujibu wa Mwanasanaajadiiya Prof Dkt, Sheikh Sengo T. Y. S. M). Pia mtafiti aliweza kueleza namna ya kufanya uteuzi wa watafitiwa.

Njia kuu ya kukusanyia data ilikuwa ni njia ya usaili. Njia hii iliambatana na ushuhudiaji. Kama ada hakuna kizuri kisicho na kasoro. Matatizo ya gharama na

muda yalitawala utafiti huu. Mungu si Athumani, kila tatizo lilipojitokeza pasi nguvu za kutoka juu kungekuwa na mtihani mkubwa zaidi. Familiya, wafanyakazi wenza na rafiki walimshika mkono na kumvusha pasi hiyana wala choyo ya rupia au muda wao kuutumia kwa ajili ya utafiti huu.

Sura ya tano ilihusu uwasilishaji wa data na uchambuzi wa data za utafiti. Hapa mtafiti aliwasilisha mambo yote yaliyohusiyana na utafiti. Licha ya kuwa na maswali ya kumwongoza katika kusaili, mtafiti alijikuta akiwasaili watafitiwa msamiati kana kwamba hawajui Kiswahili au Kibungu. Lengo lilikuwa ni kujenga uelewa, umakini, na kuwarejesha katika ujumi wao uliohatarini kupotea kwa sababu ya utandawazi uliofikiya ngazi ya . Maneno kama maana ya miiko, maana ya maadili na maana ya ushirikina yaliulizwa na kupatiwa majawabu, ingawa neno ushirikina bado linahitajika kufanyiwa kazi na kuwekwa wazi katika makamusi kama kitomeo kilicho na maana zaidi ya moja pasi kuongeza mifano ya sentensi maridhawa zinazokosekana katika makamusi ya Kiswahili.

Miiki mia moja kumi ilikusanywa na kuwekwa katika makundi yafuatayo; miiko ya adabu na heshima, miiko ya watoto, miiko ya ndoa, miiko ya viongozi, miiko ya bahari na uvuvi na miiko ya uwindaji. Licha ya miiko hii pia makundi mengine ya miiko ni miiko ya kilimo, miiko ya wanawake, miiko ya wanaume, miiko ya maradhi, miiko ya usafiri, miiko ya usafi miiko ya utunzaji wa watoto na kundi la mwisho ni la miiko mingine. Mtafiti ana hakika hii si miiko yote ya Jamii ya Wabungu. Matatizo ya elimu na dini kuwa na mtazamo hasi zilimtia wasiwasi mtafiti, ingawa alijipa moyo kuwa huu ni mtihani wa mfumo wa elimu na maadili ya

wanajamii kwa ujumla. Pia kundi la watoto na viongozi waliosailiwa lilimpa mtafiti wasiwasi kuhusu hatima ya jamii ya Wabungu kimaadili.

Mwisho kabisa mtafiti alikuwa na sura ya sita katika kazi yake ya kusaka ukweli kuhusu Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili ya Jamii ya Wabungu. Katika sura hii mtafiti aliweza kuyaweka mawazo yote pamoja. Hapa mtafiti alitowa muhtasari wa kazi hii kwa kila sura, matokeo yalibainishwa, Hitimisho lilitolewa na mwisho mapendekezo yalitolewa kwa serikali, Wabungu na watafiti wa sanajadiiya.

## 6.3 Matokeo ya Utafiti

Mtafiti aliyaona mengi katika utafiti huu ambayo yanathibitisha kuwa jamii ya Wabungu inakabiliwa na mtihani wa kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili. Hili si jambo jema katika jamii yoyote ulimwenguni. Hata katika jamii ya hayawani kama kuna mmoja wao ameoneka kuuacha uhayawani, hayawani wengine watakuja juu na kumlaumu hayawani huyo kwa nini amewasaliti. Hali kadhalika katika jamii ya wastaarabu baba wa wastaarabu duniani wanapofikwa na donda ndugu kama hilo basi hukaa pamoja na kwa kutumia sanaajadiiya wakalikemea kwa nguvu zote ili janga liwaondokee.

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni mahususi matatu, ambayo kwayo mtafiti aliyatumiya kama mwega wa kufikia Hitimisho lake. Kuchunguza asili, maana na aina ya miiko, uhusiano uliopo kati ya miiko na maadili ya mtu binafsi lilikuwa ni dhumuni la kwanza. Matokeo yanaonesha kuwa, miiko ya Wabungu asili yake ni Ubunguni na si vinginevyo. Nadharia ya taalimu ina kwao na fasihi ina kwao

inashadidia kauli hii. Wabungu waliposailiwa hawakutoa marejeleo ya miiko hiyo kutoka ughaibuni. Waliwarejelea Wabungu wa asili, babu na mababu wa babu wao.

Miiko ilirejeleya sheria, makatazo haya yalihusishwa na utakatifu na mamlaka ya Wabungu wenyewe. Makatazo ya wanawake wa Kibungu kuoga baharini ni mwiko wa Wabungu na katika bahari ya Wabungu iliyoko Ubunguni (ziwa Rukwa). Uzunguni huu si mwiko. Taalimu ina kwao na Fasihi ina kwao, ili kulijuwa hili kwa kinaga ubaga inakupasa uijuwe jamii Ndani nje hapo ndipo unapoweza kuona ujumi wa kila jamii na huu ni ujumi wa Mbungu si ujumi wa Mzungu.

Watafitiwa wote walikiri kuwepo kwa miiko katika jamii ya Wabungu tangu utangu. Miiko ilikuwa ni kipimo cha utu wa Mbungu. Maadili ya mtu yalipimwa kwa mtu huyo kuhakikisha hasababishi matatizo kwa wanajamii wengine. Kitendo cha mtu kushindwa au kumsababishiya mtu mwingine shida ni kukosa maadili watafitiwa walishadidia. Lengo kuu la miiko lilikuwa ni kuleta heshima, utengamano na umoja katika jamii. Kitendo cha kupuuza miiko kulileta zahama katika jamii ya Wabungu. Jamii nyingi za Waafrika zilikuwa na miiko na hali hii inathibitisha kuwa miiko ina mizizi na mashiko yake katika jamii za Kiafrika.

Katika utafiti huu mtafiti pia alichunguza kufuwawa kwa miiko ya jamii ya Wabungu. Wazee walionesha wasiwasi wa moja kwa moja kuhusu kufuwawa kwa miiko ambako kunajitokeza kwa nguvu sana. Wanajamii wanakiri kuwepo hali ya kukenguka kimaadili katika jamii. Katika sehemu hii mtafiti alielezwa kuhusu salamu. Siku hizi salamu hazitolewi kwa kufuata misingi ipasayo ya Kibungu. Salamu ilichukuwa dakika kadhaa lakini sasa watu wanatowa salamu kana kwamba

wapo Uzunguni wakiwa wanazungumza na mashine tu. Huu si ujumi wa jamii ya Wabungu. “Taalimu hii, hapa Ubunguni si kwao, imepoteya njia inawapasa Wabungu kuikataa kwani wanajuwa ilikotoka. Wabungu wawarudishie wenye nayo”. Watafitiwa walibainisha haya katika kukiri hali hii ya kukengeuka kwa maadili katika jamii ya Wabungu.

Utu wa Mbungu haupimwi kwa kilo au kwa kibaba. Utu huu hupimwa kwa misingi halisi ya maadili ya jamii ambayo humjenga mtu kuaminika, kuthaminiwa na kuwekwa katika nafasi ya kuwa mshauri wa wanajamii. Hivyo miiko inakemea wanajamii kuiba, kuwa wavivu, kutabii mavazi na mienendo bila kujua ulimbe wake au umalaya ambao unaweza kusababisha ugonjwa wa VVU/UKIMWI. Haya yote yamo katika ulimbe wa miiko mingi ya jamii ya Wabungu.

Uchambuzi wa data za utafiti huu umetowa matokeo mengi chanya ambayo yakizingatiwa pengine yanaweza kuiweka jamii ya Wabungu mahali pazuri, mathalani, mtafiti aligundua kuwa ulinzi wa miiko ya jamii ni wa wanajamii wenyewe. Wabungu ndio wenye dhamana ya kutunza miiko kwa kuitumiya. Mfano wa shauri la mwanamke aliyekutwa akioga ziwani. Mwanakijiji aliyemwona na kuchukuwa hatua ya mumweleza mumewe lilikuwa jambo jema la ulinzi wa miiko ya jamii ya Wabungu. Kwa kuwa mume alikuwa na kiburi, basi shauri lilifikishwa kwa viongozi wa kimila kijijini na hatua za kimila zilichukuliwa.

Mtafiti hakuishia hapo, aliendelea kubainisha katika ugunduzi wake kuwa jamii ya Wabungu iko njia panda. Watafitiwa wengi wanaonekana kulalamika tu kuhusu kufuwawa kwa miiko na kukengeuka kwa wanajamii kimaadili pasi kuchukuwa

hatua za kukemea kwa nguvu hali hiyo katika jamii. Walibainisha kuwa baadhi ya vyanzo vya kukengeuka kwa maadili ni matumizi ya runinga na video ambapo watoto wanakwenda katika kumbi za kuoneshea video na kuangalia picha. Mara nyingi picha hizi hazina heshima, picha za utupu na uchafu mwingine lukuki. Picha hizi mbazo hazina ithibati lakini zimetamalaki kila kona. Picha hizi hazifai kuangaliwa na watoto, kwani ni picha za vita, mauji  na ngono kinyume na maadili ya Kibungu. Pia walitaja baadhi ya magazeti ya udaku kuwa picha na maelezo yake mara nyingine ni tatizo kwa malezi ya watoto na hata watu wazima. Aghalabu taswira inayojengwa na uhuru huu wa kupata habari usiokuwa na mipaka na kuuvunjia heshima utu wa Mbungu na Uafrika wake.

Utafiti umeainisha kuwa utandawazi nao ni tatizo jingine kubwa hasa kwa vijana wanaopata nafasi ya kutumia mitandao. Vijana wanaangaliya picha za ngono na mauaji katika mtandao na kwa hali hiyo wanajijengea mawazo kuwa hiyo ni tabia ya kawaida na wao wanakwenda kufanya mazoezi ya ngono. Hali hii inaambatana na kutabii mavazi ya nguo za kubana na nguo fupi kwa vijana au uvaaji wa hereni kwa wanaume,  kutabii maisha ya mijini  Vijana  wanaporudi kutoka mijini wanafanya mazoezi ya kuvaa nguo ambazo ni mwiko na kuwafanya vijana wa vijijini waige na kuanza kuvaa. Pia wanaiga kwa kuona mifano kutoka katika maonesho ya warembo, televisheni, magazeti ya udaku na mitandao, na huo kwao ni kielezeo cha ustaraabu. Watafitiwa wanaona kuwa huo ni usataarabu uchwara. Ustaarabu huu unapaswa kutafutiwa tiba mapema ili kukinusuru kizazi kilichopo na kijacho. Ustaarabu unaowatenga watoto na wazazi katika kusimulia hadithi, metali, vitendawili na miiko kutoka kwa wajomba na shangazi zao.

Kwa upande mwingine watafitiwa wanaona kuwa dini imechangia kuwaweka Wabungu njia panda, wengi wao wasijue wafuate mwelekeo upi. Hii ni kutokana na dini kukataza jamii kutumia miiko kwa kisingizio cha kumkosea Muumba wao. Hawakujua iwapo wajitome katika utamaduni mpya ambao hawakuwa na mizizi nao au la. Hali hii inawafanya Wabungu kushika mila za wageni na kuacha au kudharau mila na utamaduni wao, utamaduni uliowakuza. Wanajikuta wakiwa katika migongano inayoondoa umoja wao wa tangu utangu kwa sentensi isiyo na mashiko kuwa dini inakataza.

Sanaajadiiya hadi sasa inakabiliwa na matatizo ya uchache wa tafiti zilizokwishafanywa. Kwa hali hiyo mafundisho ya kina yanayohusiyana na maadili kuegemea nusu upande. Watu wanakosa maadili ya kidini na kwa wakati huo huo hawapati maadili ya wazazi au ya babu zao. Maadili ya ndani ya mtu huanzia nyumbani na katika jamii ambamo hulelewa. Dini huyaendeleza maadili mema yaliyoendeleza msingi wa maadili alio nao mja huyo. Kwa hali ilivyo sasa, utafiti wa utafiti wa Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kawa Maadili hunaonesha ufa mkubwa unaotanuka kila uchao kutokana na kufuwawa kwa miiko ya Wabungu.

Mtafiti alishuhudiya kuwa hazina muhimu za sanaajadiiya zilizopo bado zina ukiritimba mkubwa katika upatikanaji wake. Kutokuwekwa wazi kwa tafiti hizi kwa matumizi ya jamii, kunasababisha upungufu wa maandishi ya miiko kwani si waandishi wote wanaopenda kufanya utafiti. Kazi hizi zinahitaji kuchambuliwa na kukosolewa kila uchao ili kuufahamisha Ulimwengu ujumi uliomo katika kazi hizi hasa kazi za sanaajadiiya utanzu wa Miiko. Bado hitaji la tafiti ni kubwa sana hasa katika uwanda wa sanaajadiiya utanzu wa miiko kuwa bado haujafanyiwa utafiti wa

kutosha ili kuwaelimisha Wabungu waweze kuiishi miiko yao. Mtafiti anaona kuwa ni vema sasa kwa wanataalimu kusisitiza utafiti wa sanaajadiiya katika kila ngazi ya Kiakademia kwenye uga wa sanaajadiiya na vikumbo vyake vyote hasa miiko.

Mtafiti alibainisha kuwa watafitiwa wengi wanaona kuwa, sanaajadiiya ililinda utu kwa kujali mgawanyo wa kazi. Katika kila jamii ya watu, wanawake na wanaume hawakufanya kazi moja. Kazi za kutumia nguvu nyingi walipewa wanaume. Sanaajadiiya ni chimbuko la wanataalimu wa sayansi. Watu hawa walijuwa ulimbe wa kila kitu katika jamii iwayo ile. Ni kichaa tu ambaye hawezi kumheshimu hata mama yake mzazi. Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao. Mgawanyo huu wa kazi kwa kufuata jinsi kwao ni Ubunguni, kama katika jamii nyingine wanaona hii si haki ya binadamu basi Ubunguni ni haki ya Binadamu, waende Ubunguni wakajifunze haki hizo. Kwanza waimanye jamii ndani nje, kwani Taalimu ina Kwao na Fasihi ina Kwao na pia watajuwa kuwa kila jamii ina Ujumi wake.

Mwana umleavyo ndivyo akuavyo. Miiko ni nyenzo ya malezi yenye uwadilifu. Mtafiti aligunduwa kuwa katika jamii ya Wabungu, miiko ilikuwa ni msingi mkuu wa malezi na mwenendo mwema. Watoto walifundishwa kusalimia, kuwaheshimu wakubwa na kuwasaidiya kazi na kuwapa nafasi ya kupumzika ikiwezekana. Sasa mtoto anamwacha mzee anasimama katika basi wakati yeye amekaa, kwa maringo anasema mzee kachelewa kuingia garini. Huu ni usasa. Huu ni usawa wa kisasa unaodaiwa na wanaharakati. Huu si ujumi wa kujivunia na kwao si Ubunguni. Kwa hakika miiko ni chombo cha kutoleya elimu ya asili, sasa imefuwawa na kusababisha kupotoka maadili ya Wabungu.

Pia miiko ni chombo cha udhibiti wa mazingira na mabadiliko ya jamii na kinga ya maradhi. Katika utafiti huu mtafiti amebainisha masuala haya kwa kinaga ubaga. Kuna mifano maridhawa katika kushadidia dhana hizi. Mtafiti alipata mifano kama ya sanaajadiiya, utanzu wa miiko ulivyotumiwa na wanataalimu na watafiti wa sayansi ya bahari ili kurejelea utunzaji wa matumbawe Zanzibar. Kongole kwa kazi hii adhimu kwa Taifa na Ulimwengu kwa ujumla. Utafiti huu uwe chachu na mtafiti yuko tayari kushiriki kwa namna yoyote katika kuuendeleza utafiti wa miiko, kwani anajuwa kuwa kazi hii ni ndogo sana ukilinganisha na mahitaji kamili ya jamii na Taifa. Hili ni tone dogo la maji katika bahari.

Vitu hivi vyote ndivyo vilivyotoa ithibati ya kufanya utafiti huu wa Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili Katika Jamii ya Wabungu.

## 6.4 Mapendekezo

Ingawa Wabungu wanatumia lugha yao Ubunguni na nje ya Ubunguni, lakini bado kuna haja kubwa ya Wabungu kuitumia miiko yao katika mazingira mbali mbali. Kwa hali hiyo Mtafiti anapendekeza kuwa kutokana na utafiti huu. Kwanza serikali kwa kupitia Wizara ya Utamaduni izisaidie jamii katika kuhamasisha wanajamii kuiishi miiko na mila za jamii.

Pia serikali kwa kupitiya Serikali za mitaa, itumiye nafasi ya mafunzo kwa viongozi wa vijiji kuwafundisha kutumia busara katika kutumia miiko katika kuzuwia ukengeukaji wa maadili katika jamii za Watanzania badala ya kutumia sheria za dola ambazo mtafiti anafikiri hazipunguzi uhalifu.

Maadili ya mtu hujengwa ndani ya mtu angali mdogo. *Asiyefunzwa na mamaye, hufunzwa na ulimwengu*. Huu ni msemo wa kawaida sana katika malezi. Mashiko ya msemo huu yanakosa msisitizo pale ambapo mtu alitakiwa kuonywa na kuambiwa kwa hakika kitu ukifanyacho ni mwiko. Hapo jamii itaweza kuwahukumu watu wa aina hiyo kwa haki. Mwiko haupindishwi, wala hauliwi mlungula. Mwiko unavunjwa au unalindwa tu. Miiko itumiwe katika harakati zote za maisha na jamii ipewe nafasi ya kuitumiya.

Wizara ya Elimu wakishirikiana na Wizara ya Utamaduni ndio wenye wajibu wa kuwalea watoto kimaadili. Kwa hali hiyo Wizara wakishirikiana na wadau wote wa elimu waandae na kuingiza mtaala wa utamaduni unaohusisha miiko kwa malezi ya jamii katika kujenga jamii yenye maadili mema na kuondokana na uguberi.

Elimu ina kwao na fasihi ina kwao, kwa hali hiyo wanataalim, wanazuoni, na wanafunzi wa Ndaki mbali mbali katika sanaajadiiya wajitowe kimasomaso katika kuhamasisha kuandika na kufanya tafiti kuhusu miiko katika jamii za Tanzania. Hapa ni tafiti za ndani ya Tanzania tu, zitakazo bainisha maadili ya Watanzania. Ndaki za ughaibuni zitaibua maadili ya ughaibuni na si maadili ya Wabungu.

Katika jamii ya Wabungu, wazazi wairejelee miiko na kuanza kuitumiya katika maisha ya kawaida. Miiko si lazima ifundishwe kama hisabati. Wanajamii wanaweza kuitumiya katika kuwaonya watoto wao. Pia wazee wanaweza kuitumia miiko hiyo katika kuwakumbusha wazee wenzao waliokengeuka kuwa wamevunja mwiko na madhara ya kuvunja mwiko huo.

Taasisi zinazohusika na kudhibiti filamu na mitandao, wajitowe kimasomaso kutafuta njia sahihi za kiteknolojia katika kupitia na kutoa ithibati sahihi kwa picha za senema zinazooneshwa katika mtandao, runinga na santuri za DVD. Hata hivyo magazeti yasisahaulike kuhaririwa hasa magazeti ya udaku.

Elimu ni chombo cha kumkomboa mwanadamu. Elimu hiyo ikitumika vibaya basi inakuwa ni chombo cha kumwangamiza mtoto, kimaadili, kiroho na kiakili. Mitaala ya sanaajadiiya ilenge kuwafundisha watoto ujumi wa jamii zao na waelewe kuwa Taalimu ina kwao na fasihi ina kwao. Madhumuni ya elimu ya ughaibuni ni kueneza kuabudiwa na wanaoipata elimu hiyo. Mitaala ya ughaibuni ni kwa ajili yao, kwa hali hiyo watoto wa Kibungu wanaosoma ugaibuni wanakuwa “huku hawako na kule hawako”. Watu hawa wanakuwa popo, si ndege, si wanyama. Wasomi hawa wamekuwa popo, si wanyama si ndege. Uzalendo na utaifa sasa haupo tena kwani asili, taalimu na ujumi wa Mbungu haupo tena.

Hereni ni pambo zuri kwa mwanamke, je mwanaume akivaa hereni katika ujumi wa Mbungu awekwe kundi gani? *Dalili ya mvua ni mawingu*. Taifa linaangamia kwa kukosa wanataalimu au viongozi wanaolionesha njia, na kufikiri kuwa misaada ya kutoka Ughaibuni ndiyo suluhu ya matatizo kumbe laa! Katika jamii ya Wabungu jambo hili si la kujivunia hata chembe.

Utafiti huu ni sawa na kijitone cha maji katika bahari. Watafiti wanapaswa kuchukuwa chachu hii na kuanza tafiti za tanzu hii ya sanaajadiiya. Kwanza utafiti wa miiko zaidi unahitajika ili kuwa na hazina adhimu katika jamii zote za walio na mapisi yao Afrika.

Licha ya kukusanya miiko bado kuna pengo la kuchunguza lugha katika miiko, ulimbe katika miiko, miiko na sheria, miiko na athari zake katika jamii na tafiti nyingine nyingi. Pia wanataalimu wa sanaajadiiya wachunguze na kuandika kuhusu Utanzu huu wa Miiko kama zilivyo tanzu nyingine za methali na nahau.

## 6.5 Hitimisho

Utafiti huu ulifanywa kwa mapenzi makubwa ya jamii ya Wabungu. Msaada mkubwa uliotolewa na Prof. Dkt Sheikh Sengo T.Y.S.M. ndio uliozaa kazi hii ya heshima kwa jamii ya Wabungu na wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kukamilisha kazi hii, Mungu awabariki.

Mtafiti anaamini kuwa Tasnifu hii itakuwa chachu ya kuwachagiza wanazuoni waliopo na wajao katika kuzama zaidi katika utanzu huu wa miiko ili kuiweka bayana hazina iliyomo ndani yake kwa kuwa utanzu huu haujashughulikiwa katika kuandikwa na kufanyiwa utafiti kama zilivyo tanzu nyingine za sanaajadiiya.

Mtafiti anaamini kuwa kazi hii maridhawa itauweka utanzu huu wa miiko kwenye nuru ili uweze kuonwa na watafiti wengine katika wizani sawia na tanzu kama methali, nahau, vitendawili na misemo, kwani hauonekani kuwa ni utanzu kamili wa sanaajadiiya. Utanzu huu unaweza kuchukuwa nafasi adhimu katika kuiauni jamii ya Wabungu, Wanyakyusa, Wasukuma, Waswahili, Watanzania na Waafrika kwa ujumla wake ambao, ujumi wao unatishiwa kumezwa na ujumi wa Uzunguni.

Mtafiti anaamini kuwa tasnifu hii itafungua ukurasa mpya kwa kuvunja makufuli ya utamaduni chapwa wa kufungia kazi mama za utafiti katika makasiki badala ya

kuziweka sebuleni peupe ili zionwe, ziliwe na kufanyiwa upembuzi yakinifu na wengine kwa manufaa ya Wabungu wenyewe na Watanzania kwa ujumla kwa manufaa ya Taifa la Muumba ambaye ndiye ukweli. Kwa kutimiza adhima hii mtafiti ataiweka kazi hii katika Makumbusho Kuu ya Taifa Dar es Salaam na katika maktaba ya Wilaya ya Chunya iliyoko Mkwajuni - Mbeya.

Mtafiti anaamini kazi hii itakuwa mwanzo mpya na mzuri wa kuthamini lugha adhimu ya Kiswahili kwa kuwa imekidhi nia ya kufanya Utafiti huu wa Kufuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili Uchunguzi Kifani wa Jamii ya Wabungu.

## MAREJELEO

Achebe, C. (1958). *Things Fall Apart.* Nairobi, East African Educational Publishers Ltd.

Allan, K. & Burridge, K. (2006). *Forbidden Words Taboo and Censoring of Language*, Cambridge, Cambridge University Press

Balisidya, M. L. (1982). *Uchunguzi katika Fasihi Simulizi vizingiti na Mkabala* (Makala za Semina). Dar es Salaam, TUKI.

Barry, P (2009). *Beginning Theory*, Manchester, Manchester University Press

Bathawab S.S. na Sengo T.S.Y.M, (2007*). Utendi wa Mambo Mambo S na S***.** Dar es Salaam, Al-Amin Educational and Research Academy (AKADEMIYA)

Carrick, J. (2010). *Nouveac Realism,1960s.* Canada, Ashgate Press

Chisenga, J. (2002). *Indigenous Knowledge: African's Opportunity to Global Information Content.* Johannesburg, LIASA 100, 2002

Creswell, J. W. (2003). *Research Design, Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches.* California, Sage Publications, Inc.

Farsi, S. S. (1965). *Swahili Sayings – 2.* Dar es Salaam, EALB

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*, London, Oxford University Press

Gichuru, S. M (1971). *Stories from Masailand***,** London, Macmillan Education Ltd

Haralambos, M. Holborn, M. na Heald, R. (2004). *Sociology Themes and Perspectives. London*, Harper Collins Publishers Ltd

Hart, C (1998). *Doing Literature Review***,** New Delhi, SAGE Publications

Horkheimer, M (1947) *The Eclipse of Reason*, London, Oxford University Press

Hussein, E. (1967). *Wakati Ukuta,* Nairobi, E.A.P.H.

Idara ya Maendeleo – Tanzania (1971). *Utamaduni na Mila Zetu***,** Dar es Salaam, Printpark Tanzania Ltd.

Jastrow, M. (2009). *Handbooks on The History of Religions. Vol. IV***.** London, Humphrey Milford Oxford University Press

Karama, S. Na Saidi, M. (1983), *Maelezo ya Methali za Kiswahili***,** Nairobi, Longhorn Publishers

Kisanji, J. A. N. (2010) *Miiko ya Jamii ya Wabungu,* Dar Es Salaam. (Muswada)

Kothari, C. R. (1985). *Research Methodology Methods & Techniques***,** New Delhi, New Age International (P) Ltd

Leedy, P. D. (1989). *Practical Research: Planning and Design. 4th edition,* New York, Macmillan Publishers Company

Levi-Strauss, C. (1966) *The Savage Mind*, Chicago, University of Chicago Press

Lindgren, H.C, na Byrne, D. (1974). *Psychology An Introduction to Behavioral Science, 4th Edition,* London, John Wiley & Sons, Inc.

Masalu, D. C. P, Shalli, M. S na Kitula, R. A. (2010). *Customs and Taboos*, Melbourne, Currie Communications.

Matteru, M.L.B (1981). *Fasihi. Makala za Semina ya KimaTaifa ya Waandishi wa Kiswahili II,* TUKI. Dar es Salaam

Mbiti, S. John (1975). *Introduction to African Religion*, Praeger, New York,

Mdee, J. S. na Mbogo, E. (1978). *Mulika Na. 17***.** Dar es Salaam, TUKI

Mlacha, S.A.K. na Hurskainen (1995). Lugha, Utamaduni na Fasihi ya Kiswahili, Dar es Salaam, TUKI (Dar es Salaam/DAAS Helsinki)

Mponda, L. Y. (1962). *Adabu Njema***,** Dar es Salaam, East African Literature Bureau

Mtesigwa, P. C. K. (1989). *Methali ni nini? Mulika Juzuu Na 56,* Dar es Salaam, TUKI

Mulokozi, M.M, Massamba, D.P.B, (1985). *Kiswahili- Juzuu 52/1&52/2,* Dar es Salaam. TUKI

Mulokozi, M.M, na Kahigi K.K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu***,** Dar es Salaam, TPH.

Mulokozi M.M. na wenzake (2004). Toleo la Pili, *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Nairobi, Oxford University Press East Africa

Mulokozi M.M. na wenzake (2001). *TUKI Kamusi ya Kiswahili – Kiingereza,* Dar es Salaam, TUKI

Musso, M. (1968). *Mukwava na Jamii yake***.** Arusha, Eastern Africa Publication Ltd.

Mwanga, Z. (1984). *Hiba ya Wivu*, Dar es Salaam, Ruvu Publishers

Nchimbi, B. R. (1979). *Wachawi wa Afrika***,** Dar es Salaam, Ruvu Publishers

Njogu, K. Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi – Nadharia na Mbinu, Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation

Njoroge, J na wenzake (2011). *Kamusi ya Karne ya 21,* Nairobi, Longhorn Publishers

Nkwera, F. V. Fr (2009). *Tamrini za Fasihi Simulizi Sekondari na Vyuo***,** Dar es Salaam, Business Printers Ltd

Ntaragwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi***,** Rock Island, Augustina College.

Ogechi, N. O, Shitemi, N. I. Na Simala, K. I. (2008). *Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.* Eldoret. Moi University Press.

Okot p'Bitek (1972). *Song of Lawino and Ocol*. Nairobi, East Africa Educational Publishers

Omari, C. K. Mvungi, M. (1981). *Urithi wa Utamaduni Wetu***,** Dar es Saala, TPH

Onions C.T. (1960). *Shorter Oxford English Dictionary Vol. 11 N-Z*. Oxford, at the Clarendon Press

Owino, J. J. (1978). *Faharasa ya Utafiti wa Amali za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam TUKI

Parmer, F. R. (1976). *Semantics***.** Melbourne, Cambridge University

Planning Commission (1997). *Chunya District Socio-Economic Profile***.** Dar Es Salaam

Robson, C (1993). *Real World Research***,** Massachusetts, Blackwell Publishers Inc.

Rugemalira, J. na Muzale, H. (2009). *Atlasi ya Lugha za Tanzania***.** Dar es Salaam, InfoBridge Consultants Ltd

Said, A. M. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili*, East African Educational Publishers Ltd. Nairobi

Sarantakos, S. (2005). *Social Research***,** New York, Palgrave Macmillan

Sengo T. S. Y. (1985). *THE Indian Ocean Complex and Kiswahili Folklore:- The case study of Zanzibarian Tale – Performance vol, 1, 2 & 3.* Desertation for PHD in Folklore, Department of Folklore Institute of African & Asian Studies, University of Khartoum

Sengo, T. S.Y.M (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi***.** Dar es Salaam, Al-Amin Educational and Research Academy (AKADEMIYA)

Sengo, T.S.Y. (1978). *Mfululizo wa Mihadhara Juu ya Fasihi – Zanzibar***.** Dar es Salaam, TUKI

Sengo, T.S.Y. na Honero, L.N. (1978). *Mulika,* Dar es Salaam, KIUTA

Sengo, T.Y.M. (2008). *Tafakuri ya Utu na Uhai,* Dar es Salaam, Huda Publishers

Sengo. T na Kiango S.D. (1973). *Hisi Zetu***,** Dar es Salaam, Chuo cha Uhunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Senkoro, F.E.M.K (1982). *Fasihi.* Press and Publicity Centre. Dar es Salaam

Simeon, K. V. (1977).*Mila na Desturi za Wapare***,** Soni, Vuga Press

Sithole, J. (2006). *The Challenges Faced by African Libraries and Information Centers in Documenting and Preserving Indigenous Knowledge***.** Seoul, www.ifla.org/iv.ifla72/index.htm

Taylor, R. B. (1973). *Introduction to Cultural Anthropology***.** Boston, Allyn and Baccon, Inc

Temu, C.W. (1983). *Makala za Semina ya KimaTaifa ya Waandishi wa Kiswahili III FASIHI.* Dar es Salaam, TUKI

Thiong'o N. (2009). *Re-membering Africa.* Nairobi, East African Education Publishers Ltd

Tigiti, K.M (SYS) (2009). *Tungizi za Mnyagatwa***,** Dar es Salaam, Al-Amin Educational and Research Academy (AKADEMIYA)

Vuzo, M, A. C. Amina. (1989). *Lugha na Fasihi*, Nairobi, Oxford University Press.

Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia, Historia na Maendeleo Yake***,** Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi – Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W (2008). *Kanzi ya Fasihi – Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi***,** Nairobi, Vide ~ Muwa Publisherws Ltd.

Warren, M. D. (1995). *The Cultural Dimension of Development: Indiginous Knowledge Systerms.* London, Intermediate Technology Publication

Watts, L.S. (2007). *Encyclopedia of American Folklore***.** New York, Checkmark Books

Wizara ya Elimu. (1997). *Sera ya Utamaduni*. Dar es Salaam

Zirimu, P. and Gurr Andrew (1971). *Black Aesrhetics.* Nairobi, E. A. L. B

Agyekum, K. (2006). *The Sociolinguistic Of Akan Personal Names*. Nordic Journal of African studies 15(2): 206 – 235 (2006)

Dale G (1895). *An Account of the Principal Customs and Habits of the Natives Inhabiting the Bondei Country*. The Journal of the Anthropological Institute of Great Britain and Ireland, Vol. 25 pp. 181-239. Royal Anthropological Institute of Great Britain and Ireland. http://www.jstor.org/stable/2842244.

Dekeba, A (2012). *Basics of Marketing Research Methods***.**

www.globusz.com/ebooks/ MarketingResearch/Index.htm

Kipacha, A (2009). *Journal of Humanities Vol.1 No 1*. Dodoma, The University of Dodoma

Hartwig, G.W. (1971). *Oral Traditions concerning Early Iron Age in Northwesten Tanzania.* African Historical Studies, Vol. 4, No. 1, pp. 93-114. Boston University African Studies Center. http://www.jstor.org/stable/216270.

Matororo, J (2004). *Gazeti la Alasiri.* namba 6429 tarehe 3/2/2004

Naehausi, I (2002). *Bodies, Heat, and Taboos: Conseptualizing Modern Persnhood in the South African***,** Lowveld Journal Article of Ethnology, Vol. 41, 2002

Shorter, A (1968). *Nyungu ya Mawe and The Empire of The Ruga-Rugas, Journal of African History.* Cambridge University Press

Sengo T.S.Y. (1992). *Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini – Unguja***,** Nordic Journal of African Studies 1(1): uk. 53-79

Werner, A. (1909). *The Bantu Element in Swahili Folklore*, Folklore, Vol. 20, No. 4 pp. 432-456. Taylor & Francis, Ltd. on behalf of Folklore Enterprises, Ltd. http://www.jstor.org/stable/1254437

Agyekum, K. (2006). *The Sociolinguistic Of Akan Personal Names*. Nordic Journal of African studies 15(2): 206 – 235 (2006)

Colding, J. (2000). *Taboo System*. www.findarticles.com/p/articles/mi

Colding, J. and, Folke, C. (1997). *The relationship among threatened species and their protection taboos*. www.ecologyandsociety.org/vol1/iss1/art6/

David and Liz (1988) *The African Tribes and Culture – Kikuyu***.** www.theafricantribes. com/samples/

Hartwig, G.W. (1971). *Oral Traditions concerning Early Iron Age in Northwestern Tanzania.* African Historical Studies, Vol. 4, No. 1, pp. 93-114. Boston University African Studies Center. http://www.jstor.org/stable/216270.

Ikee, (2008). *History of African Literature*. http://writinghood.com/ literature/national/

Janetius. (2009). *Sex Taboo and Changing Indian Society***.** IIT Delhi. http://www. anetius.pag.tl

Kidibone, M. (2007). The Potential Role of Social Taboos, http://bcb706.blogspot. com/2007/03/potential-role-of-social-taboos-in_482.html

Kvale, (1996). *An introduction to Qualitative Research* – www.snapad.org.za/ phase3/index.php

Kweka, D. (2004). *The Role of Local Knowledge and Institution in the Conversation of Forest Resources in Eastern Usambara*. http://www.unesco.org/mab/ bursaries/mysrept/2003/kweka/finalRep.pdf.

Matveev, A.V. (2002). *Qualitative Theory*. http://www.russcomm.ru/eng/rca_ biblio/m/matveev01_eng.shtml

Mirambo, I (1999). *Oral Literature of Sukuma.* www.folklore.ee/folkrole/ vol26/mirambo.pdf

Mkilya, P (2008). *Sukuma Culture*. Sunday, April, 20th. 2:09 am www.petermkilya. blogspot.com/2008/04/sukuma.html

Naehausi, I (2002). *Bodies, Heat, and Taboos: Conceptualizing Modern Persnhood in the South African***.** Lowveld Journal Article of Ethnology, Vol. 41, 2002

Osei, J. (2002). *The Values of African Taboos for Biodiversity and Sustainable Development***.** www.africantaboos/

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi***.** Nairobi, Focus Publications

The Free Encyclopedia (2009). *Literary Theory*. Imepakuliwa tar. 1/6/2011 www.en.wikipedia.org/wiki/Literary_theory

Werner, A. (1909). *The Bantu Element in Swahili Folklore*. Folklore, Vol. 20, No. 4 pp. 432-456. Taylor & Francis, Ltd. on behalf of Folklore Enterprises, Ltd. http://www.jstor.org/stable/1254437

# VIAMBATISHI

## Kiambatishi I: Msamiati

| | |
|---|---|
| Bayana | wazi, kinagaubaga |
| Chunguza | fanya utafiti / tafuta habari kwa undani |
| Dhima | wajibu mkubwa pamoja na uwezo wa kufanya jambo |
| Dizeli | pombe ya kienyeji inayotengenezwa kwa mahindi |
| Elekezi | enye kuelekeza jambo |
| Falsafa | elimu ya asili, busara, hekima |
| Firigisi | ni sehemu ya utumbo wa ndege inayosaga chakula, finingi |
| Imani | jambo analolikubali mtu kuwa ni la kweli na analifuata, itikadi, dini |
| Jamii | watu wenye asili moja hasa lugha moja |
| Kangara | pombe ya kienyeji inayotengenezwa kwa mahindi na asali |
| Katizika | kwazwika, kwazwa, |
| Kilema | ulemavu katika mwili |
| Kirombo | mafunzo, elimu ya unyago/ jando |
| Kitenzi | neno linaloarifu tendo linalofanyika |
| Koundanda | ikulu/nyumbani kwa mwene |
| Kufunda | kufundisha mafundisho ya nyumbani, unyago |
| Kufuwawa | kuacha kutumia kitu, kukitelekeza kitu muhimu bila kukitumia |
| Kuhalifu | tenda kinyume cha taratibu au sheria, kataa kutii |
| Kukaidi | kataa kupokea nasaha / ushauri, shindani, babaka |
| Kusotea | enda kwa makalio |
| Laana | ukosefu wa radhi ya mwenyezi Mungu/ wazazi, apizo apewalo mtu ili afikwe na ubaya |
| Maadili | Mwenendo au tabia njema inayokubalika katika jamii husika |
| Makala | ngoma ya asili ya Wabungu |
| Mizungu | mafunzo ya hekima hususan katika kumbi za uganga yatolewayo kwa siri |
| Mkimbizi | mtu akimbiliaye nchi nyingine, mtu asiye na kwao |
| Mwanataalimu | mwanaakademia (mwanataaluma) |
| Mwene | chifu mtawala wa jadi wa eneo la jamii |

| | |
|---|---|
| Mwiko | marufuku, jambo akatazwalo mtu kulifanya au kutumia kwa hofu ya kudhurika |
| Nuhusi | mkosi, niksi |
| Rijali | mwanaume mwenye nguvu za kiume |
| Rimbuka | majivuno yasiyo na maana |
| Shadidia | shikilia msimamo kwa nguvu |
| Shetani | ibilisi, milihoi, rajimi, malaika aliyelaaniwa na Mungu kwa kwa kukataa kufuata amri zake mwenyezi Mungu |
| Simbakaleindei | wimbo wa ngoma ya makala |
| Subira | uvumilivu wa jambo ili kupata matokeo ya mwisho, |
| Ufafanuzi | maelezo ya kina ya kuchambua jambo |
| Uhabithi | uovu, ufisidi, ujini |
| Ulimbe | sayansi |
| Utangu | asili |
| Utaratibu | namna maalumu ya kutekeleza jambo |
| Wajibati | jukumu, wajibu, madaraka |
| Wasungo | watu wasiopata elimu ya jadi, unyago/ jando |
| Visado | kopo kubwa  la ujazo wa lita nne, la rangi ya sadolini |

**Kiambatishi II: Gharama za Utafiti**

Mchanganuo wa Gharama Tarajiwa za Utafiti

Rasilimali zinazotarajiwa kutumika ni fedha taslimu za Kitanzania zisizopungua shilingi milioni tatu, na kumi na saba elfu, na mia tano tu (7,813,000**TSh**). Matumizi yatakuwa kama ifuatavyo;

| **TUKIO/KIFAA** | **IDADI** | **GHARAMA@** TSh | **JUMLA** (Fedha) |
|---|---|---|---|
| Usafiri (Arusha – Mbeya) | 2 | 130,000 x 2 | 260,000 |
| Chakula | siku 60 | 10,000 x 2 | 1,200,000 |
| Malazi | Siku 60 | 20,000 x 2 | 2,400,000 |
| Usafiri Chunya Pikipiki | Siku 10 | 25,000x 2 | 500,000 |
| *Flash* | 1 | 150,000 | 150,000 |
| Kinasa-Picha | 1 | 400,000 | 400,000 |
| Karatasi nyeupe | Mabunda 4 | 7,000 | 21,000 |
| Kalamu<br>Penseli<br>Rula | 5<br>5<br>2 | 500<br>200<br>500 | 2,500<br>1,000<br>1,000 |
| Shajara (file) | 1 | 3000 | 3,000 |
| Banio (Stapler)<br>Kitoboleo (Punching) | 1<br>1 | 3500<br>6,000 | 3,500<br>6,000 |
| Posho kwa washiriki | - | - | 300,000 |
| Uchapishaji (Printing) | Pendekezo (6)<br>Ripoti (2) | 250 x 1000<br>500 x 1000 | 1,500,000<br>500,000 |
| Uvuvulishaji (Photocopy)<br>Vitabu | Pendekezo(10)<br>Ripoti (8) | 250 x 50<br>8 x 25,000 | 125,000<br>200,000 |
| Gharama nyiginezo | - | - | 500,000 |
| **JUMLA YOTE** | - | - | **7,813,000** |

**Kiambatishi III: Ratiba ya Utafiti**

Utafiti huu unatarajiwa kufanyika katika kipindi cha miezi ishirini na maja tangu Oktoba, 2009 hadi Juni, 2011. Mchakato wa matukio utakuwa kama ifuatavyo;

| Na: | Shughuli | Muda wa Kutekelezwa | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **2009** | | | | | | | | | | | |
| | | J | F | M | A | M | J | J | A | S | O | N | D |
| 1 | Kuandaa muswada wa utafiti | | | | | | | | | | | | |
| | | **2010** | | | | | | | | | | | |
| | | J | F | M | A | M | J | J | A | S | O | N | D |
| 2 | Kuandaa muswada wa utafiti na kuuwasilisha | | | | | | | | | | | | |
| 3 | Kuwasilisha na kurekebisha muswada wa utafiti kufuatana na maoni ya wataalamu | | | | | | | | | | | | |
| 4 | Kukusanya data | | | | | | | | | | | | |
| 5 | Uchambuzi wa awali wa data | | | | | | | | | | | | |
| 6 | Kuandika sura ya 1 – 3 | | | | | | | | | | | | |
| 7 | Kurekebisha sura 1 – 3 kufuatana na maoni ya wataalamu | | | | | | | | | | | | |
| 8 | Kuandika sura ya 4 na kuiwasilisha | | | | | | | | | | | | |
| | | **2011** | | | | | | | | | | | |
| | | J | F | M | A | M | J | J | A | S | O | N | D |
| 9 | Kurekebisha sura ya 4 kufuatana na maoni ya wataalamu | | | | | | | | | | | | |
| 10 | Kuandika sura ya 5, kuiwasilisha na kuirekebisha | | | | | | | | | | | | |
| 11 | Kuiwasilisha rasimu ya kwanza ya matokeo ya utafiti kwenye semina | | | | | | | | | | | | |
| 12 | Kuifanyia marekebisho rasimu ya kwanza kufuatana na maoni ya wataalamu | | | | | | | | | | | | |
| 13 | Kuwasilisha na kutetea / kufafanua matokeo ya utafiti | | | | | | | | | | | | |

Tarehe **Julai, 2010**
Jina **Joachim A.N. Kisanji**
Sahihi: ………………………………………
Maoni ya Msimamizi…………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
Tarehe:……………………………………..……………………………………
Jina ………………………………………………………………………………
Sahihi: ……………………………………………………………………………

**Kiambatishi IV: Maswali ya utafiti**

**Hojaji kwa Watu Wazima**

1. Kuna ulimbe gani katika miiko ya Wabungu?
    - Je, unajua miiko yoyote katika jamii ya Wabungu?
    - Nitajie baadhi ya miiko unayoifahamu
    - Uliijuwaje miiko hii?
    - Je, unafikiri wabungu wote wanaifahamu miiko hii?
    - Wabungu wanaitumia miiko katika shughuli zao za kila siku?
    - Kama ndiyo / kama hapana, kwa nini?
    - Wewe unaitumia miiko hii?
    - Ni miiko gani unaitumia zaidi? Kwa nini?
    - Miiko hii uliitumia kwa nani?
    - Miiko hii uliitumia katika mazingira gani?/ uliona nini kilichokufanya kutumia miiko hii?
    - Uliitumia miiko hii baada ya kuona nini?
    - Kuna matatizo gani yanayoweza kujitokeza kama watu hawataitumia miiko hii?
    - Kuna shughuli gani za kimila zinazotumia miiko zaidi?

    Ngoma / harusi / misiba / uganga / kilimo / uvuvi / uwindaji nk.

    - kwa namna gani?

2. Mambo gani yanaifanya miiko isitumike katika jamii ya Wabungu?
    - Mtu anayevunja mwiko huchukuliwa hatua gani?
    - Zamani mtu aliyevunja mwiko alichukuliwa hatua gani?
    - Vitu gani vinasababisha mtu kuvunja mwiko?
    - Wabungu wanaichukuliaje miiko sasa?
    - Ni vitu gani vya kisasa vinavyosababisha mtu kuvunja mwiko?
    - Ni vitu gani vya asili vilivyosababisha mtu kuvunja mwiko?
    - Ulishawahi kumsikia kiongozi akitumia miiko kuonya jambo lolote?
    - Ni kwa namna gani? Toa mfano.
    - Ni kwa namna gani utajiri wa mtu unasaidia kulinda miiko?

- Ni kwa namna gani utajiri wa mtu unasaidia kuvunja miiko?

3. Ni mambo gani yafanyike ili Wabungu waitumie miiko yao?
    - Miiko gani ungependa watu waifuate?
    - Kwa nini unapenda waifuate?
    - Ni miiko gani kama watu wataifuata watakuwa na maadili mema?
    - Miiko gani unayoijua ambayo hupendi watu wasiifuate? Kwa nini?

**Hojaji kwa Viongozi:**

1. Kuna ulimbe gani katika miiko ya Wabungu?
    - Wewe kama kiongozi katika jamii ya Wabungu;
    - Unajua miiko yoyote katika jamii ya Wabungu?
    - Nitajie baadhi ya miiko unayoifahamu
    - Uliijuwaje miiko hii?
    - Unafikiri wabungu wote wanaifahamu miiko hii?
    - Wabungu wanaitumia miiko katika shughuli zao za kila siku za malezi ya vijana?
    - Kama ndiyo / kama hapana, kwa nini?
    - Wewe unaitumia miiko katika shughuli za uongozi?
    - Ni miiko gani unaitumia zaidi? Kwa nini?
    - Unakumbuka tukio lolote ambalo wewe au kiongozi mwenzako alitumia mwiko kuonya au kuhukumu?
    - Uliona nini kilichokufanya kutumia miiko?
    - Uliitumia miiko hii baada ya kuona nini?
    - Kuna matatizo gani yanayoweza kujitokeza kama watu hawataitumia miiko?
    - Kuna shughuli gani za kimila zinazotumia miiko zaidi?
      Ngoma / harusi / misiba / uganga / kilimo / uvuvi / uwindaji nk.
      - kwa namna gani?

2. Mambo gani yanaifanya miiko isitumike katika jamii ya Wabungu?
    - Zamani mtu aliyevunja mwiko alichukuliwa hatua gani?
    - Vitu gani vinasababisha mtu kuvunja mwiko?

- Ni miiko gani mtu akivunja anakuwa amepotoka kimaadili?
- Wabungu / viongozi wanaichukuliaje miiko sasa?
- Ni vitu gani vya kisasa vinavyosababisha mtu kuvunja mwiko?
- Ni vitu gani vya asili vilivyosababisha mtu kuvunja mwiko?
- Ulishawahi kumsikia kiongozi mwenzako akitumia miiko kuonya jambo lolote?
- Ni kwa namna gani? Toa mfano.

3. Ni mambo gani yafanyike ili Wabungu waitumie miiko yao?
    - Miiko gani watu wakiifuata watarahisisha kazi yako ya uongozi?
    - Kwa namna gani kazi yako itakuwa rahisi?
    - Miiko gani unayoijua ambayo inaleta matatizo katika uongozi? Kwa namna gani?
    - Ni miiko gani unafikiri inaimarisha maadili ya jamii ya Wabungu?

**Hojaji kwa Watoto**

1. Kuna ulimbe gani katika miiko ya Wabungu?
    - Je, unajua miiko yoyote katika jamii ya Wabungu?
    - Nitajie baadhi ya miiko unayoifahamu
    - Uliijuwaje miiko hii?
    - Je, unafikiri watoto wote wa Kibungu wanaifahamu miiko hii?
    - Wabungu wanaitumia miiko katika shughuli zao za kila siku?
    - Wewe unaitumia miiko hii kwa wenzako?
    - Ni miiko gani ulishawahi kuitumia?
    - Uliona nini au mwenzako alifanya nini hadi ukautumia?
    - Kuna shughuli gani za kimila ambazo watu wanatumia miiko?

      Ngoma / harusi / misiba / uganga / kilimo / uvuvi / uwindaji nk.

      - kwa namna gani?

2. Mambo gani yanaifanya miiko isitumike katika jamii ya Wabungu?
    - Mtu anayevunja mwiko huchukuliwa hatua gani?

- Vitu gani vinasababisha mtu kuvunja mwiko?
- Wabungu wanaichukuliaje miiko sasa?
- Ni vitu gani vya kisasa vinavyosababisha mtu kuvunja mwiko?
- Ni vitu gani vya asili vilivyosababisha mtu kuvunja mwiko?
- Ulishawahi kumsikia kiongozi/ mwalimu akitumia miiko kuonya jambo lolote? Toa mfano.
- Ni kwa namna gani utajiri wa mtu unasaidia kulinda au kuvunja miiko?

3. Ni mambo gani yafanyike ili Wabungu waitumie miiko yao?
   - Miiko ga ni ungependa watu waifuate?
   - Kwa nini unapenda waifuate?
   - Ni miiko gani kama watu wataifuata watakuwa na tabia njema?
   - Miiko gani unayoijua ambayo hupendi watu wasiifuate? Kwa nini?

## Kiambatishi V: Miiko ya Kibungu na Tafsiri

### Miiko kuhusu adabu na heshima

1. Mwiko koupeita pakasi ya awandou wana wapanga

   Ni mwiko kupita katikati ya watu wanaozungumza

2. Mwiko koulamka akali oukou oumakwenda, noulei ouwabyeda

   Ni mwiko kusalimia/ amkia wakubwa ukiwa unaendelea kutembeya, ni kuonesha dharau

3. Mwiko oundumendo kouleka koupeoukeika akali eizeila

   Ni mwiko kwa vijana kuacha kupisha watu wazima njia

4. Mwiko koukoumpa ounkali amazei au eichindou oukou ouimeilile nangaa koutungama

   Ni mwiko kumpa mtu mzima maji au kitu ukiwa umesimama bila kupiga magoti

5. Mwiko kouchelewa koukoudya piwaza, naoulei wa nsini

   Ni mwiko kuchelewa muda wa kula wote, ni tabia ya uchoyo

6. Mwiko kuokoumpeita ounkali nge alei noumligo nangaa koukountangana

   Ni mwiko kumpita mtu mzima kama ana mzigo bila kumpokeya

7. Mwiko koukwiwa, oulaweine iwala

   Ni mwiko kuiba, utaugua ukoma

8. Mwiko koupeita pakasi ya akali / awandou

   Ni mwiko kupita katikati ya wakubwa au watu

### Miiko kuhusu watoto

9. Mwiko awana koukwikala kouyeni nangaa koukwavwa eimileimo

   Ni mwiko kwa watoto ugenini kukaa bila kusaidia kazi

10. Mwiko koukana koutoumiwa na akali

    Ni mwiko kukataa kutumwa na wakubwa

11. Mwiko koukwangoula pana oukoumweita ounkali

    Ni mwiko kumwita mtu mzima kwa kupiga yowe

12. Mwiko koukana oulweito wakanaya oulounongwa

    Ni mwiko kukataa wito, kataa neno

13. Mwiko alumendo koukona enumba eingoulou yeina wakonaya alezi

    Ni mwiko kwa vijana kulala nyumba kubwa wanayolala wazazi

14. Mwiko koutoukana eindousi

    Ni mwiko kutukana matusi

15. Mwiko acheichei koukwanda koukalawa na koukoudya ngei akali wacheilei

    Ni mwiko kwa watoto kuanza kunawa na kula kabla ya watu wazima

16. Mwiko awana koukolela kououka piwaza pana wakoudya na kouleka akali

    Ni mwiko kwa mtoto au kijana kutanguliya kuondoka mezani wanapokula chakula kabla ya watu wazima

17. Mwiko acheichei koukwanda koukoudya einani ngei watapasiwa na akali

    Ni mwiko kwa watoto kuanza kula mboga kabla ya kugwiwa na watu wazima

18. Nwiko kououka pana nge wampa amazei ounjeni au ounkali

    Ni mwiko kuondoka baada ya kumpa maji mgeni au mtu mzima

**Miiko kuhusu ndoa**

19. Mwiko akoi koukona enumba eidyeimu na wana/ akoi

    Ni mwiko kwa wakwe kulala nyumba moja na watoto/ wakwe

20. Mwiko koukoudya eichakoudya na akoi/ oumaivyala nou taivyala

    Ni mwiko kula chakula na wakwe / mama mkwe na baba mkwe

21. Mwiko koukoudya eichakoudya ouimeilile, oulaloole au koulooliwa koutani

    Ni mwiko kula chakula ukiwa umesimama, utaoa au kuolewa mbali

22. Mwiko kouloola nangaa kouweivwa alezi wakwe (ataei)

    Ni mwiko kuoa bila kuwasikiliza wazazi

23. Mwiko koupanga einongwa zya kali ngei koulei awana acheche

    Ni mwiko kuzungumza masuala ya ngono kama kuna watoto

24. Mwiko kouloola au koulooliwa nangaa alezi kouzumeila

    Ni mwiko kuoa au kuolewa bila ridhaa ya wazazi/ bila ya wazazi kukubali

25. Mwiko kwa ouwacheiloume koufuma pazi ngei ounchima aleineinda, einda eilafume

    Ni mwiko mume kutoka nje ya ndoa kama mkewe ni mja mzito, mimba itatoka

26. Mwiko koufuma pazi ngei ouwazile kounseizo, ouleipate eimidyoungou nnzeila

    Ni mwiko kwa mume kutoka nje ya ndoa kama anakwenda safari, atapata matatizo njiani

**Miiko kuhusu viongozi (Mwene)**

27. Mwiko koupanga einongwa zya kwikumbo lya akali kouzi/ kwa wandou chaka

    Ni mwiko kuzungumza habari za baraza la wazee kwa asiyehusika

28. Mwiko oumwene koukwinjeila kounsei ya mwene ouweinjei ngei watampozya

    Ni mwiko kwa mwene mmoja kuingia ndani ya eneo la mwene mwingine bila taarifa

29. Mwiko koukwikaleila eicheitei cha mwene

    Ni mwiko kukalia kiti cha mwene

30. Mwiko koukana einongwa ya mwene

    Ni mwiko kukataa neon/ amri ya mwene

31. Mwiko koufunya eingama zya mwene kwa wandou awachaka na apeimbeilei

    Ni mwiko kutoa siri za mwene kwa watu wasiohusika na wageni

32. Mwiko oumwene kouwala koucheinda / kousawa koumbana / kouloukouwa

    Ni mwiko kwa mwene kwenda kuoga au kuogelea mtoni au ziwani

33. Mwiko oumwene kouwala kouvweima nndonde

    Ni mwiko kwa mwene kwenda kuwinda porini

34. Mwiko kouwala koutimbana kouloukweimba nei sao au eivyakoudya koufuma kouzi ya Kwiwoungou

    Ni mwiko kwenda kutambika kwimba na mali au vyakula kutoka nje ya nnchi ya Wabungu

35. Mwiko oumwene koulola ounfyule.

    Nimwiko kwa mwene kuangalia maiti ya mtu.

**Miiko kuhusu vijana**

36. Mwiko kouloola / koulooliwa noundou ouwacheilema, mlalele awana awacheilema

    Ni mwiko kuoa au kuolewa na mtu mwenye kilema, mtazaa watoto walemavu

37. Mwiko oundumendo koukwikala kouwawetekela alezi (ise nou nina) wampe cheila cheindou, ataleiloole

    Ni mwiko kwa kijana kuwategemeya wazazi kumpa kila kitu, hawezi kuoa

38. Mwiko ouwachichima kousenda einda ngei acheilei atalooliwa

    Ni mwiko kwa msichana/ mwanamke kubeba mimba kabla hajaolewa

39. Mwiko achichima kouvwala ounsomeko/ eisalawili

    Ni mwiko kwa wanawake kuvaa suruali

40. Mwiko kouvwala eimmyenya yeina eilemile oumbeilei

Ni mwiko kuvaa nguo za kubana mwilini

41. Mwiko achichima kouvwala eimyenda eimipi

    Ni mwiko kwa wanawake kuvaa nguo fupi

42. Mwiko koukwiyeileila eitabiya eizyachaka koufuma kwa peimbeilei

    Ni mwiko kuiga tabia / kutabii tabia mbaya kutoka kwa wageni

43. Mwiko alumendou kowetekela cheilacheindou koufuma kwaalezi wakwe (nouko nouso)

    Ni mwiko kwa vijana kuwategemeya wazazi kwa kila kitu

44. Mwiko ouwachichima kousenda einda ngei oucheilei utalooliwa

    Ni mwiko kwa msichana kubeba mimba kabla ya kuolewa

45. Mwiko koukoumpa ouwachichima einda ngei atalooliwa

    Ni mwiko kwa mvulana kumpa msichana mimba kabla ya kuoa

46. Mwiko koukwinjeleila eipangwe lya akali

    Ni mwiko kwa vijana kuingilia mazungumzo ya watu wazima

47. Mwiko kouloola nangaa koulooliwa koulouko louna loulei neiiwala / eimeina

    Ni mwiko kuoa au kuolewa katika ukoo wenye ukoma au ugonjwa wa kuambukiza

48. Mwiko koukwikaleila ouloupe, ouleilembe amapoumba koumatako

    Ni mwiko kukalia ungo, utota majipu matakoni

49. Mwiko koukwikaleila eitoulei, oulaloola achichima wazumaleika

    Ni mwiko kulalia kinu, kila ukioa mke atakuwa anakufa

50. Mwiko koukwikuseila oulousanga lwa koumbana au kouloukouwa, oumalengela alezi wafwe eicheikalakashe

    Ni mwiko kujisugulia mchanga unapooga ufukweni mtoni au baharini, utakuwa unawaombea wazazi kufa haraka

**Miiko kuhusu vyakula**

51. Mwiko ouwachichima ouwanda koukoudya amayei, aleilele oumwana youna atakola einyele

    Ni mwiko kwa mwanamke mjamzito kula mayai, atazaa mtoto asiyekuwa na nywele/ mwenye upara

52. Mwiko ouwachichima koukoudya einyondo, aleiwe ni byedo kwa ndoume

    Ni mwiko kwa mwanamke kula filigisi, atakuwa na dharau kwa mumewe

53. Mwiko koudyeila eichakoudya einchisi, mleidye ni lindou

    Ni mwiko kula chakula gizani, mtakula na shetani/ jini/ jinamizi

54. Mwiko ouwachichima koukoudya einyama eiya nyama yeina eileineinda, pana wa Leila aleipate eimidyoungou

    Ni mwiko mwanamke kula nyama ya myama mwenye mimba, wakati wa kujifungua atapata shida

**Miiko kuhusu bahari na uvuvi**

55. Mwiko koukuseila eivindou vina vilei neivilo koumbana au kouloukouwa, eiswei zeileitame

    Ni mwiko kusafishia vyombo vyenye masizi mtoni au ziwani, samaki wataadimika

56. Mwiko achichima kouchendeila koumbana / kouloukouwa, eiswei zeileitame

    Ni mwiko kwa wanawake kuoga mtoni/ ziwani, samaki wataadimika

57. Mwiko achichima kouwala koumbana / kouloukouwa ngei waweinile, eiswei zeileitame

    Ni mwiko kwa wanawake kwenda mtoni/ ziwani wakiwa katika siku zao, samaki wataadimika

58. Mwiko koukwinjeila mmbwato neindyato

    Ni mwiko kuingia ndani ya mtumbwi na viatu

59. Mwiko kotwala einungou eivilyo koumbana / kouloukouwa

    Ni mwiko kupeleka chungu chenye masizi mtoni / baharini

60. Mwiko kouwala kouloukouwa kouchina au koukwendanga outoupou

    Ni mwiko kwenda ziwani kucheza au kutembea bila sababu

**Miiko kuhusu uwindaji**

61. Mwiko koukoma oulououzi ousikou, oumakweita eizoka

    Ni mwiko kupiga mluzi usiku, unaita nyoka

62. Mwiko ouwachichima koukoma oulououzi, oumakweita eizoka

    Ni mwiko kwa mwanamke kupiga mluzi, unaita nyoka

63. Mwiko kouwala kwivweimo ngei koukaya ouleikile iwo/ ngei mfumile koukoulwa, ouleikomengane neisama

    Ni mwiko kwenda mawindoni kama nyumbani umeacha ugomvi au umetoka kugombana na mtu, utapata balaa/ utapambana na wanyama wakali

64. Mwiko ouwachichima kouwala nndonde kouvweima, einyama zeileitame

    Ni mwiko kwa mwanamke kwenda msituni kuwinda, wanyama wataadimika

65. Nwiko koufuma pazi ngei ouwazile mwivweimo, mtaleikomange

Ni mwiko kutoka nje ya ndoa unapokwenda mawindoni, utapata balaa/ hautaua mnyama

66. Mwiko koukoma eichongo nndonde, mlatyege eizeila

Ni mwiko kupiga kelele mawindoni, mtapotea njia

67. Mwiko koumanga enyama yeina mwakomanga, awandou waleipweke

Ni mwiko kuruka nyama mliyoua, walaji wataharisha

68. Mwiko koukung’unda ouncheila pana moufyounda enyama, awandou waleipweke

Ni mwiko kukung’uta mkia wa myama mnapochuna nyama, walaji wataharisha

69. Mwiko koucheilanda/ koumanga igogo/ ikwi, eizoka ngei yakouluma outaleipoulouke

Ni mwiko kuruka gogo, nyoka akikuuma huwezi kupona

70. Mwiko ounhali koulema eimidusi, outaleikomange/ aleikoupe ivumo

Ni mwiko kwa hawara kishika bunduki, utapata mikosi huwezi kuua mnyama

71. Mwiko koudyata eindouwalouwa nndonde, ulatyege kousouwa koukaya.

Ni mwiko kukanyaga maua ya kafauongo msituni, utapotea njia ya kurudi nyumbani

**Miiko kuhusu kilimo**

72. Mwiko koukoudya nchalo nge ouimeilile, einyama zya ndonde zeileikoudya / kouluwanga eivyanchalo

Ni mwiko kula chakula ukiwa umesimama shambani, wanyama wa msituni watakula au kuharibu mazao shambani

73. Mwiko koucheimbeila nchalo, eingoulouwe zeilakwinjeila nchalo

Ni mwiko kukimbia shambani, nguruwe watakuwa wanaingia na kuharibu mazao shambani

74. Mwiko koukoumpa oundou eimbeyu kounkono, zeitaleikome eivinonu

Ni mwiko kumpa mtu mbegu mkononi (zinawekwa chini), mazao hayatakomaa vizuri

75. Mwiko koukwinjeizya eivindou vina vilei neivilo nchalo, eivyakoulya vitaleikome eivinonu

Ni mwiko kuingiza vitu vyenye masizi shambani, mazao hayataweza kukomaa vizuri

76. Mwiko koukwinjeila nchalo cha mbalala neindyato/ eindala, oulepate amampoo

Ni mwiko kuingia na viatu au kandambili katika shamba la Karanga, haziwezi kukomaa vizuri

**Miiko kuhusu wanawake**

77. Mwiko ouwachichima koukwikala pakasi ya ndyango, aleilooliwe koutani

Ni mwiko kwa msichana kukaa katikati ya kizingiti cha mlango, atakuja kuolewa mbali

78. Mwiko ouwachichima kouteleka ngei alei nsikou, ngei waweina eicheifua cheitaleipone oulouweilo

Ni mwiko kwa mwanamke akiwa katika siku zake kupika, akiugua kifua hakitapona haraka

79. Mwiko ouwachichima ngei aleinsikou kouyawa einani eizyamatoundou nchalo, zeilakale

Ni mwiko kwa mwanamke akiwa katika siku zake kuchuma mboga za majani shambani, zilizobaki zitakauka

80. Mwiko ouwachichima ngei aleinsikou koulema omwana oumemba youna kasi oumwanakwe

Ni mwiko kwa mwanamke akiwa katika siku zake kumshika mtoto mchanga asiye wake

81. Mwiko ouwachichima koukoumpa oundoume eichakoudya ngei atayozya

Ni mwiko kwa mke kumpa chakula mumewe bila kuonja

82. Mwiko ouwachichima koupakoula ouwalei nangaa kouwanda, iyazi kwa nina

Ni mwiko kwa mwanamke kupakuwa ugali bila kuuviringa vizuri, ni aibu kwa mama yake

83. Mwiko ouwachichima koufuma pazi ngei oundoume aleindonde/ kounseizo, oundoume aleipate eiminkosi

Ni mwiko kwa mke kutoka nje ya ndoa mumewe akiwa mawindoni/ safarini, mumewe atapata balaa/ mikosi

84. Mwiko ouwachichima koukwiyaleila oundyango/ oulwiye ounsanankoulou ngei oundoume aleindonde kwivweimo, akouwa wiyaleila ipolu ataleikomange

Ni mwiko kwa mke kufunga mlango wa nyumba mchana kama mume amekwenda kuwinda, atakuwa amefunga pori mumewe huko porini hawezi kuona wala kuua mnyama

85. Mwiko achichima kouwala koucheinda koumbana / kouloukouwa, eiswei zelatame

Ni mwiko kwa wanawake kwenda kuoga mtoni / ziwani, samaki wataadimika

86. Mwiko achichima koukoma oulououzi

Ni mwiko kwa wanawake kupiga mluzi

87. Mwiko koukoumpilimya ouwachichima ouwanda amazei kwitundwe, oulousikou oulwalela amazei aminji yaleifume

    Ni mwiko kumzungusha maji mjamzito, siku ya kujifungua maji mengi yatamwagika

88. Mwiko ouwachichima kouwala kounseizo na koukwikala kouyeni mpaka eisikou zyakwe zeipeite, aleimeikekei koulela

    Ni mwiko kwa mwanamke kusafiri na kukaa ugenini hadi siku zake zipite kabala ya kurudi nyumbani kwake, atasimamaisha uzazi

**Miiko kuhusu wanaume**

89. Mwiko ouwacheiloume kouteleka

    Ni mwiko kwa mwanamume kuingia kupika jikoni

90. Mwiko koutoundeila moumbana au mmazei

    Ni mwiko kukojolea ndani ya mto/ majini

91. Mwiko kousuleila mwitoulei, ngei waloola achimako waleizumaleika

    Ni mwiko kujambia ndani ya kinu, ukijaoa wake wako watakuwa wanakufa

**Miiko kuhusu maradhi**

92. Mwiko kousangeila eivindou nou oundou ouwiwala

    Ni mwiko kuchangia vitu na mgonjwa wa ukoma

93. Mwiko koukwikala einumba eidyeimu noundou ouwiwala

    Ni mwiko kukaa nyumba moja na mtu mwenye ukoma

**Miiko kuhusu safari**

94. Mwiko ouwachichima ouwanda kouwala ounseizo ousikou

    Ni mwiko kwa mwanamke mjamzito kusafiri umbali mrefu usiku

95. Mwiko koupozya awandou oulousikou oulwanseizo

    Ni mwiko kutangaza kwa watu siku ya safari

96. Mwiko koukona nouwachichima mmbwato

    Ni mwiko kufanya ngono ndani ya mtumbwi

**Miiko kuhusu usafi**

97. Mwiko koupyela ousikou

    Ni mwiko kufagia usiku

98. Mwiko kousoumba vina wapyela ousikou

Ni mwiko kutupa takataka ulizozifagia usiku

99. Mwiko kouleka ountingo noukoko ngei wamala kouomba

Ni mwiko kuacha mwiko na ukoko baada ya kumaliza kupika chakula

**Miiko kuhusu utunzaji wa watoto**

100. Mwiko kouchindoula oumwana ouncheche

Ni mwiko kumsitua mtoto mdogo

101. Mwiko koukandeila eimyenda ya mwana oumemba moumbana

Ni mwiko kufulia nguo cha mtoto mchanga mtoni au ziwani

102. Mwiko kouwa nei mbapo eiyapapeila oumwana oumemba koulouwaya

Ni mwiko kwenda na mbeleko ya kumbebea mtoto mchanga chooni

**Miiko mingine**

103. Mwiko koukwitoumbeka koukwinyonga

Ni mwiko kujinyonga

104. Mwiko kousousa eimyienda ngei ouvwite moumbeilei

Ni mwiko kushona nguo ukiwa umevaa mwilini

105. Mwiko kouvulounganya eichakoudya noulwambei, awandou waleiweinei mounda koupweka oulanda

Ni mwiko kukoroga chakula kwa kutumia kisu, walaji wataumwa tumbo la kukata na kuhara damu

106. Mwiko kolamba ouwacheiloume neicheifute

Ni mwiko kumpiga mwanaume na ufagio

107. Mwiko kouwala kounsima ousikou, mlakomenganei neilindou

Ni mwiko kwenda kisimani usiku mtakutana na shetani/ jini/ jinamizi

108. Mwiko kouwala koukala oumunu ousukou

Ni mwiko kwenda kununua chumvi dukani usiku

109. Mwiko koukwieteikeila ousikou ilingou itoupou ngei outambona oundou, ilingou leilasendiwe

Ni mwiko kuitika sauti tupu usiku bila kumwona mtu, sauti itapotea

110. Mwiko kousouseila eimyenda ngei ouvwite moumbeilei, outaleikale eimyenda eimipya

Ni mwiko kushonea nguo ukiwa umevaa mwilini, huwezi kupata/ kununua nguo mpya

111. Mwiko koukwinjeila mmakala ngei kasi wi lombwe

Ni mwiko kuingia katika ngoma ya Makala kama si mhusika

112. Mwiko koudyela eichakoudya nnumba/ koumbele, ousini

Ni mwiko kulia chakula chumbani, ni uchoyo


113. Mwiko koucheilanda amanama yanndou youna atambalizye

Ni mwiko kuruka miguu ya mtu aliyekaa na kunyoosha miguu

114. Mwiko koukwifunuganya naakali

Ni mwiko kijibizana na watu wazima kwa hasira

**Kiambatishi VI: Ramani ya Eneo la Utafiti**




Eneo la rangi ya kijani lenye vijiji vya Kapalala, Mbangala na Mkwajuni ndilo lililohusika na utafiti huu

Chanzo cha ramani ni Atlasi ya Lugha za Tanzania (2009)

**Angalizo:** Uwazi uliopo ziwa Rukwa kijiji cha Udinde haupo